Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

EQUIPPING CHURCH LEADERS
• EAST AFRICA •

**HUDUMA YA KUWAWEZESHA VIONGOZI WA KANISA AFRIKA MASHARIKI**

# 1 TIMOTHEO: DONDOO/MWONGOZO MFUPI; UCHAMBUZI; KIJARIDA CHA MAFUNZO YA KIUTENDAJI

**na**
**Jonathan M. Menn**

**B.A., University of Wisconsin-Madison, 1974**
**J.D., Cornell Law School, 1977**
**M.Div., Trinity Evangelical Divinity School, 2007**

**Equipping Church Leaders East Africa, Inc.**
**714 S. Summit St., Appleton, WI 54914**
**+1-920-2846841 (mobile and WhatsApp)**
**jonathanmenn@yahoo.com**
**www.eclea.net**

Julai 2007; marudio Julai 2013.

Kitabu cha Timotheo wa Kwanza ni mojawapo ya vitabu muhimu sana katika Agano Jipya, kikiwa na malengo mawili ya fundisho la kimaandiko na mwenendo wa kimatendo. Kinashughulikia mambo muhimu ya tabia ya imani yetu: wokovu ulioko kwa neema itokanayo na imani iliyo kwa Yesu Kristo; umuhimu wa maombi; kiwango kinacho mfaa mtu kuwa kiongozi wa kanisa; na umuhimu wa Yesu. Kitabu hiki pia kinashughulikia hali halisi kimatendo kwa mambo muhimu: yaliyo ya kweli na yaliyo kinyume na mafundisho ya uongo; nidhamu ya maisha ya kiroho yahusuyo mtu; kumadibisha na kumshauri mtu; wajibu wa kanisa kwa maskini na wenye mahitaji; hali zihuzuzo wazee wa kanisa; na injili na fedha. Kitabu hiki kimebeba fupisho fafanuzi, na muhtasari juu ya, kitabu cha 1 Timotheo. "Kijarida cha mafunzo kwenye Kitabu hiki" mfululizo wa maswali katika sehemu za 1 Timotheo kwa ajili ya mjadala katika vikundi vidogo vidogo, kuwasaidia Wakristo kwa jumla na viongozi wa kanisa ili hasa waweze kutathmini maisha yao ya kiroho na hali halisikwenye makanisa yao.

**(Nukuu zote za maandiko matakatifu ni kutoka bibilia ya Swahili Union Version © 1997, ama sivyo ni kwa maelezo maalum)**

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO


1 TIMOTHEO: DONDOO / MWONGOZO MFUPI ........................................................................2
1 Tim 1:1-2:15—Mafundisho ya Uongo Kinyume na Uaminifu wa Injili........................................2
1 Tim 3:1-13—Sifa za kuwa Kiongozi wa Kanisa..............................................................3
1 Tim 3:14-4:16—Utauwa wa kweli Kinyume na Utauwa Batili.....................................................4
1 Tim 5:1-6:21—Matatizo ya Kitendaji na Mambo Yawakabiliyo Viongozi wa Kanisa.........................5

1 TIMOTHEO: UCHAMBUZI..7
1 Tim 1:1-2:15—Mafundisho ya Uongo kinyume na Uaminifu wa Injili.......................................7
1:1-2.........................................................................................7
1:3-4.........................................................................................10
1:5...........................................................................................11
1:6-11........................................................................................12
1:12-16.......................................................................................13
1:17..........................................................................................15
1:18-20.......................................................................................16
2:1-7.........................................................................................17
2:8-15........................................................................................20
1 Tim 3:1-13—Sifa za kuwa Kiongozi wa Kanisa ..............................................................26
3:1-7.........................................................................................26
3:8-13........................................................................................29
1 Tim 3:14-4:16—Utauwa wa kweli Kinyume na Utauwa Batili.....................................................30
3:14-16.......................................................................................30
4:1-7a........................................................................................31
4:7b-16.......................................................................................35
1 Tim 5:1-6:21—Matatizo ya Kiutendaji na Mambo Yawakabiliyo Viongozi wa Kanisa.........................38
5:1-2.........................................................................................38
5:3-16........................................................................................39
5:17-18.......................................................................................42
5:19-25.......................................................................................43
6:1-2a........................................................................................45
6:2:b-16......................................................................................46
6:17-19.......................................................................................51
6:20-21.......................................................................................53

1 TIMOTHEO: KIJARIDA CHA MAFUNZO YA KIUTENDAJI.................................................................54
1 Timotheo 1:1-7...............................................................................54
1 Timotheo 1:8-20..............................................................................57
1 Timotheo 2:1-7...............................................................................59
1 Timotheo 2:8-15..............................................................................59
1 Timotheo 3:1-13..............................................................................60
1 Timotheo 3:14-16.............................................................................62
1 Timotheo 4:1-7a..............................................................................64
1 Timotheo 4:7b-16.............................................................................65
1 Timotheo 5:1-2...............................................................................66
1 Timotheo 5:3-16..............................................................................67
1 Timotheo 5:17-25.............................................................................68
1 Timotheo 6:1-2a..............................................................................68
1 Timotheo 6:2b-19.............................................................................69
1 Timotheo 6:20-21.............................................................................71

BIBLIOGRAFIA.......................................................................................71

MWANDISHI..........................................................................................73

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

# 1 TIMOTHEO: DONDOO / MWONGOZO MFUPI

## 1 Tim 1:1-2:15—Mafundisho ya Uongo Kinyume na Uaminifu wa Injili

**I. Utangulizi wa Nyaraka (1:1-2)**

**A. Kutoka kwa Paulo—**Mtume wa Kristo Yesu
**B. Kwa Timotheo**—Mtoto halisi wa Paulo Katika imani
**C. Salam**—"Neema, rehema, na amani"

**II. Utangulizi wa Ujumbe Mkuu: Mafundisho Potofu kinyume cha ya Ukweli (1:3-11)**

**A. Mafundisho ya uongo kanisani (1:3-4)**
1. Usiwaruhusu watu kufundisha elimu nyingine
2. Wala usiwaache watu wasikilize mafundisho potofu
   a. Hadithi
   b. Nasaba zisizo na ukomo.
3. Madhara ya mafundisho potofu katika Kanisa:
   a. Huleta maswali (mashindano; utata)
   b. Huleta maswali katika madaraka ya Mungu (yaliyo katika imani)

**B. Kusudi la mafundisho ya kweli ni upendo (1:5)**
1. Utokao katika moyo safi
2. Utokao katika dhamiri njema
3. Utokao katika imani isiyo na unafiki

**C. Wengine wakiyakosa hayo wamegeukia maneno ya sheria (1:6-7)**
1. Wamegeukia maneno "yasiyo na chochote"
2. Wanakosa ufahamu.

**D. Sheria yenyewe ni njema, kama ikitumiwa kwa njia iliyo halali (1:8-11)**
1. Sheria HAIKUANDALIWA kwa ajili ya: mtu wa haki **(1:9a)**
2. Sheria NI kwa ajili ya: waasi, na wasio wataratibu, na makafiri, na wenye dhambi na wasiomcha Mungu **(1:9b)**
3. Mfano wa wale waliowekewa sheria ni: Wazinifu na wafiraji; na waibao watu; na waongo; na waapao kwa uongo; na neno lolote lingine lisilopatana na mafundisho yenye uzima **(1:9c-10)**
4. Kiwango cha kipimo cha mafundisho ya uzima: Injili **(1:11)**
   a. Ni ya ki-utukufu
   b. Ni ya Mungu
   c. Iliwekewa amana kwa Paulo

**III. Paulo na Injili (1:12-17)**

**A. Mfano binafsi wa Paulo (1:12-16)**
1. Kristo alimbariki Paulo **(1:12)**:
   a. Alimtia nguvu
   b. Alimwona kuwa mwaminifu
   c. Alimuweka katika huduma
2. Paulo hakustahili baraka hizo **(1:13)**:
   a. Mtukanaji
   b. Mtesaji
   c. Mtu mkatili
3. Msingi wa kibali cha Kristo kwa Paulo **(1:14)**:
   a. Rehema (Paulo alikuwa anafanya hivyo kwa ujinga katika kutoamini)
   b. Neema (Iliyozidi)
   c. Imani na upendo wa Yesu Kristo
4. Kristo anaokoa wenye dhambi (ambao wa kwanza wao ni Paulo) **(1:15)**
5. Kristo kumwokoa Paulo ni kielelezo cha uvumilivu wake kwa wale wamwaminio **(1:16)**

**B. Wimbo wa kusifu (1:17)**

**IV. Agizo Kudumu katika Uaminifu (1:18-2:15)**

**A. Uvipige vile vita vizuri vya imani (1:18-19)**

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

1. Agizo la Paulo kwa Timotheo
2. Kulingana na unabii uliotangulia juu yake
3. Uaminifu na dhamiri njema huenda pamoja.

**B. Kukana Uaminifu na dhamiri njema huiharibu imani (1:19-20)**

1. Himenayo na Aleksanda wameikana imani
2. Watu kama hao "wamekabidhiwa kwa Shetani"
3. "Kuwakabidhi kwa Shetani" kutawawezessha kufundishwa wasimtukane Mungu

**C. Uaminifu utokane na maombi ya maisha yenye utakatifu (2:1-15)**

1. Maombi yafanyike kwa ajili ya watu wote (**2:1**)
   a. Aina zote za maombi
   b. Kwa ajili ya watu wote
2. Maombi hasa yafanyike kwa ajili ya wenye mamlaka (**2:2**)
   a. Maombi kwa ajili ya wote walio kwenye mamlaka
   b. Lengo hasa ili tuishi maisha yenye utulivu na amani katika utauwa wote na ustahilivu
3. Maombi na uchaji wa Mungu husaidia kueneza Injili (**2:3-7**)
   a. Mungu hutaka watu wote waokolewe **(2:4)**
   b. Kristo ndiye pekee mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu **(2:5)**
   c. Kristo alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajil ya wote **(2:6)**
   d. Paulo aliteuliwa kama mhubiri, mtume na mwalimu wa injili kwa Mataifa **(2:7)**
4. Wajibu wa mwanaume (**2:8**):
   a. Wasalishe kila mahali
   b. "Wainue mikono iliyotakasika"
   c. Bila hasira wala majadiliano
5. Wajibu wa mwanamke (**2:9-15**):
   a. Wajipambe mavazi ya kujistiri **(2:9-10)**
   b. Kazi njema
   c. Kujifunza katika utulivu **(2:11)**
   d. "Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanaume" (**2:12**):
      (1) Adamu aliumbwa kwanza, na Eva baadaye **(2:13)**
      (2) Eva alidanganywa, sio Adamu **(2:14)**
      (3) "Lakini Walakini ataokolewa kwa uzazi wake, kama wakidumu katika imani na upendo, na utakaso, pamoja na moyo wa kiasi" **(2:15)**

**<u>1 Tim 3:1-13—Sifa za kuwa Kiongozi wa Kanisa</u>**

**I. <u>Mwangalizi (wazee; maaskofu; wachungaji) (3:1-7)</u>**

**A. Yeyote apendaye kazi ya uaskofu atamani kazi njema (3:1)**

**B. Ili kuwa askofu, mtu anapsaswa kuwa (3:2-7):**

1. Asiyelaumika
2. "Mume wa mke mmoja"
3. Mwenye kiasi
4. Utaratibu
5. Busara
6. Mkaribishaji
7. Ajuaye kufundisha
8. Asiye mtu wa kuzoelea ulevi
9. Si mpiga watu
10. Awe mpole
11. Si mtu wa kujadiliana
12. Asiwe mtu wa kupenda fedha
13. Anawezaye kusimamia nyumba yake mwenyewe
14. Asiwe mtu aliyeongoka karibuni
15. Awe ni mtu mwenye kushuhudiwa mema na watu wa nje ya kanisa

**II. <u>Mashemasi (3:8-13)</u>**

**A. Vivyo hivyo mashemansi lazima wawe (3:8-10, 12):**

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

1. Wastahivu
2. Si wenye kauli mbili
3. Si watu wa kutumia mvinyo
4. Si watu wanaotamani fedha ya aibu
5. Wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi
6. Wajaribiwe kwanza
7. Wasiolaumika
8. "Wawe na mke mmoja"
9. Wakisimamia watoto wao vizuri

**B. Viongozi wanawake (3:11)**

Vivyo hivyo wanawake wawe:

1. Wastahilivu
2. Si wasingiziaji
3. Watu wa kiasi
4. Waaminifu katika mambo yote.

**C. Wale watendao vema kazi ya shemasi hujipatia (3:13):**

1. Daraja zuri; na
2. Ujasiri mwingi katika imani

**<u>1 Tim 3:14-4:16—Utauwa wa kweli Kinyume na Utauwa Batili</u>**

**I. <u>Utauwa wa Kweli (3:14-16)</u>**

**A. Kusudi la kuandika:** Namna unavyopaswa kuwa katika kanisa **(3:14-15)**

**B. Sura na maelezo kuhusu kanisa (3:15)**

1. Nyumba ya Mungu
2. Kanisa la Mungu Aliye Hai
3. Nguzo na Egemeo la Kweli

**C. Ukiri kuhusu utauwa wa kweli (3:16)**

1. Kristo alidhihirishwa katika mwili
2. Kristo akajulikana kuwa na haki katika roho
3. Kristo alionekana na malaika
4. Kristo akahubiriwa katika mataifa
5. Kristo akaaminiwa katika ulimwengu
6. Kristo akachukuliwa juu katika utukufu

**II. <u>Waasi na Utauwa wa Uongo (4:1-7a)</u>**

**A. Utangulizi:** Roho anena waziwazi ujumbe huu **(4:1a)**

**B. *Wakati* uasi utakapoanza:** "nyakati za mwisho" **(4:1a)**

**C. *Nani* watajitenga:** Wale wanaosikiliza roho zidanganyazo **(4:1b)**

**D. *Asili* ya uasi ni:** roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani **(4:1b)**

**E. *Njia* itumikayo kuleta uasi:** unafiki na uongo **(4:2a)**

**F. *Madhara* kwa wale wanaosikiliza mafundisho ya uongo:** kuchomwa dhamiri zao wenyewe **(4:2b)**

**G. *Mfano* wa mafundisho ya uongo (4:3a)**

1. Kuzuia watu wasioane
2. Kuwazuia wajiepushe na vyakula

**H. *Ufumbuzi* kwa uasi na utauwa wa uongo**

1. <u>Kujua Neno la Mungu:</u> Pima mafundisho kwa Neno **(4:3b-5)**
2. <u>Fundisha Neno la Mungu:</u> Fichua utauwa batili kwa neno la Mungu **(4:6)**

**I. Ufupisho:** Kataa kabisa utauwa wa uongo **(4:7a)**

**III. <u>Nidhamu ya Kuishi Maisha ya Utauwa wa Kweli (4:7b-16)</u>**

**A. Jizoeze kupata utauwa (4:7b-10)**

1. Mazoezi ya kimwili yafaa kidogo **(4:8a)**
2. Nidhamu ya kiroho ni ya muhimu zaidi kuliko mazoezi ya kiwili **(4:7b-8b)**
    a. Nidhamu ya kiroho ina ahadi kwa uzima wa sasa
    b. Nidhamu ya kiroho ina ahadi ya uzima ujao.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

c. Uzima ujao ni wa umuhimu wa kipekee. **(4:9-10)**
(1) Kwa kuwa twafanya juhudi na kujitahidi kwa kusudi hili
(2) Kwa sababu tumeweka mtumaini kwa Mungu aliye hai
(3) Ni Mwokozi anayetupa uzima wa milele

**B. Maelezo ya nidhamu ya kiroho:** Mambo kumi ya muhimu sana **(4:11-16)**
1. Agiza (amuru) mambo haya **(4:11)**
2. Fundisha mambo haya **(4:11)**
3. Mtu awaye yeyote asiudharau ujana wako **(4:12a)**
4. Uwe kielelezo kwao waminio katika:
   a. Usemi
   b. Mwenendo
   c. Upendo
   d. Imani
   e. Usafi **(4:12b)**
5. Ufanye juhudi katika kusoma na kuonya na kufundisha maandiko pamoja na:
   a. Kuonya
   b. Kufundisha **(4:13)**
6. Usiache kutumia karama ile iliyoko ndani yako **(4:14)**
7. Uyatafakari hayo **(4:15a)**
8. Ukae katika hayo **(4:15b)**
9. Jitunze nafsi yako na mafundisho yako **(4:16a)**
10. Dumu katika mambo hayo, maana kwa kufanya hivyo utajiokoa:
   a. Nafsi yako
   b. Wale wakusikiao **(4:16b)**

## 1 Tim 5:1-6:21—Matatizo ya Kitendaji na Mambo Yawakabiliyo Viongozi wa Kanisa

### I. Kukemea/Kushauri Watu (5:1-2)

**A. Usikemee kwa maneno makali**

**B. Wahudumie watu kama jamii ya familia yako**
1. Mzee kama baba
2. Vijana kama ndugu
3. Wanawake wazee kama mama
4. Wanawake vijana kama ndugu wa kike

**C. Wahudumie wanawake "katika usafi wote"**

### II. Kuhudumia Mahitaji Wajane Wanaostahili (5:3-16)

**A. Wajane ambao wanapaswa kusaidiwa na kanisa (5:3, 5-7, 16)**
1. Wasio na msaada mwingine wowote
2. Waliomwekea Mungu tumaini lao
3. Wanaojizuia nafsi zao.

**B. Wajane ambao wanapaswa "kuorodheshwa" (5:9-10)**
1. Umri angalau wa miaka sitini
2. Ushuhuda wa matendo mema
3. Mkaribishaji wageni
4. Aliyewatumikia wengine.

**C. Wajane walio vijana wnapaswa kuolewa tena na wasisaidiwe na kanisa (5:11-15)**
1. Kanisa lisiwahudumie wajane vijana kwasababu:
   a. Wanayo tamaa ya kimwili nao wataka kuolewa **(5:11)**
   b. Wanaweza kuacha kiapo chao cha imani **(5:12)**
   c. Wanaweza kuwa wavivu na kuwa wadhambi, kama wengine tayari walivyofanya. **(5:13, 15)**
2. Kuolewa tena na kuzaa watoto kutawafanya waishi maisha ambayo si ya kulalamika **(5:14)**

**D. Wanafamilia wanapaswa kuwahudumia wajane (5:4, 8, 16)**
1. Watoto wana wajibu kuwatunza na kuwasaidia wazazi na wazee wao wasiojiweza **(5:4)**
2. Kushindwa kuwahudumia wazazi tegemezi na wazee:

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

a. Ni sawa na aliyeikana imani **(5:8)**
b. Ni mzigo kwa kanisa **(5:16)**

**III. <u>Kuwahudumia Wazee wa Kanisa (5:17-25)</u>**

**A. Wazee wanaohubiri na kufundisha wanapaswa kulipwa na kanisa (5:17-18)**

**B. Mashitaka juu ya mwenendo wa wazee (5:19-20)**

1. Mashitaka yanapaswa kuthibitishwa (mashahidi "2 au 3")
2. Wazee wadumuo kutenda dhambi uwakemee mbele ya wote

**C. Mambo yote ya wazee yashughulikiwe bila upendeleo au lawama (5:21)**

**D. Kuwekea mikono wazee (5:22, 24-25)**

1. Usimweke wakfu ("kuwekea mikono") mtu haraka-haraka **(5:22a)**
2. Kwa kumuwekea mikono mtu, unashiriki dhambi yake—hivyo jilinde nafsi yakoi **(5:22b, c)**
    a. Dhambi za mtu zitadhihirika **(5:24)**
    b. Vivyo hivyo matendo mema ya mtu yatadhihirika. **(5:25)**

**(E. Rasmi kwaTimotheo:** Tumia mvinyo kidogo, kwa ajili ya dawa ya tumbo lako **[5:23])**

**IV. <u>Mwenendo wa Watumwa katika Kazi Zao (6:1-2a)</u>**

**A. Watumwa wanapaswa kuwaheshimu bwana zao:** Ili Jina la Mungu na Injili visitukanwe.

**B. Na wale walio na bwana waaminio wasiwadharau bali wawatumikie:**

1. Wawatumikie vyema *kwa sababu* ni waaumini
2. Wawatumikie vyema katika upendo

**V. <u>Injili na Mali (6:2b-19)</u>**

**A. Fundisha na kuhubiri kanuni hizi (6:2b)**

**B. Walimu wa uongo (6:3-5b)**

1. Mafundisho yao **(6:3)**
    a. Yasiyo sahihi
    b. Hayakubaliani na mafundisho ya Kristo
    c. Hayaendani na utauwa.
2. Tabia yao **(6:4a, 5b)**
    a. Wanajivuna
    b. Hawafahamu neno lolote
    c. Wana wazimu
    d. Wameikosa kweli
3. Lengo lao **(6:4b)**
    a. Maswali ya udadisi
    b. Mashindano ya maneno.
4. Matokeo yake **(6:4c-5a)**
    a. Husuda
    b. Ugomvi
    c. Matukano
    d. Shauku mbaya
    e. Kuharibika akili zao
5. Motisha yao **(6:5c):** utauwa ni njia ya "kujitajirisha" (m.y., utauwa ni njia ya kupatia utajiri)

**C. Uhusiano wa kweli kati ya utauwa na mali za kidunia (6:6-10)**

1. Uchaji wa Mungu ni "faida kubwa" (m.y., utauwa ni kupata uzima wa milele) **(6:6a)**
2. Ile "faida kubwa" ya utauwa hupaswa kutokana na kuridhika na kile alicho nacho mtu **(6:6b-8)**
    a. Hatukuja na kitu duniani **(6:7)**
    b. Hatuwezi kutoka na kitu duniani **(6:7)**
    c. Kwa hiyo, tukiwa na chakula na nguo twaridhika **(6:8)**

**D. Hatari ya kutamani kuwa na mali (6:9-10)**

1. Kutamani mali ni kitanzi **(6:9)**
    a. Kutamani mali hutupelekea katika upotefu na tamaa mbaya
    b. Upotofu na tamaa mbaya huwapelekea watu katika uharibifu
2. Kupenda fedha ni shina la mabaya yote **(6:10)**

a. Kutamani fedha huwafanya watu wafarakane na imani
b. Kutamani fedha husababisha kujichoma kwa maumivu mengi

**E. Mwitikio mzuri kuhusu mali na kutamani fedha (6:11-14)**

1. Uyakimbie mambo hayo **(6:11a)**
2. Ufuate haki, utauwa, imani, upendo, saburi, na upole **(6:11b)**
3. Udumu katika imani (m.y., "uvipige vita vizuri vya imani") **(6:12)**
   a. Uaminifu huandamia uzima wa milele
   b. Ndio ulioitiwa
   c. Ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi
4. Uaminifu unahusisha mambo yafuatayo **(6:13-14):**
   a. Kuilinda maagizo ya Kristo
   b. Bila kuwa na mawaa wala lawama ya dhambi
   c. Kuvumilia hadi kuja kwake Kristo

(5. Wimbo wa kusifu **[6:15-16]**)

**F. Utumiaji mzuri wa utajiri (6:17-19)**

1. Mtazamo mzuri wa wale walio na mali **(6:17a)**
   a. Wasijivune
   b. Wala wasitumainie utajiri usio yakini
   c. Waweke tumaini lao kwa Mungu
2. Chanzo cha vitu vyote: Mungu **(6:17b)**
3. Kusudi la Mungu kuwapatia watu utajiri **(6:17c-18)**
   a. Furaha
   b. Kwa kutenda wema
   c. Kuwa matajiri kwa mambo mema
   d. Kuwa wakarimu
   e. Kushirikiana na wengine
4. Matokeo ya kuutumia utajiri kwa wema **(6:19)**
   a. Watoaji wenyewe wanajiwekea msingi wa hazina nzuri kwa wakati ujao
   b. Wanapata uzima wa kweli (wa milele)

**VI. Hitimisho (6:20-21)**

**A. Ilinde hiyo amana (6:20a)**

1. Jiepushe na maneno yasiyo ya dini na mashindano ya maneno. **(6:20b)**
2. Kusimamia elimu "ya uongo" kumewafanya wengine waikose imani **(6:21a)**

**B. "Neema na iwe pamoja nanyi" (6:21b)**

## 1 TIMOTHEO: UCHAMBUZI

### 1 Tim 1:1-2:15—Mafundisho ya Uongo Kinyume na Uaminifu wa Injili

**1:1-2:** ***[1]Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa amri ya Mungu Mwokozi wetu na Kristo Yesu, taraja letu; [2]kwa Timotheo, mwanangu hasa katika imani. Neema na iwe kwako, na rehema, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Kristo Yesu Bwana wetu.***

***Paulo, mtume wa Kristo Yesu:*** 1. "Mtume"huzungumzia mtu aliyeteuliwa na kutumwa akiwa na mamlaka ya kutenda kusudio fulani. Ni jina linalotokana na neno la Kiyunani *apostello* ("kutuma"). Maana muhimu ya "mtume" hupatikana katika maneno kama vile "balozi,"mwakilishi "," au "mjumbe."

2. Yesu, kwa kule kujenga kanisa kwa msingi wa wanafunzi 12/ mitume 12 ni ishara kwamba alikuwa anajenga Israeli mpya, ya kiroho. Uchaguzi wa Yesu wa wanafunzi 12/ mitume 12 (**Mat 10:1-2; Mk 3:13-19; Lk 6:12-26**) ni ishara ya makabila 12 ya Israeli. Kusema ukweli kwenye milango kumi na miwili ya Yerusalemu Mpya kumeandikwa "*majina kumi na mbili ya kabila za Israeli"* (**Ufu 21:12**), na kwenye mawe kumi na mbili ya msingi ya Yerusalemu Mpya kumeandikwa "*majina kumi na mbili yamitume wa Mwana Kondoo"* (**Ufu 21:14**). Mitume wenyewe walitambua umuhimu wa hiyo "12." Katika **Mdo 1: 12-26** waliamua kwamba ni lazima kuziba nafasi ya Yuda Iskarioti kama mtume. Ingawaje Paulo alikuwa mtume (**Rum 1:1; 1 Kor 1:1; 9:1**), Agano Jipya (na Paulo mwenyewe) hutambua utofauti kati ya utume wa Paulo na "wale Kumi na Wawili" (ona **Mdo 6:2; 1 Kor 15:5, 8).** Hili laweza kutokana na ukweli kuwa huduma ya Paulo kimsingi

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

ilikuwa kwa Mataifa (**Mdo 9:15; 13:8; Rum 11:13; Gal 1:16; 2:7**), ambapo Petro, kiongozi wao dhahiri na mnenaji wa wale Kumi na Wawili, kimsingi alikuwa mtume kwa Wayahudi (ona Wagal 2:7-8).

3. Agano Jipya linatambua aina mbili za msingi za mitume: (A) Mitume *wa msingi*; na (B) Mitume *watumwao na kanisa.* Mitume *wa msingi*; walikuwa ni wale waliokuwa pamoja na Yesu, walioshuhudia ufufuo, na waliitwa rasmi wawe mashahidi na Yesu mwenyewe (ona **Mat 10:1-5; Mk 6:7, 30; Lk 6:13; Yoh 15:27; Mdo 1:21-22**). Waliweza kuthibitisha nafasi yao hiyo maalum kwa kutenda miujiza (ona **Mt 10:1-8; Mk 6:7; Mdo 2:43; 2 Kor 12:12**). Mitume wa msingi walikuwa viongozi wa kanisa la mwanzo na "msingi" wa kanisa lenyewe (**Efe 2:19-20).** Kwa hiyo, wale wenye mamlaka ya mitume wa msingi hawajatokea tena baada ya wale wenyewe kufa (msingi moja tu waweza kuwekwa kwa ajili ya jengo. "Mitume watumwao" na kanisa ni watu waume na wanawake ambao wametumwa na kanisa kwenda kuhubiri Injili, kupanda makanisa, na kulijenga kanisa (ona **Mdo 13:1-3; 14:14; Rum 16:7; 1 Kor 9:5-6; 12:28; 1 Thes 1:1; 2:6**). Aina zote mbili za mitume wameunganishwa katika mtu kama Paulo (ona **Mdo 9:1-16; 13:1-3; 1 Kor 9:1; 15:6-10; Gal 1:11-17; 1 Tim 2:7**). Mitume waliotumwa na Kanisa wanaweza wasiwe na mamlaka zaidi kuliko kutumwa na kanisa. Kanisa ni mwili wa Kristo duniani (**1 Kor 12:27; Efe 1:22-23; 4:15-16; Kol 1:18**). Kanisa ni hekalu la Roho Mtakatifu (**1 Kor 3:16-17**). Kristo ameliweka wakfu kanisa na akalipa mamlaka Yake. (**Mat 16:18-19**). Hivyo basi, Kristo anaweza kutarajiwa kutenda kazi kupitia kanisa Lake, na wala si kwa utengano mbali nalo. Kwa kuwapa mitume mamlaka, kanisa pia linawapa kuwaamini, na wajibu wenye heshima kwa kanisa lenyewe na hata machoni pa ulimwengu pia.

4. Kanisa linahitaji kuwapima watu wajiitao wenyewe mitume ili kujua kama ni mitume wa kweli au ni wa uongo (**1 Yn 4:1-6;** pia ona **2 Kor 11:3-4, 13; Ufu 3:2**). Watu wengi siku hizi hupenda kujiweka wenyewe kuwa 'mitume." Hilo ni kinyume na mkondo wa Agano Jipya (Mitume wa Agano Jipya hawakujichagua wenyewe). Wengi wa hawa "mitume" waliojiinua wenyewe hudai kutenda miujiza. Hata hivyo, kule kutenda miujiza *siyo* lazima kuwe ndiyo ishara kwamba mtu huyo ameitwa na Mungu (**Mat 7:15-23; 2 Tim 3:1-9** [ona **Kut 7:10-12, 20-22; 8:6-7, 16-19**]). Katika Afrika, "kuibuka kwa manabii na mitume wa Ki-Afrika kulileta mtazamo kwamba watu weusi na weupe wanalingana kiimani na kihuduma (Gal 3:28; Kol 3:11). Pia kulisababisha kanuni inayotofautisha imani ya Ki-Kristo na utendaji wa viungo vyote vya siasa za kikoloni." (Quedraogo 2006: 1434). Bahati mbaya, hata hivyo, "manabii na mitume wengi wa Ki-Afrika hawaichukulii Biblia kuwa ndio msingi wa imani na mwenendo wao.... Huchukulia [kile wanachodai kuwa ni mafunuo ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu] kama nyongeza ya Biblia. Hata hivyo, Biblia inaonya kuhusu kuongeza hata kidogo tu kwenye Neno (Ufu 22:18-19). Manabii na mitume wengi wa Ki-Afrika pia hujihusisha na imani danganyifu za binafsi . . . wengine hata hujiita kuwa wamechukua nafasi ya Kristo au ndio Kristo mwingine. Madai kama hayo yanawafanya wao kuwa vyombo vya kuabudiwa. Kwa masikitiko makubwa, wengi wao hukamata kabisafahamu za wafuasi wao. Agano Jipya linatuonya kuhusu watu kama hao (Math 24:11; Yuda 4- 16)." (Ibid.) "Mitume" wa siku za leo wanapaswa kutambuliwa kwa mafundisho yao (ona **Mdo 17:11; 1 Tim 6:3-5**) na jinsi wanavyoishi (ona **Mat 20:25-28; Mk 10:42-45; Lk 22:24-27; Yoh 13:12-17; Mdo 18:3; 1 Kor 9:11-18; 2 Kor 11:7; 12:13**).

5. Paulo anaandika katika nafasi yake, na katika mamlaka yote, ya mtume wa Kristo Yesu. Ingawaje Timotheo alimjua Paulo kama mtume, Paulo anamtajia ukweli wa hoja hiyo ili kukazia nafasi ambayo yeye anamwandikia kwayo, na kusisitiza mamlaka anayoinenea. Hilo linafanya maneno na mafundisho yake yalingane na na mafundisho ya Yesu Kristo mwenyewe (ona **1 Tim 6:3**). Tangu ujumbe huu uliposomwa kanisani, (na bado unasomwa hata leo), tunahitaji kukumbuka kwamba Paulo bado ananena kama mtume wa Kristo.

***Kristo Yesu, aliye tumaini letu:*** Paulo alisema katika **1 Kor 15:19**, *"Kama katika maisha haya tu tumemtumaini Kristo, sisi tu masikini kuliko watu wote."* Hata hivyo, Paulo alitambua kwamba dunia hii na maisha haya siyo kila kitu kilichopo. Badala yake, kuna umilele: Kutakuwa na dunia mpya, na uzima wa milele, (unaoanzia sasa), kwa watu waliompokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wao. Ufufuo wa Yesu ni "matokeo ya kwanza" na uhakika kwamba wale walio katika Kristo watafufuliwa na kukutana na uzima wa milele katika dunia mpya. (**1 Kor 15:29-23).**

***Timotheo, mwanangu hasa wa imani:*** 1. Paulo alimwona kwa mara ya kwanza Timotheo katika mji wa Listra, mwanzoni mwa safari yake ya ki-utume (**Mdo 16:1-2**). Hilo lilitokea muda mfupi baada ya kikao cha baraza muhimu cha Yerusalemu. Baraza hilo lilikaa karibu kwenye mwaka 50 BK. 1 Timotheo iliandikwa huenda kwenye mwaka 62-63 BK.

2. Timotheo tayari alikuwa mwamini wakati anakutana na Paulo (**Mdo 16:1-2; 2 Tim 1:1-5; 3:14-15**). Paulo almchukua Timotheo kwenda naye. Baada ya hapo, Timotheo alisafiri na kufanya kazi kwa ukaribu sana

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

na Paulo Uyunani yote, na Jimbo la Ki-Rumi kule Asia (ambayo ni Uturuki kwa sasa), na Rumi yenyewe (ona **Mdo 16:3-12; 17:10-15; 19:21-22; 20:4; Flp 1:1; 2:19; Kol 1:1; Flm 1:1; 1 Thes 3:1-2; 2 Tim 4:13**).Timotheo anaonyesha kuwa mwenzi wa karibu zaidi kwa Paulo kuliko wengine. Alimtumikia Paulo hadi wakati wa kifo chake paulo kunako 66 BK (ona **2 Tim 4:13**). Timotheo ametajwa mara nyingi zaidi kuliko yeyote mwingine kti ya waliolelewa na Paulo.

***Neema, rehema na amani kutoka kwa Mungu aliye Baba, na Kristo Yesu Bwana wetu:*** 1. Paulo kikawaida huanza nyaraka zake kwa salamu "neema na amani." Ni katika 1 Timotheo na 2 Timotheo anaongezea maneno "rehema" kwenye salamu zake. "Neema" kimsingi humaanisha "kibali ambacho hukustahili" (m.y., kupewa zawadi nzuri ambayo hukuifanyia kazi wala hustahili kabisa). "Rehema" mara zote huonyesha wazo kumtakia huruma na fadhili mtu aliye na uhitaji. Mnenaji moja alitofautisha mawazo kuhusu "rehema" na "neema" kwa njia hii: "[Rehema] siku zote hushughulikia kile tukionacho kama cha kuumiza, mkasa, au huzuni, matokeo haya ya dhambi; na [neema] siku zote hushughulikia dhambi na kosa lenyewe. Moja huleta faraja, jingine msamaha; moja huponya, hutibu, husaidia; wakati jingine husafisha na kurejeza upya." (Knight 1992: 66) Kwa vile katika dhana hii rehema hutumika pamoja na neema, waweza kuitazama rehema kama kutopokea matokeo mabaya (m.y., ghadhabu ya Mungu, mauti ya milele, na moto wa milele ambayo ndio ujira wako na umestahili. "Amani" ndiyo: hitaji kuu zaidi ya mengine yote tuliyonayo wanadam: ndani ya nafsi zetu; miongoni mwetu; na kati yetu na Mungu. Yesu pekee ndiye atupaye hiyo amani. Amani Atupayo *"ipitayo akili zote"* (**Flp 4:6-7**) kwa kuwa amani itokanayo na Yesu *"sivyo kama ulimwengu utupavyo"* (**Yoh 14:27**). Sababu ni kuwa anatuunganisha kwake, hutubadilisha toka ndani, na kutupatia Roho Mtakatifu (**Yoh 14:16-17, 26**), ili kwamba tuwe kama alivyo (**Rum 8:29**). Hivyo basi hutupatia uwezo wa kukumbana na ugumu wowote kwa amani, ama uwe wa ndani au nje, tukijua ya kwamba tumethibitishwa na Baba, ndani ya Kristo, na kuwa tusalama mikononi mwake. (**Rum 8:28-39**).

2. Kutumika kwa "neema, rehema, na amani" pamoja kunahitimisha mkasa wa hali ya mwanadamu na ufumbuzi wa Mungu kwa hali yetu hiyo. Biblia huwaona watu wote kuwa mamoja na Adamu (katika "Adamu"), na Adamu akitenda kama kichwa chetu au kama mwakilishi wetu (ona **Rum 5:12-19; 1 Kor 15:21- 22;** cf.. **Ebr 7:9-10).** Tatizo la mwanadamu ni kwamba, kama matokeo ya dhambi ya Adamu, kizazi cha wanadamu wote hupata kuhesabiwa "hatia" na uharibifu (**Zab 51:5; Yer 17:9; Rum 3:9; 7:14-25**), ambayo huwapeleka kwenye dhambi ya pamoja kwa kila mtu (**Rum 3:10-18,23**), na hatimaye kwa kukosa kwa kila mtu binafsi.. Jinsi ilivyotokea haswa na kwa nini vizazi vilivyofuata baada yake vimetiwa hatiani na kuonekana vina uharibifu kutokana na dhambi ya Adamu, ni swala la kujadiliwa. Lakini matokeo kwa watu wote ni kuwa kwa juhudi zetu binafsi, pasipo Kristo, "*tumekufa katika makosa yetu na dhambi zetu* (**Efe 2:1).** Hii inamaanisha kwamba kuna upungufu mkubwa au uharibifu mkubwa kumhusu kila mwanadamu (uitwao pia nguvu ya dhambi ikaayo ndani [ona **Rum 7:14-23**]) ambayo inaathiri kila kitu kituhusucho, vikiwamo jinsi tunavyofikiri, mawazo, uongeaji, matendo, kujisikia, na uhusiano wetu na watu na Mungu. Matokeo ya uharibifu huu ni kuwa, pasipo kuingilia Kristo, watu wote: hawako tayari wala hawana uwezo wa kuja kwa Kristo na kumwamini yeye (**Yoh 6:44, 65; Efe 2:8-9**); hawako tayari na hata hawana uwezo wa kuuona ufalme wa Mungu (**Yoh 3:3, 5**); hawako tayari na hawana uwezo wa kujitoa kwa sheria ya Mungu na kumtii (**Rum 8:6-8**); hawako tayari wala hawana uwezo wa kuelewa ukweli wa kiroho kumhusu Mungu (**Efe 2:1; Kol 2:13**); hawako tayari na hawana uwezo wa kumpendeza Mungu (**Ebr 11:6**); ni watumwa wa dhambi, dunia, mwili, na ibilisi (**Rum 6:17; Efe 2:1-3**); wamepungukiwa uzima wa milele (**Efe 2:1; Kol 2:13**); nao wanakabiliwa na ghadhabu ya Mungu na hukumu yake (**Rum 6:16-17; Efe 2:1-3**). Kwa hiyo wanadamu hawana amani ndani yao (wanajua wanatakiwa wafanye nini lakini, kwa sababu ya nguvu ya dhambi ikaayo ndani yao, hawatendi hayo). Matokeo ni kuwa hakuna amani kati ya watu mbali-mbali (familia, ukoo, makabila, na mataifa), na hakuna amani kati ya watu na Mungu.

3. Juhudi za mwanadamu kutatua tatizo hili ni kupitia dini zenye misingi ya ki-matendo. Ingawaje kuna dini nyingi sana duniani (Uislamu, Wahindu, Ubudha, Dini za mila za Ki-Afrika, nk) kwenye kiini kabisa cha kila dini kunamsingi unaofanana: mtu lazima afanye "matendo" fulani (k.m; atende matendo mema ya kutosha, atoe dhabihu, ajikane mwenyewe vitu fulani, afanye sala mara tano kwa siku) ili kujaribu "kuziba lile pengo" kati ya Mungu Mtakatifu na mwanadamu mdhambi na hivyo kukubaliwa na Mungu na kupata uzima, mbingu, au kiyama ya raha tele. Dini zote hizo uelekeo wake ni kushindwa, kwa sababu hazina uelewa wa kutosha wa hali kamili ya mwanadamu. Tatizo la mwanadamu ni *ndani yetu -kuna kitu kilichoharibika mno kuhusiana na "moyo" wetu - na hatuwezi kubadili moyo wetu sisi wenyewe.* Hakuna kiasi cha "matendo" ya nje (k.m matendo mema, dhabihu, kujikana mambo, kusali au maombi) yanayoweza kubadili asili yetu ya dhambi ya ndani (ona **Kol 2:20-23**). Ni Biblia peke yake inalielewa hilo kiusahihi kabisa, kwamba kwa jinsi yetu wenyewe "*hatuna tumaini na [hatuna] mungu duniani"* (**Efe 2:12**).

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

4. <u>Ukristo haufanani na dini yoyote duniani.</u> Ukristo pekee hutambua kwamba uanadamu peke yake hauwezi kuziba pengo kati yake na Mungu. Ni Mungu peke yake anaweza kufanya lile ambalo mwanadamu hawezi kufanya – *kutupatia moyo mpya*. Alilifanya hili kwa kupitia mtu na kazi ya Yesu Kristo. Kristo alikuwa tofauti katika historia yote: Mungu alifanyika mtu ndani ya mwanadamu Yesu Kristo; Kristo alikuwa yote mawili Mungu kamili na mwanadamu kamili wakati huo-huo. Yeye peke yake alikuwa hana dhambi. Kwa hiyo, ni yeye peke yake alikuwa na uwezo wa kuwa dhabihu kamili kwa dhambi zetu. Kristo alijitoa mwenyewe kwa ajili yetu wakati tukiwa *adui* wake (**Rum 5:8-10**). Pale msalabani alizichukua dhambi zetu, hatia, na adhabu yetu tuliyoistahili ikawa juu yake mwenyewe. Kwa upande mwingine, utii wake na haki yake inawekwa kwetu kwa imani yetu kwake. Kwa maneno mengine, anayatwaa yote yaliyo mabaya kutoka kwetu, na kutupatia ile hali ya ubora ulioko ndani yake. Yesu alikuwa "Adamu wa pili": kama vile yule Adamu wa kwanza alivyoingiza dhambi kwa wanadamu, ndivyo Kristo anaingiza msamaha na uzima kwa wale walio "katika Kristo" (**Rum 3:21-26; 5:6-21; Kol 2:13-14**). Ufufuo wa Kristo unaonyesha kwamba Baba aliikubali dhabihu ya Kristo kwa ajili yetu (**Yoh 1:29, 36; 1 Kor 15:20-23, 42-49, 56-57; Ebr 9:11-10:18; Ufu 5:6-8**). Kwa hiyo, Ukristo, tofauti na dini nyingine zote duniani, haihusu nini tunakifanya kuhusu Mungu, au cha kufanya ili kujaribu kumfikia Mungu, bali inahusu nini Mungu katufanyia sisi katika Kristo. Twaweza tu kuokolewa kwa kipawa cha bure cha neema ya Mungu kwa imani katika Kristo (**Efe 1:3-14; 2:8-9**). Ndipo mungu huondoa "mioyo yetu ya jiwe" na kutupatia "Mioyo mipya ya nyama" (**Eze 36:26; 2 Kor 3:2-3; 5:17**). Hutupatia Roho Mtakatifu anayekuja kuishi ndani yetu (**Yoh 14:16-17; Rum 8:14-15; 1 Kor 3:16; 6:19; 2 Kor 6:16**), na kutuwezesha kuishi maisha yanayoendana na mapenzi yake (**Eze 36:27; Efe 2:10**). Kupitia neema na rehema yake, tuna amani na Mungu, na watu wengine, na tuna amani ndani yetu wenyewe (ona **Yoh 14:26-27; 16:33; Efe 2:14; Flp 4:7; Kol 3:15**).

**<u>1:3-4:</u>** ***[3]Kama vile nilivyokusihi ukae Efeso, nilipokuwa nikisafiri kwenda Makedonia,ili uwakataze wengine wasifundishe elimu nyingine. [4]Wala wasiangalie hadithi na nasaba zisizo na ukomo, ziletazo maswali, wala si madaraka ya Mungu yaliyo katika imani; basi ufanye hivyo.***

***Ukae Efeso:*** Efeso ulikuwa mji mkubwa kuliko yote na wa muhimu kwa himaya ya Kirumi ya Asia. Unakaa pwani ya Magharibi mwa Uturuki ya leo. Ulikuwa makao ya mojawapo ya "Ajabu Saba za dunia ya kale," na hekalu la mungu mke aitwaye Artemis (au "Diana," kama Warumi walivyomwita), na ukumbi wa kuketisha watu 25,000 (ona **Mdo 19:28-29**). Kanisa la Efeso lilikuwa ni kitovu na muhimu katika Asia kwa wakati ule. Paulo alipokwenda Efeso mara ya kwanza, aliwakuta baadhi ya wanafunzi tayari wako kule (**Mdo 19:1-7**). Alikaa pale kwa miaka miwili na kupafanya ngome yake ya kuenezea Injili sehemu yote ya jimbo la Asia (**Mdo 19:8-10**). Pauloaliporudi Efeso na kuondoka kwa mara ya mwisho, aliondoka akilipenda na kulitakia mema kanisa lile (**Mdo 20:16-38**). Paulo aliandika 1 Wakorintho akiwa Efeso (**1 Kor 16:8**). Yohana aliandika maneno ya Yesu kwa kanisa akiwa Efeso katika **Ufu 2:1-7**. Kwa sababu ya umuhimu wake, Paulo alimtaka Timotheo akae pale ili kukabili mafundisho ya upotofu yaliyokuwa yakitokea katika kanisa la Efeso.

***Mafundisho mengine, hadithi, na nasaba:*** 1. <u>Neno lililotafsiriwa kama *"mafundisho mengine"* latumika tena katika **1 Tim 6:3** (ambapo linatafsiriwa kama *"elimu nyingine"*).</u> Kimsingi, linamaanisha "kufundisha mafundisho ambayo ni tofauti na yale ya Injili ya Paulo." Ingawaje mafundisho potofu hayo anayoyazungumzia Paulo hayatajwi kabisa, inaonyesha yanahusiana na: kupenda mambo ya historia na desturi na vizazi. [m.y., mila za watu zilivyotokea] (**1 Tim 1:4, 4:7; 2 Tim 4:4; Tito 1:14, 3:9**); mambo ya sheria za Wayahudi (**1 Tim 1:7; Tito 1:10, 14, 3:9**); kupenda kuchunguza mambo, maswali na mabishano (**1 Tim 1:4, 6; 6:4; 2 Tim 2:14, 16, 23; Tito 1:10; 3:9**); udanganyifu (**1 Tim 4:1-3; 2 Tim 3:6-13; Tito 1:10-13**); kukiuka maadili (**1 Tim 1:19-20; 2 Tim 2:16, 19** na **2 Tim 3; Tito 1:15-16**); kuwakataza watu wasioe au kuolewa, au kula nyama (**1 Tim 4:1-5**); na tamaa ya kujipatia mali kwa njia ya mafundisho yao (**1 Tim 6:5; 2 Tim 3:2, 4; Tito 1:11**). Mafundisho ya uongo pia yaweza kuhusu habari kwamba ufufuo wa wafu umeshatokea (**2 Tim 2:18**). Kama mnenaji moja alivyohitimisha, mafundisho ya uongo "yalichanganya kwa sehemu desturi za Uyahudi, imani za uzushi, na huenda na uchawi" (Mounce, 2000: lxxv).

2. <u>Swala la *"kizazi kisichokoma"* ni muhimu sana.</u> Ni vizuri kujua tunatokea familia gani, ukoo, kabila, rangi ya ngozi, na taifa tutokealo. Sote tunatambulika kwa njia hizo. Hata hivyo, kusimamia kutambulika kwetu kwa njia hizo ni kinyume cha Ukristo, dhambi, na kwaweza kuletesha mgawanyiko wa kutishana uovu (k.m., maangamizi ya Wayahudi katika Vita Kuu ya dunia ya 2, na mauaji ya Rwanda mwaka 1994). Ubaguzi wa rangi, ukabila, au kubaguana kijamii hakukubaliki kwa yeyote anayelichukua Jina la Kristo. Wakristo wa rangi zote na makabila yote lazimawajione wenyewe kama *Wakristo* kwanza, kisha rangi, kabila, taifa, siasa, kiuchumi, au makundi mengine nafasi ya pili. Ni kweli kwamba "damu ni nzito kuliko maji." Lakini, kwa

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

Wakristo, damu ya *Kristo* lazima itazamwe kama ni damu ya pamoja inayotuunganisha pamoja, siyo damu ya familia, kabila, au rangi ya ngozi. Kusema ukweli, hakuna ngozi, kabila, ukoo, au jamii yoyote ile yenye "damu yake yenyewe"—damu ya watu wote ni nyekundu na huingiliana. "Theolojia" yoyote yenye nguzo yake ya kuegemea kwenye kundi lolote la kijamii (kama vile rangi ya ngozi, kabila, jinsia, au daraja fulani) haliwezi kuwa la Ki-Biblia, kwa sababu Injili *ni ya desturi zote* na hupinga ubaguzi wa kijamii (k.m., **Gal 3:28; Efe 2:14-16; Kol 3:11; Ufu 5:9; 7:9**). Sala yamwisho ya Kristo "ya kikuhani" kabla hajasulubiwa ilikuwa, *"ili wote wawe na umoja; kamawewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma"* (**Yoh 17:21**). Kuna mwili moja tu wa Kristo, ingawaje ule mwili moja una viungo vingi vinavyotakiwa kufanya kazi pamoja kwa mshikamano (**1 Kor 12:12- 26**). Theolojia" yoyote yenye nguzo yake ya kuegemea kwenye kundi lolote la kijamii huuparaganyisha mwili wa Kristo kinyume chake wenyewe. Kristo alionya, *"Kila ufalme ukifitinika juu ya nafsi yake, hufanyika ukiwa; tena mji, au nyumba yoyote ikifitinika juu ya nafsi yake haitasimama."* (**Mat 12:25**). Kwa kifupi, Wakristo lazima waone kwamba kuishi kwao, na jinsi wanavyohusiana na wengine wenye historia tofauti na zao kuongozwe na theolojia yao—na theolojia hiyo iwahesabie wote kulingana; isichuje kupitia chujio ya miwani ya ukoo, kabila, rangi, jinsia, daraja, au utaifa.

**<u>1:5:</u> *Walakini mwisho wa agizo hilo ni upendo utokao katika moyo safi na dhamiri njema, na imani isiyo na unafiki.***

***Walakini mwisho (au lengo):*** 1. <u>Neno "walakini" (Kiyunani = *de*) ni neno la *kutofautishia.*</u> Paulo anatofautisha mafundisho ya *potofu* (**1:3-4**), ambayo mtu hatakiwi kuyafuata, na lengo la mafundisho *ya kweli*, ambayo yanapaswa kukaziwa. Dhana hii ya mlinganisho kati ya mafundisho potofu na ya kweli yanaendelea kitabu chote.

2. <u>Kuunganisha maneno kama "walakini" ni muhimu. Hutusaidi kuona mkondo wa wazo la mwandishi.</u> Pia hutusaidia kujilinda kutoka mawazo kwamba kila mstari "unasimama peke yake" kama kipengele kamili cha wazo. "Vpande vya mawazo" vya msingi kabisa vya Biblia huwa ni vifungu (paragrafu), au mistari. Zaidi ya hapo, "ufunguo kwa maana ya mstari wowote hutokea katika kifungu husika, siyo siyo kutoka kwa maneno binafsi" (Koukl 2001: n.p.). Sababu yake ni kwamba "dhana huunda mstari, na huupatia maana maalum Hili hufanya kazi kwa sababu ya kanuni ya msingi ya mawasiliano yoyote: Maana siku zote hububujika kutoka juu kuja chini, kutokea kwenye vipande vikubwa kueleka vidogo zaidi, siyo kinyume chake" (Ibid.). "Paragrafu au kifungu hutokana na dhana maalum. Ingawaje dhana hii inaweza kuundwa na vipengele tofauti, hata hivyo vipengele hivyo vitaungana kushughulikia hoja hiyo." (Wolvaardt 2005: 99). Maneno yanapaswa yaeleweke kulingana na hoja ya mstari ambao yanatokea; mistari inapaswa itafsiriwe kuendana na dhana ya kifungu inakotokea; vifungu vinatakiwa kutafsiriwa kuendana na vifungu vinavyokizunguka; vyote hivyo vinahitajika kueleweka kuendana na dhana ya sura ya somo, sehemu, na kitabu kwa ujumla. Hili ni muhimu kiasi kwamba Koukl huliweka kwa jinsi hii: "sheria ya msingi" ni, "*Kamwe usisome mstari wa Biblia.* Badala yake soma kifungu, angalau. Siku zote angalia hoja. Chunga mkondo wa mawazo. Ndipo ukazie kwenye mstari Ni somo la muhimu zaidi kimatendo nililowahi kujifunza na [ni] kitu pekee kimoja muhimu zaidi niwezacho kukufundisha." (Koukl 2001: n.p.).

***Lengo la maagizo yetu ni upendo:*** 1. <u>Kama hujui lengo lako ni lipi, kamwe hutalifikia.</u> Ikiwa unalenga shabaha, nawe hujui shabaha yenyewe ni ipi, kamwe hutaipiga. Ikiwa unasafiri kuelekea mahali fulani, lakini hujui wapi unaenda, kamwe hutafika huko. Katika mstari huu Pauloametupatia lengo la maagizo ya kweli. Lengo hilo ni UPENDO.

2. <u>Kama ilivyo kwamba Ukristo uko tofauti na dini nyingine yeyote duniani kwa uelewa wake wa tatizo la mwanadamu la msingi, na na ufum wa tatizo hilo, kwa hiyo Ukristo ni tofauti na dini nyinginezo katika dunia kwa lengo lake.</u> Lengo na makusudi ya Uislamu ni *jihad*. Dini za Mashariki ya Kati (Hindu na Buddha) malengo yao ni "kuushinda ulimwengu," kupitia kutojihusisha na dunia. Ubeberu wa mali wa Kimagharibi una lengo lake na kusudio pia "Amani ya binafsi na utoshelevu." Ni Ukristo pekee uwekao upendo kwa wengine nafasi ya kwanza.

3. <u>Upendo ndio *kitovu* cha Ukristo.</u> Je upendo ni wa muhimu kiasi gani? Yesu alisema Agano la kale lote hutegemea amri hizi mbili: *"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote"* na *"Mpende jirani yako kama nafsi yako"* (**Mat 22:36-40**). Je upendo ni wa muhimu kiasi gani? Usiku ule kabla hajafa, Kristo aliwaambia wanafunzi wake, *"Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi"* (**Yoh 13:34-35**). Kristo aliwapenda watu *ki-ukweli:*

hakusema tu kwamba aliwapenda, bali aliwaonyesha watu kwamba anawapenda kwa kuwalisha wenye njaa, kuwaponya wagonjwa, kuwafariji wauguao, na kuwa rafiki wa wale ambao wengine waliwadharau. Kristo aliwapenda watu *kwa usawa:* hakuonyesha upendo kwa Wayahudi wenzake peke yake, bali kwa watu, na kwa Wasamaria na kwa Wamataifa; alionyesha upendo kwa matajiri na, kwa masikini, watu wa kawaida, na kwa wasiopendwa. Kristo aliwapenda watu *kwa kujitoa:* Aliweka hoja zetu, hata hoja za adui zake, juu ya maisha yake mwenyewe. Anawaagiza wanafunzi wake kuwapenda wengine katika kweli, ki-usawa, na kwa kujitoa. Kama Paulo asemavyo, *"Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo"* (**Gal 6:2**). Je upendo ni wa muhimu kiasi gani? Katika **1 Kor 13:1-3** Paulo anasema kuwa waweza *"kunena kwa lugha za watu na za malaika,"* lakini kama huna upendo, wewe *"shaba iliayo na upatu uvumao";* unaweza kuwa na uelewa mkubwa sana na imani yenye nguvu sana, lakini kama huna upendo, wewe *"si kitu";* waweza kutoa mali zako zote kuwalisha masikini na hata kutoa mwili wako uungue, lakini kama huna upendo *"ni bure."* Anahitimisha kwa kusema, *"imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo"* (**1 Kor 13:13**). Katika **Gal 5:14** alisema kuwa *"Maana torati yote imetimilika katika neno moja, nalo ni hili, 'umpende jirani yako kama nafsi yako.'"* Je upendo ni wa muhimu kiasi gani? Katika **1 Yoh 4:20** Yohana anatuambia, *"Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona."* Kwa maneno mengine, tutawezaje kuonyesha upendo kwa watu (m.y., jinsi tunavyoitendea kazi ile amri kuu ya "pili" ["kumpenda jirani yako kama nafsi yako mwenyewe"] ni kipimo—alama ya nje yenye kuonekana—kuonyesha kama kweli tunaitekeleza ile amri kuu ya "kwanza" ["Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na nguvu zako zote"]).

***Upendo utokao kwenye moyo safi na dhamiri njema na imani ya kweli:*** "Moyo" ni "makao ya uhai wa mwili, kiroho, na kiakili," ndipo "kiini na chanzo cha uzimawote wa ndani, na mawazo yake, na uwezo wa kuamua" (Danker 2000: 508). Ni "Kiini cha utu wetu ambako uzima hububujikia. Ndiko kunakotoa mwelekeo wa kila kitu tukifanyacho" (Willard 1997: 206). Moyo huonyesha "uhalisi wetu"—jinsi tulivyo hasa kwa ndani. Kuwa na moyo "safi" kunamaanisha siyo tu kwamba tumesamehewa katika Kristo, bali tunabadilishwa kuwa mfano wake Kristo (**Rum 8:29; 12:1-2**) kwa kukaa katika *" Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo"* (**Flp 4:8**). "Dhamiri njema" humaanisha kuwa tunajua tunatakiwa kufanya nini, na tunalifanya hilo. "Imani ya kweli" humaanisha kile tunachokiamini. Kule kuwa na uelewa wa kichwa, au kuamini, hoja fulani hakutoshi. Mtume Yakobo anasema hatutakiwi kuwa *"wasikiaji tu wa Neno"* bali *"watendaji wa Neno"* (**Yak 1:22-25**). Hicho ndicho kipimo kama imani yetu ni "Ya kweli." Kwa maneno mengine, utu wetu wote, ndani na nje—jinsi tulivyo, nini tunakiamini, na jinsi tunavyotenda—huhusika tunapokuwa Wakristo na kuendelea kueleka lengo.

**<u>1:6-11:</u>** ***6 Wengine wakiyakosa hayo wamegeukia maneno ya ubatili; 7 wapenda kuwa waalimu wa sheria, ingawa hawayafahamu wasemayo wala mambo yale wayanenayo kwa uthabiti. 8 Lakini twajua ya kuwa sheria ni njema, kama mtu akiitumia kwa njia iliyo halali; 9 akilifahamu neno hili, ya kuwa sheria haimhusu mtu wa haki, bali waasi na wasio wataratibu, na makafiri, na wenye dhambi, na wanajisi, na wasiomcha Mungu, na wapigao baba zao, na wapigao mama zao, na wauaji, 10 na wazinifu, na wafiraji, na waibao watu, na waongo, nao waapao kwa uongo; na likiwapo neno lo lote linginelo lisilopatana na mafundisho yenye uzima; 11 kama vile ilivyonenwa katka Habari Njema ya utukufu wa Mungu ahimidiwaye, niliyowekewa amana.***

***Wengine wakiyakosa hayo wamegeukia maneno ya ubatili:*** Mtu asipotunza kuangalia lengo lake, atakwenda kando ya njia anayotakiwa kuiendea, na kamwe hatafikia lengo lake. Matokeo yatakuwa "kutozaa matunda," na kupoteza wakati. (**Mat 13:3-23; 21:18-19; Mk 4:2-20; 11:12-14; Lk 3:7-9; 13:6-9; Yuda 4, 11-12**). Hili ni muhimu, kwa sababu Kristo alisema zaidi ya mara moja, *"mti hujulikana kwa matunda yake"* (**Mat 7:15-20; 12:33-37; Lk 6:43-45; Yoh 15:1-8;** ona pia **Yak 3:10-12**).

***Wapenda kuwa waalimu wa sheria:*** Kwa Wayahudi, Sheria ya Musa ilikuwa kila kitu. Mtazamo wao ulikuwa kama ule wa Waislamu, ambao kwao *sharia* ni kila kitu. Tatizo kubwa, hata hivyo, ni kuwa *mtu hawezi kufikia lengo la upendo kwa njia ya Sheria.* Utii wetu kwa Sheria siku zote ni sehemu, kwa sababu tuna mioyo ambayo ni ya uharibifu, na ya dhambi. Hii ndiyo maana *hatuwezi* "kujipatia" wokovu wetu kwa matendo mema au kwa kutii sheria. Ni Kristo tu alikamilisha utimilifu wa Sheria ya Mungu. Ni neema na rehema ya Mungu peke yake iwezayo kutupatia amani itokanayo na mahusiano yaliyorejeshwa upya, na yaliyo sahihi kwa Mungu na kwa

wengine.

***Lakini twajua ya kuwa sheria ni njema, kama mtu akiitumia kwa njia iliyo halali; [9]akilifahamu neno hili, ya kuwa sheria haimhusu mtu wa haki:*** Ili ya kwamba tuweze kufahamu badiliko la nyakati lililoletwa na ujio wa Yesu, umuhimu mkuu badiliko katika Kristo linalotokana na, mafundisho yake, na tangazo lake la Ufalme. ilivyokuwa ikiheshimu Amri 10 na sheria ya A/K (torati) kwa ujumla, ambalo ndilo angalizo la sehemu hii. Paulo atambua ya kwamba hata kama sheria ya A/K ilikuwa takatifu, ya kiroho, na njema au nzuri (**Rum 7:12, 14, 16**), haikuwa imeundwa au kuwezasha kuhuisha uzima (**Gal 3:21**). Katika **Gal 3:22-4:11** Paulo anateta ya kuwa sheria ilikuwa ni kama *"mtangulizi"* (**2:24-25**), *"wakili na mtunzaji"* (**Gal 4:2**), ilikuwa mlezi kuwatunza *"watoto wachanga"* (**Gal 4:1-3**). Haikuweza kuwapa watu haki (**Rum 3:21; Gal 3:11).** Hakiwa kigezo cha kuwahesabiwa haki (**Gal 3:21**). Hata hivyo, kama Sheria *ingekuwa* ndiyo njia ya uzima, basi Kristo asingekuwa na haja ya kuja (tazama **Gal 3:11-13, 19-24; 4:4-5**). Hivyo basi ndiposa, Paulo anatuambia ya kwamba "sheria haikufanywa kwa mtu mwenye haki" (**1 Tim 1:9**). Njia ya pekee ya mtu kuwa na haki ni kwa njia ya Kristo. Twaweza tu kuja kwa Kristo tutambuapo kutokuwa na haki kwetu na Kushinndwa kwetu ili kuifikia haki kwa jitihada zetu sisi wenyewe (kama., kujaribu "kushika sheria"). Sheria, hata hivyo, ni ya watu wasiohaki kwa ajili kudhibiti tabia zao mbaya. Kithiolijia, hata kama, Sheri ya A/K iliundwa kuwa ya kitambo tu na iweze kuleta muundo fulani kwenye tukio ambalo limewatayarisha watu ili wakutane na Kristo (**Gal 3:15-4:31**; ona pia **Rum 7:24-25**). Kwanza, inadhihirisha utakatifu wake Mungu, ambao kwa umedhihirishwa ndani ya Yesu Kristo. Pili, inaonyesha watu kuwa, wajaribu wawezavyo, hawangeweza kuishika sheria hiyo kikamilifu. Hivyo basi, imewafunulia ya kwamba kama wangetaka kuwa na msimamo msimamo sahihi mbele za Mungu, ingefanyika hivyo kwa njia zingine. Tatu, iliwaelekeza watu kwa Yesu Kristo na kwa neema ya Mungu kama njia pekee ya wokovukwa kuwa ni Yesu tuu *angeweza na aliweza* kuishika sheria yote na.kwa neema Mungu huwekeza ukamilifu wa haki wa Kristo kwa wale waliojiunga nae kwa njia ya imani.

Mchambuzi mmoja anaiweka kama hivi: "[kazi ya sheria] ni kama ya yule msimamizi ambaye kwa msisitizo hutumia sheria kali kuwachunga watu wa Mungu kwa majira ya kiroho yaliyo dhaifu. Kama tu kanuni za kiasili ya ulimwengu [**Gal 4:3, 9**], Sheria ilikuwa kila siku inatuongoza kwenye mambo yake yenyewe hadi pale uwana ulipotambulikana. Ilianzishwa kuwa ya kitambo tu lakini yenye ushawishi muhimu wa kimwili katika kanuni tendaji za dhambi kama 'lijamu' kwa watu waliozoelea dhambi. Ikiweka bayana mapenzi halisi ya Mungu kama wajibu wa msingi wa agano. Ikiwemo, hata hivyo, kuja kwa imani ndani ya Kristo, kazi ya Sheria kama mlinzi na msimamizi ilikoma na Roho akawa ndiye kanuni ya uongozi ya ndani." (Belleville 1986: 70) Ndiposa, wakati Yesu alipotokea, Aliwalazimisha watu wa nyakati zake wa zama hizi kuchagua: "jee uaminifu wa Mungu wa Israeli una maana gani kwa Myahudi aliye Mpalestina aliyekutana na tangazo lakuwa ule ufalme- ulitazamiwa sana sasa umewadia? Yesu hamu yake kuu kwa nyakati hizo angelisema hivi: Torati ilitoa kipimo cha uaminifu kwa Mungu wa Israeli na kwa agano lake. Yesu alisema: kinachohitajika ni kunifuata mimi." (Wright 1996: 381) Hali hiyo hiyo hata sasa ndiyo tunayokumbana nayo hata leo. Hali hiyo hiyo ndiyo tunayokabiliana nayo leo hii: katika uchaguzi wa kimatendo, kitabia na kimaadili tunaokabiliana nao: "Wakati waandishi wa Agano Jipya walipokabiliana na matatizo ya kimaadili kwenye makanisa mbali mabali waliyoyaandikia, ingelikuwa rahisi kwao kuhusiana na kuzirai Amri kumi. Hili hawakulifanya. Hebu natuseme ukweli huu kama ilivyo sheria ya dole gumba: kwa Agano Jipya maadili mema si tena kwa Musa akiwa pale Sinai lakini kwa Kristo akiwa pale Kalvari.....Kwa kushughulika na, mambo ya kimaadili hasa mambo yote yahusuyo kufanya maamuzi (kimaadili au vinginevyo), swali tunalopaswa kujihoji sisi wenyewe, 'Jee tendo gani au tabia gani ilinganayo na injili?'" (Goldsworthy 2000: 96) Matokeo, ni injili ambayo sasa Paulo inaigeukia (**1 Tim 1:11**).

***Na likiwapo neno lo lote linginelo lisilopatana na mafundisho yenye uzima; [11]kama vile ilivyonenwa katka Habari Njema ya utukufu wa Mungu ahimidiwaye:*** Katika **1:9-10** Paulo ameorodhesha mifano ya aina za watu na tabia ambazo zililazimisha kuwako kwa sheria. Hakuna tabia yoyote kati ya hizo inayopaswa kuwa na Mkristo yeyote, kwa sababu tumebadilishwa kwa ndani (tumepewa mioyo mipya) ambayo itasababisha matokeo ya tabia ya nje. Kwetu wa Agano Jipya, *lengo* la "mafundisho yenye uzima" ni "upendo" (**1:5**); *kipimo* cha "mafundisho yenye uzima" ni "Injili yenye utukufu" (**1:11**)— Injili ile ya utukufu ni habari Njema za Kristo: Yeye ni nani; amefanya nini; anafanya nini; na atafanya nini. Hivyo, chochote kinyume na upendo na Kristo kinahukumiwa pamoja na wale wote wakosaji, watenda dhambi, na wasiomcha Mungu na zile tabia mbovu zilizotajwa katika **1:9-10.**

**<u>1:12-16:</u>** ***[12]Nami namshukuru Kristo Yesu Bwana wetu, aliyenitia nguvu kwa sababu aliniona kuwa mwaminifu, akaniweka katika utumishi wake; [13]ingawa hapo kwanza nalikuwa mtukanaji, mwenye kuudhi***

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

***watu, mwenye jeuri; lakini nalipata rehema kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga, na kwa kutokuwa na imani. [14]Na neema ya Bwana wetu ilizidi sana, pamoja na imani na pendo lililo katika Kristo Yesu. [15]Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi; ambao wa kwanza wao ni mimi. [16]Lakini kwa ajili hii nalipata rehema, ili katika mimi wa kwanza, Yesu Kristo audhihirishe uvumilivu wake wote; niwe kielelezo kwa wale watakaomwamini baadaye, wapate uzima wa milele.***

***Nami namshukuru Kristo Yesu Bwana wetu, aliyenitia nguvu kwa sababu aliniona kuwa mwaminifu, akaniweka katika utumishi wake:*** Hoja muhimu katika sentensi hii ni *"namshukuru Kristo . . . kwa sababu aliniona mwaminifu [au, 'wa kufaa']."* Sehemu iliyobakia ya senetnsi ile ina maneno yanayotegemeza hoja iliyotajwa. Kristo angeweza kuuona uaminifu wa Paulo kwa vile hujua mwisho wetu tangu mwanzo. Hata mwanzoni kabisa mwa kuongoka kwa Paulo, Mungu alijua siyo tu wapi atakofanyia ushuhuda wake kwa ajili ya Kristo (**Mdo 9:15**), bali pia *"yalivyo mengi yatakayompasa kuteswa kwa ajili ya Jina langu"* (**Mdo 9:16;** ona **2 Kor 11:23-33**). Paulo anaonyesha mshangao wake na shukurani kwamba Mungu alimwona mwaminifu, akikumbuka yale aliyoyafanya zamani kabla hajakutana na Kristo akiwa njiani kwenda Damaskus (**Mdo 9:1- 19**). Ili kuwa na sifa za "kuwekwa katika utumishi," Paulo alihitaji miaka14 ya kufundishwa huko Arabia, Syria, na Kilikia (**Gal 1:15-2:1**). Kamwe tusipuuze mafunzo au mwanzo mdogo (**Ayu 8:7; Eze 4:10; Mk 4:30-32; Lk 16:10**). Ni kwa sababu Paulo alichukua muda kujifunza vizuri, na kujithibisha mwaminifu katika mambo madogo, ndipo Mungu akamkirimia mambo makubwa baadaye.

***Ingawa hapo kwanza nalikuwa mtukanaji, mwenye kuudhi watu, mwenye jeuri:*** Kabla ya kuongoka kwake kwa Kristo, Paulo alikuwa Mfarisayo wa dhati aliyelelewa chini ya Gamalieli, mwalimu mashuhuri siku hizo, (**Mdo 22:3-5; Flp 3:5-6**). Hata hivyo, kule kujitosa kwake kwenye Sheria ile ndiko kulikomfanya mtukanaji jeuri wa kuudhi Wakristo (**Mdo 8:1-3; 9:1-2; 22:4-5; Gal 1:13-14; Flp 3:6**). Alihusika na vifo vya Wakristo wengi (**Mdo 26:9-11**). Paulo alikuwa na mtazamo kama *mauaji* ya Wa-Rwanda. Maisha yake ni mfano wa jinsi Sheria haiwezi kuubadilisha moyo wa mtu, na badala yake huufanya uwe mgumu. Alikuwa "mkufuru" kwa sababu alikuwa anatumia jina la Mungu na Sheria ya Mungu kufanya kitu kilichokuwa kinyume kabisa na "amri kuu" za Mungu mwenyewe (kumpenda Mungu na kumpenda jirani yako). Alikuwa anatumia Sheria ya Mungu *kumwakilisha vibaya Mungu na tabia yake* (Mungu ni upendo—**1 Yoh 4:8**). Matokeo ya kuongoka kwake kwa Kristo, Paulo akatoka kuwa mtesaji na kuingia kuteswa (**2 Kor 11:23-33**). Hata hivyo, kwa kuwa alikuwa na Kristo, *"alijifunza kuwa radhi na hali yo yote aliyo nayo."* (**Flp 4:11-13**). Maisha ya Paulo yanatuonyesha kwamba hata *mauaji ya kimbari* yanaweza kuokolewa na kubadilishwa. Hakuna yeyote aliye nje ya mkono wa Mungu.

***Lakini nalipata rehema kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga, na kwa kutokuwa na imani:*** Paulo alikuwa miongoni mwa wasomi wakubwa wa siku zile. Aliyajua Maandiko "ki-mbele na ki-nyuma." Hata hivyo, ni mpaka Mungu alipoyafungua moyo na akili zake, Paulo (kama ilivyo mtu yeyote mwingine) hakuweza kabisa kuuona ufalme wa Mungu (**Yoh 3:3**). Tunadhani tunajua kile tukifanyacho, lakini kama Mungu hafungui macho yetu, sote tunatenda *"kwa ujinga na pasipo imani."* Kwa hiyo, Yesu aliomba akiwa msalabani, *"Baba, Uwasamehe; maana hawajui watendalo"* (**Lk 23:34**).

***Na neema ya Bwana wetu ilizidi sana:*** Paulo anatumia mfano wa maisha yake mwenyewe kama kielelezo kiendanacho na kila mtu. Hapa paulo anaipokea "neema" aliyoitaja katika **1:2**. Neema ya Mungu ni kubwa zaidi kuliko hata dhambi kuu (ona **1 Kor 15:9-10**). Neema yake ni kubwa zaidi kuliko maumivu yoyote makuu (ona, **2 Kor 12:7-10**). Ni neema itofautishayo Ukristo na dini nyingine zote duniani. Ni neema peke yake itupayo tumaini, kwa sababu kwa jinsi yetu wenyewe, tunakuwa *"wafu kwa makosa na dhambi zetu"* (**Efe 2:1, 5**), na *"Hakuna mwenye haki hata mmoja; hakuna afahamuye; hakuna amtafutaye Mungu; wote wamepotoka; wameoza wote pia; hakuna mtenda mema; la hata mmoja."* (**Rum 3:10-12**). Hata hivyo, Mungu ni *"mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu"* (**Efe 2:4-5**). Dhambi inapokuwa nyingi, neema huwa nyingi zaidi (**Rum 5:20-21**).

***Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi:*** 1. <u>Yesu alivyo, kile alichokuja kukifanya, na kile lichokifanya, ni ya kipekee katika historia yote kabisa.</u> "Maelezo ya [Kristo] kuwa amekuja 'ulimwenguni' ni dalili kwamba alitokea mahali kwingine. Anakotokea ni mbinguni (Yohn 6:38)." (Ngewa 2009: 30) Yesu alikuja duniani kufanya kile ambacho hakuna mwingine angeweza kukifanya: kumpatanisha Mungu Mtakatifu na wanadamu wadhambi, na walioasi. Hakuna kiongozi mwingine wa kidini (k.m., Mohammed; Buddha)

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

aliyethubutu kusema amesamehe dhambi au kuokoa watu wadhambi. Yesu alitarajiwa kutoka Agano la Kale. **Yer 31:31-34** paliahidi Agano Jipya. Agano Jipya lingekuwa ni la milele. Ambapo Mungu ataandika sheria yake katika mioyo ya watu wake; watu wake watamjua Bwana;naye atawasamehe dhambi zao na kutozikumbuka tena (ona pia **Yer 32:38-40; 50:4-5; Ezek 11:16-20; 36:24-32; 37:15-28**). *"Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe . . . kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana. "* (**Gal 4:4-5;** ona pia **Mk 1:14-15**). Katika Karamu ya Mwisho, Yesu aliweka bayana kuwa alikuwa anafungua rasmi Agano Jipya kwa damu yake (**Lk 22:20;** ona **1 Kor 11:25**). Agano lilithibitishwa na kuhitimishwa msalabani (**Ebr 9:12-17**). Likatambuliwa rasmi Yesu alipofufuka kutoka kwa wafu, alipopaa mbinguni, na kukaa kwenye kiti cha enzi na Baba (**Ebr 10:11-18**). Agano Jipya ni pekee kati ya maagano yote ya Mungu linalotoa msamaha wa dhambi. Hilo linatekelezeka katika Kristo *"Mwana- kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwegu"* (**Yoh 1:29;** ona pia **Mat 1:21; Mdo 5:31; 1 Yoh 3:5**). Matokeo yake, kule kuutangaza msamaha wa dhambi katika Kristo, ndicho kiini cha Injili (ona **Lk 24:44-49; Mdo 2:38; 10:43; 13:38-39; 26:15-18**).

2. <u>Kauli hii kwa mara nyingine, inaonyesha umuhimu wa "lengo" (**1:5**).</u> Samuel Ngewa anaasa kuwa: "neno lililotafsiriwa hapa kuwa 'wadhambi' ni neno pana sana , na linatokana na tendo la "kukosa shabaha". Picha ni kama ya mtu anayelenga shabaha, ambayo, kwa tukio hili- ni Haki ya Mungu. Risasi ikaelekea pembeni na kupiga kwingine. Nasi sote huwa tunapiga pembeni. Hakuna yeyote kati yetu aliyeweza kupiga kwenye shabaha, maana yake, kufikisha kiwango cha haki ya Mungu (**Rum 3:23; 10:3**). Mpango wa Mungu wa wokovu ni kuturudisha kwenye shabaha. Huo ndio utume aliojia Yesu." (Ngewa 2009: 30) Katika **1:5** Paulo alituambia "lengo" au "shabaha" au kiwango cha haki ya Mungu: upendo (utokao katika moyo safi, na dhamiri safi, na imani ya kweli). Matokeo yake, "upande mwingine wa shilingi" wa kusamehe dhambi, ni kuwaelekeza watu kwenye lengo. Kwa njia hiyo, hawatakuwa wanakosea shabaha.

***Ambao katika hao, mimi ni wa kwanza wao:*** Kwa kujiita mwenyewe "wa kwanza" au kiongozi wa "watenda dhambi" (**1:15-16**) Paulo anahoji kwamba, "kwa vile Mungu aliniokoa na kunibadilisha mimi, anaweza kuokoa na kubadilisha *mtu yeyote.* Paulo alielewa kina kirefu mno cha dhambi yake. Hakuitumia elimu yake kubwa katika Maandiko, cheo, au madaraka kwa kujipatia wapenzi, fedha, au mamlaka zaidi. Badala yake, alitumia elimu yote aliyo nayo, cheo, na madaraka *kumshambulia Mungu* kwa kumtesha Kristo na mwili wake, kanisa. Elimu ya Paulo, cheo, na madaraka vilimaanisha kwamba hana *visingizio* kwa aliyoyafanya. Asingeweza kulaumu malezi mabaya, kukosa elimu, umasikini, au upungufu wowote wa kidunia kwa ajili ya dhambi zake. Kwa hiyo, kwa unyenyekevu mkubwa alitamka, *"Maana mimi ni mdogo katika mitume, nisiyestahili kuitwa mtume, kwa sababu naliliudhi Kanisa la Mungu"* (**1 Kor 15:9**).

***Lakini kwa ajili hii nalipata rehema, ili katika mimi wa kwanza, Yesu Kristo audhihirishe uvumilivu wake wote; niwe kielelezo kwa wale watakaomwamini baadaye, wapate uzima wa milele:*** 1. <u>Kama alivyosisitiza ulazima na umuhimu wa neema ya Mungu katika **1:14,** hivyo Paulo anarudia umuhimu na ulazima wa "rehema," ambayo aliitaja mwanzo katika **1:2**.</u> Katika **1:16** anarudia tena madai yake kuwa "kiongozi" wa wadhambi wote. Hoja yake ni kuwa, kwa kumwonyesha yeye rehema,, Kristo alidhihirisha *"uvumilivu wake wote."* Mungu alikuwa mvumilivu kwa Paulo maisha yake yote kabla ya kuongoka kwake. Kabla Kristo hajamtokea, njiani akieleka Damaskus, Paulo hakuonyesha dalili yoyote ya "kubadilisha" matendo yake ya kikatili. Hata hivyo Mungu hakumpiga chini. Vivyo hivyo, Mungu alikuwa mvumilivu sana kwetu, kwa yote mawili-kabla na baada ya kuongoka kwetu. Je sisi tu wavumilivu kwa wengine?

2. <u>Msisitizo wa "uvumilivu" wa Kristo, kuhusiana na "uzima wa milele" unadhihirisha ukweli kuwa Uzima wa milele ni *namna ya maisha,* siyo tu kuishi maisha yasiyo na mwisho.</u> "Uzima wa milele unamaanisha zaidi ya kuishi maisha marefu; unamaanisha uzima ulio katika maisha ndani ya Kristo. Baraka namba ya kwanza inayotoa ni uwepo wa Mungu. Tunahitaji kusisitiza hoja hii kwa sababu katika nchi nyingi za Kiafrika, wahubiri wengi husisitiza baraka za mali ambazo Mungu anatupatia kuliko ukweli kwamba Mungu yupo pamoja nasi bila kujali tunapitia hali gani (**2 Kor 12:9-10**). Kwa vile uzima wa milele ni swala la uthamani kuliko uwingi, twaweza kuanza kuufurahia hapa duniani, ingawaje tutakuja kujua utimilifu wake wote siku za baadaye." (Ngewa 2009: 31) Kwa vile sasa tunaishi "katika Kristo," tunapaswa kuonyesha uzima ule mpya kwa *jinsi* tunavyoishi. Saburi na uvumilivu ni ishara za upendo (**1 Kor 13:4**). Ni sehemu ya tunda la Roho (**Gal 5:22**). Kwa hiyo, lazima tuwavumilie wengine. Lazima tuwaombee kwa uvumilivu, tuwaelekeze kwenye lengo, tuwafundishe na kuwashauri kwa Neno la Mungu, na kuwaonyesha kuishi kama Wakristo.

<u>**1:17:**</u> ***Sasa kwa Mfalme wa milele, asiyeweza kuona uharibifu, asiyeonekana, Mungu peke yake, na iwe heshima na utukufu milele na milele. Amina.***

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

1. Dhana mara moja iliyomsababisha Paulo kufumuka kwenye sifa za Uungu (wasifa wa kumtukuza Mungu), ilikuwa ni *uvumilivu* wa Kristo kwa kumwonyesha rehema na kumwokoa. Hii ni kuonyesha tena kwamba wokovu wetu kutokea mwanzo hadi mwisho ni kazi ya Mungu Mwenyezi, si kitu ambacho tumekifanyia kazi wenyewe.

2. Ingawaje kule kusema kwa "Mfalme wa milele" na "Mungu peke yake" ungeweza kuchukuliwa kumhusu Baba, dhana inaashiria kwamba Paulo anamzungumzia Kristo. Kwanza, dhana ianziayo ni **1:16** ambayo inamzungumzia Kristo. Pili, Kristo *ni* Mungu (ona, **Yoh 1:1; 10:30; 14:6-11; 20:26-29**). Ni wa milele (ona **Yoh 1:1-2; 8:54-58**). Uasili wake wa mbinguni ulishaonyeshwa katika **1:15**. Anatawala sasa (ona **Mdo 2:29-36; 1 Kor 15:20-28; Efe 1:18-22; Ebr 1:1-4**). Tatu, hiki ni kifungu cha kwanza kati ya vitatu katika 1 Timotheo ambapo Paulo anamkazia Kristo katika namna ya undani. Vingine ni **3:16** na **6:14-16.** Vifungu vyote vitatu vinaungana pamoja kama jumuiko kamili. **1:17** huzungumzia asili ya umilele wa Kristo; **3:16** huzungumzia kutwaa mwili na kupaa kwake; **6:14-16** huzungumzia kuja kwa Kristo kwa mara ya pili. Kwa hiyo, vifungu vyote vitatu hutoa theolojia kamili ya Yesu Kristo, katika mpangilio sahihi!

**1:18-20:** ***[18]Mwanangu Timotheo, nakukabidhi agizo hilo liwe akiba, kwa ajili ya maneno ya unabii yaliyotangulia juu yako, ili katika hayo uvipige vile vita vizuri; [19]uwe mwenye imani na dhamiri njema, ambayo wengine wameisukumia mbali, wakaangamia kwa habari ya Imani. [20]Katika hao wamo Himenayo na Iskanda, ambao nimempa Shetani watu hao, ili wafundishwe wasimtukane Mungu.***

***Kwa ajili ya maneno ya unabii yaliyotangulia juu yako:*** Ni dhahiri, wakati Timotheo alipotumwa kwa umishinari au kazi ya umisheni, baraza la kanisa na Paulo mwenyewe (**2 Tim 1:6**) walimwekea mikono wakati wanamweka wakfu. Mtu moja akatoa unabii kuhusiana na karama ya kiroho ya Timotheo (**1 Tim 4:14**). Biblia haituelezei unabii ulikuwaje wala rama ilikuwa ipi

***Uvipige vile vita vizuri; uwe mwenye imani na dhamiri njema:*** 1. Tunaposoma Biblia, tunahitaji kuzingatia siyo tu kwa *asemacho* mwandishi, bali pia *jinsi* anavyokisema. Katika **1:18-19** Paulo hamwambii tu Timotheo "kudumu katika uaminifu," ingawaje hilo ni sehemu ya agizo, anamwambia Timotheo *"kuvipiga vita vizuri."* Paulo anapangilia maneno yake kinamna kwa vile anajua kudumisha uaminifu siyo rahisi —ni "vita." Sote tunajaribiwa kuangukia dhambini au kukengeuka. Zaidi ya hapo, kanisa leo, kama lilivokuwa kanisa la Efeso alipokuwapo Timotheo, linakabiliwa na walimu wa uongo. Kwa hiyo, ni lazima *"kuvipiga vita vizuri."* katika njia nzuri, siku zote *"tukiinena kweli katika upendo"* (**Efe 4:15**). Lazima tujue kwamba vita hivi ni "vita vizuri." Naam, vita vya kudumisha uaminifu kwa Injili ni vita bora kuliko vyote, kwa sababu hutofautisha kati ya uzima wa milele na mauti.

2. Wakati *"Tukivipiga vita vizuri"* vya *"kudumu katika imani,"* lazima tukumbuke kwamba kwetu ni vita vya ndani na pia vya nje. Paulo anataja umuhimu wa kudumisha *"dhamiri njema."* Alianzia kuitaja *"dhamiri njema"* katika **1:5** akihusisha kufanikisha lengo la upendo. Kama hatudumu katika dhamiri njema, hatuwezi kutimiza lengo. Uzima wetu wa ndani lazima uendane na matendo yetu ya nje. Kama hatudumu katika dhamiri njema, tunageuka kuwa wanafiki. Unafiki siyo *"kuitunza imani."* Matokeo yake, tunahitaji kupima mara kwa mara siyo tu *nini* tunafanya, lakini pia *kwa nini* tunafanya hilo.

***Wengine wameisukumia mbali, wakaangamia kwa habari ya Imani. Katika hao wamo Himenayo na Iskanda:*** 1. Paulo anamwonya Timotheo *"kuvipiga vita vizuri"* kwa sababu uwezekano wa kukengeuka siku zote upo. Kukengeuka kunaweza kutokea hata kati ya viongozi wa kanisa. Ndiyo maana waamini wote, hasa viongozi, wanapaswa kusaidia, kutia moyo, na kumfanya kila mtu awajibike. Vikundi vya selli au vikundi vya uwajibikaji ni njia mojawapo ya kufanyia hili. Mara kwa mara, kukutana na marafiki Wakristo waliokua kiroho, wenye kutumainika, ambako waweza *"kuungamiana dhambi zenu ninyi kwa ninyi"* (**Yak 5:16**) ni njia nyingine ya kudumisha uaminifu. Hata hivyo, viongozi wale wanaodhani hawawajibiki kwa yeyote isipokuwa Mungu na wasiokuwa na muundo wa uwajibikaji, tayari wako katika hatari ya kuanguka au kukengeuka kwa sababu ya kiburi. Swala hili ni muhimu kwa viongozi, kwani imani yao inapokuwa "imepotoka" kikawaida hubeba watu wengi—ambao walikuwa wanawategemea na kuwatazama wao—huzama chini pamoja nao.

2. Paulo haogopi kuwataja watu wawili mashuhuri, Himenayo na Iskanda, waliokengeuka. Sehemu nyingine pekee inayowataja watu hawa—Himenayo (**2 Tim 2:16-18**); Iskanda (**2 Tim 4:14-15**)—baada ya kuandikwa 1 Timotheo inaonyesha kwamba walikuwa bado wamekengeuka, na kwa kuipinga Injili, walikuwa wameumiza imani za watu wengine. Mungu anamjua kila moja kwa jina. Watu hao wawili wamekumbukwa zaidi ya miaka 2000 ya historia kuwa ni watu waasi wa imani wenye jina baya. Je tuna jina la aina gani?

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

***Ambao nimempa Shetani watu hao, ili wafundishwe wasimtukane Mungu:*** 1. Paulo haelezei "kuwakabidhi kwa Shetani" ni kufanyeje, lakini, kwa kuona vifungu vingine, twaweza kufikia uamuzi wa kufaa kujua. "Kumkabidhi Shetani"ni dhahiri aina mojawapo ya uwajibishaji kikanisa. Kifungu kingine pekee kinachozungumzia mtu *"aliyekabidhiwa kwa Shetani [au 'kumpa'] Shetani"* ni **1 Wakor 5:5**. Pale, ni mtu aliyekuwa akilala na mke wa baba yake. Sehemu zote mbili, **1 Tim 1:20** na **1 Wakor 5:5** panahusisha matatizo mazito sana ndani ya kanisa: mafundisho ya uongo ya kutopuuzika kabisa (ona **1 Tim 1:3-4; 4:1-7a; 6:3-5; 2 Tim 2:16-18**); na kashfa ya hadharani ya uzinzi (**1 Kor 5:1**).

2. Katika **2 Kor 2:5-11** Paulo anaonekana kuzungumzia hali ile ilealiyoinena katika **1 Kor 5:5**. **2 Kor 2:6** panaonyesha kuwa "adhabu" [m.y., kule "kukabidhiwa kwa Shetani"] kuliathiri walio wengi" (ama wazee wa kanisa wa Korintho, na wengi wa washirika wa kanisa). Kwa hiyo, iliaonekana kuna *hatua ya kuadibisha* iliyotolewa. Hatua inayoelekea sana ni "kuadibishwa kwa mwendelezo" iliyotajwa katika **Mat 18:15-17.** Kule "kukabidhiwa kwa Shetani" kunaonekana ni hatua ya mwisho ya hiyo hatua, na yaonyesha ni kumwondoa mhusika asiyetubu kutoka kanisani (ona **1 Kor 5:2**), huenda kunafanana na Mungu kuwaachilia watu kwenye dhambi zao (ona **Rum 1:24, 26, 28**). Hii inaonyesha kuwa nidhamu ya kanisa haipaswi "kupuuzika chini-chini au kubezwa." Lazima kuwe na viwango vya mwingiliano kwa viongozi wa kanisa, na viwango vya adhabu, kulingana na ukubwa wa kosa. Ukweli kwamba viongozi wa kanisa wanapaswa kuzingatia ukubwa wa adahabu inayotolewa, pamoja na: kwamba kosa linajulikana na wote au hapana, toba ya mtuhumiwa, kama kuna mabadiliko yameonekana (ambayo ni ishara moja wapo ya toba ya kweli), na mambo mengine.

3. Lengo la msingi katika "kumkabidhi Shetani," au aina yoyote ya kuadibishwa, ni toba na kujirekebisha kwa mkosaji. Katika **1 Tim 1:20** Paulo anasema kuwa sababu ya "kuwakabidhi kwa Shetani" ni ili wakosaji *"ili wafundishwe wasimtukane Mungu."* Katika **1 Kor 5:5** kukabidhi kwa Shetani kulikuwa *"ili mwili uadhibiwe, ili na roho iokolewe katika siku ya Bwana Yesu."* Itokeapo mkosaji *anatubu kikweli na kubadilika,* hata hivyo, Paulo anasema kuwa kanisa linapaswa *"kumsamehe na kumfariji, mtu kama huyo asije akamezwa katika huzuni yake ipitayo kiasi. Kwa hiyo nawasihi kumthibitibishia upendo wenu."* (**2 Kor 2:7-8**). Ni juu ya kanisa kuamua kama toba ni halisi au siyo (ona **2 Kor 7:10**). Matokeo yake, hata itokeapo mtu fulani katika kanisa "amekabidhiwa kwa Shetani," kiongozi wa kanisa awe anawasiliana na mtu huyo, akimshauri, na kujaribu kumrudisha tena kwa Bwana (ona **Gal 6 :1**).

**2:1-7:** ***[1]Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote; [2]kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu. [3]Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu; [4]ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli. [5]Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu; [6]ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote, utakaoshuhudiwa kwa majira yake. [7]Nami kwa ajili ya huo naliwekwa niwe mhubiri na mtume, (nasema kweli, sisemi uongo), mwalimu wa Mataifa katika imani na kweli.***

***Kabla ya mambo yote:*** 1. Ingawaje Paulo anaingia kwenye swala jipya—sala—kifungu hiki kinachoanzia **2:1** kinaunganisha ayasemayo katika sura ya 2 na yale aliyokwisha kuyanena katika kumalizia sura ya 1. Lile neno la Kiyunani la "basi" (Kiyunani = *oun*) kimsingi hutafsiriwa "kwa hiyo." Kile anachokisema Paulo ni kuwa: "Kwa hiyo, kama mwataka kubaki katika uaminifu [m.y., hiyo 'kwa hiyo' au 'basi' inahusisha kile alichokwisha kukisema katika **1:18-19**], swala la umuhimu wa kwanza ni sala (maombi)." Kusema ukweli, sura yote ya 2 (naam, sehemu yote ya kitabu iliyobakia) yaweza kuonekana kama kidokezo kuhusu jinsi ya kudumisha uaminifu, na uaminifu unaonekanaje utumikapo kwa waume na wanawake.

2. Maneno ya ufunguzi ya **2:1** yatukumbushe kuwa, tunaposoma Biblia zetu, tunapaswa kukaza macho kwenye maneno yaunganishayo na kichwa cha somo. Wakati mwingine, sura ya somo, na namba za mistari hutusababisha tuwaze kuwa kila sura au mstari "unajisimamia wenyewe". Utenganisho wa sura hizi zilizopo haukuweko hadi ilipofika miaka ya 1,200; namba za mistari ya Agano la Kale haukuwepo hadi miaka ya 1,400; na namba za mistari ya Agano la Kale haikuwekwa hadi mwaka 1,551 (Metzger na Coogan 1993: 105-07). Kwa vile sura na namba za mistari iliwekwa hasa kwa ajili ya kusaidia kukumbuka, *"si mara zote huendana vizuri na wazo asilia la dhana nzima"* (Ibid.: 105). Tunahitajika kuangalia mtiririko wa mawazo ya mwandishi ambao unaweza, kama ulivyo hapa, kuunganika kati ya sura.

***Nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote:*** Maneno tofauti yaliyotajwa kuhusiana na sala yaliyotumiwa katika **2:1** yanaashiria kwamba mamombi ya aina zote yafanyike kwa ajili ya watu wote. Maisha yetu ya maombi yanaonyesha uhusiano wetu na Mungu. Kwa vile daima tuko mbele za Mungu, tunapaswa siku zote tuwe na mawasiliano naye (kwa yote mawili; kusema naye na kumsikiliza).

Maombi yetu yahusishe kumtukuza na kumsifu Mungu, kuungama dhambi zetu, shukurani kwa yale aliyoyafanya na yale atakayoyafanya, na pia kujiombea na kuwaombea wengine. Kwa hiyo, katika **1 Thes 5:16- 18** Paulo anatuambia *"Furahini sikuzote; ombeni bila kukoma; shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu."*

***Kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu:*** Ukristo na jamii huingiliana na kugusa pande zote. Matokeo yake, Wakristo wanapaswa kuwa kutokulaumika kwa jinsi wanavyoishi , ili kwamba serikali na wasio Wakristo katika jamii wasiwe na sababu ya kulishambulia kanisa (ona **Mat 22:15-21; Rum 13:1-14; 1 Tim 6:1-2; 1 Pet 2:13-17**). Ili kuweza kuishi *"maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu"* kutasaidia sana katika kueneza Injili—na kuishi, na kueneza Injili kunapaswa siku zote kuzingatiwe.

***Ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli:*** 1. Mstari huu inaungana na **2:2-3** na hutuambia sababu husika ya sisi kufanya maombi na kuishi maisha ya utauwa. Jinsi tunavyoishi na picha ya Yesu na Injili. Kutaka kwa Mungu ni wokovu kwa watu. Maisha yetu ni ushuhuda wa Kristo. Kama tukiishi maisha ya *"utauwa na ustahivu"* (**2:2**) tutawavuta watu kwa Kristo. Kwa hiyo, mambi yetu kwa watu wote, hasa kwa viongozi, ili tuweze kuishi maisha yenye utauwa, haswa husimamia kwenye lengo la kueneza Injili.

2. Mstari huu usiondolewe nje ya dhana ya mpango wa Mungu wa Biblia yote kwa ajili ya wokovu. Biblia inaonyesha kwamba, ingawaje ni "shauku" ya Mungu kuwa watu wote waokolewe. *Siyo* watu wote, kusema ukweli, wataokolewa. (ona **Mat 7:13-14; 13:24-30, 36-43; 25:31-46**). Ziko njia muhimu mbili kushughulika na utofauti huu kati ya "kutaka" kwa Mungu na nini hasa kinatokea. Njia moja kushughulika na hili nini kusema kwamba *"watu wote"*ilivyonenwa katika **2:4** ikimaanisha "*watu wa aina* zote"—kwa maneno mengine, "watu wote *pasipo kuwabagua"* (kwa rangi, kabila, lugha, kiuchumi, n.k.—ona **Ufu 5:9; 7:9**), *siyo* "watu wote *pasipo kuwatofautisha"* (m.y., kila mtu binafsi duniani).

3. Njia nyingine kushughulika na hili ni kutambua kuwa, kinamna fulani, kuna "mapenzi" mawili katika Mungu. "Ni lazima tutofautishe kati ya kile ambacho Mungu angependa kukiona kikitokea, na kile ambacho ni mapenzi yake kitokee; na yote mawili hunenwa kama ni mapenzi ya Mungu" (Marshall 1989: 56). Kwa maneno mengine: "Maandiko yanaonyesha mapenzi ya Mungu kwa kitu fulani, ambacho hicho-hicho kwa mtazamo mwingine hakipendi" (Piper 2000: 110). Mfano ufuatao unaonyesha hilo: (A) *Kifo cha Kristo*—**Luka 22-23** panatuonyesha kwamba kusalitiwa na kufa kwa Kristo kilikuwa ni tendo la dhambi lililochochewa na Shetani; ingawa, **Mdo 2:23, 4:27-28** na **Isa 53:4, 10** panaonyesha kwamba matukio haya yalitendeka kwa lengo na kusudi la Mungu. (B)*Vita dhidi ya Mwana Kondoo*—**Ufu 17:16-17** panasema pembe kumi za wafalme (wenye dhambi) vita zidi ya Kristo, lakini pia inasema ni Mungu ambaye *"anaweka ndani ya mioyo yao kutimiza kusudi lake."* (C) *Kuifanya kazi ya Mungu kuwa ngumu*—**Kut 8:1** panaonyesha kwamba lilikuwa ni kusudi la Mungu kwamba Farao awaachilie wana wa Izraeli waondoke Misri. Ingawa, **Kut 4:21** na vifungu vingine vinaonyesha kwamba mapennzi ya Mungu yalikuwa ni kuufanya mgumu moyo wa Farao. Vivyo hivyo, **Warm 10-11** panaonyesha kwamba, ingawa Mungu ananyosha mkono wake kwa ajili ya wokovu wa Israeli, alifanya mioyo yao kuwa migumu kwa kitambo kama sehemu ya mpango wake. (D) *Ni haki ya Mungu kuzuia mabaya na ni mapenzi yake yasitokee*—**Mwa 20:6, 1 Sam 2:22-25, Rum 1:24-28** na vifungu vingine vinaonyesha kwamba Mungu ana haki na nguvu kuzuia dhambi za watu. Mara nyingine anafanya, lakini wakati mwingine hafanyi. Kwa hilo la pili, mapenzi yake ni dhambi kuongezeka (ingawa dhambi ni kinyume na mapenzi yake ), ili kwamba awe na haki ya kuadhibu wenye dhambi. Katika haya na mengine, mapenzi ya Mungu kwa upande mwingine yana shauku ya jambo fulani, lakini kwa upande mwingine mapenzi yake ni kuona upinzani unatokea (Piper 2000: 111-19). Haya "mapenzi mawili" wakati mwingine yanaitwa "maagizo" [au, "maadili"] (m.y., yale anayowaagiza watu wayafanye) na "maadili" yake (m.f., au uhalisi wa maonyo yatakavyotokea), au "kijifunua" mapenzi yake na "nyapo zake." Kama Ngewa anavyofafanua, "Neno la Kigiriki 'kutaka' [katika **1 Tim 2:4**] halina maana kuwa haya ndio mapenzi halisi ya Mungu, na lisichukuliwe kijumla. Badala yake, Paulo anatumia neno linaloonyesha kuwa Mungu pekee ana kusudi kwa watu—Anatoa wokovu kwa wote. Kwa namna nyimgine, Paulo hasemi kwamba mapenzi ya Mungu ni 'kuokoa watu wote', bali ni mapenzi yake kwamba 'wote waokolewe'." (Ngewa 2009: 42) Ngewa analifafanua hili kwa njia nyingine: "Harusi na misiba katika Afrika hualika kila mtu anayetaka kuhudhuria. Hakuna anayerudishwa kwa sababu hana mwaliko. Kila anayefika anakaribishwa . . . kwa njia hiyo hiyo, kila mmoja anaalikwa kufurahia wokovu wa Mungu. Kila anayekuja anakaribishwa, lakini kusudi la Mungu litasimama hata kama wengine wataamua kutokuokoka." (Ibid.: 42-43) Kuhusu wokovu, inapaswa kueleweka kwamba, ingawa kuna mwaliko wa jumla kumwamini Kristo na kuokoka, *hakuna mtu,* kwa kweli, ambaye atachagua kufanya hivyo kwa uweza wake. Isipokuwa ni wale tu ambao mioyo yao imebadilishwa na Mungu (m.y., iliyoumbwa upya) wataimwitikia kwa

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

imani (ona **Yoh 3:3; Mdo 13:48; Rum 3:9-18; Efe 2:1-9**). Tunapoeneza habari njema ya Kristo, Mungu anatutumia kama vyombo vyake kujifunua kwa wale ambao amewachagua, na kufanya kazi ndani ya mioyo yao.

4. **1 Tim 2:4** haisemi kwa *nini* Mungu anatamani watu wote waokolewe, na haionyeshi kwa kweli kwamba watu wote,, wataokolewa. Jibu la swali hilo linaathiri mambo mengine mengi. Misimamo miwili ya Kitheolojia—Calvinism na Arminianism—yote hukubaliana kwamba uamuzi wa Mungu kutomwokoa kila mtu, ingawa amesema "shauku yake " kwamba wote waokolewe, inawezakana ni sababu "amejitoa kwa ajili ya jambo fulani ambalo ni zaidi ya kuokoa wote" (Piper 2000: 124). Haikubaliani kuhusu jambo lenyewe ni lipi. Kwa upande wa Arminians, kule kuheshimu uhuru wa mapenzi ya mwanadamu kunathaminiwa zaidi ya mapenzi yake yasemayo wote waokolewe. Kwa hiyo, Mtazamo Wa-Arminians huona ile dhabihu yenyewe kama tu *fursa* ya wokovu kwa *wote*, lakini *haitupi* wala kuhakikisha wokovu kwa *kila mtu.* Kwa upande mwingine, Wa-Calvinists wanatambua kwamba Mungu anajishughulisha zaidi na mambo ya ulimwengu kuliko Mungu wa Wa-Arminians. Mungu huhusika na "udhibiti wa majanga yote na njaa yanayotokana na maumbile au na mwanadamu " (m.f., **Amos 3:6; Isa 45:7**), amehusika na mateso ya watu wake (m.f., **1 Pet 3:17, 4:19**), na amechukua nafasi ya utawala juu ya undani wa maisha ya kila mmoja (m.f., **Mit 16:9; Mdo 18:21; Yak 4:15**) (tazama Piper 2000: 119-22). Kwa Wa-Calvinists, mwingilio wa Mungu ni udhihirishi wa ukamilifu wake wa utukufu wake mpana katika ghadhabu na rehema (**Rum 9:22-23**), na unyenyekevu wa mwanadamu ili kwamba mwanadamu afurahie kumpa Mungu utukufu wote kwa ajili ya wokovu (**1 Kor 1:29**). Wa-Calvinists wanatazama kifo cha Kristo katika msalaba *kusema kweli,* sio kwa hisia kama Wa-Arminians wanavyokiona, dhabihu kwa ajili ya dhambi, na kuhakikishiwa wokovu kwa ajili ya wale wote ambao Mungu amewaita (ona **Yoh 1:12-13; 6:37-39, 44, 65; 10:25-29; Mdo 13:48; Rum 8:30**).

***Kwa sababu Mungu ni mmoja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, mwanadamu Kristo Yesu:*** 1.Kuna ufa mkubwa kati ya Mungu na wanadamu. Mungu alimuumba mwanadamu kwa mfano wake (**Mwa 1:26-27**), na akafanya ushirika pamoja nao katika bustani ya Edeni (**Mwa 2:15-25; 3:8**). Mungu aliupenda ulimwengu (**Yoh 3:16**) na alitaka wanadamu wangefurahia ndani yake milele kama watu wake, pamoja naye kama Mungu wao (**Zab 144:15; Yoh 10:10; Flp 4:4; Kol 1:16; 1 Yoh 2:25; Ufu 21:3-4**). Badala ya kufurahia ndani ya Mungu na kufanya ushirika naye, watu wote wamegeukia njia yao mbali na Mungu na kufanya dhambi na kuasi mbele yake (**Mwa 3:1-7; Mhu 7:20; Rum 1:18-32; 3:9-18, 23; 8:7; 1 Yoh 1:8, 10; 2:25**). Watu wote wana asili ya nguvu ya dhambi ikaayo ndani yao (**Mat 7:10-11, 15-20; Mk 7:14-23; Rum 7:14-24**). Kama matokeo ya hili, watu hawawezi kufikia viwango vyao, Mungu pekee ndiye mkamilifu (**Mat 5:48**). Yeye ni mkamilifu: mwenye upendo (**1 Yoh 4:8**); hekima (**Zab 104:24; Rum 11:33-34**); mwema (**Zab 107:8; Rum 2:4**); mtakatifu (**1 Pet 1:15-16; Ufu 15:4**); haki (**Mwa 18:25; Kut 34:6-7; Kumb 32:4; Zab 96:13**); na mkweli (**Zab 86:15; 117:2; Efe 6:18**). Kwas ababu Mungu ni mkamilifu na mtakatifu, hawezi kuwa na ushirika na dhambi (**Isa 59:2; Yoh 9:31; 1 Yoh 1:5-7**). Badala yake, katika haki yake atahukumu watenda dhambi wote (**Rum 1:18; Efe 5:6; Ebr 9:27**). Matokeo ya dhambi ni mauti na kutengwa na Mungu milele (**Mwa 2:17; Ezek 18:4; Math 25:46; Rum 6:23; Mdo 17:30; 2 Thes 1:6-9; Ufu 20:11-15**). Kwasababu ya dhambi zao, ni vigumu kwa watu "kugharimia "au "kufanyia kazi" kustahilisha haki ili kuleta ushirikia na Mungu (**Mdo 13:39; Gal 2:16; 3:11; Efe 2:1-3, 12**).

2. Yesu pekee ndiye awezaye "kuziba ufa" kati ya Mungu na mwanadamu, kwa sababu Yesu pekee ndiye Mungu aliyekamilika na ni mwanadamu kamili ambaye hakutenda dhambi kamwe. "Mpatanishi" ni yule ambaye analeta pamoja na kupatanisha pande mbili ambazo zinapingana. Mpatanishi lazima awe na uwezo wa kuchukuliana na pande zote mbili. Kwa swala hili la Mungu na mwanadamu, Kristo alikuwa Mungu kamili (**Mk 14:61-64; Yoh 1:1; 5:18; 8:58-59; 10:30-33; 20:28; Kol 1:15; 2:9; Tito 2:13; Ebr 1:1-3; 2 Pet 1:1; 1 Yoh 5:20**). Hivyo anaweza kuchukuliana na Mungu. Yesu pia alikuwa mwanadamu kamili (**Mat 13:54-57; Luka 2:5-7, 40, 52; Yoh 4:6; 11:35; 19:28, 34; Ebr 2:17**). Hivyo anaweza kuchukuliana na mwanadamu. Tofauti na watu wengine, Yesu hakutenda dhambi (**Lk 23:14-15, 41; 2 Kor 5:21; Ebr 4:15; 1 Pet 2:21-22; 1 Yoh 3:5**). Hivyo anaweza kumwakilisha Mungu kwa mwanadamu, na pia kusimama mbele za Mungu kama mtu. Hivyo basi, Yesu pekee ndiye awezaye kutupatanisha kati ya Mungu mtakatifu na mwanadamu mwenye dhambi.Yeye pekee anao uwezo kuwapatia wanadamu uzima wa milele na kumuunganisha Mungu na mwanadamu (**Yoh 14:6; Mdo 4:12; Rum 8:34; Kol 1:19-20; 1 Tim 1:15; 2:5; Ebr 2:14-18; 7:24-27; 9:11-15; 1 Yoh 2:1, 23**).

***Ambaye alijitoa yeye mwenyewe kuma dhabihu kwa wote:*** 1. Yesu alizibeba dhambi zetu mwilini mwake juu ya msalaba (**Isa 53:6; 2 Kor 5:21; 1 Pet 2:24**). Kwa kujitoa mwenyewe sadaka msalabani —akizibeba dhambi zetu japo aliishi maisha yasiyo na dhambi, na kufa badala yetu—Yeu alilipa deni la dhambi zetu (**Isa 52:10-11; Mat 27:46; Rum 5:8; Gal 3:13-14; 4:4-5; Kol 2:13-14; 1 Pet 3:18; 1 Yoh 1:7; 4:9-10**). Yesu aliishi maisha

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

ambayo tulipaswa kuishi (m.f., kuwa huru mbali na dhambi kumtukuza Baba kwa ukamilifu), na akafa kifo ambacho tulistahili kufia (m.f., alilipa deni la dhambi badala yetu, ili kwamba tusidaiwe). Mungu Baba alipokea dhabihu yake Yesu msalabani. Na hili lilithibitishwa na ufufuo (**Mdo 2:22-36; Rum 1:4; 3:21-25; 4:25; Efe 1:18-2:7; Ebr 10:11-14; Ufu 5:1-14**). Uzima wa milele na urejesho wa ushirika na Mungu hauwezi "kupatikana," kwa sababu sisi wote tulikuwa wenye dhambi na hatuwezi kujibadilisha wenyewe kutoka ndani- nje. Badala yake, Yesu anatupatia uzima wa milele na kurejesha ushirika wetu na Mungu kama kipawa kwa kila mtu anayemwamini (**Yohn 6:47-51; 10:10; Rum 5:8-21; 6:23; 1 Kor 1:21; 2 Kor 5:18-21; Efe 2:8-9; Kol 1:19-22**).

2. Neno "dhabihu" linazungumzia malipo ya gharama ya kukomboa mtu fulani au kitu fulani; lilikuja kuhusishwa na malipo kwa ajili ya kumnunua mtumwa kwa ajili ya kumwachilia awe huru. Agano Jipya linaonyesha kwamba tulikuwa watumwa wa dhambi (**Yoh 8:34-36; Rum 6:17-20; Efe 2:1-5; 2 Tim 2:25-26**). Ingawa, Kristo alilipa malipo ya dhabihu ili kutununua na kutuweka huru katika yeye (**Mat 1:21; 1 Kor 6:19- 20; Efe 1:7; Tito 2:14; 1 Pet 1:18-19; Ufu 5:9**).

3. Msemo *"wote"* unaweza kumaanisha tu "wote bila kutofautisha," au "wote ni kondoo wake," sio "wote bila kubagua." Kama Kristo alilipa gharama ya dhabihu kwa ajili ya dhambi zote za watu bila kubagua, hapo linaibuka jambo la "utata mara mbili". Kwa maneno mengine, kama dhambi za watu wote zimelipwa na Kristo, basi hakuna jambo walilobakiza kulipa. Hivyo ingekuwa si haki kumtupa yeyote Jehanamu tena, kwani dhambi za watu wote, kiuhalisi, tayari zimelipwa (kama vile, mahakama itanilipisha kwa kuvunja sheria fulani, lakini kaka yangu akalipa faini, hivyo Serikali haina haki kudai malipo ya pili kwangu, wakati kiasi chote cha malipo kimelipwa tayari). Kama mmoja angesema, "Wasioamini watatupwa kuzimu kwa sababu ya kutokuamini kwao," hapo swali linakuja: "Kutokuamini ni dhambi?" Jibu ni, "Ndiyo—kutokuamini ndiyo asili ya dhambi." Kama kutokuamini ni dhambi, basi tayari ameshalipa kwa ajili ya hiyo (vilevile, kama kaka yangu alivyolipa faini yangu lakini sikujua kuwa ameshafanya hivyo, nitakapoenda mahakamani kulipa faini, hawatakuwa na haki ya kuchukua pesa zangu hizo, kwani madai ya kisheria yatakuwa yameshatimizwa). Madhara yake, tunapoangalia kifungu hiki pamoja na vingine vinavyoshughulikia dhabihu, mantiki na sehemu ya Biblia, inaonekana kama kile kinachoitwa "Upatanisho maalum au rasmi: Kifo cha Yesu kiuhalisi kilimgusa au kilimhakikishia wokovu kila mtu "bila utofauti" kwa wale aliowafilia msalabani (m.y., kondoo wake—**Yoh 10:25-29**).

**2:8-15:** ***[8]Basi nataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata, pasipo hasira wala majadiliano. [9]Vivyo hiyo, wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi, si kwa kusuka nywele wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani, [10]bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu. [11]Mwanamke na ajifunze katika utulivu, akitii kwa kila namna. [12]Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwamume bali awe katika utulivu. [13]Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye. [14]Wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa, akaingia katika hali ya kukosa. [15]Walakini ataokolewa kwa uzazi wake kama wakidumu katika imani na upendo na utakaso pamoja na moyo wa–kiasi.***

Mwanzoni katika **2:8-9** Paulo *analinganisha* kile alichokuwa akisema kuhusu sala, kwanza kwa *wanaume* ndipo kwa *wanawake.* "Lengo kubwa la maagizo katika 1 Timotheo 2:8-10 sio amri ya *tendo* la maombi (amri ya maombi tayari ilishatolewa katika mstari. 1-2) bali kitabia kwa wote- wanaume na wanawake *wakiwa* katika maombi na kuabudu . . . Paulo anashughulikia na mwonekano wa maadili katika kuhusiana na utendaji katika mambo ya kiroho kwa wanaume na wanawake. Anatilia mkazo kwamba muonekano wa nje haupaswi kuwa na kutofautiana na tabia ndani." (Liefeld 1999: 95)

***Basi nataka wanaume wasalishe kila mahali:*** Neno "Basi" linaunganisha **2:8** na kile yaliyotangulia kabla. Ujumla wa uhalisi **2:8** ni maombi. Jambo lenyewe ni maombi ili kwamba tuishi maisha yanayompendeza Mungu ili Injili ienee na watu waokolewe. Wanaume wa Kikristo wanapaswa kuwa kielelezo. Maombi hayaishii kwenye shughuli zinazotendeka Jumapili kanisani. Isipokuwa, kwa sababu maombi yanaonyesha uhusiano wetu na Kristo, na daima tuko ndani yake, ukristo wetu unapaswa kudumu na kuendelea wakati wote *"kila mahali"* Kwa hiyo, kwa vile maombi ni jambo la umuhimu wa kwanza, la kudumu katika uaminifu (**2:1**), tunapaswa kuwa na tabia ya kuomba kwa wakati wote na *"kila mahali."*

***Wakiinua mikono iliyotakata, pasipo hasira wala majadiliano:*** 1. *"Kuinua mikono iliyotakata"* silo hitaji la namna tunavyopaswa kuiweka miili yetu (m.y., mikono ya mwili) tunapoomba. Badala yake, *"Kuinua mikono iliyotakata"* ni *mantiki ya* uombaji *katika maisha ya utakatifu.* Tunajua hili kwa sababu nyingi: (A) Dhana ni

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

kuomba ili tuweze kuishi maisha yanayompendeza Mungu. Tunaweza kurejea kuona kwamba Paulo analihusisha zaidi na wanaume, kile anachosema kitaendana na dhana ya kuishi maisha ya utauwa. (B) "Utakatifu " ni neno la Kiroho, silo la kimwili. Kutawadha mikono ya mtu hakumfanyi mtu kuwa mtakatifu ikiwa mtu anaishi maisha ya dhambi (ona **Mith 6:16-19; Isa 1:10-17**). (C) Aya inayofuata, *"pasipo hasira wala majadiliano,"* huhusika na kustahilisha *"kuinua mikono."* Aya hii inaendana na uthamani wa maisha ya mtu, sio hali ya mikono ya mwili ya mtu. (D) Watu wanaweza kuomba katika hali yoyote ile: kuinamisha vichwa chini (**Mwa 24:26**); kulala kifudi-fudi (**Yosh 5:15; 7:6**); kuinamisha kichwa chini ya miguu yao (**1 Fal 18:42**); kupiga magoti (**Zab 95:6; Dan 6:10**); kuinua mikono (**Omb 3:41**). Mwingine anaweza kuomba akiwa amesimama na kichwa kuelekea juu. Hali ya mwili utakavyokaa sio muhimu sana; Ila hali ya moyo ndiyo muhimu. (E) Tofauti na Agano la Kale, ambapo Waisraeli waliwekewa *mfumo* wa kuabudu; katika Agano Jipya kuna "Utofauti mkubwa wa jinsi ya muonekano wa kuabudu ki-nje; kwa jinsi ulivyo wa kina kirefu katika yale yatendekayo ndani ya moyo " (Piper 2003: 215-16). Yesu alisema, *"saa inakija ambayo hawatamwabudu Baba katika mlima huu, wala kule Yerusalemu siku inakuja ambayo . . . waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli"* (**Yoh 4:21-23**). Sababu muhimu ya Agano Jipya kuondokana na masharti au sheria za kimwili katika kuabudu ni kwa vile "Agano Jipya ni maono ya yenye kusudi ambalo huweza kutumiwa kati ya desturi maelfu; kwa hiyo isingeweza kubeba mambo ya ki-nje nje" (Piper 2003: 215). Hata hivyo, ijapokuwa AJ halitoi amri maalum juu ya taratibu za kisheria za kutimiza ibada au juu ya mkao wa kimwili wakati wa maombi au ibada, tabia zetu za nje zinaonyesha na kudhihirisha hali ya utu wa ndani wa moyo wa muhusika. Hivyo basi, tabia zetu za nje zawezakuwa ni njia iliyo na umuhimu kwetu sisi kutathmini maisha yetu ya ndani ya kiroho, na hata pia kwa wale wasioamini watatazama na kutathmini kanisa, Wakristo binafsi, na Ukristo kwa jumla. Kwa hivyo, tunahitaji kuyatilia maanani juu ya yale tuyatendayo, hata kama (au hasa kwa sababu) AJ linatupa uhuru kwa mambo kama hayo yaliyo matendo ya nje.

2. <u>*"Bila hasira wala majadiliano"* ni *mfano* wa *aina ya dhambi ya wanaume* ambayo huwazuia</u> <u>wasiombe kutoka katika maisha ya matakatifu (m.y., itawazuia *"kuinua mikono mitakatifu "*).</u> Hasira, majadilino, kugombana, na matukano ni aina za tabia za wanaume za kujiinua na kujiona binafsi. Ni kinyume kabisa cha mtazamo wa unyenyekevu, ambao humweka Mungu na mapenzi yake nafasi ya kwanza. Matokeo yake, wanaume waaombao wakati wana*"hasira na majadiliano"* wasitegemee kwamba Mungu atawasikiliza wala maombi yao.

3. <u>Neno lililotafsriwa "majadiliano " (NASB; "mashindano," NIV; "kubishana," RSV, ESV) (Kiyunani = *dialogismos*) linaweza pia kutafsiriwa kama "kuogopa " (KJV, NKJV).</u> Maana yake ya msingi linahusiana na mchakato wa kufikiria: m.y., mabadilishano ya maneno yanayotokea wakati wa mabishano. ("majadiliano, mabishano, migongano"—ona **Lk 9:46-47; Fil 2:14**); au mantiki inayoleta ("wasiwasi"—ona **Lk 24:38**). Ni mantiki iliyomo katika dhana iliyopo ndiyo inaweza kuleta maana husika. Katika **2:8** ziko sababu tatu zinazoonyesha kwa nini Paulo aliyataja "majadilianao/ mabishano/ mashindano" kuwa ndiyo tafsiri yake aliyoilenga: (A) Hasira na majadilianao ni mambo yanayohusiana. Mashindano ni matokeo ya hasira. Maneno hayo mawili yameunganishwa na neno "na." Kwa upande mwingine, "wasiwasi " hauna ukaribu na hasira. Kama "wasiwasi" ulikuwa ndiyo maana yake, mtu angetegemea neno "au" kati ya "hasira" na "wasiwasi." (B) Mantiki ya dhana ya sura ya 2 inahusika na mtazamo wa mtu na matendo yake *kwa watu wengine* kama udhihirisho wa moyo wa mtu mbele za Mungu. Katika **2:8** "hasira" imeelekezwa kwa watu wengine. Katika **2:9-13** ni nguvu ya mienendo ya wanawake kwa watu wengine. Katika **2:1-7** msingi wa maombi tunapaswa kuangalia mahusiano kwa watu wengine (m.y., tunapaswa kuwaombea wote kwa sababu Mungu anawajali wote, na pia omba ili serikali na jamii watuwezeshe tuishi maisha ya ustahivu). "Majadiliano" au "mashindano" vilevile ni mambo ambayo yanagusa watu wengine, ambapo "wasiwasi" hauna maafa kama mifano ya maneno yaliyotolewa katika sura yote. (C) Paulo anajadili kuhusu wanaume, na anashughulikia dhambi na mienendo halisi ya wanume. "Wasiwasi " unaonekana wa wa ki-ujumla zaidi, na labda ndio unapatikana kote-kwa wanaume na wanawake, na siyo kuwa zaidi kwa wanaume; ambapo mabishano au majadiliano huwa zaidi ni tabia za wanaume.

***Vivyo hivyo, wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri:*** Neno "vivyo hivyo" (au, "pia"), analoanzia Paulo **2:9** kujadili kuhusu wanawake, ni katika dhana ile ile inayohusu wanaume: ambayo ni, maombi—hasa, maombi ya kutaka kuishi maisha matakatifu. Katika **2:8** Paulo amesema kuhusu dhambi ambayo inafanyika zaidi na wanaume; katika **2:9** anafanya vivyo kwa wanawake. Ingawa wanawake wanapata hasira na kubishana, tabia kama hiyo haipo sana kwa wanawake kama ilivyo kwa wanaume. Zaidi kwa upande wa wanawake ni kuhusu muonekano wao na uzuri wao na uzinzi. "Katika mistari ya 9-10 mfano wa ndani wa wanawake ni kuwa na matendo mema. Katika Ugiriki ya zamani, na hata wakati wa Paulo Mavazi ya thamani, kusuka nywele, na lulu yalizingatiwa sana katika kuhusisha kuwa na adabu na mtu kuitwa mkamilifu.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

Ndiyo maana, Wanawake wa Kikristo walipaswa kuvaa mavazi ya 'kujisitiri.' Maelezo ya aina ya mavazi, kusuka nywele, na lulu yanaonyesha sababu mbili kwa nini hayakurusiwa. (1) Moja ni ughali. Kutajwa kwa dhahabu kunaonyesha wazi hali hiyo; pia neno lililotumika kuelezea kutokuruhusu mavazi ni 'ya thamani' (2) Lingine ni kuchanganyikana na mienendo mibaya kiutamaduni." (Liefeld 1999: 95-96). Katika mambo yote, kwa aina ya mwenendo wao wa dhambi wa kike na wa kiume wote wanawavutia watu wengine kwao na kuwaweka mbali na Bwana. Kujiona kama huko ni tabia ya akili na maisha ambayo ni kinyume na tabia nzuri ya kuabudu. Haionyeshi tabia ya Mungu wala kwa majirani zetu. Kama tuna tabia na mwenendo wa namna hiyo, hatuwezi kufikia lengo la upendo. Paulo anaweka wazi kwamba maeneo yote ya maisha yetu—hisia zetu, kung'ang'ania mambo yetu, hata namna tunavyovaa—vyote vionyeshe kile tunachofikiri kuhusu Yesu na watu wengine.

***Si kwa kusuka nywele wala kwa dhahabu au lulu, wala nguo za thamani, bali kwa matendo mema:*** 1. Swala la mtindo wa nywele (*"si kwa kusuka nywele"*) ni mfano mojawapo unaotufanya tuwe makini kulingana na mazingira ya *kihistoria (kitamaduni) ya dhana* ambayo Paulo aliandikia. Historia (au, utamaduni) muktadha wake ni "tamamaduni, desturi, lugha, imani, na historia ya mwandishi na asili ya watu wake" (Doriani 1996: 31). Muktadha wa historia unaweza kutupatia taarifa ya historia ambayo inaweza kuelezea umuhimu wa maneno, aya, desturi, watu, mahali, na matukio ambayo mwandishi alikuwa anayazungumzia. Biblia iliandikwa kwenye matukio maalumu, katika tamaduni maalumu, kwa watu maalumu, ambao walikuwa kwenye mazingira maalumu. Hata hivyo, iliandikwa ili itumike kama mjumbe kwa ajili ya watu wote baada ya hayo. Matokeo yake, "Changamoto kubwa ya kimantiki kwa matumizi ya Maandiko ni *kuunganisha ufa kati ya tamaduni za Kibiblia na tamaduni zilizopo"* (Doriani 1996: 143). Kwa maneno mengine: Je maelekezo (maagizo) ya Kibiblia —hata yale ya Agano Jipya—yanaagizwa kwa watu wote, kwa wakati wote na kila mahali; au yalihusu zile desturi maalum na dhana iliyokuwako wakati ule walipopewa maagizo hayo tu?

2. Kushindwa kutofautisha kati ya maagizo yanayolenga tamaduni fulani, na "Maelekezo" yanayotekelezeka na tamaduni zote, ndilo swala kuu linalosababisha makosa yapelekeayo uhuru mno, au sheria mno. "Hatutaki kufanya kitu ambacho ni cha tamaduni zote kukifanya kiwe cha mpaka wa utamaduni fulani. Kwa upande mwingine, hatutaki kufanya kile ambacho hakikubaliki katika utamaduni fulani kiwe sheria kwa kila tamaduni." (Webb 2001: 24) *Uhalalisho wa uhuru* kwa kiwango kikubwa, hujumuisha mambo "yaliyoagizwa" na Biblia kwa wale waliokusudiwa kwa wakati ule, na kwa mtu mwingine yeyote pia, na kuyaona kama yalikusudiwa kwa walengwa wa awali tu, bali yaweza kutokutiliwa maanani na watu wengine. Msimamo wa usheria kimsingi hutazama kila kitu kwa mwelekeo wa kufunganishwa na utamaduni. *Usheria huo* ni kinyume. Hao wa mkondo huo wa Usheria huchukulia sehemu zile za Biblia ambazo ni za "mahusisho" zilizokusudiwa tu kwa wale waliolengwa mwanzoni, na kuzichukulia kama "lazima" kwa ajili ya kila mtu. Kimsingi, hao wa mfumo wa Usheria huangalia tu *mfumo* wa amri za Biblia, lakini hawazingatii muktadha wa tamaduni au kanuni inayosimamia nyuma ya mfumo huo. Kujaribu kutofautisha kati ya muktadha wa Biblia "kamili" ambao unagusa tamaduni zote (m.y., yale ambayo yanakubalika na watu wote kwa wakati wote na kila mahali); na yale ambayo "yanahusishwa" au "yanayohusu tamaduni maalum (m.y, yale yanayohusika na desturi na mazingira fulani tu ya Biblia ambayo mwandishi alikuwa anayaandikia, au yana hutumiwa kwa kiwango fulani kwa sababu nyinginezo—huweza kuwa vigumu sana. Dhana ya kitamaduni daima haitajwi wazi kwenye Biblia, kwa sababu historia na desturi za mazingira ya Kibiblia zilijulikana sana na waandishi wa Biblia, na wale waandishi wake asilia. Ndiyo maana nyenzo nje ya Biblia, kama vile Kamusi, na vitabu vingine vya rejea, huenda vikahitajika.

3. Inapoonekana kwamba agizo la Ki-Bibila ni la uelekeo wa kitamaduni, bado tunapaswa kutafuta ikiwa kuna kanuni inayofaa leo kwa tamaduni zote inayoendana na agizo hilo (ingawaje *mfumo* ambao kanuni itatumika katika desturi zetu utaonekana tofauti na jinsi kanuni hiyo ilivyotumika nyakati za kuandikwa Biblia). Mbinu zifuatazo ni kutokana na Doriani (1996: 146-47) na Hays (2001: 30-35). (A) *Tambua maana yake ya asili na ilivyotumika.* Hii inatuhitaji tutumie ustadi wetu wa kuelewa tafsri ya Biblia na kuelewa nyakati za kuandikwa kwake. (B) *Tambua kanuni inayoingilia tamaduni zote katika hilo agizo.* Kutambua nini ambacho kilikuwa "Kinawahusu " watu ambao agizo hilo la Ki-Biblia ilielekezwa kwao; tofautisha na "agizo kamili" (m.y., linawahusu siyo tu wale walioandikiwa wakati ule, lakini kwa waumini wote wa kila mahali na wakati wote) ndiyo moyo wa jambo. Hili linaweza kutuhitaji tutofautishe kati ya *mfumo* wa amri na *kiini* (m.y., maana, hoja, "ukamili," au kanuni inayosimamia amri). "Itokeapo tuna wasiwasi kama kitu fulani kinahusika na tamaduni au ni cha lazima ki-utimilifu, ni bora kukiingiza kwenye ile dhana pana ya ujumbe wa Biblia " (Wolvaardt 2005: 300). Ili kufanya hivyo, kunatuhitaji tuwe na ufahamu wa kutosha wa simulizi ya Bibilia kiujumla, na yale yapasikayo, mafundisho, na mifano inayoiunda. "Kadiri uelewa wa mtu kuhusu ujumbe wa Biblia unavyokuwa mpana zaidi, ndivyo itakavyokuwa rahisi zaidi kwa mtu kutofautisha kati ya yale ya ukamili

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

na na yale yasiyo ya ulazima sana" (Ibid.: 28). Mara nyingi (lakini kwa vyovyote si zote) yote mawili - mfumo wa amri na kanuni inayoisimamia huweza kueleweka, na inaweza kutumika sawasawa na ilivyoelezwa, hasa kwa maagizo ya Agano Jipya. Hata hivyo, lazima tuwe waangalifu "kutokuzidisha" ile amri, kanuni, qau matumizi yake. (C) *Igundue hali inayofanana nayo kwa leo.* Hii inatuhitaji tuwe wakweli katika kutafsiri tamaduni zetu. Kufanya haya tunapaswa kujua tofauti muhimu zinazotofautisha kati ya watu wa wakati ule na waumini wa sasa. Tunapawsa kufikiri kiundani *kwa nini* hali fulani ya sasa inafanana na ile ya Biblia. Sheria zote za Agano la Kale, amri, na sheria, na maagizo mengine muhimu mengi katika Agano Jipya za, *hutumikwa kwa mrandano, kama zitatumiwa.* Kutumika kwake kwafaa tu ikiwa hali iliyopo inafanana kabisa na ile iliyomo kwenye Biblia (m.y; yanafanana kwa kiwango kikubwa). (D) *Pendekeza matumizi yenye kufaa ambayoni sehemu ya ile kanuni mama.* Katika kutekeleza, twaweza kihalali kabisa: 1. Kupanua amri za Biblia. Kwa mfano, kutotamani punda wa jirani yako (**Kut 20:17**) utekelezaji wake ni mpana (m.f., usitamani gari la jirani yako ). 2. Kubadili amri za Biblia anbazo zimewekwa kwenye misingi ya mazingira ya tamaduni tofauti-tofauti. Kwa mfano, badala ya kusalimiana kwa "busu takatifu" (**Rum 16:16**), kushikana mikono ya dhati au kukumbatia kwaweza kutumiwa. 3. Weka mipaka ya amri za Biblia. Kwa mfano, badala ya kunywa mvinyo kidodo kwa ajili ya ugonjwa wa tumbo (**1 Tim 5:23**) tunaweza kutumia dawa ya kuponya Tindikali au maji ya chupa au vinywaji vingine vilivyopo. 4. Hata kugeuza amri za Ki-Biblia ikiwa utekelezaji "kimatendo" wa agizo hilo kutakuwa kinyume cha sababu au kanuni nyuma yake. Kwa mfano, katika **1 Tim 5:3-16** mjane wa zaidi ya miaka sitini asiye na au wajukuu, ingawaje kimsingi ni kupishana na maagizo ya Paulo, anaweza asisaidiwe ikiwa atapokea urithi, akawa na pensheni, au atapokea msaada wa Serikali (mambo ambayo hata moja Paulo hakulitaja). Kwa upande mwingine, mjane kijana zaidi mwenye watoto anaweza kusaidiwa vizuri ikiwa watoto wake hawawezi kumtegemeza (wanweza kuwa bado wadogo mno, au familia yake inaweza kuwa imemtenga, kwa mfano, ikiwa amehamia Ukristo kutoka Uislamu, ikiwa matarajio mema ya ndoa, (kwa mfano, kama ana HIV/AIDS), au kwa sababu nyingine. (E) *Linganisha matumizi yetu yaliyopendekezwa, kwa Maandiko mengine, hasa katika mafundisho ya Agano Jipya.* Ikama matumizi yetu yanaelekeana na vifungu vingi vya Biblia, tunapata ujasiri katika hilo. Tunapaswa kuwa na tahadhari tunapokutana na agizo ambalo linaonekana kuwa pembeni kabisa na hali yoyote ya siku za leo. Mifano ya Biblia inaweza kuthibitisha, au kutokuthibitisha, utekelezaji tunaoutarajia.

4. Muktadha wa kihistoria au wa tamaduni katika **2:9-10** na aya sambamba yake zaonyesha kwamba *mitazamo* ya maelezo ya Paulo kuhusu kusuka nywele na mavazi ni ya utamaduni ulei, lakini kanuni ya kujisitiri kwa ujumla yahusu tamaduni zote. Blomberg aweka bayana, "Hii 'lugha ya mavazi' ni ishara kuonyesha jinsi wanawake matajiri wa Efeso walivyokuwa walengwa wa msingi wa agizo hili. Wao pekee ndio waliokuwa na uwezo wa kusuka nywele kama ilivyoelezwa. Kwa kweli, tafsiri ya Kiyunani inasomeka wazi zaidi, si kwa kusuka nywele '*na dhahabu au lulu* …' Hakukuwa na tatizo lolote baya kuhusu kusuka nywele zenyewe, lakini mapambo ya mtindo ambayo yalihusisha kufumia vito vya thamani katika nywele za mwanamke, kama njia mojawapo ya kushikiza nywele, kulihitaji masaa mengi kwa ajili ya mwonekano wa nje tu, na mara nyingi kulihitaji gharama sana." (Blomberg 1999: 207) Earle anaongeza, "Kwa ubaya zaidi, hivi ndivyo makahaba walivyofanya. Kwa kiwango cha juu zaidi, huonyesha kiburi na kuji-ona, hayo yote ni kinyume cha mapenzi ya Roho wa Kristo." (Earle 1978: 361) Zaidi, **2:9-10** kimsingi panaendana na **1 Pet 3:3-4**, Amapo pana sema mwanamke *"kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje—yaani kusuka nywele, na kujitia dhahabu na kuvalia mavazi, bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mambo yasiyoharibika yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu."* Andiko la Kiyunani "halionyeshi neno la kiutendaji la kurekebisha *uvaaji* (*thamani*) na andishi kimsingi lasema, 'Kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje yaani kusuka nywele, kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi.' Kwa hiyo ni makosa, kutumia andiko hili kuwakataza wanawake kusuka nywele au kuvalia vito vya thamani, au kuvaa mavazi; kwani kwa sababu hizo hizo ingebidi kukataza "kuvaa nguo". Hoja ya Paulo si kukataza lolote kati ya hayo, bali kujipamba kwa mwanamke kusiwe ndiyo "Chanzo cha uzuri," (Grudem 1988: 140) na kwamba **1 Kor 11:5-6** panazungumzia kuhusu mwanamke kufunika kichwa kwa sababu kutokufunika kichwa chake*"kunaabisha kichwa chake"* na kumfanya sawa na *"mwanamke ambaye kichwa chake kimenyolewa,"* na kwamba *"ni aibu kwa mwanamke kuwa na nywele zilizonyolewa.au kukatwa"* Katika tamaduni au desturi nyakati za Paulo, mwanamke aliyepatikana na uzinzi alipaswa kunyolewa nywele na kushushwa hadhi kijamii na kuwekwa daraja la kahaba (Winter 2001: 128). Katika desturi nyingi leo, hilo halifanyiki. Kiukweli, katika nchi nyingi za Ki-Afrika wanawake wengi hunyoa nywele zao au hukata ziwe fupi. Hakuna unyanyapaa wowote katika hilo. Kama ilivyoonekana mwanzoni, Ukristo umeundika katika hali inayotekelezeka katika maelfu ya kila tamaduni ulimwenguni. Matokeo yake, kutajwa kwa maswala ya Ki-Biblia kama vile mavazi na mitindo ya nywele inaonyesha dhahiri kwamba mambo hayo yalikuwa kwa ajili ya mipaka ya tamaduni fulani (kwa vile staili za mavazi zimetofautiana sana ulimwenguni, na hata aina za nywele zenyewe zinatofautiana sana kati ya jamii za

watu tofauti). Hata hivyo, kanuni pana zaidi ya ustahiki wa mavazi, na kutochochea zinaa au mali, unahusu tamaduni zote—lakini mfumo wa kuvaa, mitindo ya nywele, na tabia zinayokubalika, hutofautiana kati ya tamaduni moja na nyingine.

***Mwanamke na ajifunze katika utulivu akitii kwa kila namna. Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu. Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa wa kwanza, na hawa baadaye, wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa, akaingia katika hali ya kukosa:***

1. Vifungu hivi vimeleta mabishano makubwa miongoni mwa wasomi wa Biblia kuhusu mipaka ya utekelezaji wake kanuni zake kitamaduni, au kati ya tamaduni nyingi. Wote wanakubaliana kwamba *"mwanamke kujifunza katika kutii"* na *"kuwa mtulivu"* hakuwezi kumaanisha awe kimya kabisa, kwa sababu sehemu nyingine katika Biblia panasema kuhusu wanawake kuomba na kutabiri katika kanisa (ona **Mdo 21:9; 1 Kor 11:5**). Moja ya ishara ya kujazwa na Roho Mtakatifu (ambayo inafanya kazi kwa wanaume na wanawake—ona **Mdo 2:17-18**) ni *"Mkisemezana kwa Zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni"* (**Efe 5:18-19**). Vifungu hivi vinaibua maswali yenye tafsiri nyingi. Ngewa ametaja mambo mengi katika haya: "Je hili linatendeka? [m.y., Msemo wa Paulo kusema *'simpi mwanmke ruhusa ya kufundisha'*] hufanyika katika ufalme wa Mungu wakati wote? Kitenzi chenyewe kipo katika wakati uliopo, ambacho kinaweza kutumika kuonyesha kweli ya kila mahali, au panaweza kutafsiriwa 'Sitoi ruhusa', kuonyesha kwamba uamuzi ule ulihusika tu na mazingira yaliyokuwako katika kanisa la Efeso kwa wakati ule. Pia kuna mjadala kuhusu kile ambacho Paulo alimaanisha alimpozungumzia kuhusu 'mwanamke'. Je inawezekana alimaanisha mwanamke mmoja tu aliyekuwa anamtawala mwanamume wakati ule? Au anatumia mfumo wa kujumuisha, ili kwamba 'mwanamke' awawakilishe wanawake wote? Kama ndivyo, ni wanawake wote wa Efeso waliokuwa wameharibiwa na walimu wa uongo? Au wanawake wote wa Efeso? Au wanawake wote Wakristo wa wakati ule? Au wanawake Wakristo wa karne zote? Tufanye tunaweza kutatua tatizo hilo linalowahusu wanawake, bado tunakabiliwa na tatizo lingine. Ni akina nani ambao wanawake walikuwa hawarusiwa kuwafundisha? Je ni kila mtu kabisa, wanume kwa ujumla, waume zao, au waangalizi? . . .Mara tunapotatua tatizo la wale ambao wanawake walikuwa hawaruhusiwi kuwafundisha, tunakuja kwenye tatizo la kujua nini walichokatazwa kufundisha. Miongoni mwake ni pamoja na kutokueneza mafundisho ya uongo, au kutokufundisha kweli ya Injili; ama kutokufundisha chochote kabisa, ikiwamo kweli ya Injili." (Ngewa 2009: 52-53) Hakuna mshangao, hivyo basi, hiki ni kifungu kigumu, hasa tukiwa na "uwanja mpana wa tamaduni" za mbali" kati ya tamaduni zilizopo sasa na hali iliyokuwapo katika Efeso ya kale (ambayo tunaielewa kidogo sana).

2. Jambo la msingi lililoibuliwa na mistari hii ni kuhusu kiwango ambacho wanawake wanaweza kihalali *"kufundisha au kuwa na mamlaka juu ya mwanume ."* Kila mahali wanawake wana majukumu mengi ya huduma katika kanisa: wanfundisha wanawake wenzao; wanafundisha watoto katika shule ya Jumapili; hutoa huduma kwa wanaume na wanawake katika nafasi tofauti. "Swala la msingi" ni je wnawake wana uhalali wa kuwekewa mikono ili wawe na mamlaka sawasawa juu ya wanaume kama mchungaji mkuu au askofu. Kitabu kimojawapo amabacho kina maelezo ya kina yaliyotolewa na waandishi wa pande zote mbili- wakiume na wakike kuhusu swala hili ni James Beck and Craig Blomberg, ed., *Two Views on Women in Ministry* (Grand Rapids, Mich.: Zondervan, 2001). Madhehebu mbali mbali yana mitazamo tofauti kuhusu jambo hili, na utofauti ndani ya madhehebu upo pia. Zaidi, aya nyingi sana, kote-kote katika Agano la Kale na Jipya, zinagusa swala hili, na zinaipaswa kusaidia kutoa jibu la kueleweka la swali hili. Pasipo kujaribu kumaliza wala kuongeza tafsiri, vifuatavyo ni baadhi ya vidokezo vya utata mkuu, na majibi ya utata huo mkuu, kwa pande mbili:

| **Wanawake wanaweza kutumika katika nafasi zote** | | **Wanawake wasiwe na mamlaka kuu** |
|---|---|---|
| *Hoja:* **Gal 3:28** inajenga kanuni za msingi wa Kibiblia kwamba katika Kristo hakuna tena tofauti za kijinsia (au za kikabila, au nyinginezo). | ==> | *Majibu:* Ni kweli tuna usawa katika Kristo, lakini hiyo haiondoi tofauti za kimajukumu (m.f; huwa ni mwanamke pekee anayeweza kuzaa watoto, bali waume bado wana thamani). |
| | | ↓ |
| *Majibu:* Sehemu nyingine (**Warumi 5**) Paulo aweka wazi kuwa Adamu, siyo Hawa, ndiye aliyesababisha anguko la mwanadamu. Hawa hakupokea maagizo moja kwa moja kutoka kwa Mungu, kwa hiyo (kama ilivyokuwa kwa wanawake walio wengi nyakati za Paulo), hakuwa na "uelewa" ule ule aliokuwa nao Adamu. Kwa sasa, wanawake wanaweza kuelimishwa vile vile. Kila mahali katika Biblia, hali ya uzaliwa wa kwanza inageuzwa. Neno hapa la Kiyunani la "mamlaka" ni neno adimu linalomaanisha ukali au | <== | *Hoja:* Paulo anakazia hoja yake kuhusu majukumu ya wanawake kwa utaratibu wa kiuumbaji na anguko, kuonyesha kwamba hii ni hali ya ulimwengu mzima tofauti na kulenga tatizo maalum lililokuwepo kanisa la Efeso. Pia, ingawa wanaume walikuwa wanahusika na kufundisha hayo mafundisho ya uongo pale Efeso (ona **1 Tim 1:19-20**) Paulo hawakatazi waume kufundisha wala kuwa na mamlaka, bali wanawake tu. |

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

| | | |
|---|---|---|
| kutawala, siyo mamlaka yapendezayo. Hii ilikuwa ni shauku yake Paulo binafsi kwa kanisa la Efeso, na siyo kwa makanisa yote wakati wote. | | |

↓

| | | |
|---|---|---|
| *Hoja:* Biblia inayo mifano mingi ya wanawake Waliokuwa na madaraka ya juu kabisa ya uongozi: k.m, Debora (**Waamuzi 4**— alikuwa nabii na Mwamuzi wa Israeli); manabii wa kike wa Agano jipya katika kanisa (**Mdo 21:9; 1 Kor 11:5**); Prisila (mwanamke) alimfundisha mwanaume (Apolo) (**Mdo 18:24-26**); Yunia (mwanamke) anaitwa "mtume" (**Rum 16:7**). | ==> | *Majibu:* Haiwezekani kupuuzwa kuwa wanawake wanaweza kufanya mambo mengi muhimu katika kanisa. Hata hivyo, hakuna mifano ya wanawake kuwa wachungaji wakuu, au maaskofu katika Biblia. Prisila alimfundisha Apolo; lakini alifanya kwa siri nyumbani kwake na mumewe, siyo hadharani katika madhabahu. Angalau kuna ushahidi kuwa Yunia anaweza kuwa ndiye "Yunia" (jina la kiume). |

↓

| | | |
|---|---|---|
| *Majibu:* Paulo anatumia jinsia ya kiume katika **1 Tim 3:2** kwa sababu wazee wengi wa kanisa. Hata hivyo, hilo haliwazuii wanawake kuwa wazee wa kanisa zaidi ya **1 Tim 5:3**, panapoliagiza kanisa kuwasaidia wajane, na panalikataza kanisa kuwasaidia wenye wajane au wengine wenye uhitaji. | <== | *Hoja:* Katika **1 Tim 3:2** sifa mojawapo inayotakiwa ili kuwa mzee wa kanisa, ni "kuwa mume wa mke moja" (m.y; kuwa mwanaume). Pia, Mitume wa Kristo na kwa wote wale walio viongozi wa mfano katika Biblia ni wanaume. |

3. Aya hii inaonyesha umuhimu wa kutofautisha kati ya maswala ya kimsingi, na ya ziada, na mambo ambayo mwanadamu ameyatengeneza. "Mambo ya msingi ni yale yanayojikita katika imani, na ambayo Wakristo wote wanapaswa kukubaliana nayo: Biblia ni Neno la Mungu; Mungu yuko katika Utatu; Wanadamu wamepotea katika anguko la dhambi na hawawezi kujiokoa wenyewe; Yesu ni Mungu kamili na mwanadamu kamili; Kristo ni njia pekee ya wokovu; tunaokolewa tu kwa neema ya Mungu kupitia imani katika Kristo; tumeitwa ili kuishi maisha ya upendo. "Yale ya ziada" ni mambo ambayo Biblia inayasema, lakini si bayana kabisa. Mambo hayo ni kama vile: je watoto wanapaswa kubatizwa au wale tu ambao wanaweza kuikiri imani? Je uongozi wa kanisa unapaswa uweje? Je Kristo huwepo kwa njia maalumu wakati wa chakula cha Bwana au la? "Mambo yaliyotengenezwa na mwanadamu" ni yale ambayo hata Biblia haiyasemi kabisa, lakini watu wamekuja na maagizo fulani au mipangilio yao wenyewe. Mambo yaliyoyengenezwa na wanadamu ni kama vile: utaratibu wa ibada; uvaaji wa nguo maalumu; na aina ya shuguli fulani (m.f., muziki, filamu, vyakula na vinywaji) vinavyokubalika kwa Wakristo. Kutofautiana kwetu katika haya ya Pili, na mambo tuliyojitengenezea wenyewe hakudhuru wokovu wetu, na yasidhuru ushirika wetu. Kwa bahati mbaya, hata hivyo, matengano mengi kati ya madhehebu na miongoni mwa Wakristo yanatokana na yale ya ziada, na mambo tuliyojitengenezea wanadamu—m.y., mambo yale ambayo *si* ya muhimu kabisa. Swala la mwanamuke kuwekwa kwenye huduma ni swala la ziada. Kudumisha ukaribu wa uhusianao na waumini, kanisa, na madhehebu hakupaswi kutuathirika kwa vile wanatofautiana na mitazamo yetu kwa mamba haya. Kristo aliomba kwamba *"wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu nami ndani yako, hao nao wawe ndani yetu, ulimwengu upate kusadiki kwamba wewe ndiye uliyenituma"* (**Yoh 17:21**). Mengi yanatuunganisha kuliko yale yanayotugawanya. Tunapaswa kudumisha umoja kusimamia yale mambo ya ki- msingi, na kuwa na upendo kwa waumini wenzetu kuhusu mambo ya ziada na yaliyotengenezwa na wanadamu.

***Walakini ataokolewa kwa uzazi wake, kama wakidumu katika imani na upendo na utakaso pamoja na moyo wa kiasi:*** Hiki ni kimojawapo ya vifungu visivyo wazi na vigumu katika Agano Jipya. Tafsiri ya juu na NASB (ambayo ni moja ya tafsiri nzuri kutoka lugha ya Kiyunani) sio kamili hapa. Kiyunani panasomeka: *"Walakini ata [moja] okolewa kwa uzazi wake kama wata [uwingi] wakidumu katika imani na upendo na utakaso pamoja na moyo wa kiasi."* Neno "okolewa" linaweza kuwa na maana ya wokovu wa kiroho (ndiyo maana halisi katika Agano Jipya) au kusalimisha kimwili (kwa mfano, kutoka kwenye dhoruba—**Mdo 27:20**). Hapa hapamaanishi kuokolewa kimwili wakati wa kuzaa mtoto, kwa sababu hiyo ingemaanisha kwamba kifo cha mwanamke yeyote wakati wa kuzaa kingetafsirika kuwa ni kwa vile si mwamini (ambayo inaonyesha si kweli). Kuna mitazamo mikuu miwili kuhusu msemo *"Kuokolewa kwa uzazi wake"*: (A) *"Sehemu ya kuzaliwa kwa Masiha":* Mtazamo huu unachukuliwa kama ni hatua ya kuanzia **2:14** ambao unazungumzia kuhusu "mwanamke" aliyeangukia kwenye dhambi. Inadumisha hoja hiyo kwamba **2:15** ni hakika kwamba dhambi ya Hawa haikuwa ya kumuua yeye au wala wanawake wote. Kwa hiyo, **2:15** Kisanifu ianazia pale **2:14** ilipoachia, kwa kusema "*a* taokolewa," na kuendeleza ahadi iliyotolewa kwa Hawa katika **Mwa 3:15** kwamba wokovu utakuja kupitia *"uzao wako."* Hii ilitokea wakati Mariamu alipomzaa Yesu. Mtazamo huu unasisitiza kwamba Paulo angeweza kutumia kitenzi cha kuzaa kama angekuwa anataka kuzungumzia kuhusu wanawake kuzaa watoto. Lakini

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

hakufanya hivyo. Badala yake alitumia nomino isiyo ya kawaida "uzao" Zaidi ya hayo, anatumia neno ("u") katika neno "kuzaa" ambalo inaonyesha uzazi maalum (m.y., Masiha) ndiko kunakolengwa. Kwa upande mwingine katika **5:14** alipotaka kusema kwamba wanawake vijana wajane katika kanisa waolewe na kupata watoto hakutumia neno la kitendo (kitenzi, neno alilotumia katika **2:15**). Msemo wa masharti (*"kama watadumu . . ."*) Unahama kutoka kwa Hawa kwenda kwa wanawake wote kwa jumla (au waonyesha Hawa kama mwakilishi wa wanawake wote "katika kukosa" [**2:14**] kuonyesha wokovu ulivyokuja kutokana na kuzaliwa kwa Masiha unafanyika kwa wanawake kwa kupitia imani (kama unavyothibitishwa kwa maisha ya utauwa).

(B) *"Wanawake katika nafasi kama wazaaji watoto":* Mtazamo huu unatokana na mjadala alioanza nao Paulo katika **2:11-12**. Kulingana na hilo, **2:15** maana yake wanawake wasijaribu kunyang'anya kazi za wanaume kama walimu na wenye mamlaka. Badala yake, wanawake wanapaswa kukubali na kufurahia jukumu lao kama Mungu alivyowaumba na kuwapangia, ambayo ni kuzaa watoto. Mchepuo wa Ngewa ni wa muhimu katika hili. Anatambua kwamba ni ujinga kusema kuna "kuokolewa" milele kupitia "kupokea majukumu." Hivyo basi, anakubaliana na tafsiri ya NASB "kuhifadhi," na anasema **2:15** maana yake: "Kama wanawake watabakia katika jukumu lao la kuzaa watoto na chngamoto zinazoendana na hilo, wataweza kuepuka [m.y., watakingwa na] matatizo yaliyowakumba wanwake wengine huko Efeso. Lakini kazi peke yake haikuhakikishii kukwepa matatizo. Kunapaswa kwenda mkono kwa mkono na maamuzi ya kutendea kazi mambo ya "imani na upendo na utakaso pamoja na moyo wa kiasi": (Biblia ya NASB). Paulo anafundisha wanawake wa Efeso namna ya kukaa mbali na matatizo kwa kufanya shughuli na kuishi maisha ya Kikristo." (Ngewa 2009: 56) Hawa "wanawake kama wazaaji wa watoto" hutazama matatizo kuwa sawa na neno lililotumika la "uzazi wao" katika **2:15** na **5:14** (yanapatana: m.y., moja liko katika mfumo wa jina na jingine katika kitenzi yakiwa ni neno hilo hilo la msingi). Pia yanakazia kwamba Paulo anaonekana kukazia hoja ile ile ya **5:12-15** kama afanyavyo hapa: m.y., kwa kuolewa na kuzaa watoto, wanawake wataepuka matatizo, dhambi na kumfuata Shetani.

**<u>1 Tim 3:1-13—Sifa za kuwa Kiongozi wa Kanisa</u>**

**<u>3:1-7:</u>** ***[1]Ni neno la kuaminiwa: mtu akitaka kazi ya uaskofu, atamani kazi njema. [2]Basi imempasa askofu, awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi, na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, ajuaye kufundisha, [3]si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu, bali awe mpole, si mtu wa kujadiliana wala asiwe mwenye kupenda fedha. [4]Mwenye kusimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu [5](yaani mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje kanisa la Mungu?), [6]wala asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi. [7]Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje, ili asianguke katika lawama na mtego wa Ibilisi.***

Kanisa ni mwili unaoshirikiana, sio mkusanyiko tu wa watu. Hivyo basi linapaswa kuwa na muundo fulani ili kufanya kazi vizuri na kutimiza wito. Kanisa la kwanza lilikuwa na ngazi mbili za uongozi: ngazi ya juu, ilijulikana kama wazee au waangalizi; na ngazi ya pili, ilijulikana kama mashemasi (ona **Fil 1:1**). Shirika lolote linakuwa zuri, imara na la kufanikiwa kama ulivyo uongozi wake. Hivyo basi Paulo anarudi kwenye sifa za viongozi katika kanisa.

***Mtu akitamani kazi ya uaskofu atamani, kazi njema:*** Neno la Kiyunani la "mwangalizi" ni *episkopos* ambalo wakati mwingine limetafsiriwa kama "askofu." Ni sawa tu, na mara nyingine linabadilishwa kwa neno, *presbuteros* ("mzee") (ona **Mdo 20:17, 28; Tit 1:5, 7**). Kimsingi, kinachonenwa hapo ndio ngazi ya juu ya uongozi katika kanisa, haijalishi wanaitwa wachungaji, askofu, waangalizi, au wazee. Hawa ndio watu wanaotengeneza sera na kujihusisha na huduma ya neno (kuhubiri, kufundisha, kushauri, uinjilisti, kuadibisha nk.). Sifa ni zile zile zinahitajika kwa wale walio katika nafasi ya uongozi katika makanisa yote. "Ni muhimu kuona kwamba hapa katika 1 Timotheo 3:1 Paulo anaeleza kuwa mwangalizi kama utendaji ('kazi ya utumishi'), siyo umaarufu au ofisi. Hawatii moyo watu kuangalia umashuhuri, bali uwajibikaji." (Liefeld 1999: 116)

***Askofu, ndipo, anapaswa:*** Paulo anataja mahitaji 15 ya kuwa kiongozi wa ngazi ya juu ya uongozi wa kanisa. Mambo mawili lazima yatazamwe. Kwanza, Paulo hasemi ili mtu awe katika uongozi, anapaswa kutimiza moja, au matano, au hata mengi ya masharti haya yanayohitajika. Badala yake, kuwa kiongozi katika kanisa, mtu anapaswa kutimiza masharti yote. Cha kushangaza katika masharti ni kwamba (ukiachia uwezo wa mtu kufundisha na asiwe ameokoka hivi karibuni), zote ni sifa ambazo *kila Mkristo* anapaswa kuwa nazo. Hakuna sifa maalumu kuhusu kiwango cha elimu ya mtu, mali alizo nazo, au mambo mengine" yanayoonekana kwa nje". Badala yake, hizi sifa zote huhusika na "*tabia*" ya mtu. La kushangaza, katika **1:9-10** Paulo ametaja

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

mifano 15 ya watu wasio haki ambao walitiishwa na sheria. Hapa Paulo anasema tabia yetu kama viongozi zinapaswa kuwa *kinyume* na aina ya watu hawa ambao lazima watiishwe na sheria, kwa sababu *hatuko tena chini ya* sheria ya zamani. Badala yake, tunapaswa kuwa na tabia ya Kristo, kwa sababu tunaongozwa na "sheria ya Kristo." Mwenendo wetu ububujike kutokana na tabia zetu. Kama vile tabia zetu zinavyo kinyume kabisa na wasio haki, basi mienendo yetu inapaswa kuwa kinyume na ile orodha iliyotajwa katika **1:9-10**. Sifa za nafasi ya ushemasi (**3:8-13**) kimsingi yanaendana na yale yaliyo katika nafasi za uaskofu. Watu walio katika nafasi za uongozi katika kanisa wanaonekana sana maana ni wawakilishi wa Kristo kwenye mikusanyiko na kwa wasio waumini katika jamii. Hivyo basi, ni muhimu wawe na tabia ya Kristo na kumuiga kiuthabiti kwa namna wanavyoishi.

***Asiyelaumika:*** Sifa ile-ile inatakiwa kwa mashemansi (**3:10;** ona pia **5:7; 6:14**). Neno kwa ajili ya "Asiyelaumika" maana ya msingi ni kwamba mtu asiwe na sababu ya kushitakiwa au kulaumiwa kwa kufanya mabaya. Hii inaonyesha kwamba mtu ni msafi ndani na nje. Wazo ni sawa na lile la maneno ya Yohana yasemayo "kuenenda katika nuru" (**1 Yoh 1:5-7**). Moja ya eneo la nuru ni uwazi: hakuna kilichofichika ndani ya nuru; yote yako wazi. Vivyo hivyo, mtu ambaye "asiyelaumika " hana dhambi iliyofichika. Ndani yake na tabia yake ya nje ni wazi kwa wote.

***Mume wa mke mmoja:*** 1. Hitaji hili halina maana kwamba mtu *anatakiwa* aoe ili awe askofu. Pia Yesu wala Paulo hawakuwa wameoa, na wote bila shaka walikuwa na sifa za kuwa waangalizi /askofu katika kanisa. Ingawa, kama mtu ameoa, anapaswa kuwa na mke mmoja tu, sio wa wake wengi. Mwenye wake wengi anaweza kuwa mkristo, na anaweza kufanya shughuli nyingi za muhimu katika kanisa (ingawa hapaswi kuwa tena na wake wengine baada ya kuwa Mkristo). Viongozi wa kanisa, hata hivyo, wawe kielelezo cha wazo la Mungu. Wazo la Mungu kuhusu ndoa ni mke mmoja (ona **Mwa 2:18-24; Mat 19:3-6**). Ndoa ni picha ya ushirika kati ya Kristo na bibi harusi wake, kanisa (**Efe 5:25-32; Ufu 19:7-8**). Kristo ana bibi harusi mmoja tu na ni mwaminifu kwake. Viongozi wa kanisa ambao wameoa wanapaswa kuwa hivyo.

2. Maneno halisi ya aya ya Kiyunanii hapa ni "mume wa mke mmoja." Maneno Hayo-hayo yametumika kwa mashemasi (**3:12;** ona pia **5:9** ["mke wa mume mmoja"]). Hii inaonyesha kwamba mwanaume anapaswa kuwa mwaminifu kwa mke wake "kwa ndani na kwa nje." Kwa maneno mengine, siyo tu kwamba asifanye uzinzi kwa kulala na wanawake wengine, bali asifanye *uzinzi* katika moyo wake kwa kuwangalia kiuzinifu na kuwatamani "wanawake wengine" (ona **Mat 5:27-28**).

***Mwenye kiasi, na busara:*** Maneno haya yanafanana na yanabeba wazo la kuwa na akili ya utulivu: m.y., kuwa na akili ya njema; mwenye kupambanua; mwenye-kiasi. "Mwenye kiasi" hutumika pia kwa viongozi wanawake (**3:11;** ona pia **Tito 1:8; 2:2, 5**). Viongozi wanpaswa kutoa ushauri wa hekima kwa waumini wa kanisa. Hao waumini wa kanisa wanpaswa kujua kwamba viongozi ni waelewa, kwamba maamuzi yao hayashinikizwa na mawazo mabaya.

***Mstahivu:*** Neno kwa ajili ya "mstahivuu" ni neno lilelile lililotafsiriwa "kujisitiri" katika **2:9.** Maana ya msingi "mtstahivuu," na mara nyingine limetafsiriwa "mheshimiwa." Watu hutaka kuonyesha heshima kwa viongozi kwa sababu ya nafasi zao za mamlaka na uwajibikaji ambao viongozi wanao. Ingawa, viongozi wanapaswa kujihoji wenyewe: "Je *nastahili* kupata heshima ya watu?" na "Kama watu wangeona jinsi nilivyo sirini je bado wangeniheshimu?"

***Mkaribishaji:*** Kuwa "mkaribishaji" maana yake halisi unapenda au unajali watu au wageni (ona pia **Tito 1:8; 1 Pet 4:9**). Hili ni la muhimu, kwa sababu kiongozi anahitaji kujua watu wake vizuri. Kujua matatizo yao, matumaini, hofu zao, nk. hukusaidia kuwa mchungaji mzuri. Kujua nguvu zao, madhaifu yao, vipawa na uwezo wao, hukusaidia wewe kukuza viongozi wapya, ili kutumia viungo vyote ya mwili katika huduma. Hiyo inajenga na kuchochea kanisa zima. Hata hivyo, ukarimu unakuja kwa gharama fulani. Wachungaji wengi wanategemewa kutoa chakula na malazi kwa kila mtu anayekuja kwenye nyumba zao, lakini kanisa halimpatii mchungaji fedha au chanzo chochote ili kumsaidia mchungaji kwa ajili ya hili. Kama kanisa litategemea mchungaji kuwapa mahitaji watu wanaokuja kwake, basi kanisa linao wajibu wa kumuwezesha mchungaji kwa ajili ya swala hilo (ona **5:17-18**). Zaidi sana, kuwa mkaribishaji kwa watu wa aina zote (m.y., watu kutoka makabila tofauti, wenye uchumi tofauti, watu wenye HIV/AIDS) mchungaji anaweza kuwakwaza watu fulani wa kanisa. Hili ndilo lililomletea lawama Yesu: kwani alikuwa*"rafiki wa watoza ushuru na wenye dhambi"* (**Mat 11:19; Lk 7:34**). Hilo halikumzuia Yesu kuonyesha upendo na huruma kwa watu wa aina zote. Vivyo hivyo, Haipaswi viongozi wa kanisa kuacha kuonyesha ukarimu kwa watu wa aina zote.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

***Ajuaye kufundisha:*** Hii ni tofauti yenyewe kati ya sifa za kuwa mwangalizi/askofu na shemasi. Mashemasi wanaweza kuwa na uwezo wa kufundisha (Stefano—**Mdo 6:8-7:60;** Philipo—**Mdo 8:4-6, 26-40**), lakini si hitaji la lazima kwa nafasi zao. Kuna njia nyingi ambazo mtu anaweza kufundisha: kutoka kwenye mimbali siku za Jumapili au siku za katikati ya wiki; kuongoza shule ya Jumapili au elimu ya darasa la watu wazima; kwa kuongoza usomaji wa Biblia nyumbani au kwenye ushirika wa vikundi vya seli. Waangalizi wote wanapaswa kufanyia mazoezi uwezo wao kwa njia fulani.

***Si mtu wa kuzoelea ulevi:*** Swala hapa linaonyesha mtu ambaye "ametawaliwa na " au "amezoelea"mvinyo, au mlevi. Ni sifa ileile inatakiwa kwa mashemasi (**3:8;** ona pia **Tito 1:7**). Nyakati za Paulo ilikuwa ni desturi kunywa mvinyo. Maeneo mengi katika ulimwengu (m.f., kanisa la Afrika) halina tamaduni za kunywa mvinyo**.** Kanuni ya "kutozoelea" au kutotumia kilevi"bado inatumika, hata kama kiongozi hanywi aina yoyote ya pombe au vinywaji kwa ujumla. Kwa bahati mbaya, hata hivyo, watu wengi ndani ya kanisa wanakazia swala la unywaji wa pombe, bila kujali kanuni yenyewe inayohusika. Hivyo viongozi wengi wa kanisa hawawezi kunywa pombe, lakini ni walevi wa vitu vingine kama kutumia nguvu, udanganyifu na utumiaji mbaya wa madaraka, nk. mambo hayo yanaharibu zaidi watu kuliko kunywa mvinyo. Viongozi wa kanisa hawapaswi kutumia chochote, haijalishi ni kitu kama mvinyo au kitu ambacho hakionekani kwa macho kama nguvu, huwatawala.

***Si mpiga watu, bali awe mpole, mpenda amani:*** "Si mpiga watu maana yake ni "ugomvi," ama "vurugu" mtu "anayewatishia" wengine. Mtu anaweza kuwa wa vurugu kwa namna nyingi zaidi ya ngumi - m.y, kwa kauli ya ulimi, ama hata namna anavyowaangalia wengine. "Upole" ni kiyume chake. Watu wengi wanafikiri vibaya kwamba, "upole" ni sawa na kuwa "mdhaifu." Hakuna lililo karibu na ukweli. Yesu alikuwa *"mpole na mnyenyekevu wa moyo"* (**Mat 11:29**), lakini hakuwa mtu dhaifu. Upole huchukua taswira ya nguvu. Yesu alionyesha nguvu za upole wake alipokabiliwa vibaya na washitaki wake kwa kutowavurumisha (ona **Mat 26:57-63; 27:11-14**). "kupenda amani" huonyesha mtu "wa ujeuri" na "asiye mgomvi" (ona **Tito 3:2**). Viongozi wanapaswa kuwa wajenga maridhiano, na wala siyo wanaochochea kutokuelewana. Wanapaswa kutafuta nia ya Kristo na kwa kuongozwa na Roho, ambako kutaleta umoja, badala ya kila mara kusisitizia wanayotaka wao tu.

***Kutokupenda fedha:*** Ni kigezo kingine kwa mashemasi (**3:8**; ona pia **Tito 1:7**). Kutokupenda fedha ni sifa mojawapo iliyoainishwa (ona **Ebr 13:5**). Hii ni muhimu kiasi kwamba Paulo anaonya kwa urefu kuhusu hatari za kupenda fedha katika **6:6-11.** Kusema kweli, Yesu anaasa kuwa kutamani mali huenda ndiyo hatari kubwa zaidi kwa hali ya kiroho ya mtu (ona **Mat 6:19-24; Mk 10:17-25; Lk 12:13-34; 16:1-13**). Swala hapa siyo kiasi cha uwingi au udogo wa fedha alizo nacho mtu. Swala ni kwamba: mtu anaweka tumaini lake kwa nani au wapi? Nini kitu muhimu zaidi kwa mtu? Mtu anafikiria nini, anatamani nini, na tumaini lake ni nini, na ndoto zake zipi? Nani au nini kinatuhamasisha? Kwa kitu gani tunapima mafanikio yetu?

***Mtu ajuaye kuisimamia vema nyumba yake:*** Ni kigezo kingine kwa mashemasi (**3:12**). Paulo anavuta hisia za uliganisho kati ya familia ya kaya moja, na familia ya Mungu. Sababu ni kwamba, Kanisa siyo shirika la kibiashara au serikali; ni familia. Tumeingizwa katika familia ya Mungu (**Rum 8:15, 23; 9:4; Gal 4:5; Efe 1:5**). Katika **3:15** analiita kanisa nyumba au familia ya Mungu. Anasisitiza hoja hiyo tena katika **5:1-2**. Kwa hiyo familia zetu wenyewe ni mahali pa kupimwa kuonyesha uwezo wetu wa kusimamia familia ya Mungu. Swala la utii wa watoto (ona **3:4)** siyo tu utii na kuonyesha heshima kwa nje. Swa ni *kwa nini* watoto wetu wana matendo waliyo nayo. Je wana utii na kuonyesha heshima kwa sababu ya upendo na heshima kwa wazazi, au ni sababu ya hofu? Swala ni ikiwa tunasimamia "vyema" au hapana.

***Asiwe mtu aliyeongoka karibuni:*** Ni kigezo kingine kwa mashemasi (*"nao wajaribiwe kwanza"*—**3:10**). Paulo anasisitiza jambo hilo hilo katika **5:22** anaposema, *"Usimuwekee mtu mikono kwa haraka, wala usizishiriki dhambi za watu wengine."* Hoja ni kwamba, kwa "kuweka mikono" juu ya mtu (m.y, kumsimika mtu katika nafasi ya uzee wa kanisa) unadhamini tabia yake na sifa alizo nazo. Sababu ya Paulo kuyaeleza haya katika **3:6** kuhusu kutomfanya aliyeongoka karibuni kuwa mwangalizi, ni swala la tabia ya mtu, anaweza *"akaanguka"* ikiwa atainuliwa nafasi ya juu mapema mno. Kwa hiyo ni lazima kumfahamu mtu vizuri. Mpe madaraka kidogo na umwangalie kama ni mwaminifu kwa hayo. *"Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana, huwa mwaminifu katika lililo kubwa pia."*—**Lk 16:10**). Ikiwa ni mwaminifu basi mpe mamlaka makubwa zaidi. Kimfanyacho mtu "mwongofu mpya" hutofautiana kutokana na mazingira. Paulo hasemi ni muda gani mtu anatakiwa kuwa mwamini kabla hajawa mwangalizi. Siku za akina Paulo, waamini wote walipokuwa waamini wapya, wazee ambao Paulo na Timotheo waliwachagua huenda walikuwa waamini kwa majuma machache tu

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

au miezi. Hata hivyo, wale waliopewa nafasi za uongozi, walikuwa waamini wamepevuka walio waaminifu, wenye tabia njema na wacha Mungu.

***Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje:*** Kanisa haliwi tu lenyewe. Liko ili liwe *"chumvi ya dunia,"* na *"nuru ya ulimwengu"* (**Mat 5:13-16**). Kanisa liko *"ulimwenguni"* ingawaje sio la *"ulimwengu"* (**Yoh 17:11, 15-16**). Kwa hiyo sifa yetu kwa wasioamini duniani ni ya muhimu sana. Wanachokiona kwetu ama kitawavuta waje kwa Kristo, au kuwaondosha mbali na Kristo. Paulo anamalizia maelezo ya sifa za vigezo vinazotakiwa kama alivyoanza ujumbe wake, kwa kuzungumzia viongozi wa kanisa kutojiingiza ama kuanguka kwenye "kutoaminika. Vigezo vyote 15 vya kiongozi vinahusu tabia zetu, moja kwa moja au kinamna fulani. Iwapo makanisa yangefuata vigezo hivi kwa dhati katika kuchagua viongozi wake, badala ya kutumia vigezo vya kidunia, makanisa huenda yangeonekana tofauti na kutenda kwa namna tofauti, na jinsi yanavyoonekana na kutenda hivi leo. Pia yangekuwa yana nguvu zaidi katika kuwaleta watu kwa Kristo na kuwabadilisha waamini wamfananie Kristo, kwa sababu yangekuwa ndiyo makanisa ambayo Mungu anataka kuyaona.

**<u>3:8-13:</u>** ***[8]Vivyo hivyo mashemasi na wawe wastahivu; si wenye kauli mbili, si watu wa kutumia mvinyo sana, si watu wanaotamani fedha ya aibu; [9]wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi. [10]Hawa pia na wajaribiwe kwanza; baadaye waitende kazi ya shemasi, wakiisha kuonekana kuwa hawana hatia. [11]Vivyo hivyo wake zao na wawe wastahivu; si wasingiziaji; watu wa kiasi, waaminifu katika mambo yote. [12]Mashemasi na wawe waume wa mke mmoja, wakiwasimamia watoto wao vizuri, na nyumba zao. [13]Kwa maana watendao vema kazi ya shemasi hujipatia daraja nzuri, na ujasiri mwingi katika imani iliyo katika Kristo Yesu.***

1. <u>Nafasi ya Mashemasi asili yake ni **Mdo 6:1-7.**</u> Kazi hasa hasa ya mashemasi ni kusaidia, kutumikia, na kuhudumia mahitaji ya kimwili kwa washirika wa kanisa. Neno "shemasi" ni neno la Kiyunani *"diakonos"* likiwa na maana ya wale wanaowatumikia wengine; wasaidizi, ni wasaidiaji wa wengine (ona Danker 2000: 230-31). Jukumu la shemasi ni jukumu muhimu sana la kiroho. "Ili kutekeleza malengo ya mashemasi wa kwanza, mambo matatu ni ya lazima: (1) Makanisa lazima yaazimie kwa makusudi kutafuta waume na wanawake wenye unyofu wa kiroho kama ilivyoelezwa katika 1 Timothy 3. (2) watu hao lazima wawe na maono, moyo na nia ya utumishi, wakiwa tayari wanaonyesha matendo ya wema hata kabla hawajachaguliwa. Wanapaswa *wawe* mashemasi kabla *hawajaitwa* mashemasi. (3) Kanisa lazima lichukulie huduma hii kwa umakini mkubwa kwa niaba ya mwili mzima. Lazima ionekane kwa jamii yote kwa ujumla, ili kwamba wanajamii siyo tu *wanufaike*, bali *waielewe* huduma ya upendo wa kanisa.." (Liefeld 1999: 138-39)

2. <u>Mengi kuhusu sifa za mashemasi tayari zimeshatajwa hapo juu kuhusiana na sifa za waangalizi.</u> Kusema kweli Paulo anatumia neno "Vivyo hivyo" mwanzoni mwa **3:8**, neno lilelile ambalo aliazia nalo **2:9**. Jambo hili huleta muktadha wa kigezo muhimu cha kuwa tabia nzuri na ya kumfanania Kristo ambayo waangalizi lazima wawe nayo, kama ambavyo mashemasi wanavyotakiwa kuwa nazo. Ijapokuwa Paulo anatumia maneno tofauti ya sifa za mashemasi na yale ya kwa waangalizi, vigezo vyote hulenga tabia ya wale walio katika nafasi ya mashemasi, kama inavyoonyeshwa hapo chini.

***Wastahivu:*** Neno pekee linalotajwa kote kwenye orodha za sifa za wazee (**3:4**), mashemasi (**3:8**), na wanawake (**3:11**) ni "usitahivu"au "kustahili" (kitenzi cha neno la kiyunani lililotumika katika **3:4**; na hali ya jina katika **3:8, 11**). Neno hilo hilo linatajwa tena mwishoni mwa **1 Tim 2:2**. Neno linamaanisha "tabia ama mwenendo unaoonyesha hali ya mtu kuwa ngazi ya juu kustahili *heshima maalum*." Kama viongozi wa kanisa wangekuwa na hizo sifa nyingine za kuwa maaskofu au mashemasi, bsi "wastahili heshima maalum."

***Si wenye kauli mbili:*** Kimsingi neno hili linamaanisha "mkweli"—kutosema hili kwa huyu na neno jingine kwa mtu mwingine. Uaminifu ni wa lazima kwa yeyote aliye mwamini, na hasa kwa mtu aliye katika nafasi ya uongozi katika kanisa.

***Wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi:*** *"Siri ya imani"* huzungumzia yale yaliofichika hapo awali na sasa yamefunuliwa: m.y., wokovu ni kwa kupitia neema ya Mungu peke yake kwa njia ya imani katika Kristo Yesu (ona **3:16; Rum 16:25-26**), na kwamba katika Kristo, wokovu hutolewa sawa kwa wote, Wayahudi na Mataifa pia. (ona **Efe 3:2-6; Kol 1:26-27**). Kwa umuhimu wa kipekee, hata kwa wale wanaosaidia na kuwahudumua wengine lazima wawe na ufahamu mzuri sana wa *"siri ya Imani"* yeyote kwenye uongozi wa kanisa lazima aweze kufahamu na kuamini vipengele muhimu kuhusu Ukristo ni nini. Hata kama "uwezo wa kufunndisha" si kigezo kwa kwa mashemasi, waamini wote wanatakiwa waweze "kuwaeleza watu juu ya

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

tumaini lililo ndani yenu" (**1 Pet 3:15**). Siri hiyo inapatikana tu katika "*siri ya imani*" kumhusu Yesu Kristo. Zaidi ya hayo, mashemasi (na wote walio katika uongozi wa kanisa) wanatakiwa kudumisha "*imani yenye dhamira safi.*" Hiyo ndiyo namna pekee ya kufikia lengo la upendo (ona **1:5, 19**). Kila aliye kwenye nafasi ya uongozi, awe mwangalizi ama shemasi, ni mfano kwa wengine, na anapaswa awaelekeze wengine kwenye lengo. Kwa hiyo, mashemasi wanatakiwa "kuishika" imani yao, ikimaanisha kuishi maisha yake kwayo huku akiielewa na kuiamini (kwa sababu mtu asipoishi sawa na hiyo imani, hilo litaonyesha haiamini).

***Vivyo hivyo wake zao na wawe wastahivu; si wasingiziaji; watu wa kiasi, waaminifu katika mambo yote:*** Neno la Kiyunani (*gynē*), hutafsiriwa kama "wake zao," laweza kumaanisha ama "mke wa" au "mwanamke". Wengine wameutazama mstari huu kuwa unawahusu wake za mashemasi (ingawaje hakuna maelezo linganifu kwa wake za maaskofu). Wengine wanauhusisha na wanawake mashemasi (m.y, mashemasi wa kike), kama vile Fibi, aitwaye "mhudumu au mtumishi" katika **Rum 16:1**. Katika **Rum 16:1** neno la Kiyunani litafsiriwalo "mhuduma au mtumishi" ni *diakonos,* ambalo ni sawa na neno "shemasi au mtumishi wa kanisa" katika **1 Tim 3:8, 12**, ijapokuwa neno hilo lina maana nyingi tofauti, na si lazima kumaanisha cheo cha ushemashi. Neno "vivyo hivyo" (lililotumika pia katika **2:9** na **3:8**) laonyesha uhusiano wa karibu kati ya mke wa **3:11** na mashemasi. Bila kujali kama wana cheo maalum au huduma yenye heshima ndani ya kanisa, kwa hakika wanawake wanaweza kuwa ni wa muhimu kwa majukumu fulani matokeo yake, vigezo vile vile vya tabia, uaminifu, and kutumainika, kama vilivyotumika kwa waangalizi na mashemasi wa kiume, vivyo hivyo hutenda kazi kwa wanawake.

**<u>1 Tim 3:14-4:16—Utauwa wa kweli Kinyume na Utauwa Batili</u>**

**<u>3:14-16:</u>** ***[14]Nakuandikia hayo nikitaraji kuja kwako hivi karibu. [15]Lakini nikikawia, upate kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli. [16] Na bila shaka siri ya utauwa ni kuu. Mungu alidhihirishwa katika mwili, Akajulikana kuwa na haki katika roho, Akaonekana na malaika, Akahubiriwa katika mataifa, Akaaminiwa katika ulimwengu, Akachukuliwa juu katika utukufu.***

***Nawaandikia haya mpate kufahamu jinsi ipasavyo mtu kuenenda:*** Paulo hapa anatueleza wazi wazi kwa nini anatuandikia waraka huu. Kwenye lugha ya kiyunani mlengwa wa tendo la "kuenenda" hakutajwa.Kwa hiyo, aweza kuwa ama Timotheo kabisa, au wakristo (hasa viongozi wa kanisa) kiujumla. 1Timotheo kiuwazi kabisa huwalenga Wakristo wote (hasa viongozi wa kanisa) kwa ujumla, himizo au sheria za kimwenendo ziliandikwa kwa ajili ya Timotheo. Matokeo yake, hata Biblia ya NKJV isemapo, *"Ili mpate kufahamu jinsi ipasavyo mtu kuenenda"* hufanya mwelekeo wa kiujumla (m.y, Timotheo ni mwakilishi wa Viongozi wa kanisa kwa ujumla).

***Nyumba ya Mungu:*** 1. <u>Haya ni maelezo ya kwanza kati ya matatu yanayotajwa na Paulo kuhusu kanisa.</u> Neno la kiyunani analolitumia (*oikos*) laweza kutafsiriwa kama ama "nyumba" au "jamaa au familia." Kanisa wakati mwingine limelinganishwa na jengo ama hekalu, ingawa hata hivyo hutajwa kama "lililo hai" au "linalokua" (ona **1 Kor 3:16-17; 6:19; 2 Kor 6:16; Efe 2:20-22; 1 Pet 2:5**). Hata hivyo "jamaa" au "familia" ni neno lenye maana sahihi hapa (ona **Ebr 3:6; 1 Pet 4:17**). Hili linaendana na muunganiko anaouweka Paulo kila mahali katika 1 Timotheo kati ya jamaa ya mtu duniani na ile jamaa ya Mungu, zote kwa neno moja, *oikos* (**3:4-5, 12; 5:4, 8**). Paulo anatilia mkazo hoja ya "kanisa kama familia," kwa kutumia lugha ya kifamilia katika 5:1-2, pale asemapo wazee wanatakiwa uwaonye kama baba; na vijana kama ndugu, wanawake wazee kama mama; wanawake vijana kama ndugu wa kike." Kanisa linao watu walio hai—watu walio hai wa Mungu aliye hai. Hilo linaweka bayana kwamba kanisa ni familia. Kwa upande mwingine, ile dhana kwamba "kanisa ni jengo" hudhihirika katika maelekezo ya tatu ya paulo katika **3:15** (*"nguzo na msingi wa kweli"*).

2. <u>Muktadha kwamba kanisa ni familia una uwanda mpana wa matokeo.</u> Kitheolojia, ni kweli kwamba, waaamini wote wamefanywa kuwa wana katika jamaa ya Mungu (**Rum 8:15, 23; 9:4; Gal 4:5; Efe 1:5**). Kwa hiyo, kanisa *ni* jamaa (familia) ambayo itakaa pamoja milele kwenye nchi mpya. Hata hivyo, kutokana na mtazamo wa kiutendaji, makanisa mengi *hayatendi* kama familia. Ukabila, ubaguzi kati ya matajiri na masikini, pia mafarakano na magomvi yatokanayo na mambo mengine mengi hutawala makanisa mengi ya mahali pamoja. Tatizo halijaishia kugawanya katika makanisa ya mahali pamoja tu. Kama kuna kingine zaidi, basi tatizo la magawanyo ni baya zaidi kati ya madhehebu tofauti. Hili linakwamisha sana ushuhuda wa kanisa kwa ulimwengu. Umoja wetu, au kukosekana umoja wetu huathiri moja kwa moja imani ya ulimwengu kuwa Yesu ndiye Kristo (ona **Yoh 17:21, 23**). Kama makanisa hayaanzi kuwahudumia washirika wake wenyewe, na

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

makanisa mengine, kama ndugu wapendwa wa jamaa moja, basi dunia itaendelea (kwa haki) kulidhihaki kanisa na kuhoji "kwa nini tuwe Wakristo, ikiwa ninyi Wakristo hata hamwezi kuvumiliana?"

***Kanisa la Mungu aliye hai:*** Neno linaloelezea "kanisa" hapa kwa Kiyunani ni *ekklēsia,* ambalo kimsingi linamaanisha *"mkusanyiko"* wa Wakristo, ikimaanisha mshikamano wa washirika. Ukweli kwamba sisi ni kanisa la "Mungu aliye hai", ni muhimu. Kwanza, linakazia tamko kwamba kanisa ni familia, siyo jengo. Kama vile Stefano alivyoonyesha kwa kusema *"ila Yeye Aliye juu hakai katika nyumba zilizofanywa kwa mikono ya wanadamu"* (**Mdo 7:48**). Badala yake yeye ni Mungu aliye hai, anayekaa ndani ya watu walio hai (ona **Yoh 14:17; 1 Kor 3:16; 6:19; 2 Kor 6:16**). Tunapokusanyika kwa jina lake yeye yupo katikati yetu (**Mat 18:20**). Pili, kama "Mungu aliye hai" huwapa uzima watu wake (ona **Yoh 10:10**). Nasi tunatakiwa "*tuenende katika upya wa uzima*" (**Rum 6:4**). Hii maana yake tunapaswa kuacha kuishi maisha ya kidunia, wasiobadilishwa, bali tuweke kando utu wa zamani na njia za kale, na kuuvaa utu mpya na njia mpya za kuishi (**Efe 4:17-32; Kol 3:9- 17**). Ni tu kwa njia ya kuishi kama jamaa inayopendana kwa jinsi tunavyotakiwa, ndipo tunaionyesha dunia (na sisi wenyewe) ile kweli—kwamba Mungu *ni* "Mungu aliye hai" na kwamba sisi *ni* watu wake.

***Nguzo na msingi wa kweli:*** Kama mwili wake duniani, kanisa ni "*nguzo na msingi wa kweli"* wa injili. "Egemeo" (au "msingi) hushikilia jengo kwa uimara; "nguzo" siyo tu hutegemeza paa, bali huliinua juu hadi liweze kuonekana kutoka mbali. Maneno hayo huonyesha umuhimu wa kanisa kuifundisha kweli ya Neno la Mungu (ambalo ndiyo kweli—**Yoh 17:17**) kwa ulimwengu, na kupinga mafundisho ya uongo, na pia kutunza ushuhuda wa kanisa kwa ajili ya Kristo (aliye *"kweli, njia na uzima"*—**Yoh 14:6**) kwa kwenda na kufanya wanafunzi katika mataifa yote ulimwenguni kote (ona **Mat 28:18-20; Ufu 5:9; 7:9**). Hata hivyo, kanisa kama *"nguzo na msingi wa kweli"* pia huzungumzia umuhimu wa jinsi Wakristo *wanavyoishi,* kwa sababu tunafundisha kwa njia mbili—kwa yale tunayosema na jinsi tunavyoishi. Kimsingi, jinsi tunavyoishi ni muhimu zaidi kati ya hayo mawili. Ikiwa maneno yetu hayaligani na matendo yetu, basi watu watakataa tunayosema kwa sababu tunakuwa wanafiki, Kwa upande mwingine, ikiwa Wakristo binafsi watakuwa waaminifu katika namna ya kuishi kwao na ushuhuda wao wa Kristo, Kristo anaahidi *"kutufanya nguzo katika hekalu la Mungu wangu."* (**Ufu 3:12**). Taswira au picha hizi tatu za kanisa ambazo Paulo anazieleza katika **3:15** zinaonyesha kiini kamili na umuhimu wa kanisa. Tunapaswa kutathimnini kwa dhati jinsi tunavyoenenda kama kanisa, na kujirudi kwenye wito mkuu ambao Paulo ameuweka kwa ajili yetu.

***Siri ya utauwa ni kuu: alidhihirishwa katika mwili . . . akachukuliwa juu katika utukufu:*** Kanisa lapaswa kulinda na kuitangaza kweli. Katika **3:16** Paulo anazungumzia wimbo wa kanisa unaoelezea kitovu cha kweli—na yote ni kuhusiana na nafsi na kazi ya Yesu. Wachambuzi wengi wa mambo wanayaona haya katika sura kuu tatu zenye vipengele viwili-viwili, kulingana na jinsi *vinavyogongana* kati ya "mwili" "roho," "malaika" na "mataifa," "dunia" na "utukufu." Ushabihiano kuunga hilo ni wa J. N. D. Kelly: "Kwanza, Kristo aliuvaa mwili na hivyo katika hali ya mtumishi anaonekana mwenye haki katika kufufuka kwake [ufunuo wa Kristo]. Pili, Kristo apokea heshima ya aabudiwa na malaika na anahubiriwa katika mataifa yote ya wanadamu, m.y; awekwa wazi mbele ya viumbe vilivyo chini ya nchi, viumbe vya kimbingu, viumbe chini ya nchi [kumtangaza Kristo]. Tatu, anaaminiwa pote ulimwenguni (Wakolosai 1:23) na katika ulimwengu wa roho wenyewe [kupokelewa kwa Kristo]." (Kelly 1960: 92; ona Gundry 1970: 208; Ham 2000: 218-28) Wengine wana maoni tofauti kuhusu dhana hii. Kwa mfano, Robert Gundry anaona mstari wa 1 na wa 6 kuwa inatengeneza unganiko ambalo "linaunda kiumakini mstari mzima," na mistari 2/3 na 4/5 ikiwa inafungamana *si* kwa msingi wa kupishana, bali kwa usambamba wa *kujitengeneza* (m.y; inajengana moja juu ya mwenzake) (Gundry 1970: 208). Kwa maneno mengine, "kuhesabiwa haki kwa Kristo" (mstari wa 2) kunaongoza katika kuonekana mbele za malaika (mstari wa 3) [hali zote mbili ni za ulimwengu usioonekana]. Kama ambavyo, kuonekana kwa Kristo katika mwili (mstari wa 1) kunafikia upeo wake kwa kupaa kwake kwenda mbinguni (mstari wa 6)." (Ham 2000: 218). Haijalishi mtu ananyambua **3:16,** ni wazi kuwa mstari unakazia nafsi na kazi ya Kristo, kuanzia kutwaa mwili kwake hadi kufufuka kwake, kupaa kwake, na kupewa kwake enzi. Huu ndio moyo wa imani ya Ukristo. Mfululizo mkuu mwingine wa kazi ya Kristo utakuwa baada ya kurudi kwake duniani ("kuja kwake kwa mara ya pili"), ambako Paulo anakunenea katika **6:14-16.**

***<u>4:1-7a:</u> [1]Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani; [2] kwa unafiki wa watu wasemao uongo, wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe; [3]wakiwazuia watu wasioe, na kuwaamuru wajiepushe na vyakula, ambavyo Mungu aliviumba vipokewe kwa shukrani na walio na imani wenye kuijua hiyo kweli. [4]Kwa maana kila kiumbe cha Mungu ni kizuri, wala hakuna cha kukataliwa, kama kikipokewa kwa shukrani; [5]kwa kuwa***

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

***kimetakaswa kwa neno la Mungu na kwa kuomba. [6]Uwakumbushe ndugu mambo hayo, nawe utakuwa mtumishi mwema wa Kristo Yesu, na mzoevu wa maneno ya imani, na mafundisho mazuri yale uliyoyafuata. [7]Bali hadithi za kizee, zisizokuwa za dini, uzikatae; nawe ujizoeze kupata utauwa.***

Paulo amemaliza tu kuelezea *"siri ya utauw [wa kweli]."* Sasa anarudia upande wa tatizo la *utauwa wa uongo.* Awali alijadili kwa kina juu ya uaminifu unamaanisha nini, akihusisha mafundisho lengo la mafundisho ya kweli (**1:5**); Injili ya wokovu kwa neema (**1:12-17**); na umuhimu wa kudumu kuwa mwaminifu (**1:18-20**); ulazima wa maombi yatokanayo na maisha matakatifu, ili watu wafikie ufahamu wa neema iokoayo ya Kristo (**2:1-15**); sifa za watu wanaotakiwa kuliongoza kanisa (**3:1-13**); na sura ya kanisa lenyewe (**3:15**); na "siri kuu ya utauwa" kuhusu Yesu Kristo, ambayo kanisa inaamini na kuitangaza (**3:16**). Alianzia katika 1 Timotheo kwa kuelezea tatizo katika kanisa la Efeso lililotokana na mafundisho ya uongo ya watu fulani (**1 Tim 1:3-4, 19-20**). Katika sehemu hii ya pili, Paulo anatoa maelekezo ya kina kuhusu sura ya mafundisho ya uongo na walimu wa uongo, na jinsi ya kuwashinda.

***Bali Roho anena waziwazi akisema:*** Paulo hapa anakazia umuhimu wa kile anachotaka kukisema kwa kusema kwamba ni Roho Mtakatifu ndiye asemaye haya. Kwa bahati mbaya, siku zetu: "wengine wametumia kifungu hiki kukazia mambo yao wenyewe, wakijijengea hoja kusimamia "mafunuo maalum yao" kutoka kwa Roho, matokeo yake tumekuwa na mfumuko wa unabii katika makanisa ya Afrika. Nabii hizo zinaonekana kutokana na kupuuza usomaji wa Neno la Mungu, ambalo kikawaida Mungu hujifunua kwa hilo kwetu leo. Tunahitaji kukumbuka tofauti kati ya mitume na sisi. Wao waliwekezwa imani moja kwa moja na Yesu mwenyewe, na baadaye wakayaweka katika maandiko (2 Tim 1:14). Paulo kama mtume, alipokea siri ya imani moja kwa moja kutoka kwa Bwana (1 Cor 11:23; Gal 1:11-12)." (Andria 2006: 1473). Kama ilivyoonekana hapo mwanzoni, kanisa linao wajibu wa *"kuzijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea dunia."* (**1 Yoh 4:1**).

***Nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani:*** Kila wakati Agano Jipya linapozungumzia "nyakati za mwisho," "nyakati za mwisho," au kutumia maneno yafananayo na hayo, huzungumzia nyakati tunazoishi *sasa*. Nyakati hizo ni kuanzia kipindi kizima kati ya kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo, na Kuja Kwake kwa Mara ya Pili. Kwa hiyo, ile Siku ya Pentekoste, wakati wanafunzi walipoanza kunena kwa lugha mpya, Petro akaelezea kile kinachotokea kwa kunukuu kutoka nabii Yoeli (**Yoeli 2:28-32**) aliyesema: *"Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono'"* (**Mdo 2:17**). Kwa hiyo, "siku za mwisho" zilianzia angalau ile Siku ya Pentekoste. **Ebr 1:2** panatuambia kwamba "mwisho wa siku hizi [Mungu] amesema na sisi katika Mwana" (ona pia **1 Pet 1:20**). Katika **1 Yoh 2:18** Yohana asema mara mbili kwamba, hata alipokuwa akiandika kuwa *"ni nyakati za mwisho."* **Yuda 17-18** panazungumzia wazo lile lile la Paulo la **1 Tim 4:1**. Anawakumbusha waamini kuwa mitume walishaonya kuwa*"Nyakati za mwsiho watu watakwa wakidhihaki, wakifuata tamaa zao wenyewe."*Kipindi chote hadi Kristo atakaporudi, kitajaa matukio ya watu kuijia imani, na kwa wengine wakikiri imani ya uongo na kukengeuka (ona **Mat 13:24-30, 36-43**). Ndiyo maana Paulo anatadhadharisha tena na tena katika 1 Timotheo kuhusu mafundisho ya uongo, na kuwahimiza waamini kudumu katika imani (**1:3-4, 6-7, 18-20; 4:1-10; 6:3-5, 11-14, 20-21**).

***Kusikiliza (kufuatia):*** Katika maneno haya, Paulo anatuelezea *ni nani* watakaokengeuka. Wale watakaokengeuka watakuwa ni wale *"wanaosikiliza"* waalimu wa uongo na mafundisho batili. Mwanzoni mwa kitabu, Paulo anamuasa Timotheo *"kutosikiliza hadith za kizee na nasaba zisizokoma"* (**1:4**). Kwa upande mwingine, katika **4:13, 16** Paulo anamuasa Timotheo nini cha "kusikiliza (kufuatia)": *"kusoma na kuonya na kufundisha."* na *"kijilinda nafsi na mafundisho yako,"* Maandiko ndiyo kiini chetu kikuu cha ukweli, na kipimo ambacho tunaishi maisha yetu. Matokeo yake, **4:13, 16** anapomwambia Timotheo kile cha "kufuatia", anaanzia na Andiko. Kisha anarudia "mafundisho" (m.y; kitu cha kuamini) mara mbili, kwani kile tunachoamini kinapangilia jinsi ya kuishi. Kule kukazia jambo la kujali "mwenyewe" kwaonyesha jinsi ambavyo mara kwa mara tunapaswa kujipima maisha yetu yote (mawazo, maneno, matendo, hisia, shauku, upendo, chuki, nk.) kwa nuru ya Injili na Biblia.

***Roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani:*** Hapa Paulo anatuelezea *chimbuko* la mafundisho ya uongo ambayo hupotosha watu: *"roho zidang'anyazo na mafundisho ya mashetani."* Ingawaje wanadamu ndio waandishi na wanenaji wa hayo mafundisho ya uongo, nyuma ya midomo ya hao wanadamu ni mashetani na mapepo. Huu ni udhihirisho mojawapo wa ukweli kwamba, nyuma ya tuonayo kwa macho, kuna ulimwengu mkubwa wa kiroho, ikiwako pia vita kubwa ya kiroho (ona **1 Sam 16:14-23; 1 Wafalme 22:19-23; 2 Wafalme**

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

**6:15-18; 19:35; Ayu 1:6-2:10; Dan 10:1-14; Mk 5:1-20**). Mara nyingi zaidi, huwa hatuelewi hili, lakini lile tulifanyalo hapa duniani lina matokeo ya kiroho (ona **Mat 16:19**).

***Kwa unafiki wa watu wasemao uongo:*** Hapa Paulo anatueleza *mbinu* isababishayo watu waanguke (wakengeuke): *"kwa uanafiki wa watu wasemao uongo."* Shetani ni *"baba wa uongo"* (**Yoh 8:44**). Neno litambulishalo hapa "*kwa"* (linalotafsiriwa kutoka neno la Kiyunani *"en"* laonyesha kwamba hawa waalimu wa uongo ndio vyombo vya kupotosha wale walio wa imani. Hii ni moja ya sababu za Yesu kuwa mkali sana kwa Mafarisayo na wanafiki wengine: alijua yote mawili, chimbuko lao, na uharibifu mkubwa, na wa kudumu ambao unafiki na udanganyifu unaweza kusababisha (ona **Mat 6:2-5, 16; 15:5-9; 22:15-21; 23:13-33; 24:45- 51**). Hii pia ni sababu kwa nini tunahitaji kuwapima waalimu kwa *yale wayasemayo* (ona **Mdo 17:11** na kwa *jinsi waishivyo* (ona **Mat 7:15-16; Yak 5:1-5**). Kama vile Shetani mwenyewe anavyojifanya kuwa kama *"malaika wa nuru"* (**2 Kor 11:14**), walimu wa uongo huja kama *"watu wakubwa wa Mungu."* Wanaweza kudai kufanya, au hata wakafanya kabisa, miujiza na ishara kuu. Waweza kutumia Mamilioni mengi ya fedha kwenye televisheni. Hata hivo, watu hao huishi kwa ajili ya kujitajirisha wenyewe. Ni wanafiki wasioishi kama Yesu, mitume, au Wakristo wengi walivyoishi historia yote iliyopita. Unafiki wao umajulikana na Bwana na unapaswa ujulikane kwetu. Kule kulitumia Jina la Yesu hakumpumbazi Yesu (ona **Mat 7:21-23),** na kusitupumbaze sisi.

***Wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe (kama kwa chuma iunguzayo):*** Aya hii inazungumzia juu maafa ya kusikiliza waalimu wa uongo na mafundisho yao. Dhamiri zao wenyewe zimechomwa (m.y; zimechomwa na kuwa na makovu) kama zimeunguzwa na chuma cha moto (kama vile ng'ombe wanavyowekewa alama kwenye ngozi na chuma ya moto). Hii ina matokeo mawili yanayohusiana: (1) Hata kilicho muhimu zaidi, kule kuwekwa alama ya kuchomwa kunaonyesha nani anayewamiliki. "Walimu hawa wanabeba alama za Shetani katika dhamiri zao, kuonyesha kwamba ni mali ya mwingine aliye tofauti na Mungu ambaye waamini wanamilikiwa naye" (Ngewa 2009: 88). Madhara hayo hayo yatatokea kwa wanaowasikiliza kama "watatega masikio" kusikiliza walimu wa uongo. Sote hupenda kufanana na wale tunaowasikiliza. Hii ni mara ya tatu Paulo katika 1 Timotheo anataja "Dhamiri." Katika **1:5** alisema moja ya sehemu ya kufikia lengo la upendo ni kuwa na *"dhamira safi."* Katika **3:9** alizungumzia juu ya *"kuishika siri ya imani katika dhamira safi"* Na sasa anazungumzia "*dhamira iliyochomwa"*. Hili lingepaswa kutuonya tusiwasikilize waalimu wa unongo, kwani kutatuzuia tusifikie lengo la upendo, na kukosa sifa za kumtumikia Bwana katika kanisa.

***Wakiwazuia watu wasioe na kujiepusha na vyakula:*** 1. <u>Hapa Paulo anatoa *mifano* miwili ya utauwa wa uongo: wanaowazuia watu kuoa; na kuwazuia watu kula aina fulani ya vyakula.</u> Swala la nini kiliwe linaanzia kwenye Sheria ya Musa. Hata hivyo, Kristo alituweka huru kutoka sheria ya Agano la Kale, na akatangaza vyakula vyote kuwa ni safi (**Mk 7:19; Mdo 10:9-16;** ona pia **Rum 6:14; Gal 3:13; 5:1-6; Kol 2:13-14; Ebr 7:11-12; 8:13; 10:9**). Paulo amefundisha mahali pengine kwa kina juu ya vyakula na vinywaji (ona **Rum 14:1- 23; 1 Kor 8:1-9:4; 10:23-30**). Wale wanaowazuia wengine kuoa pengine walikaribia swala la "malaika wa nuru": m.f., "Si ungelipenda kumfanania zaidi Yesu, si ndiyo hivyo? Yesu hakuwa ameoa. Kwa hiyo kama kweli unataka kuwa wa kiroho kabisa kama yeye, nawe usioe vivyo hivyo." Ingawaje maneno kama hayo yanasikia ya kiroho, yanaruka ukweli kwamba Mungu ndiye aliyeianzisha ndoa (**Mwa 2:18-24; Math 19:3-6**). Ndoa ni taswira ya mahusiano kati ya Kristo na kanisa (**Efe 5:22-32**). Ingawaje Paulo mwenyewe alikuwa hajaoa na, *"kwa mtazamo wa hali ngumu aliyokuwa nayo"*(**1 Kor 7:26**), aliona ni vyema watu wasioe, akitambua kuwa ndoa ni halali na ni kipawa kutoka kwa Mungu (**1 Kor 7:7; 9:5**), hakuwa anajaribu *"kuweka kifungu kwako"* (**1 Kor 7:35**). Kusema ukweli, sehemu nyingine katika 1 Timotheo anawashauri wanawake vijana waolewe na kuzitunza familia zao (**5:14**).

2. <u>Kanuni nyuma ya utaua wa uongo zinagusa kwenye moyo wa nafsi na kazi ya Kristo.</u> Paulo hashambulii kila kosa, kutokuelewana, au mawazo yenye makosa ambayo watu wanaweza kuwa nayo au wanaweza kufundisha. Kusema ukweli, kwa muonekano wake, kutokuoa, na kuacha kutumia vyakula fulani-fulani, au matendo yanayofanana na hayo, kwaweza kuonekana si kwa maana. Mwingine anaweza kusema Paulo amezidi ukali mno kwa kuyaita mambo kama hayo *"mafundisho ya mashetani."* Paulo hazidishi ukali. Kile anachokifanya ni kushambulia mafundisho hayo, elimu, na sheria, ambazo, zikifikiriwa kwa undani zaidi, zinagonga kwenye moyo wa Ukristo na kile alichokifanya. Kanuni nyuma ya maagizo huwezi kuoa wala kula vyakula fulani-fulani" kimsingi ni kinyume na Kristo angalau kwa sababu mbili: (A) *Maagizo yaliyoundwa na wanadamu kama hayo hukataa utoshelevu na kazi ya Kristo ya kuokoa na kuwatakasa watu.* Kileanachokisema Paulo *si* uamuzi wa binafsi wa mwamini kupanga kutokuoa au kutokula au kutokunywa vitu fulani (ona **Rum 14:1-2; 1 Kor 8:7, 10**). Badala yake, anazungumzia *sheria zilizoundwa na wanadamu au amri kwa wengine* ambazo, kinamna zinasema: Kama unataka kuokoka, au ikiwa unataka kuwa mtakatifu, basi hupaswi kuoa au

kula vitu fulani." Sheria zote hizo zinakana utoshelevu wa Kristo pekee kuokoa na kututakasa. Sheria zote hizo si za Ki-Biblia: haziko katika Biblia; na pia ni sawa na kusema kwamba imani katika Kristo, na Neno lake hakutosheleza—badala yake, katika imani na kutii huko, unapaswa kuongeza sheria za mwanadamu. Twaokolewa kwa neema pekee, kupitia imani pekee, katika Kristo (ona **Efe 2:8-9**). Tumewekwa huru kutoka Sheria ya kale (ona **Rum 6:14; Gal 3:13; 5:1-6; Kol 2:13-14; Ebr 7:11-12; 8:13; 10:9**). Sasa tuko chini ya sheria ya Kristo (**Luka 22:20; 1 Wakor 11:25; 2 Kor 3:6; Ebr 8:8-13; 9:15**). "Sheria ya Kristo" ni mafundisho ya Yesu na ya waandishi wa Agano Jipya (ona, k.m., **Yoh 14:24-26; 16:12-15; 17:8, 18-20; 1 Kor 14:37; Gal 1:11-12; Efe 2:20; 1 Thes 2:13; 2 Thes 2:15; 3:6, 14; Ebr 2:3; Ufu 1:11**). Yesu alisema kama "Tutakaa" au "kudumu" katika neno lake (siyo katika neno lililoundwa na mwalimu wa uongo), ndipo *"mtaifahamu kweli nayo hiyo kweli itawaweka huru"* (**Yoh 8:31-32**). (B) *Amri zilizoundwa na wanadamu kama hizo ni kinyume na kile Kristo alichokifanya kwa sababu zinaunda makundi ya "dhahiri" mawili ya Wakristo: hao "watakatifu" wanaofuata sheria zilizoundwa na wanadamu, na wa ngazi ya chini, walio wa kawaida wasiozifuata.* Kristo alikuja kumuumba *"mtu mpya mmoja"* ndani yake, siyo wawili (**Efe 2:14-16**). Wale wote walio wanafunzi wake wanafanana naye (**Gal 3:28; Kol 3:10-11; Ufu 5:9; 7:9**). Kushikila kuwa kuna madaraja mawili ya Wakristo, daraja la kwanza na daraja la pili, kulingana na sheria zilizoletwa na mwanadamu-ambazo hazimo kwenye Biblia, zinagonga kile alichokifanya Kristo. Kinamweka Mkristo moja kinyume na mwingine, na jumla yake ni kusema kwamba umoja katika Kristo haufai.

3. Paulo alikutana na tatizo la aina hiyo hiyo, ingawaje lilikuwa ni swala jingine, katika **Gal 2:11-21**, ambapo ilifikia ampinge hata Petro. Kwa Wagalatia, swala lilikuwa kama inafaa waamini wale chakula pamoja na wamataifa wasiotahiriwa. Matokeo yake, upande moja ulikuwa "Ili mtu aokolewe, lazima afuate sheria ya Musa; au, ingawaje umeokolewa na Kristo, ili uweze kuudumisha wokovu wako ni lazima ufuate sheria ya torati ya Musa." Petro alikuwa anakubaliana na kundi hilo, huenda kwa sababu njema (kwa mfano, ili kutowakwaza Wayahudi, au hata kuwavuta kwa Kristo. Hata hivyo, Paulo alijua kitendo hicho hali kama hiyo ni ya hatari sana kwa Ukristo: "Mwishowe, hilo lingelazimisha Ukristo kuwa kipande ndani ya Uyahudi; na kungeondoa maana yote ya *utoshelevu* wa Yesu na kifo chake kwa kwa niaba ya wenye dhambi. Wamataifa wangelazimishwa kuwa Wayahudi. Mbinu ya Petro huenda ikawa na nia njema, lakini Injili yenyewe ilikuwa iko hatarini."(Carson 2002: 160)

4. Swali la lazima la kujiuliza kuhusu haya yote ambayo mtu atayadai kwa Wakristo yanahusiana na sababu, msingi, na athari zinazofikiriwa za tabia hiyo. Ikiwa swala hilo maalum ni kula au kunywa vitu fulani, nani tunaruhusiwa kufungamana naye, au kama tunaruhusiwa kuvaa aina fulani za nguo, shughuli gani tunapaswa kujihusisha nazo (kiujumla, au siku fulani), au mambo mengine kama hayo, basi tunapaswa kujiuliza maswali kama vile: Kwa nini? Je amri hizo zinatoka wapi katika sheria ya Kristo? Ni kwa sababu gani unataka haya? Kwa nini ni lazima? Na ni athari zipi huenda zikatokea kwa hali yangu ya kiroho iwapo nitayatekeleza, au kama nitakataa kuyafuata? "Paulo alishayafikiria na kuyawazia hayotangu muda mrefu. Alikuwa ... mtu mwenye ulaini. Kwa hiyo, aliweza kumtahiri kwa furaha tu Timotheo ili kwamba kijana huyu aweze kukubalika kuingia kwenye maisnagogi yao kama afanyavyo Paulo mwenyewe (Mdo 16:3). Kinyume chake, Paulo alikataa kumruhusu Tito atahiriwe (Wagal 2: 1-5), hasa kwa sababu matakwa ya kutahiriwa kwake yalifanyika kwa dhana ambayo iliiharibu Injili. Kwa maneno mengine, ikiwa mtu atadai kwamba ni lazima mtu atahiriwe kwanza ndipi aweze kuwa Mkristo, Paulo anapinga hilo kabisa, kwa sababu hilo lingepunguza utoshelevu wa Kristo; ikiwa hakuna mtu anayetoa madai kama hayo, Paulo anayo furaha kumtahiri mwamini ikiwa hilo litasukuma mbele Injili" (Carson 2002: 160). Kilichokuwa kinatokea Galatia, na kile ambacho Paulo anakijadilia katika **1 Tim 4:1-7a,** ni kule kugeuza sheria zilizofanywa na mwanadamu kuzifanya mambo ya "msingi". Lazima tuijue Injili vya kutosha sana kiasi kwamba hatuwalazimishi watu kufuata amri zilizotungwa na wanadamu, za kujitungia wenyewe, kama walivyojaribu kufanya walimu wa uongo katika Galatia na Efeso.

***Ambavyo Mungu aliviumba vipokewe kwa shukrani na walio na imani wenye kuijua hiyo kweli. Kwa maana kila kiumbe cha Mungu ni kizuri, wala hakuna cha kukataliwa, kama kikipokewa kwa shukrani; kwa kuwa kimetakaswa kwa neno la Mungu na kwa kuomba:*** Hapa Paulo anatoa *ufumbuzi* wa kwanza kuhusu tatizo la mafundisho ya uongo: lijue *Neno la Mungu* —pima kila jambo kwa njia ya Neno. Kristo ndiye kweli na Neno lake ni kweli. Biblia ndiyo kipimo cha kutathimini mafundisho ya watu na maisha yetu. Muhubiri wa kweli, mwalimu, ama mjumbe wa Mungu hatapingana na Neno la Mungu lililoandikwa. Tukilishika Neno lake na kutembea karibu na Mungu, Roho Mtakatifu atatuongoza kwenye kweli. (**Yoh 14:16- 26; 16:13-16; Rum 8:14**). Twapaswa basi kutathimini kila fundisho, na kila agizo litolewalo la jinsi ya kuishi, kwa njia ya Biblia na mwongozo atupao Roho Mtakatifu kupitia maombi. Hili linaonyesha umuhimu mkubwa wa ufahamu wa kutosha wa utendaji wa Neno. Pia linatupatia sababu nyingine kwa nini maombi yatokayo katika maisha matakatifu (**2:8**) ni muhimu sana.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

***Uwakumbushe ndugu mambo hayo, nawe utakuwa mtumishi mwema wa Kristo Yesu, na mzoevu wa maneno ya imani, na mafundisho mazuri yale uliyoyafuata:*** 1. Hili ni sehemu ya pili ya ufumbuzi wa Paulo kuhusu tatizo la mafundisho ya uongo yaliokuwa yanawasababisha watu kuangukia mbali na imani: *Kufundisha Neno la Mungu*— yaweke wazi mafundisho ya uongo kwa kutumia Neno la Mungu. Ni jukumu la wale wanaoongoza makanisa kulijua Neno la Mungu, na kulifundisha. Kujua tofauti kati ya kweli na uongo kuna maafa ya kiroho kwa watu. Kwa vile maafa yake ni makubwa mno, Paulo anarudia mara kwa mara umuhimu wa uaminifu wa kiroho na "mafundisho" katika 1 Timothy (**1:3, 5; 3:2; 4:11, 13, 16; 6:2**). Kuitangaza kweli na kuutenga uongo mbali na Neno hukusaidia wewe, mwalimu pia. Utakuwa "*mtumishi mwema wa Kristo Yesu, na mzoevu wa maneno ya imani, na mafundisho mazuri yale uliyoyafuata.*" Hii pia huonyesha umuhimu wa *kuishi* kile tunachokifundisha. "Maneno ya imani" yataweza tu "kukujenga" wewe ikiwa umekuwa "ukifuata" (m.y; kukaza masikio kusikiliza; kuyabadili maisha yako mwenyewe yaendane na) kile unachokisoma katika Neno na kuwafundisha watu. Hilo litasababisha wewe kukua katika imani yako, Hata hivyo, ikiwa *huishi* sawa sawa na kile unachokisema, ndipo unakuwa ni mnafiki—ambayo ni alama mojawapo ya mwalimu wa *uongo*. Kama kiongozi wa kanisa, wewe ni kielelezo kwa watu wako. Wewe ndiwe "Biblia inayoishi" kwao. Watu wako walio wengi ama hawana Biblia zao wenyewe, au hawazisomi. Njia pekee watakayojifunzia Neno la Mungu ni ikiwa wewe utawafundisha kiukweli na kimatendo kwao jinsi Neno linavyoonekana ukilifuata.

2. Kuwa *"mtumishi mwema wa Krsito Yesu"* pia husisitiza kwamba mtazamo wa kiongozi wa kanisa na tabia yake ni vya muhimu zaidi. Viongozi wengi wa makanisa wanapenda kujifikiria wenyewe kama watu "wakuu wa Mungu" walio ngazi ya juu zaidi ya washirika wao. Utaona katika **4:6** Paulo anamwita Timotheo "mtumishi" wa Kristo Yesu. Neno la "mtumishi" hapo ni neno lile lile lililotafsiriwa "shemasi" katika **3:8**: neno la Kiyunani *diakonos.* Ikiwa wachungaji, wazee, waangalizi, na maaskofu hawatambui kuwa kwanza wao ni *watumishi* watumishi wa Kristo na watumishi wa watu wa Kristo, kanisa—basi hawaweza kumwakilisha Kristo, na hawatakuwa wakitekeleza kikamilifu kazi yao. Kama ilivyo kwa mambo mengine mengi, yote hulenga "kumpenda Mungu, na kuwapenda wengine." Mtu hawatumikii wengine au kuonyesha upendo kwa kuonyesha nia ya kuwakandamiza wengine. Kristo ndiye mkuu wetu. Anawapenda watu wake, na anatutaka sisi tuwe vyombo vyake kuwaonyesha jinsi anavyowapenda (ona **Yoh 13:5-16**). Ikiwa kweli "tunawapenda jirani zetu kama nafsi zetu" (**Mat 22:39**) basi tutajali kiasi hicho hicho, na kuonyesha juhudi hizo hizo, nguvu, na gharama kuhakikisha majirani zetu wanaishi vizuri kama sisi tuishivyo. Kristo alifanya hivyo. Anawaagiza viongozi wa kanisa kufanya vivyo hivyo.

***Bali hadithi za kizee, zisizokuwa za dini, uzikatae:*** Paulo anamalizia sehemu hii ya maonyo na mafundisho ya uongo, kwa kusema mambo mawili. Kwanza, mtu *"ajiepushe"* na udanganyifu (ona pia **1:4; Tito 1:14**). Sababu inaonyeshwa na mithali ya Malgache kutoka Madagascar, "Chungu cha maji masafi hakiwezi kuzuia maji machafu kuingia." Kwa maneno mengine, "Hata maji machafu kidogo yanatosha kuharibu chombo kizima kilichojaa maji safi. Kwa hiyo, hata kama wapo watu wachache tu wenye mafundisho ambayo yataharibu kanisa, kila juhudi lazima ifanyike kuwaweka mbali na wale wenye mafundisho safi." (Andria 2006: 1470) Pili, *anayadhihaki* mafundisho ya uongo kwa kusema kuwa mafundisho ya uongo si lolote isipokuwa *hadithi za kizee*." Kwa mara nyingine anatumia neno "hadithi" alilolitumia katika **1:4.** Hadithi kama hizo hazina msingi na haziaminiki. Ni watu wasiofikiri na wapumbavu ndio huzisikiliza. Bali, kama watu wako hawana mafundisho ya kutosha, watanaswa na "manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa-mwitu wakali" iwa yamevaa (**Mat 7:15**) ambao *"wanakula kwenye nyumba za wajane."*(**Lk 20:47**).

**4:7b-16:** ***[7b]Nawe ujizoeze kupata utauwa. [8]Kwa maana kujizoeza kupata nguvu za mwili kwafaa kidogo, lakini utauwa hufaa kwa mambo yote; yaani, unayo ahadi ya uzima wa sasa, na ya ule utakaokuwapo baadaye. [9]Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa; [10]kwa maana twajitaabisha na kujitahidi kwa kusudi hili, kwa sababu tunamtumaini Mungu aliye hai, aliye Mwokozi wa watu wote, hasa wa waaminio. [11]Mambo hayo uyaagize na kuyafundisha. [12]Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi. [13]Hata nitakapokuja, ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha. [14]Usiache kuitumia karama ile iliyomo ndani yako, uliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya wazee. [15]Uyatafakari hayo; ukae katika hayo; ili kuendelea kwako kuwe dhahiri kwa watu wote. [16]Jitunze nafsi yako, na mafundisho yako. Dumu katika mambo hayo; maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia.***

***Nawe ujizoeze kupata utauwa . . . yaani, unayo ahadi ya uzima wa sasa, na ya ule utakaokuwapo baadaye:*** 1. Paulo hapa anabadilisha majadiliano yake kutoka *waalimu wa uongo* kwenda *utaua wa kweli* hususan, jinsi mtu (hasa kiongozi wa kanisa) anavyopaswa aenende kiushuhuda. Utofauti wa dhana ya mjadala pia

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

unaonekana wazi kwenye tafsiri ya Kiyunani ya Biblia iitwayo NASB ya neno *de* (ambalo kikawaida hutafsiriwa "lakini") kuwa "kwa upande mwingine."

2. Ingawaje kujizoeza kupata nguvu za mwili kwafaa kidogo, lakini utauwa hufaa kwa mambo yote; kwa maana kunahusika na "*uzima wa sasa, na ya ule utakaokuwapo baadaye"* ila maozezi ya kimwili yafaa kwa maisha haya tu. Nidhamu (mazoezi) huhutaji kudumishwa na juhudi. Kama ilivyo kweli kwa mazoezi ya kimwili, ingepaswa iwe kweli zaidi kuhusu nidhamu ya rohoni. "*Ahadi ya uzima wa sasa"* haulingani na mali za kidunia, bali hujumuisha kubarikiwa kiutauwa. Licha ya mazingira ya sasa ya kidunia, Mkristo anaweza kwa uhakika akaambiwa kuwa na ubora wa maisha yote mawili sasa na yajayo." (Guthrie 1990: 107)

***Kwa maana twajitaabisha na kujitahidi kwa kusudi hili:*** Paulo anasisitiza tena kwamba kudumisha maisha ya imani si rahisi. Katika **1:18** anatumia mlinganisho wa kupigana ngumi au kupigana *"kuvipiga vita vizuri."* Katika **4:7-8** ametumia neno la Kiyunani *gumnaze* kumaanisha "nidhamu (mazoezi)" ambao ni msemo wa kimichezo ambao "bila shaka unaonyesha nidhamu ya kimichezo . . . mbalo kwalo twapata 'gymnasium'" (Earle 1978: 373). Sasa anatumia mlinganisho wa namna mbili: mlinganisho wa ajira au kazini wa neno *"kujitaabisha"* na neno jingine *"kujitahidi"* (Kiyunani = *agōnizomai*) ambalo lilifungamana na mashindano ya riadha. Katika **Fil 2:12-16** Paulo anatumia neno hilo hilo mara ya pili anapotuambia: *"utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka; kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema . . . mkishika neno la uzima; nipate sababu ya kuona fahari katika siku ya Kristo ya kuwa sikupiga mbio bure wala sikujitaabisha bure."* Hata kama Kristo yuko pamoja nasi, na ndani yetu na anatuongoza, maisha yetu hayapaswi kuwa ya uvivu na kulegea; bali ya kuenenda na kuvumilia katika uaminifu.

***Kwa sababu tunamtumaini Mungu aliye hai:*** Katika **1:1** Paulo alimuunganisha Baba na Kristo, aliye Mwokozi, (ona **Luka 2:11; Yoh 4:42; Mdo 5:31; 13:23**), kwa kumuita *"Mungu mwokozi wetu,"* usemi ambao unapatikana tu katika nyaraka za Paulo (ona **1 Tim 2:3; 4:10** na **Tito 1:3; 2:10; 3:4**). Katika **1:1** alisema pia Kristo ndiye *"tumaini letu"* (ona pia **Kol 1:27**—*"Kristo ni tumaini la utukufu"*). Sasa anakazia umoja wa Baba na Mwana kwa kusema ni *"Mungu aliye hai*" aliye "*tumaini letu." "Mungu aliye hai"* huibua msemo ule ule alioutumia Paulo katika **3:15.** *"Tumeweka tumaini letu"* ni kitenzi kamilifu cha Kiyunani, kinachoonyesha kitu tayari kimefanyika siku za nyuma, ambacho madhara yake bado yanaendelea kuonekana hadi sasa. Kwa maneno mengine, tumaini letu linaendelea na ni la uhakika linaloathiri maisha yetu sasa na maisha yajayo ambayo "*tunajitaabisha na kujitahidi kwayo."* Anachosema Paulo hapa ni kama kinashabihiana, kama alivyosema katika **Fil 2:12-13** *(utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka; kwa maana ndiye Mungu [m.y; "Mungu aliye hai"] atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema")*: (1) Tumeweka tumaini letu, si katika dunia hii au mambo ya dunia hii, bali katika Mungu. "Mwamba" ambao sisi "tumekazia" matumaini yetu ni salama na wa uhakika, si kama kutumainia dunia hii au mambo ya dunia hii (ona **Mat 7:24-27; 1 Tim 6:17**). hatma yetu ni salama mikononi mwake—amewahakikishia uzima wa milele wale wote walio wake (ona **Rum 12:39; 1 Kor 15:20-22**). (2) Ni *kwa sababu* tumaini letu sasa liko kwa Mungu katika Kristo na uzima wetu wa milele ni salama ndani yake, ndipo tunajitahidi kufanana naye. Kwa kuwa twajua sasa hatma yetu ni salama, baadhi ya watu huwa wavivu na legelege, pasipo kujali jinsi tunavyoishi hapa na sasa. Kinyume chake Paulo anasema kwa vile tunajua siku zetu za mbeleni ni salama "tunajitahidi na kujihimiza" kuwa wacha Mungu wafanyao kila kitu tuwezacho kufikia lengo la upendo sasa kwani tunajua kuwa jinsi tunavyoishi huleta tofauti pande zote- sasa na umilele wetu, na katika maisha ya wengine.

***Aliye Mwokozi wa watu wote, hasa wa waaminio:*** Aya hii imesababisha utata fulani. Kulingana na vifungu vingine vingi vinavyoonyesha kwamba siyo watu wote wataookolewa katika milele (ona majadiliano ya **2:4**), hii haimaanishi kwamba Mungu milele ijayo ataokoa "kila mtu pasipo kutotofautisha." Kama ilivyo kwa neno "okoa" lenyewe, "mwokozi" (Kiyunani = *sōtēr* linaweza kumaanisha kitu cha " kuhifadhia", au likamaanisha "mwokozi" wa milele (ona majadiliano ya **2:15**). Kusema ukweli sehemu ya mwisho ya mstari wa 10, ambayo inawaweka rasmi waamini kuwa ndio walengwa wa nguvu ya wokovu wa Mungu, kinaashiria kwamba neno *mwokozi* hapa linatumiwa kwa maana mbili" (Guthrie 1990: 108). Kwa hiyo, Mungu kweli ni mwokozi (kwa maana ya "mhifadhi") wa watu wote. Hiyo ni "neema ya wote" ambayo inampa kila mtu uzima, na uwingi duniani wa kufurahia (ona **Zab 147:8-9; Mat 5:45; Luka 6:35; Mdo 14:17; 17:25-28; Kol 1:17; Ebr 1:2-3**). Kwa upande mwingine, yeye ni Mokozi (kwa maana ya "mwokozi wa milele") wa watu wake (waaminio; kanisa). Maneno hayo basi, huimarisha fikira za **2:4-6**.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

***Mambo hayo uyaagize na kuyafundisha . . . bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi:*** 1. **4:11-16** hutoa "maagizo 10" (au, "misimamo") inayoonyesha "nidhamu ya kiroho" (m,y; **4:7b-10**) kwa kiongozi wa kanisa. Kila amri iko katika mpangilio kama ifuatavyo: (1) "Uyaagize" mambo haya, **4:11**; (2) "Uyafundishe" mambo haya, **4:11**; (3) "Mtu yoyote asiudharau" ujana wako, **4:12**; (4) "Uwe" mfano, **4:12**; (5) "Ufanye bidii" katika kusoma Maandiko, **4:13**; (6) "Usiache" kutumia karama iliyomo ndani yako. **4:14**; (7) "Uyatafakari" hayo **4:15**; (8) "Ukae" katika mambo hayo **4:15**; (9) "Jitunze" nafsi yako na mafundisho yako **4:16**; (10) "Kujiokoka" katika mambo hayo. **4:16**.

2. Maagizo haya 10 yaweza kuwekwa katika makundi kulingana na mada kuu ambazo Paulo amekuwa akiziibua kote katika 1 Timotheo. Paulo amekuwa akikazia *kile tunachoamini na kufundisha* (ona, **1:3-11; 3:16-4:7a**), na *tabia ya maisha yetu* (ona **1:5; 2:8-3:15**). Katika yote, kuhusiana na yote mawili kuamini na kuishi, Amekuwa akimhimiza Timotheo *kudumu, uaminifu, kuvumilia* (ona **1:16, 18-20; 4:7b-10; 6:20-21**). Vivyo hivyo, maagizo 1, 2, 5, na 9b, yote huhusiana kimsingi na mafundisho, kuamini, au ufundishaji. Maagizo 7, 8, 9 (kiujumla wake), na 10 yote huhimiza kudumu, uaminifu, na uvumilivu.

3. Maagizo ya "mafundisho" yanahusu kila kipengele cha maisha yetu. Wakati mwandishi wa Biblia anaporudia mwenyewe, lengo kikawaida huwa ni kukazia jambo la muhimu. Hilo hasa huwa wakati mwandishi ananzia orodha ya maagizo kwa kusema kitu kimoja, na kunmalizia kitu hicho hicho. Umuhimu unaimarishwa zaidi wakati hoja hiyo hiyo inapatikana mwanzoni, mwishoni, na pia kati kati ya orodha. Paulo amelifanya hilo hapa na "mafundisho" ambalo linapatikana mwanzoni. (**4:11**), kati kati (**4:13**), na mwishoni (**4:16**) mwa maagizo yake 10 ya nidhamu ya kiroho. Inashangaza kuona kufundisha kunaambatana na nini katika kila mstari. Katika **4:11** kufundisha kumeambatana na "maagizo" (au "amri") kwa mambo hayo. Kwa maneno mengine, Injili pamoja na yote yanayoendana nayo kuhusu yale tunyotakiwa kuamini na jinsi tunavyotakiwa kuishi siyo "vya kujiamulia." Kwa Wakristo, haya ndiyo maisha yaliyopangwa na Mungu, na mtu anayetangaza Injili anapaswa afanye hivyo kwa mamlaka na mwenendo wa umakini mkubwa. Katika **4:13** Paulo anaunganisha kufundisha na kusoma hadharani kwa Maandiko na "kuhimiza." Kwa maneno mengine, mamlaka ya kuhubiri kwetu yanatokana katika Neno la Mungu, Biblia. Si mamlaka yetu wenyewe kama wachungaji au viongozi wa makanisa. Watu wanapaswa kuhimizwa wafanye *nini,* lakini pia wanhitaji kufundishwa ni *kwa nini* na *jinsi* ya kufanya. Kama *hawaelewi* vizuri nini kinachosemwa na Biblia, hatuwezi kuwategemea *kufanya* kile kinachosemwa. Katika **4:16** Paulo anaunganisha kufundisha na "Wewe mwenyewe," m.y., maisha yako mwenyewe. Mamlaka halisi ya mchungaji yanatokea kimsingi kwenye Neno la Mungu. Hata hivyo, kama maisha yake hayaendani na lile Neno, ndipo watu wanaomsikiliza hawatamwamini wala kumfuata. Kwa hiyo, maisha yetu ni lazima kabisa yaendane na kile tunachokisema. Hatuwezi "kuagiza" au "kusihi" wengine kufanya chochote ambacho sisi wenyewe hatukifanyi.

4. Maagizo yahusuyo "tabia/mwenendo" hayaamwathiri mtu binafsi peke yake, bali yanaathiri huduma na watu wengine. Watu wazee kikawaida hupenda "kuwadharau " vijana, kwa sababu vijana huelekea kupungukiwa ufahamu na uzoefu unaotokana na umri, au hekima inayotokana na ufahamu na uzoefu. Ufumbuzi wa Paulo kwa tatizo hili katika **4:12** kimsingi "tabia ina nguvu zaidi ya umri na uzoefu." Matokeo yake, kama kijana kiongozi ni *"kielelzo kwa waaminio"* katika maeneo muhimu ya *usemi, mwenendo, upendo ,imani , na usafi,"* ndipo watu wote, hata wazee, watamtazama yeye. Ikiwa ile tabia ya kumfanania Kristo ya kiongozi itaangaza, hata wazee watawaza, "laiti kama mtoto wangu angelikuwa kama huyu" (au hata, ningependa mimi mwenyewe niwe kama huyu"). Kama vile Kristo alivyo mfano wetu (**1:16**). Matendo hunena kwa sauti zaidi ya maneno. Kama tutasema maneno yote sahihi, lakini maisha yetu wenyewe hayafanani na yale tunayoyafundisha, tunayoagiza, na kuhimiza, basi ushuhuda wetu wa maisha yetu utazamisha yale tuyasemayo. Kwa upande mwingine, ikiwa sisi hatujajaliwa kipawa cha usemaji, lakini maisha yetu yakaangaza popote kama vielelezo vya tabia ya kumfanania Kristo, basi Mungu atatumia hayo kujaziliza maneno yetu, na wasikiaji wetu wataelewa, wataamini, na kutufuata.

5. Maagizo yanayotuelekeza sisi kuendelea kudumu na kuwa waaminifu yanahusisha maeneo yote ya maisha yetu, nayo hudumu siku zote za maisha yetu. Katika **4:15** neno la Kiyunani *meleta,* lililotafsiriwa "uyatafakari", katika Biblia ya NASB linabeba pia wazo la "kuboresha kwa umakini au kujifunza," "kutenda," "kutumia," na pia wazo la "Elekeza akili kwenye," "fikiria," "tafakari juu ya." Uwepo wetu wote—mwilii, akili, na nafsi—huhitaji kuhusishwa kama tunataka kuwa aina ya watu ambao Mungu anawataka (na anawatarajia) viongozi wa kanisa lake wawe. Hilo linatuongoza tulikotoka katika agizo lifuatalo katika **4:15** ambalo kimsingi linasema *"ukae katika"* mambo hayo, na katika **4:16** panaposema *"jitunze nafsi yako."* Umuhimu wa kutoanguka—hoja aliyoanza nayo Paulo katika kitabu (**1:18-20**), na ambayo itahitimisha kitabu (**6:20-21**)—inasisitizwa katika **4:16**, ambayo inatuhimiza kwenye *uvumilivu.*

6. Kote **4:15** na **4:16** panaonyesha kuwa uaminifu *wetu* unagusa *watu wengine.* Kwanza, wengine *wataona maendeleo yetu* tunavyoendelea kumfanania Kristo na kukaribia kwenye lengo. Siyo tu maendeleo yetu

*yatakuwa* ni *"dhahiri kwa wote,"* lakini *yanapaswa kuwa* dhahiri kwa wote. Pili, uaminifu wetu *"utaiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia."* Mojawapo ya umuhimu wa uaminifu ni, iwapo maisha ya Timotheo na mafundisho yake yanadumu kuwa kielelezo cha Kristo, "yeye na wasikilizaji wake wataokolewa, na athari za walimu wa uongo. Walimu hao sio tu walifundisha mafundisho ya uongo, bali pia waliishi maisha yaliyokuwa yasiyofaa. Kama Timotheo atajitunza katika kuishi maisha ya utauwa na kufundisha na kuhubiri mafundisho yaliyo masafi, atawalinda wale anaowafundisha kutoka katika hali ya kuchafuliwa na mafundisho yao." (Ngewa 2009: 106) Ndivyo ilivyo na kwetu. Hii ina matokeo ya *umilele*. Mungu amewapatia viongozi wa kanisa lake wajibu wa ajabu mno kwa ajili ya roho za watu na uzima wa milele kwa wanaume na wanawake. Ni mwito mkuu zaidi ambao mtu anaweza kuwa nao. Hivyo inahitajika maeneo yote ya maisha yetu kuwa katika uaminifu kwa Mungu na kwa wengine daima tuishivyo. Kma tukifanya hivyo, matokeo yatakuwa ni baraka zisizohesabika na furaha ya milele, kwa ajili yetu na wale tuliowachunga.

**<u>1 Tim 5:1-6:21—Matatizo ya Kiutendaji na Mambo Yawakabiliyo Viongozi wa Kanisa</u>**

**<u>5:1-2:</u>** ***Mzee usimkemee bali umwonye kama baba,na vijana kama ndugu, wanawake wazee kama mama, wanawake vijana kama ndugu wa kike, katika usafi wote.***

***Mzee usimkemee, bali umwonye kama baba, na vijana kama ndugu, wanawake wazee kama mama, wanawake vijana kama ndugu wa kike:*** 1. <u>Aya hii inasisitiza kwa nguvu wazo la kanisa kuwa kama familia,</u> <u>ambalo Paulo alilitaja katika **3:4-5** na **3:15**.</u> Hapa Paulo ameweka bayana kabisa jinsi ambavyo tunapaswa kuwaangalia waumini wa familia ya kanisa letu. Daima wachungaji na viongozi wengine wa makanisa wanapenda kuwa mbali na watu wengine wa ushirika. Kutoka madhabahuni, wachungaji wanaweza pasipo kujua, wakajifikiria kama wako "hapa juu," na wengine wote kama watu wa kawaida wa "kule chini." Ingawa, kama kweli tunaangalia wazee na kuwaona kama wale baba zetu waliotuzaa kidunia, na wanawake wazee kama wakina mama wa duniani waliotuzaa, na wanawake vijana kama dada zetu wa duniani, watu katika ushirika watakuwa "wa udugu zaidi" kwetu. Tunaweza hata kuanza kuwachukuliia kama wapendwa wa familia halisi.

2. <u>Kwa kutofautisha vijana na wazee, wanaume na wanawake, Paulo pia anatambua tofauti ya watu wanavyopaswa (na wanaweza) kuhudumiwa katika njia zinazotofautiana.</u> Ingawaje neno kwa ajili ya "mtu mzee" (Kiyunani = *presbuteros*) linaweza pia kutumika kwa "mzee" kwa maana ya "mtu atendaye katika ofisi ya mzee au mwangalizi katika kanisa" (kama ilivyotumika katika **5:17, 19**), muktadha hapa ni (my., utofauti wa vijana wadogo, wanawake wazee, na wanawake vijana) unaweka bayana kwamba maana katika **5:1** kwa ufupi ni "mtu mzee." Watu wote, bila kujali umri au jinsia, wanapaswa kuonyeshwa kuwa wanapendwa na kuheshimiwa. Hata hivyo, huwa kiasilia tunaonyesha (na tunapaswa kuonyesha) kiwango fulani cha heshima na tofauti kwa wazazi wetu (na watu wazee kwa ujumla) ambayo hatuionyeshi kwa kaka na dada zetu (au wenye umri mdogo kiujumla). Kwa upande mwingine, twaweza kuwa "huru zaidi" kwa wadogo zetu (na wenye umri mdogo kwa ujumla, hasa vijana wadogo). Mipangilio hii hutenda kazi kanisani pia, kwani familia ni kanisa.

3. <u>Watu hawapaswi kukemewa au kukaripiwa kwa ukali, hata kama wamekosea, bali wanapaswa kuinuliwa na kurejeshwa.</u> Maana iliyofichika ya neno lililotafsiriwa "kukaripia kwa kukemea " kimsingi ni "kupiga." Viongozi wa kanisa hawapaswi kufanya hivyo. Hivyo, kule *"kusihi"* kunaandamana na aina zote nne za watu walioorodheshwa katika **5:1-2.** Neno lililotafsiriwa *"kusihi"* ni neno la Kiyunani *parakale*ō. Hili ni neno la kivitendo la neno lililotafsiriwa kama "kusihi" katika **4:13**. Limetafsiriwa daima kama "kusihi" au "kutia moyo," lakini pia limebeba maana ya "kuomba," "kutafuta," "kufariji," "kutia moyo," na pia hata "kumuhudumia mtu kiungwana, kiheshima, au kirafiki" (Danker 2000: 764-66). Wakati unaenda kushauri watu au kusahihisha makosa, viongozi wa kanisa wanapaswa wakumbuke "kuinena kweli katik upendo" (**Efe 4:15**). Pande zote mbili za hilo ni muhimu: kweli ikinenwa pasipo upendo si kweli halisi; upendo ukitolewa bila ukweli siyo upendo halisi. Ndiyo maana ni muhimu kwa viongozi wa kanisa kuwa na unyoofu wa kiroho (**4:7b- 16**). Ndipo maneno watakayosema, na jinsi wanavyoyasema, yatakuwa picha halisi ya Neno la Mungu lililotafakariwa katika tabia ya mtu anayemfanania Kristo kimaisha.

4. <u>Hasa wakati wa kuwasahihisha wazee, kuna mbinu zinazoweza kuwasaidia watu wenye umri mdogo walio katika nafasi ya uongozi wa kanisa.</u> Kuna mambo kadhaa ambayo mchungaji kijana anaweza kufanya anaposhughulika na mtu mwenye umri mkubwa kanisani ambaye analeta matatizo. (A) Paulo analitaja katika **4:12**, ikiwa mchungaji ni kielelezo cha mfano wa Kristo katika usemi, mwenendo, upendo, imani na usafi, mamlaka yake na kiwango cha heshima yake kitaongezeka sana. Hapo kiongozi kijana anaweza kushughulika na huyo msumbufu sio tu kwa mamlaka ya nafasi yake kanisani, bali hata kwa mamlaka ya maisha yake matakatifu. (B) Usiseme na mtu ukiwa peke yako, bali nenda na wazee (iwe ni wazee wa kanisa, au hapana) ambaye huyo mtu asumbuaye anamheshimu na kumstahi. Kumwendea mtu ukiwa na "nguvu ya uwingi"

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

ulidokezwa na Yesu katika **Mat 18:15-20**. Uendapo na watu wengine wenye heshima, ikiwa huyo mtu asumbuaye hatakusikiliza, anaweza akawasikiliza hao wengine. Wanaweza wakamkabili kwa namna ambayo hukuiwazia wewe. Lile wazo la "wazee wa kijiji" ambao wanastahiwa na wote, ambalo bado linaheshimiwa kila mahali Afrika, ni muktadha ambao unapaswa kutumiwa zaidi katika kanisa. (C) Mkabala kwa mtu asumbuaye kwa mamlaka ya neno la Mungu. Maandiko yana mengi yanayozungumzia jinsi tunavyopaswa kuwa tunaishi. Kwa mfano, **Tito 2** maelekezo kwa wazee, wanawake wazee, na wanawake vijana. Kwa kuonyesha na kujadili Neno la Mungu na mtu huyo ambaye amekuwa akileta tatizo, anaweza akatambua kwamba tabia yake kimsingi haipingani na wewe, wala kanisa, bali inapingana na Mungu. Katika yote haya, hata hivyo, kumbuka kuwa hoja ya ushauri na kuonya huko ni "kumpata nduguyo" (**Mat 18:15**) arudi kwenye uzima mzuri, wa upendo, wenye kuaminika wa Kristo.

***Katika usafi wote:*** 1. Paulo anajumuisha usemi huu muhimu mwishoni mwa kifungu hiki kwa sababu ya majaribu ya kimapenzi siku zote yapo, na dhambi ya zinaa yaweza kumaliza huduma ya mtu, familia, na kanisa. Dhambi ya zinaa yaweza kuwa tatizo kubwa sana kanisani. Inaweza kuharibu heshima na huduma ya mtu awe ni mwana mme au mwana mke. Dhambi ya zinaa ndiyo usailiti wa uaminifu tuliopewa na Mungu. Hata hivyo, mtu anaweza kusema ya kwamba kanisa ni familia (haswa, ni familia ya Mungu), dhambi ya uzinzi ikiwa kanisani ni chukizo na laana kwenye jamii ya Mungu

2. Kanisa linapaswa kuwa na miongozo na sheria zinazosaidia kuzuia dhambi ya uzinzi kutokea. Watu wote wanayo nguvu ya dhambi ikaayo ndani mwao. Kwa hiyo, hata kama tunadhani "haitanitokea kwangu," inaweza. Ndiyo maana Paulo anawonya hasa viongozi wa kiume kuwatendea washirika wa kike kama vile wanavyowatendea mama na dada zao wenyewe *"katika usafi wote."* Kanisa linaweza likaweka sheria fulani zitakazosaidia swala hili. Sheria kama hizo zaweza kuwa na mambo kama yafuatayo: kiongozi wa kiume asiwe peke yake na mwanamke, hasa ikiwa milango imefungwa au ni ndani; kiongozi wa kiume ashughulike na mtu wa kike ndani ya eneo la kanisa au katika eneo la nje ambapo wengine wanaweza kumwona; wanawake wenye heshima kanisani wafundishwe na kuelekezwa vizuri kuweza kusaidia na kushughulikia matatizo ya wanawake wengine; kama ushauri wa ndoa utafanyika, mchungaji siku zote lazima awe na mke wake, au mwanamke mwingine anayesheshimika pamoja naye, na ushauri huo daima ufanyike kwa wanandoa wote wakiwa pamoja. kanuni tofauti zinaweza kutungwa kulingana na mazingira tofauti. Moja inaweza ikafanya kazi katika kanisa moja, lakini isifanye kwenye kanisa jingine. Hata hivyo, makanisa yote yanahitaji kufikiria swala hili na kufanya kitu *mapemma* kuhakikisha sheria na taratibu zipo kuwasaidia jaribu hilo ambalo siku zote lipo, lisije likafumuka kuwa moto wa dhambi kamili. Kiongozi wa kanisa moja anapaswa kutafuta makanisa na madhehebu mengine yanafanya nini kushughulikia swala hili. Hatari ni kubwa mno—kwa viongozi, wanawake, familia, kanisa, jina la Yesu katika jamii—haipaswi kuachwa tu.

**5:3-16:** ***3Uwaheshimu wajane walio wajane kweli kweli. 4Lakini mjane akiwa ana watoto au wajukuu, na wajifunze kwanza kuyatenda yaliyo wajibu wao kwa jamaa zao wenyewe, na kuwalipa wazazi wao. Kwa kuwa hili lakubalika mbele za Mungu. 5Basi yeye aliye mjane kweli kweli, ameachwa peke yake, huyo amemwekea Mungu tumaini lake, naye hudumu katika maombi na sala mchana na usiku. 6Bali, yeye asiyejizuia nafsi yake amekufa ingawa yu hai. 7Mambo hayo pia uyaagize, ili wasiwe na lawama. 8Lakini mtu ye yote asiyewatunza walio wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini. 9Mjane asiandikwe isipokuwa umri wake amepata miaka sitini; naye amekuwa mke wa mume mmoja; 10naye ameshuhudiwa kwa matendo mema; ikiwa amelea watoto, ikiwa amekaribisha wageni, ikiwa amewaosha watakatifu miguu, ikiwa amewasaidia wateswao, ikiwa amefuata kwa bidii kila tendo jema. 11Bali wajane walio vijana ukatae kuwaandika hao, maana, wakizidiwa na tamaa kinyume cha Kristo, wataka kuolewa; 12nao wana hukumu kwa kuwa wameiacha imani yao ya kwanza. 13Tena, pamoja na hayo, hujifunza kuwa wavivu, wakizunguka-zunguka nyumba kwa nyumba; wala si wavivu tu, lakini ni wachongezi na wadadisi, wakinena maneno yasiyowapasa. 14Basi napenda wajane, ambao si wazee, waolewe, wazae watoto, wawe na madaraka ya nyumbani; ili wasimpe adui nafasi ya kulaumu. 15Kwa maana wengine wamekwisha kugeuka na kumfuata Shetani. 16Mwanamke aaminiye, akiwa ana wajane, na awasaidie mwenyewe, Kanisa lisilemewe; ili liwasaidie wale walio wajane kweli kweli.***

"Lengo la kimsingi la Paulo katika kifungu hiki ni kumsaidia Timotheo kutofautisha kati ya wajane ambao kanisa linapaswa kuwasaidia na wale ambao halipaswi kuwasaidia. . . . Paulo anafundisha kwamba mjane wa kweli, mjane wanayepaswa kumsaidia, lazima peke yake, asiye na uwezo wa kusaidiwa na famia zao, na hayuko tayari kuolewa tena. Anapaswa kuwa mwanamke mcha Mungu aliyeweka tumaini lake kwa Mungu, utauwa unaothibitika kwa mwenendo wake, kama vile kuwa na juhudi katika maombi, kuwa mwaminfu kwa

mume wake, kulea watoto wake, kuonyesha ukarimu, kutawadha miguu ya watakatifu, kuwasaidia waliodhurika, na kujidhatiti kuishi maisha ya matendo mema. Pia, kwa sababu tatizo la kanisa la Efeso lilihusisha wajane wenye umri mdogo, Paulo anasema mjane angalau awe na umri wa miaka sitini kama anataka kuorodheshwa. Hii haina maana kwamba kanisa liwapuuzie wajane ambao hawana vigezo hivi. Ni kumaanisha kwamba kanisa halikupaswa kujiingiza kwenye mkataba wa kimaisha yote na wajane wasio wa aina hii." (Mounce 2000: 299)

***Waheshimu wajane ambao ni wajane kweli kweli:*** Neno "heshimu" na neno "kweli kweli"ni muhimu . (Kwenye ESV panasema *"Waheshimu wajane ambao ni wajane kweli kweli."* Biblia ya NKJV inasema *"Waheshimu wajane ambao ni wajane halisi."* Neno "kweli kweli" au "halisi" ni maneno mhimu yanayoleta sifa hapa.)

1. <u>Neno hilo hilo la Kiyunani, "heshimu," katika muundo wa kitenzi, au jina limetumika katika **5:3, 5:17,** na **6:1**.</u> Ingawaje ni neno hilo hilo limetumika, miktadha mitatu ambayo neno hilo limetumika yote inatofautiana—na muktadha unaonyesha kwamba neno "heshimu" lina maana ya kitu tofauti katika kila mara. Katika **5:3** muktadha unaonyesha bayana kwamba "kuheshimu" kunahusisha *vitu vya kuwasaidia* wajane wenye uhitaji. Hilo limeonyeswha katika **5:4-5**, ambalo linazungumzia kuhusu wajane wenye watoto au wajukuu kinyume na wale walio peke yao na hawana njia yoyote ya kuwasaidia. Wakati **5:4** panasema watoto wanapaswa *"kuwalipa wazazi wao,"* kinachosemwa hapo ni kwamba "watoto siyo kwamba wanawapatia kitu kisicho haki yao wanapowatunza wazazi—*wanawalipa deni*" (Ngewa 2009: 114). Vivyo hivyo **5:8** panaonyesha wana-familia wanao wajibu wa kimaadili *"kuwahudumia wa kwao."* Kushindwa kufanya hivyo kunamfanya mtu *"mbaya kuliko asiyeamini."* **5:16** panajumuisha kifungu hiki chote kwa kurudia kuwa wale wenye wajane wa kuwategemea *"wanapaswa kuwasaidia"* ili kwamba *"kanisa [li] silemewe, ili kwamba liweze kuwasaidia wale ambao ni wajane kwelikweli."* Katika **5:17** "kuheshimu" kunazungumzia kanisa kumlipa mchungaji, kama **5:18** panavyoweka wazi jambo hilo. Katika **6:1** "kuheshimu" kunaonyesha "heshima" (kwa kufanya kazi kwa juhudi, kufanya kitu bila kuchelewa, nk.), kama **6:2** inavyoweka wazi. Muktadha siku zote huubua maana. Hiyo ni kweli kwenye Biblia kama ilivyo pia kweli kwa maandishi mengine (ona mjadala katika **1:5**).

2. <u>Neno "halisi" ("kweli," "kamili") inaonyesha kuwa Paulo analeta utofauti kati ya aina za wanjane.</u> Kwa maelezo, mjane ni mwnamke yeyote mabaye mume wake amefariki. Kwa tafsiri, mwanamke yeyote ambaye mume wake amefariki ni "mjan halisi" ama "mjane kweli" au "mjane kamili". Kwa hiyo, kwa maana mojawapo, kila mwanamke ambaye mume wake amekufa ni "mjane kweli", au "ni mjane wa kweli" au "mjane halisi." hata hivyo, hoja ya Paulo hapa si kufafanua wajane ni nani. Hoja ya aya hii ni kuelezea ni mjane gani kanisa lina wajibu wa kuwasaidia vitu. Paulo alitambua kwamba, katika siku zake kama zilivyo zetu, kanisa linaweza lisiwe na rasilimali za kumsaidia kila mtu mhitaji. Pia, kuna wajane ambao hawahitaji kusaidiwa. Hivyo basi, Paulo anatupatia mwongozo wa kutofautisha wajane wale ambao kanisa linapaswa kuwasaidia, na wale ambao kanisa lhalipaswi kuwasaidia. Kusema ukweli, sehemu iliyobakia ya kifungu hiki (m.y., vifungu 4- 16) kimsingi hufafanua aliye mjane "kweli kweli."

3. <u>Kifungu hikii ni *mfano* wa aina mojawapo ya kundi la watu wahitaji.</u> Wajane ndio waliokuwa ni watu rahisi kudhuriwa na walikuwa tegemezi katika jamii ya nyakati hizo kwa sababu walikuwawanawategemea waume zao kabisa. Ukweli kwamba kanisa linapaswa kuwatunza wajane wa aina fulani, haina maana kwamba kanisa lisiwasaidie watu wengine wenye uhitaji. Paulo anatoa maelezo ya kiundani ya kanuni iliyotajwa katika **Yak 1:27,** *"Dini iliyo safi isiyo n a taka mbele za Mungu Baba ni hii: kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa."* Ukweri wa kuwa kwamba maongeo ya Paulo kuhusu "wanjane" katika **5:3-16** ni *mfano* wa aina ya watu walio na mahitanji ambao kanisa linafaa kusaidia inayoonekana katika **5:4** inayonena kuhusu "wazazi," na tena katika **5:8** inayonena kuhusu mtu anayehudumia "kwa watu wa nyumba yake." Habari zote mbili zinaelekeza msimamo wa kusaidia walio na ma hitanji zaindi ya "wanjane" Kanuni ambazo Paulo anazijadili zinaweza kutumiwa na kuingizwa kwenye matabaka mengine ya watu wahitaji, kama vile wazee; wasio na ajira; yatima; wagonjwa wa akili; watu wenye HIV/UKIMWI, nk.

4. <u>Kifungu kina sehemu tano za viungo kulingana na mlinganisho kati ya wale ambao kanisa linapaswa kuwasaidia na wale ambao kanisa halipaswi kuwasaidia.</u> (A) Waheshimu wajane ambao ni wajane kweli kweli (**5:3**)—lakini wale walio na familia wanapaswa kusaidiwa na familia zao (**5:4**). (B) Mjane wa kweli ameachwa peke yake, ameweka tumaini lake kwa Mungu, na kudumu katika maombi na sala (**5:5**)—bali walsiojizuia nafso zao tayari wamekufa (**5:6**). (C) Yaagize mambo haya ili kwamba wasiwe na lawama (**5:7**)—lakini mtu asiyewatunza wa nyumbani mwake ameikana Imani na ni mbaya kuliko asiyeamini (**5:8**). (D) Wajane walio watauwa, wenye umri angalau wa miaka 60 uwaorodheshe. (**5:9-10**)—bali usiwaorodheshe wajane vijana

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

kwenye orodha kwa sababu wanaweza kuolewa tena (**5:11-13**). (E) Muhtasari: wajane vijana wanpaswa kuolewa tena (**5:14-15**); wale walio na familia wanapaswa kusaidiwa na familia zao (**5:16a**)—lakini kanisa linapaswa kuwahudumia walio wajane "kweli kweli" (**5:16b**).

5. Kifungu kinashughulikia watu wa aina tatu, waliowekewa mabano pande zote kuhusu "wajane kweli kweli," kama ifuatavyo:

**5:3**—*Kuhudumia "wajane kweli kweli"*

**5:4, 7-8, 16a**—Wajibu wa familia mbele za wajane

**5:5, 9-10**—"Wajane kweli kweli"

**5:6, 11-15**—Wajane na wajane wale wanaoishi kiuhuru tu

**5:16b**—*Kanisa litasaidia "wajane kweli kweli"*

6. Kutokana na aya hii kanuni mbili zinaibuka. (A) *Zingatia hitaji la mtu*. Je mtu anayehitaji msaada ni "mhitaji kweli kweli," au ana wana ndugu au njia nyingine ya kuweza kumsaidi? Siku hizi kuna mafao ya serikali, bima, pensheni, urithi, au vyanzo vingine vya msaada vyaweza kuwako. (B) *Zingatia mwenendo wa mtu, tabia, au maisha yake anavyoishi.* (1) Je mtu huyo ni mnyenyekevu au ana kiburi ? Je ana mpango kuendelea na mtindo wake wa maisha ya dhambi au hapana? Je anamtumaini Mungu au hapana? (2) Watu wengi wanaokuja kanisani kutaka msaada hawatakuwa Wakristo na huenda wameishi maisha ya dhambi sana. Kama watu hao watakuja kanisani kwa unyenyekevu, kanisa lijaribu kuwasaidia. Kwa kuwasaidia hao, mwanya unafunguka wa kuwashuhudia kuhusu Yesu.

***Mjane asiandikwe, isipokuwa umri wake umepita miaka sitini:*** 1. "Kutimiza miaka 60" si yo "Sheria" ya kufuatwa dunia nzima. Mkanisa mengine yanatekeleza hili kama amri tu, kama agizo kwa makanisa yote kwa leo. Hata hivyo, kuelewa historia na muktadha wa tamaduni kunatupatia picha nzuri zaidi (ona mjadala **2:9-10**). "Ni muhimu kukumbuka kwamba Waefeso, kama wengi katika Afrika leo, walikuwa kwa ujumla hawajui umri wao. Jamii zao hazikutunza kumbukumbu halisi za kuzaliwa kwao. Kwa hiyo, umri wa miaka sitini ulikuwa ndio namba ya makisio kwa Paulo kwa sababu katika tamaduni ya Kiyahudi, ulikuwa ndio umri wa kuanzia uzee." (Ngewa 2009: 112) Kusema ukweli, miaka sitini ndio umri uliotambulika na ulimwengu wa kale kwamba mtu alichukuliwa kuwa kama "mzee" (Knight 1992: 223). Miaka sitini "labda inaonyesha kiwango cha juu zaidi cha umri ambacho mtu alichukuliwa kuwa ana uwezo wa kufanya kazi na kuweza kujihudumia" (Blomberg 1999: 209). Katika karne ya kwanza chinin ya 4% ya wanawake waliweza kuishi kufikia miaka 50 (Lysaught 2005: 67n.18). Walikuwa miongoni mwa watu wa mwisho, na walikuwa na rasilimali chache za kuzitegemea. "Mwanamke akifikisha miaka sitini, kulikuwa hakuna nafasi kwamba ataolewa tena" (Ngewa 2000: 112). Kinyume chake, leo, angalau katika nchi za Magharibi, miaka 60 haitazamwi kama ni "uzee." Zaidi ya hayo, kuna serikali nyingi na vyanzo vingine vya kuwashughulikia wazee ambavyo havikuwepo nyakati za Paulo wala katika tamaduni zao. Matokeo yake, swala la miaka "sitini ya uzee" lilimaanisha kitu tofauti sana na ilivyo katika tamaduni nyingi leo. Mwisho, upana wa mkitadha wa Biblia nzima hapendekezi kwamba namba sitini au umri wa miaka sitini, una umuhimu fulani (lakini k.m., **Law 27:1-7** ambapo kulikuwa na na mizani ya kupimia kwa ajili ya gharama ya kukombolea watu walioweka viapo vigumu; gharama ilikomea kwa wenye umri wa miaka sitini). Mambo haya ya kuzingatia yanaashiria kwamba sifa ya umri wa miaka 60 haitakiwi kuchukuliwa katika ulimwengu mzima kama "Sheria," bali yaweza kubadilishwa kulingana na mazingira yatakayokuwapo.

2. Inawezekana kwamba *"orodha"* iliyotajwa katika **5:9** inazungumzia wajane ambao walikuwa wameorodheshwa katika kazi ya huduma fulani rasmi kugharimia msaada wa kusaidiwa na kanisa. "Huenda ikawa, ili *kuorodheshwa* kulihitajika mfumo wa usajili wa wajane kwa kulingana na kujitoa kwao kanisani, na kujitoa kwa kanisa katika kuwasaidia wajane kipindi chote wakiwa hai. Paulo hakutaka orodha yake iwe ndefu mno, vinginevyo kanisa linaweza kushindwa kutimiza ahadi yake. Kwa hiyo alifupisha orodha kwa ajili ya wajane wenye umri zaidi ya sitini. Hata hivyo, hasemi kwamba kanisa lisiwasaidie wajane vijana nyakati za shida nzito." (Ngewa 2009: 112-13) Waandishi wengi wanaamini kwamba "orodha hiyo" ilihusu "utaratibu au idara ya wajane" ambamo wajane walioandikishwa walipewa kazi za kikanisa na huduma ya kukirimu wengine kama malipo ya misaada ya vitu wanavyohudumiwa na kanisa. Hii ni kwa sababu zile sifa katika **5:9-10** hazifanani na zile za **5:5**, na sifa zilizotajwa katika **5:9-10** zinafanana na zile za huduma za kawaida kanisani (ona **1 Tim 3:1-13**). Kusema kweli, kanisa la karne zilizofuata lilitengeneza mfumo huu wa utaratibu wa wajane uliotokana na kifumgu hiki. "Utaratibu huo wa wajane ulidumu vizuri hadi karne ya nne. Lakini iliongezeka katika maeneo tofauti ya Ukristo wa Uyunani na wa Kilatini ile ofisi au huduma ya mahsemansi, kama sehemu ya mchepuo wa 5:3-10. Wanawake viongozi walifikiriwa kuwa wanafaa sana kwenye huduma ya maombi na maswala ya utekelezaji, kuchanganya na zile ambazo zilikuwa haziwafai wanaume kuhusishwa—hususan kutoa ushauri, kutembelea, kuwekesha wakfu au kubatiza wanawake wengine." (Blomberg 1999: 209) Ingawaje

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

muktadha hauagizi kiukali tafsiri hiyo, kwa vile kihistoria kanisa liliwatumia wajane katika huduma kulipia misaada ya vitu walivyopewa, kanisa leo linapaswa kufikiria kutenda jambo kama hilo. Wazee wana hazina ya uzoefu na hekima mbazo zinaweza kutumiwa kwa ajili ya kujenga na kuimarisha mwili wa Kristo.

3. Kanisa linapaswa lijaribu kuwasaidia masikini na wahitaji ili waweze kujikimu. (A) *Watu wengi wahitaji wangefaidika zaidi kama wangewezeshwa kujitegemea binafsi kuliko kuomba misaada*. Kanisa lenyewe linaweza kuwa na uwezo wa kuwalipa watu wa usafi na kufyeka majani au kazi nyingine za kanisa. aadhi ya mapendekezo ni pamoja na: (1) Kutoa mikopo midogo-midogo kwa watu wenye uhitaji. Hili linatakiwa kwamba wahudumiwa wawe na miradi fulani iliyokubalika. Pia italazimu hatua za ufuatiliaji na uwajibikaji. Tatizo moja kubwa ni mikopo kutokulipwa. (2) Toa ajira kwa watu wenye uhitaji. Hili litalazimu kujua ni nani katika washirika wako anaweza kuwa na biashara, anahitaji mtu wa kumsaidia nyumbani, auvinginevyo anaweza kutoa ajira kwa wengine. Muktadha wa "utaratibu wa wajane" ni wazo jingine. (3) Uwapatie misaada isiyo ya kifedha. Kanisa linaweza kuwa "ghala" kama mahekalu ya zamani yalivyokuwa (ona **Mal 3:10**), kwa mavazi, vyakula visivyoharibika, au bidhaa zingine zinazohitajika. Kanisa linapaswa kujua ni mshirika gani katika ushirika ana uwezo wa kutoa chakula, nguo, au bidhaa nyingine kwa watu wenye mahitaji. Kanisa moja la PAG huko Uganda lilikuwa na wajane 43. Badla ya kuwapatia pesa, liliwanunulia mbuzi. Baada ya miaka miwili mbuzi wale 43 waliongezeka hadi kuwa mbuzi 281. Wajane wale wakawa na uwezo wa kujitosheleza wenyewe. Walikuwa na maziwa. Waliweza kuuza mbuzi ili kupata pesa. Matokeo yake, wajane wale walivutwa karibu zaidi na kanisa na wengi wao wamekuwa "wana-maombi" na watoaji waaminifu kurudishia kanisani. (B) *Kanisa linapaswa kujua vyanzo vingine vya misaada katika maeneo yao.* Kanisa la mahali haliwezi kuwa na uwezo wa kutoa vitu vyote kwa watu wote. Hata hivyo, linaweza likashirikiana na, au kuwakabidhi wenye mahitaji, kwa mashirika mengine yanayoweza kutoa vitu na huduma ambazo kanisa lenyewe haliwezi kutoa. (1) Vyanzo vingine vya mapato ni pamoja na: Wakala wa serikali; Asasi zisizo za kiserikali; mashirika ya misaada ya Kikristo na yasiyo ya Kikristo. (2) Madhehebu tofauti ya dini yana mawakala wa Huduma za misaada kwa Jamii. Kanisa la Kianglikana lina "Umoja wa Wa-mama." PAG huko Uganda wana "Sekretariet ya Mpango wa PAG na maendeleo." (3) Makanisa mbalimbali, na makanisa ya madhehebu tofauti, yanapaswa kufanya kazi pamoja kukidhi mahitaji ya maeneo yao. Kufanya hivyo pia kutaonyesha umoja, amabo ndio mwito na kusudi la kanisa.

**5:17-18:** ***17Wazee watawalao vema na wahesabiwe kustahili heshima maradufu, hasa wao wajitabishao kwa kuhutubu na kufundisha. 18Kwa maana andiko lasema, "USIMFUNGE KINYWA NG'OMBE APURAPO NAFAKA," na tena mtenda kazi astahili ujira wake."***

***Wazee . . . heshima maradufu:*** 1. Neno lilelile la Kiyunani, *presbuteros,* lilitumika katika **5:1** na sasa tena katika **5:17**. Hata hivyo, kama lilivyo neno "heshima," miktadha miwili tofauti huonyesha maana tofauti. Katika **5:1** neno limetumika kwa maana yake ya kawaida ya "mtu mzee." Hapa muktadha (wale *"watawalao vema . . .hasa wale wajitabishao kwa kuhutubu na kufundisha"*) huonyesha wazi kwamba neno lililotumika hapa ni kwa maana ya taaluma ya "mwangalizi, mchungaji, kiongozi wa kanisa."

2. Katika Biblia, makanisa yote yaliongozwa na wazee, sio mchungaji mmoja pekee. Katika **5:17** "wazee" ni uwingi. Vivyo hivyo, katika **4:14** wakati Timotheo alipowekewa mikono kuwa "kiongozi" (au, "kuwa katika baraza la wazee"). Huo ndio mkondo wa Kibiblia kwa uongozi wa kanisa: wazee wengi, siyo utawala wa mtu mmoja. Kila wakati kanisa linapotajwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume, na kila wakati Paulo na makanisa mengine mapya yalipoanzishwa, mara zote walichagua wazee kadhaa (ona **Mdo 11:30; 14:23; 15:2-6, 22-23; 16:4; 20:17-18; 21:18**). Hili linaonyesha hekima ya Ki-Biblia kuwa *"kwa wingi wa washauri, huja wokovu [au, hekima]"* (**Mith 11:14; 26:4**), na pia kama *"chuma inoavyo chuma, ndivyo mtu aunoavyo uso wa rafiki yake"* (**Mith 27:17**). Kuwa na viongozi wengi ni muhimu. Kila mmoja ana vipawa na uwezo tofauti; hakuna mtu anayejitosheleza peke yake. Wazee wakiwa wengi, hulindana kila mtu na mwenzake kimaadili, kiroho, na kifedha. Zaidi ya hapo, kama uongozi wa kanisa unashikiliwa na mtu mmoja tu, kama jambo fulani litotokea kwa mtu huyo, basi kanisa linaweza kuvunjika. Lazima kukumbuka kwamba kanisa si kutuhusu sisi, bali ni kuhusu Kristo. Kanisa ni mwili wake, sio wetu. Tunapaswa kuhakikisha kuwa kanisa linaongozwa vizuri na wanaume na wanawake wenye sifa zinazostahili (**3:1-13**), ili kwamba jambo lolote likitokea kwa mchungaji au kwa kiongozi yeyote yule, kanisa liweze kuendelea vizuri tu, kwa sababu limejengwa juu ya msingi imara wa mfumo wa uongozi.

3. Muktadha wa *"heshima maradufu"* unahusika na kuwalipa wachungaji ambao wanahubiri na kufundisha vyema. "Maradufu" si lazima imanishe "mara mbili ya wanachopata wajane wa **5:3**," au "mshahara mara mbili." Hata hivyo, panapendekeza ama "heshima inayopaswa itolewe kwa kiongozi wa kanisa anayejitaabisha na pia fidia ya kifedha," au "kutolewa vitu vya kutosha" kwa ajili ya mchungaji mzuri na

mwenye sifa zifaazo. Ingawa miktadha yote miwili ya **5:3** na **5:17** inaonyesha kwamba "heshima" inaonyesha msaada wa vitu, kuna tofauti kati ya haya mawili. Katika **5:3** sifa mojawapo ya mjane kupewa msaada wa vitu ilikuwa, ni yule *asiye na uwezo* wa kujihudumia mwenyewe, na hana chanzo kingine chochote cha kumsaidia. Katika **5:17** ni wajibu wa kanisa kumtegemeza mchungaji wake *hata kama* mchungaji ana vyanzo vingine vya kumtegemeza. Umuhimu wa uwajibikaji wa kanisa katika kuwategemeza viongozi wao wazuri unaonekana katika **5:18**, ambayo inawanukuu wote Musa (ona **Kumb 25:4**) na Yesu (ona **Mat 10:10; Luka 10:7**). *Kiasi* cha fidia ni, kwa sehemu, kinaendana na kiasi cha ubora wa kazi yake (m.y; *"atawalaye vyema"* na *"anajitaabisha"*). Kama mchungaji ana vyanzo vingine vya kipato, anaweza kuamua kwa hiari yake kutoa kiasi au sehemu fulani ya fidia kwa kanisa. Hata hivyo, kanisa lianapaswa kutambua wajibu wake wa kuwahudumia vitu wale ambao wanawalisha kiroho (ona pia **1 Kor 9:7-14; Rum 15:27; Gal 6:6**).

4. <u>Agano Jipya halitaji kiasi au njia maalum ambayo kanisa linapaswa kumlipa mchungaji wake.</u> Kwa mfano, wachungaji katika makanisa mengine wanapokea mshahara kamili; wachungaji katika makanisa mengine wanapokea sehemu ya fungu la kumi au sadaka. Pamoja na hayi, kuna kanuni kadhaa ambazo zinapaswa kuongoza ushirika katika kuwalipa wachungaji wao: (A) *Mapato ya mchungaji yanapaswa kinamna fulani yaendane na wastani wa kipato cha kundi, labda kiwango cha mshahara wa mwalimu wa shuleni.* Kutakuwa na utofauti mkubwa kati ya makanisa tofauti, na kati ya wachungaji wa vijijini na mijini, kwa vile kipato cha washirika hutofautiana sana. Hata hivyo, kama kutakuwa na familia 10 tu katika kanisa la mahali, na kila familia inatoa fungu la kumi, kanisa hilo linapaswa kuweza kumtegemeza mchungji wake. (B) *Vijijini, kwenye maisha ya kilimo, ambako fedha ni adimu, wachungaji huko wanaweza kupewa mazao ya kilimo na wanyama.* Katika maeneo kama hayo, eneo fulani la shamba linaweza kutengwa kwa ajili ya kanisa au mchungaji. Maeneo kama hayo wachungaji wanaweza kulipwa kwa kufanyiwa kazi (k.m., kujenga nyumba kwa ajili ya mchungaji, kuchimba choo, kufanya kazi katika shamba la mchungaji, nk.). (C) *Mtume Paulo, kama mwinjilisti na kama mwanzishi wa makanisa, mara nyingine alifanya "kazi za kawaida" (kutengeneza mahema) ili kupata pesa akiwa kwenye huduma ya injili* (ona **Mdo 20:33-34; 2 Kor 11:9-12; 1 Thes 2:7-9; 2 Thes 3:7- 8**). Paulo pia alipokea zawadi kutoka kwa waamini (**2 Kor 11:8; Fil 4:14-18**). (D) *Kwa vile Paulo hakuwa mchungaji wa kanisa la mahali pamoja, mazingira yake sio lazima yafanane kama ya wachungaji.* Haijalishi, iwe wachungaji wanapanda au kuanzisha makanisa, au kama makanisa ni madogo na hayana uwezo wa kuwalipa wachungaji, mchungaji anaweza kufanya kazi za nje ili ajikimu kimaisha kama alivyofanya Paulo. Hata hivyo, kadiri kanisa linavyoendelea kukua, linapaswa lielekee katika kumlipa mchungaji wake mshahara kumwezesha kuishi kulingana na kanuni za Ki-Biblia zilizotajwa hapo juu. (E) *Makanisa (na, hasa, madhehebu) yanapaswa kuweka mfuko kwa ajili ya wachungaji wanapostaafu.* Wachungaji wengi wanaostaafu, au wanaotakiwa kustaafu, huacha huduma bila chochote. Madhehebu mengi, na hata makanisa binafsi, sasa wanaanza kutambua kuwa hiyo ni dhuluma kubwa. Matokeo yake, sasa wanaandaa mpango wa malipo ya uzeeni kwa ajili ya wachungaji wanaostaafu. Kiasi kidogo kila mwezi kikiwekwa akiba hatimaye kitakua na kuwa kikubwa sana baada ya miaka mingi. Hapa ni mswala yote mawili - uwakili mzuri wa pesa, na pia ni njia ya kuwaheshimu viongozi waliotumikia ushirika wao vyema. (F) *Kuna sababu kadhaa kwa nini ni vibaya mchungaji kuendelea kujitunza mwenyewe kwa ajira ya nje baada ya kanisa lake kukomaa vizuri:* (1) Kundi hapo linapata mwanya wa kukwepa wajibu wake wa Ki-Biblia wa kumtegemeza mchungaji wao. Matokeo ya hilo ni kupungukiwa baraka za kiroho na maono. (2) Kanisa linapeteza fursa ya kuhuduwa muda wote. Kutakuwa na muda mchache wa kuwatembelea, vipindi vya Biblia vya katikati ya wiki, na vipindi vingine vya katikati ya wiki. (3) Mchungaji na huduma yake itadhurika. Atakuwa na muda mfupi na nguvu kidogo za kujifunza, maombi, kutembelea watu, na mambo mengine muhimu ya huduma. (4) Kazi ya kidunia inaweza kuwa mtego unaoweza kumvuta mchungaji aache huduma yake kabisa. (5) Kanisa kutomhudumia mchungaji wake, kunaweza kusababisha mkondo mbaya wa kudumu. Itakuwa ni ngumu kwa wachungaji wapya kuingia wito wa uchungaji, kwa sababu ushirika huenda ukawataka, na wao pia, wawe wanajitegemea. (Hodges 1953: 81)

**<u>5:19-25:</u>** ***[19]Usikubali mashitaka juu ya wazee ila kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu. [20]Wale wadumuo kutenda dhambi uwakemee mbele ya wote ili na wengine waogope. [21]Nakuagiza mbele za Mungu na mbele za Kristo Yesu na mbele za malaika wateule, uyatende hayo pasipo hukumu kwa haraka; usifanye neno lolote kwa upendeleo. [22] Usisimwekee mtu mikono kwa haraka wala usizishiriki dhambi za watu wegine; ujilinde nafsi yako. [23]Tokea sasa usinywe maji tu, lakini tumia mvinyo kidogo kwa ajili ya tumbo lako na magonjwa yakupatayo mara kwa mara. [24]Dhambi za watu wengine zi dhahiri, zatangulia kwenda hukumuni; wengine, dhambi zao zawafuata. [25]Vivyo hivyo matendo yaliyo mazuri ya dhahiri, wala yale yasiyo dhahiri hayawezi kusitirika.***

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

Sehemu hii inashughulika na kuwahudumia wazee amabo wanatenda dhambi, na kuwawekea mikono wazee. Inahusisha idadi ya kanuni ambazo mnenaji mmoja alizijumuisha kama ifuatavyo: "(1) Dhambi lazima ishughulikiwe. (2) Mashitaka lazima yawe na mashahidi wengi. (3) Sio dhambi ya bahati mbaya, bali dhambi idumuyo ndiyo inatakiwa kushughulikiwa. (4) Kukemewa hadharani kufuatie baada ya mtu kuonywa binafsi siririni. Lakini kama atakataa wakati huo, basi kukemewa hadharani kufanyike. (5) Lengo la kukemea hadharani hasa si kutoa adhabu, bali ni kuingiza hofu njema. (6) Mtu atoaye hukumu, hata kama ni mtu wa ngazi ya Timotheo, lazima ajitahidi kuwa wa haki na msafi katika hilo kwa kiwango chote kiwezekanacho. (7) Kuweka wakfu wazee ni swala nyeti sana, na kuna kuwajibika kunakomhusu yeye anayeweka wakfu kuhusiana na huyo aliyewekewa mikono. (8) Hakuna mbadala wa tahadhari au muda. Tabia ya kweli ya mtu na matendo yake, siyo siku zote yanagundulika mara moja." (Mounce 2000: 322)

***Usikubali mashataka juu ya mzee, ila kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu:*** Kanuni ambayo Paulo anaitaja inatokea nyuma kwenye **Kum 19:15** (ona pia **Kum 17:6**). Kanuniinayoambatana na ushahidi wa shahidi mwingine iliwekwa ili kuzuia hatia isiyo haki. Hata hivyo, ikiwa huu usemi wa jambo la *"mashahidi wawili au watatu"* likitumiwa kiholela, na tukaangalia tu kauli *ilivyoandikwa* na siyo *kiini* au kanuni inayosimamia, basi kinyume cha haki ndicho kitakachotendeka. Katika histori na muktadha wa tamaduni za **Kum 19:15**, Waisraeli walikuwa ni jamii isiyoendelea, tena ya wakulima. Vivyo hivyo nyakati za Paulo. Vitu kama kamera, simu za mkononi, vinasa sauti, na teknolojia nyingine kama hizo hazikuwepo. Kwa sasa vitu vyote hivyo vipo katika kila tamaduni. Zaidi, dhambi nyingi (kama vile dhambi za ngono) zinafanyika kikamilifu kwa sababu hakuna mashahidi. Kwa hiyo, kama mzee akishitakiwa kwa uzinzi, itakuwa haileti maana, na kupotosha haki, kama viongozi wengine wa kanisa watayakataa mashitaka hayo kwa kusema hakuna mashahidi wawili au watatu kwenye tukio hilo la uzinzi. Mashitaka kama hayo yanaweza kuthibitishwa kwa jumbe za simu kama meseji zilizobakia kwenye simu, picha, ushahidi wa mtu aliyemwona kiongozi na yule ambaye alizini naye mahali, au nyakati ambazo hawakutakiwa kuwa pamoja, n.k. Mazingira yote hayo ni uthibitisho wa kutosha mahakamani, na unapaswa kuzingatiwa mashitaka kama haya yakiletwa dhidi ya mzee wa kanisa. Pia Paulo alirejea kwenye kanuni katika **Kum 19:15** katika njia ya "ulaini zaidi" katika **2 Kor 13:1.** Pale, alikuwa akishughulikia dhambi na tatizo lililokuwepo katika kanisa la Korintho. Alinukuu kanuni ya Agano La Kale katika kuunganisha na ukweli kwamba *"hii ni mara ya tatu nakuja kwako."* Alikuwa akimaanisha kwamba kule kuwatembelea kwake safari zilizopita, na nyaraka zake kwa kanisa lile kulikamilisha *"mashahidi wawili au watatu"* kulikotosha kushughulika na waovu katika kanisa. Yesu alifanya vivyo hivyo katika **Yoh 8:17-18** aliposema, *"Tena katika torati yenu imeandikwa ushuhuda wa wtu wawili ni kweli. Mimi ndimi ninayejishuhudia mwenyewe naye Baba aliyenipeleka ananishuhudia."*

***Usifanye neno lolote kwa upendeleo:*** Paulo anazungumzia kuhusu nidhamu njema na kuweka wakfu wazee. Katika maeneo hayo mawili lawama ni kubwa sana, kwa sababu ya upendeleo au kuwachukia wengine. Lakini kwa mujibu wa nidhamu, Guthrie kwa usahihi kabisa aweka bayana, "Lawama mbaya daima imeletesha roho chafu na isiyovumilika, lakini kwa kupuuzia kwake kunaleta hatari kubwa zaidi. Kwenye swala la dhambi kwa wazee, hujitokeza hali ya kulegeza." (Guthrie 1990: 118-19) Tatizo hili hili linatokeza tunapowekea mikono wazee. Watoaji wakubwa kanisani, washirika walio kabila moja na mchungaji, washiriki walio katika familia ya mchugaji, na marafiki wa karibu, mara nyingi wanawekewa mikono kuwa wazee, hata kama hawana zile sifa zote za **1 Tim 3:1-7**. Zaidi ya hapo, dhambi za hao wazee hufunikwa kwa vile ni watoaji wakubwa, familia ya mchungaji, au marafiki zake, ingawaje dhambi hizo hizo zisingevumiliwa kama zingefanywa na washirika wa kanisa ambao si watoaji wakubwa, wa familia ya mchungaji, au wasio rafiki zake. Kwa hiyo, "matabaka mawili ya Wakristo yanaundika —sio kwa sababu ile ile aliyoisemea Paulo katika **1 Tim 4:1-7a**, bali kwa matokeo yanayoliharibu kanisa. Paulo anatukumbusha kwamba, kama viongozi wa kanisa, uadilifu na tabia yetu yaendane vizuri katika kila uamuzi tunaoufanya. Tutakuja kutoa hesabu kwa Kristo kwa yale tuyafanyayo kwa Jina lake kama viongozi wa kanisa lake. Kwa hiyo, ingekuwa vizuri *"kutunza kuyafanya haya pasipo upendeleo"* ili kwmba tuwe na *"moyo safi"* (**1:5**) na *"dhamiri njema"* (**3:9**) tutakaposimama mbele zake (kama tutakavyofanya siku ya hukumu, na kama tulfanyavyo kiuhalisi, wakati wote sasa).

***Usimwekee mtu mikono kwa haraka, wala usizishiriki dhambi za watu wengine:*** Wengine wanaamini kwamba kifungu hiki kinahusiana na "mawazo ya kuwarejesha wazee waliotubu wanaporudishwa tena katika ushirika wa kanisa" (Earle 1978: 381).Wengine (huenda ndiyo wengi) wanaamini kwamba kifungu hiki "kinakataza kuwekea mikono kwa haraka [ambacho] kinaendana na majadiliano mkuu wa sura hii, Na uwekaji mikono katika nyaraka hizi unaonekana mara kwa mara kwenda sambamba na uwekaji wakfu (k.m. 4:14; 2 Tim 1:7)." (Ibid.) *"Kushiriki dhambi za wengine"* kunaoneka kufanana na ukweli kwamba, kwa kumwekea mikono

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

mtu, unakubaliana na tabia na sifa zake, na hivyo unashiriki dhambi zozote atakazozifanya.

***Dhambi za watu wengine zi dhahiri, zatangulia kwenda hukumuni, wengine dhambi zao zawafuata.Vivyo hivyo matendo yaliyo mazuri ya dhahiri, wala yale yasiyo dhahiri hayawezi kusitirika:*** **5:24-25** hujenga kile ambacho Paulo amesema katika **5:22**. Maana ya mistari hi ni kwamba, "dhambi za watu wengine zi dhahiri kiasi kwamba hakuna maswali ya kutetea kuwa hawahusiki. Dhambi zawatangulia hukumuni—ya kwanza ni hukumu ya Timotheo na ya mwisho ni hukumu ya milele ya Mungu. Dhambi za watu wengine hazionekani haraka, lakini uchunguzi wa makini utazigundua. Vivyo hivyo matendo yaliyo mazuri ya mhusika yako dhahiri. Hata yale yasiyo dhahiri bado yataonekana, au yakichunguzwa zaidi; hayawezi kujificha." (Earle 1978: 382)

***Tokea sasa usinywe maji tu, lakini tumia mvinyo kidogo kwa ajili ya tumbo lako na magonjwa yakupatayo mara kwa mara:*** Mstari huu ni wa "pembeni" kwake Timotheo binafsi. "Pembeni" ni mapendekezo mafupi ya somo ambayo hayahusiki moja kwa moja na hoja ambayo ilikuwa inazungumziwa. Baada ya kumaliza kauli hii ya pembeni, Paulo mara anarudi kwenye somo kuu. Mstari huu hauhusiani na "theolojia ya pombe." Badala yake, hoja ni kwamba Timotheo alipaswa kuwa wakili mzuri wa mwili wake. Bila shaka, maji ambayo alikuwa anayatumia yalikuwa yana athari kiafya na yalikuwa yanachangia kumletea matatizo ya tumbo. Ngewa anabainisha, "Mvinyo una nguvu fulani ya kiafya, kama utatumika kwa kiasi. Hivyo Paulo anamshauri Timotheo kutumia "mvinyo kidogo" kwa sababu utasaidia mwili wake kupambana na magonjwa." (Ngewa 2009: 133). Ingawa katika tamduni nyingi, kunywa mvinyo au vinywaji vingine ambavyo vina alkoholi huchukuliwa kuwa ni makosa au ni dhambi kabisa, hata tamaduni hizo hizo zinakubaliana kwamba kutumia dawa ambazo zina alkoholi na dawa nyinginezo sio kosa. Ndicho kilichokuwa kinaendelea hapa. Katika ukisasa wa kimadawa wa wakati huu, maji ya chupa, na vinywaji vingine vya chupa leo, Paulo huenda asingemshauri kutumia mvinyo kwa ajili ya tumbo kama lile leo. Hata hivyo, kwa wakti na mahali pale, Paulo alikuwa anatoa wazo jema kabisa (ambalo hata angeweza kulipokea kutoka kwa Luka ambaye ni dakitari, kwa vile hawa wawili walikuwa wakisafiri pamoja).

**6:1-2a:** ***[1]Wowote walio chini ya kongwa hali ya utumwa na wawa hesabie bwana zao kuwa mamestahili heshima yote Jina la Mungu lisitukanwe wala mafundisho yetu. [2] Na wale walio na bwana waaminiio wasiwadharau kwa kuwa ni ndugu, bali afadhali wawatumikie kwa sababu hao waishirikio faida ya kazi yao, wamekuwa wenye imani na kupendwa .***

1. Kifungu hiki ambacho tunapaswa kukitumia kwa namna ya "Mlinganisho" siku za leo. Kifungu hiki kinazungumzia kuhusu "watumwa" na "mabwana." Uchumi wa Dola ya Kirumi ulitegemea utumwa. Asilimia kubwa ya watu walikuwa watumwa. Watumwa walifanya kila aina ya kazi: mashambani; machimboni; nyumbani; katika buashara; kama walimu, nk. Wakati mwingine waliweza kununua uhuru wao (ona **Mdo 22:25-28; 1 Kor 7:21**). Leo hii utumwa umeondolewa katika maeneo mengi ulimwenguni. Hata hivyo, katika maswala fulani, kuna mfanano muhimu (m.f., kuwiana kiasi kikubwa) kati ya utumwa na ajira ya siku hizi: katika kila mmoja, mtu fulani (mtumwa /mwajiriwa) anafanya kazi kwa mtu mwingine (bwana /mwajiri). Kila mfanano huja kukatikia sehemu fulani. Kwa mfano, watumwa walikuwa hawana haki, na walikuwa hawaweza kuacha ajira yao hata kama walikuwa hawaipendi kazi yao, au kama hawapendi jinsi wanavyotendewa. Kwa upande mwingine, waajiriwa wanazo haki za kisheria, na wanaweza kuacha kazi kama wanataka. Matokeo yake, wakati Biblia inajadili kuhusu mazingira ambayo hayafanani na nyakati za sasa, bado tunaweza kutafuta zile kanuni zinazokatiza pande zote za tamaduni zilizopo, na kuzitumia kanuni hizo kwa mlinganisho. Tunapofanya hivi tunapaswa kuwa makini tusipanue uwiano mbali mno, (m.y., lazima tuzingatie *tofauti* kati ya hali ya Ki- Biblia, pia na mambo yanayofanana). Tunapswa tuzingatie zile tofauti kati ya *umiliki* wa mwajiriwa na mwajiri (utumwa) na *uhusiano wa kimkataba* kati ya mwajiriwa na mwajiri (ajira ya siku hizi). Kanuni ya kumheshimu Mungu kwa namna ambayo mtu anachukulia madaraka/ menejiment za ajira kazini inaweza kuelezwa kwa maelezo yafuatayo: "Timiza vigezo vya mkataba wako kwa uwezo wako wote, maana yake, kwa namna ambayo inamtukuza Mungu na kuwafanya wasioamini karibu na ufalme wa Mungu" (Webb 2001: 54).

2. Muktadha wa kifungu hiki unaonyesha kwamba "Kumheshimu" bwana (au, mwajiri) kunamaanisha kwamba mtumwa (au, mwajiriwa) anapaswa kuonyesha heshima yake. Katika muktadha wa "heshima" ya ajira au "utii" kungehusisha: kuwahi kazini pasipo kuchelewa; kufanya kazi kwa bidii na kuwa mfanyakazi mzuri; siyo kumwibia mwajiri wako; kutomsengenya mwajiri uchochoroni, nk. Hilo linaonyeshwa katika **6:2** ambao unasema *"wasiwadharau"* na *"kuwatumikia zaidi."* Zingatia kwamba waajiriwa walio Wakristo wanapaswa kuwaheshimu waajiri wao pasipo kujalii kama waajiri wao sio waumini (**6:1**) au waamini (**6:2**). Baadhi ya waajiriwa walio Wakristo wanafikiria kwamba, kwa vile mwaajiri wao pia ni Mkristo, basi mfanyakazi huyo

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

anaweza kuutumia muda wao wa kazi kwa kusoma Biblia na kuzungumza na waajiriwa wenzao kuhusu Bwana. Paulo anasema Wakristo walioajiriwa *hawapaswi* kufanya hivyo wakiwa kazini Waajiriwa wanategemewa, na wanalipwa kwa kufanya kazi. Waajiri Wakristo wanategemea vile-vile kutoka kwa waajiriwa wao kama wanavyotegemea waajiri wasioamini. Paulo anasema kwamba mwaajiriwa Mkristo anaonyesha *upendo* kwa mwaajiri wake Mkristo kwa kufanyika mfanyakazi mzuri. Hatimaye, ni Paulo kuhusisha Injili, m.y., *"jina la Mungu na mafundisho yetu,"* ambaoyo ni makuu. Kila kitu afanyacho Paulo, na kutuasa kufanya au kutokufanya, kinahusu kukuza au kutokuza Injili.

**6:2b-16:** ***Mambo hayo uyafundishe na kuonya. Mtu yeyote akifundisha elimu nyingine wala hayakubali maneno yenye uzima, ya Bwana wetu Yesu Krsito, wala mafundisho yapatanayo na utauwa, [4]amejivuna wala hafahamu neno lolote; bali ana wazimu wa kuwazia habari za maswali na mashindano ya maneno ambayo katika hayo, hutoka husuda, ugomvi, matukano, shuku mbaya, [5]na majadiliano ya watu walioharibika akili zao walikosa kweli, huku wakidhani kuwa utauwa ni njia ya kupata faida. [6]Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa kubwa. [7]Kwa maana hatukuja na kitu duniani, tena hatuwezi kutoka na kitu. [8]Ila tukiwa na chakula na nguo tutaridhika na vitu hivyo. [9]Lakini nao watakao kuwa na mali huanguka katika majaribu na tanzi na tamaa nyingi zisizo na maana, zenye kudhuru ziwatosazo wanadamu katika upotevu na uharibifu. [10]Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha, ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na imani na kujichoma kwa maumivu mengi. [1]Bali wewe mtu wa Mungu, uyakimbie mambo hayo, ukafuate haki, utauwa, imani, upendo, saburi na upole. [12]Piga vita vizuri vya imani; shika uzima ule wa milele ulioitiwa, ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi. [13]Nakuagiza mbele za Mungu anyevihifadhi hai vitu vyote, na mbele za Kristo Yesu, aliyeungama maungamo mazuri yale mbele za Pontio Pilato, [14]kwamba uilinde amri hii pasipo mawaa, pasipo lawama, hata kufunuliwa kwake Bwana wetu Yesu Krsisto, [15]ambako Yeye kwa majira yake atakudhihirisha–Yeye aliyehimidiwa, mwenye uweza peke yake, mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, [16]ambaye Yeye peke yake hapatikani na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza kuharibiwa, wala hakuna mwanadamu aliyemuona wala awezaye kumuona. Heshima na uweza una yeye hata milele! Amina.***

***Mambo haya uyafundishe na kuonya. Mtu yeyote akifundisha elimu nyingine . . . ana wazimu na hafahamu neno lolote:*** 1. Hapa Paulo kwa mara nyingine anawajadili walimu wa uongo, mafundisho ya uongo, na matokeo yake. Alianza kitabu kwa namna hii-hii (**1:3-4, 19-20**), akarudia hilo katikati ya kitabu (**4:1-7a**), na sasa anamalizia kitabu kwa njia ileile. Kama ilivyoelezwa nyuma, hali ya jambo kurudiwa mara ya tatu, mwanzoni, katikati, na mwishoni, kunaonyesha umuhimu wa swala.

2. Katika mistari hii mitatu Paulo anatupa maelezo ya kina sana ya tabia ya walimu wa uongo, kama vile alivyotoa kiundani maelezo ya utauwa wa uongo na hali ya kuacha uelekeo wao katika **4:1-7a**. Paulo anafafanua maswala yafuatayo ya walimu wa uongo: (A) *Mafundisho yao **(6:3)***—siyo sahihi, hayakubaliani, na hayakubaliani na utauwa. (B) *Tabia yake **(6:4a, 5b)***—wamejivuna, wamekosa ufahamu; na wameipotosha kweli.
(C) *Wanachopendelea **(6:4b)***—wanapendelea maswali ya udadisi; na mashindano ya meneno. (D) *Matokeo yake **(6:4c-5a)***—yanasababisha husuda, ugomvi, matukano na shuku mbaya; majadiliano. (E) *Msukumo wao **(6:5b)***—kusudi lao la msingi ni kujinufaisha, kifedha. Katika kujadili "manabii wa uongo" ambao watakuja kwa Jina lake, Yesu alisema, *"Mtawatambua kwa matunda yao"* (**Mat 7:16**). Katika mistari hii Paulo anafafanua matunda ya manabii hao wa uongo. Zingatia vipengele vyote vya walimu wa uongo ambavyo vinaelezwa na Paulo vinaelekea upande ulio kinyume na *"lengo la mafundisho ya [kweli], [ambayo] ni maagizo ya upendo"* (**1:5**).

3. Maelezo ya walimu wa uongo ya wao kuwa na *"akili zilizoharibika na kutoifahamu kweli"* ni muhimu sana, kwa sababu ni makali mno. Neno la Kiyunani lililotafsiriwa "kupungukiwa" ni *diaphtheiro*. Ni neno kali sana likimaanisha "kuharibika kwa maadili, kukosekana, kubomoka" (Danker 2001: 239), "haribiwa kabisa," "kuharibiwa kwa ujumla, kupotosha " (Zodhiates 1993: 445-46), au "potoshwa kabisa" (Mounce 1993: 143). Ni aina ya neno ambalo mtu anaweza kulitumia kwenye kuharibika kimapenzi. Ni aina ya neno zito zaidi lililotumika katika **Ufu 19:2** kuhusu *"kahaba mkubwa ambaye alikuwa anaharibu ulimwengu wote kwa uzinzi wake." "Kuikosa kweli"* huunda picha ya watu ambao hawahusiki na Injili kwa vyo vyote vile. Hawafundishi Injili iliyopotoshwa; bali wanachokifundisha ni tofauti kabisa (m.y. 1 Tim 1:3). Katika PE [Nyaraka za kichungaji] *alētheia,* 'kweli,' linakaribia kuwa ni neno la kitaalamu kwa ajili ya mafundisho kamili ya Injili (m.y. 1 Tim 2:4). Wapinzani daima huonekana kama waipingao kweli ya injili (2 Tim 2:18; 3:7, 8; 4:4)." (Mounce 2000: 340) Yote mawili *"kupungukiwa na akili"* na *"kuikosa kweli"* yako katika hali ya kutokuwa katika utendaji, "labda kuashiria kuwa Shetani ndiye wakala, ambaye kila mahali katika Nyarraka za kichungaji anatambuliwa kama mtendeji katika kanisa la Efeso" (Ibid.).

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

***Huku wakidhani ya kuwa utauwa ni njia ya kupata faida:*** 1. Maelezo ya mwisho ya walimu wa uongo, *"watu walioharibika akili zao na walioikosa kweli,"* ni muhimu kwani yanatuongoza moja kwa moja kwenye maelezo ya Paulo kuhusu *msukumo wao:* wako katika shughuli ya dini kwa ajili ya kutengeneza pesa. Maelezo ya Paulo katika **6:6-10** yanonyesha kwamba kupenda fedha ndiyo msukumo mkubwa wao. Muunganiko kati ya kupungukiwa ufahamu, ukweli kwamba hawaihubiri kweli kabisa, na msukumo wao wa kutengeneza fedha huonekana kimpangilio. *"Kukosa akili," "kuikosa kweli,"* na*"ambao wakidhani kwamba utauwa ni njia ya kupta faida"* ni "vipengele vitatu vya vifungu vielezeavyo watu hao ambao ni chanzo cha maumivu ya kudumu. Ya kwanza mawili yanaonyesha kitendo endelevu kuonyesha jinsi watu walipofikia (kule kuendeleza mfumo wa utimilifu katika mstari wa 4), na ya tatu inaendana kiutendaji, ikikazia kuendelea kwa chimbuko la mafundisho yao." (Mounce 2000: 340)

2. Hwa walimu wa uongo wanalinganishwa siku hizi na waitwao walimu wa "injili ya mafanikio "— m.y., wale wanaodai kwamba ni mpango wa Mungu waumini wote wawe matajiri wa mali na kuwa na afya nzuri ya kimwili. Mara nyingi dhana ya walimu wa mafanikio huwa ni mawazo kama vile: imani ni "nguvu" ambayo inatiwa nguvu ya kiutendaji tunapoisema; tunapaswa "kutaja kitu na kukidai" (m.y., tutaje kitu tunachotaka na kukiita kwa imani); tunapaswa "kupanda mbegu ya imani" (m.y., toa pesa kwa ajili ya huduma fulani kuonyesha imani yetu); kuna "Sheria ya kurudishiwa malipo" ambayo Mungu ameshikamana nayo (m.y., kanuni ya "kupanda na kuvuna" na "Kurudishiwa mara mia") ambapo kama "tutapanda mbegu "kwenye huduma fulani kwa kutoa kiasi fulani cha fedha, kama tunakuwa na imani ya kutosha, Mungu atatupatia mara mia zaidi ya pesa tulizozi"panda." Kinamna, injili ya mafanikio inajaribu "kubatiza" mali na ujumbe wa kikawaida wa kidunia, na kuigeuza kuwa injili ya Yesu Kristo. Siyo dhambi kuwa tajiri na kuwa na afya badala ya kuwa masikini na mgonjwa. Sio dhambi kufanya kazi ili kuboresha uchumi wako na kuwa vizuri kimwili. Hata hivyo, ni makosa kuharibu Injili. Walimu wa mafanikio, walianzia Marekani, kisha wakaenea Uingereza, Afrika Kusini, Nigeria, na sasa Afrika Mashariki na sehemu nyingine ulimwenguni. Ni wazushi wanohubiri "injili ya tofauti" (ona Adeleye 1999). Ni "injili ya kigeni" inayowanyonya masikini (ona, Fee 1984: 39-43; Editorial 2001: 1-2). Ni ya "udanganyifu na ya hatari" (ona, Piper 2007). Melezo kamili ya kuikosoa injili ya mafanikia yako katika somo la EPI la "Uwakili wa Ki-Biblia," ambalo linapatikana bure katika tovuti ya EPI: www.equippingpastors.com.

3. Walimu wa mafanikio wanalaumiwa mara kwa mara popote katika Maandiko, na wanakabiliwa na hukumu ya mauti. Yesu aliwakasirikia mafarisayo kwa viapo vyao kwa dhahabu ya hekaluni (**Mat 23:16-20**). Aliwakaripia haswa kwa *"unyang'anyi na kutokuwa na-kiasi"* (**Mat 23:25**). Aliwaita *"nyoka"* na *"wana wa majoka"* (**Mat 23:33**), na akasema kwa sababu ya matokeo ya dhambi zao *"hawataepuka hukumu ya jehanamu"* (**Mat 23:33**). Petro anasema mtu anapaswa kulichunga kundi la Mungu *"sio kwa kulazimishwa"* (**1 Pet 5:2**). Katika **2 Pet 2:3** anasema kwamba walimu wa uongo *"katika ufisadi wao"* wata*"jipaatia faida,"* lakini *"hukumu yao tangu zamani haikawii, wala uvunjifu wao hausinzii"* (ona pia **2 Pet 2:14**). Paulo anawashambulia wale ambao *"wanaghoshi Neno la Mungu"* (**2 Kor 2:17**) na ambao wanakuja kusema *" wakisukumwa na tamaa zao"* (**1 Thes 2:5**). Walimu kama hao wanakabiliwa na hukumu mbaya zaidi ya watu ambao Paulo anawazungumzia katika **Rum 1:18-32**. Katika sura hiyo, watu walimjua Mungu kuwa yuko, lakini waliamua kumpuuza Mungu na kuabudu vitu walivyojitengenezea. Matokeo yake, Mungu *"aliwaacha "* waendelee katika uovu wao (**Rum 1:24, 26, 28**), na *"wakastahili kifo"* (**Rum 1:32**). Ikiwa hukumu ya Mungu ilikuwa kali kiasi kile kwa wale waliokuwa wanajua kuhusu Mungu lakini walimdharau, itakuwa mbaya kiasi gani hukumu kwa wale ambao, sio wanamdharau Mungu, lakini wanajaribu *kumtumia na kumfanyia ujanja* yeye na Neno lake kwa kusudi la kujinufaisha kwa tamaa zao za kupenda pesa?

***Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa. Kwa maana hatukuja na kitu duniani, tena hatuwezi kutoka na kitur. Ila tukiwa na chakula na nguo, tutaridhika na vitu hivyo:*** 1. Paulo ameshasema kwamba wale wanaoamini, wanaosukumwa na kufundisha wazo kwamba *"utuwa ni njia ya kupata faida"* wana *"upungufu wa akili"* na *"wameikosa kweli"* (**6:5**). Sasa ansema, *"Walakini utauwa ni faida kubwa"* (**6:6**). Je, anajichnganya mwenyewe? Jibu ni "Hapana, hajichanganyi mwenyewe." Katika **6:6** Paulo anaongezea neno "kubwa" katika faida. Neno hilo, kama atumiavyo neno" kweli-kweli" katika **5:3,** linaonyesha kwamba paulo anaweka utofauti, au anafafanua jambo kwa dhati. Katika **6:5** neno "faida" analozungumzia bayana ni pesa na mali tunazomiliki. Hata hivyo, "faida" si lazima litafsirike kuwa ni kupata mali.Katika **6:6** "faida kubwa" anayoizungumzia hapa ni injili—m.y., Kristo mwenyewe, msamaha wa dhambi zetu zote milele, uzima mapya, uzima wa milele, Roho Mtakatifu kukaa ndani yetu, kufanyika sehemu ya familia ya Mungu, uwezo wa kumfikia Baba wakati wote kupitia Kristo, mioyo ya jiwe iliyobadilishwa kuwa mioyo ya nyama, pia sifa nyingine na manufaa mengine kuhusu maisha katika Kristo. Ukifananisha hayo na pesa zote na kumiliki mali duniani, utaona si kitu. Kama Yesu alivyosema, *"Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na*

*kupata hasara ya nafsi yake?"* (**Mat 16:26; Mk 8:36;** ona pia **Lk 12:13-21**)

2. Paulo alivyotumia neno "kupata faida" katika **6:6** na "kuridhika" katika **6:8** anaonyesha kwamba *"faida kubwa"* anayoizungumzia, kwenye *haiwezi* kuwa ni pesa na mali tunazomiliki. Katika **6:8** Paulo anazungumzia kuhusu *"chakula na nguo."* Kwa kufanya hivyo anakumbusha kile Yesu alichokisema **Mat 6:25** (**Lk 12:22-23**): *"Kwa sababu hiyo nawaambieni, msisumbuke maisha yenu, mle nini au mnywe nini wala miili yenu mvae nini. Maisha je si zaidi ya chaakula? na mwili zaidi ya mavazi?"*Maisha ya Yesu mwenyewe yalidhihirishahilo. Alisema, *"Mbweha wana pango, na ndege wa angani wana viota, lakini mwana wa Adamu hana pa kulaza kichwa chake"* (**Mat 8:20**). Kitu ambacho Yesu alimiliki ni nguo aliyokuwa anavaa tu. Maskari walilichukua hilo vazi hata kabla hawajamsulubisha (ona **Mk 15:24; Lk 23:34**). Yesu alikufa akiwa uchi. Hiyo inaonyesha dhahiri kabisa hakujiwekea kitu chochote—hata aibu yake (mama yake alikuwa shahidi wakati wa kusulubiwa, kwake **Yoh 19:25-27**). Pamoja na hayo, Baba alikuwa pamoja naye daima, na hakupungukiwa na chochote. Paulo anatupa changamoto. Yesu alipotufundisha kusali, alitufiundisha kuomba kwa ajili ya *mahitaji yetu ya msingi* (*"Utupe leo riziki yetu"*) (**Mat 6:11; Lk 11:3**). Sisi wote kimsingi tuna zaidi ya tunachokula na zaidi ya mavazi. Sote tuna pesa na mali nyingi zaidi ya alizokuwa nzo Yesu. Lakini, ingawaje tuna zaidi ya alivyokuwa navyo Bwana, je tunaridhika? Yesu hakuhangaika kumlalamikia Baba akilia kuhusu umasikini wake, na kutumia uhai wake wote kuhangaika ili kutengeneza pesa lukuki. Ajabu ni kuwa, viongozi wengi wa makanisa wanahangaikia hayo. Paulo mwenyewe ilibidi ajifunze—lakini alijifunza—*"kuridhika katika hali yoyote niliyo nayo"* (**Fil 4:11-13**). Paulo alijifunza kuridhika, si kwa sababu yeye ni mtu wa ajabu, mwenye nguvu zisizo za kawaida ya wanadamu, au mazingira yalikuwa mazuri kwake. Kuridhika kwa Paulo.kumejikita katika imani inayokana kutegemea uwezo wake mwenyewe kufanya kazi na msimamo thabiti wa kumtegemea Mungu mwenyenzi. Kuridhika kwenye faida kubwa ni kule kunakotafuta usalama sio katika utajiri wa ulimwengu huu, bali katika Mungu." (Mounce 2000: 341) Hii inatuonyesha kwamba Paulo hakuwa mnafiki. Alifanya "kile alichokihubiri." Je tunaweza kujisemea wenyewe kitu hicho hicho? Tufikiapo kwenye swala la pesa, kutendea kile tuachokihubiri ni *muhimu* ajabu. Watu huugundua unafiki katika swala hili kwa haraka zaidi kuliko karibu maeneno mengine yote ya maisha. Sababu mojawapo iliyomwezesha Paulo kutumiwa na Mungu kwa nguvu sana, ilikuwa ni kwamba Paulo hakuwa mnafiki kwenye maswala ya pesa (ona **Mdo 20:31-38; 1 Kor 4:11-16; 9:11-23; 1 Thes 2:9-12; 2 Thes 3:6-10**).

3. Mjadala wote wa Paulo katika **6:6-8** unaonyesha kwamba ile *"faida kubwa"* anayoizungumzia *haiwezi* kuwa pesa na mali tunazomiliki. Hoja ya Paulo ni kwamba kwa vile "hatukuja na kitu duniani, na hatuwezi kurudi na kitu chochote kutoka duniani, basi umuhimu wa maisha yetu hauwezi kusimamia pesa au vitu tunavyoweza kujilimbikizia kwa miaka hii michache tukaapo katika dunia hii." Ukweli kwamba maisha *hayaishii* kaburini, ni ufunguo wa mjadala wake—na ufufuo wa Krsito ndio dhamana ya ukweli huo. Hivyo Paulo, na siyo "walimu wa mafanikio" au wale wanaotegemea tu ulimwengu huu tu, ndiye aliye sahihi. Paulo amefanya kimsingi hoja ileile katika **1 Kor 15:32**: *"Ikiwa kwa jinsi ya kibinadamu nalipigana na hayaani wakali kule Efeso, nina faida gani? Wasipofufuliwa wafu, natule na tunywe, maana kesho tutakufa."* Hoja yake ni kuwa, kama Kristo sio Bwana, kama hakufufuka kutoka kwa wafu, na kama hatutafufuka kutoka kwa wafu katika Kristo, basi maisha ni kujihangaisha kukupata anasa, pesa, na mali kwa ajili ya miaka michache tunayoishi katika dunia hii; baada ya hapo hakuna tena. Hata hivyo, Kristo *ni* Bwana, *amefufuka* kutoka kwa wafu, nasi *tutafufuliwa* kutoka kwa wafu katika yeye. Hivyo basi, lazima tuwe na mtazamo wa umilele katika mambo. Tunachokifanya duniani katika maisha haya kinaathiri umilele wote ujao. Kusema ukweli, kile tunachofanya kwa pesa zetu na mali zetu kinatuathiri kiroho sasa na hata milele ijayo (**Zab 41:1-3; 112:5-6; Mith 19:17; 22:9; Mat 6:3-4; 19-21; 19:21; 25:19-30; Lk 12:33-48; 16:9, 19-31; 19:15-26; Mdo 10:4; 1 Tim 6:18-19**). Kwa hiyo, Kristo alisema, *"Msijiwekee hazina duniani . . . bali jiwekeeni hazina mbinguni"* (**Mat 6:19-20**). Pesa na mali zetu ni vitu vizuri na vya lazima. Lakini, yeyote aliye katika huduma ya Kikristo ambaye *msukumo* wake ni thawabu ya pesa na mali, anafanya kama walimu wa uongo na wale wanaosema kwamba hakuna ufufuo. Hili ni swala la ngazi ya juu kabisa. Ni swala la *tabia zetu* (ona **Ebr 13:5**).

***Lakini hao watakao kuwa na mali huanguka katika majaribu na tanzi . . . na kujichoma wenyewe na maumivu mengi:*** 1. Hii ni mara ya pili ya Paulo ametaja neno "tanzi" (au, "mtego"). Katika **3:7** alizungumzia kuhusu kuangukia katika mtego wa Shetani (ona pia **2 Tim 2:26**). Paulo anatuonya katika **6:9-10** kwa njia bayana kabisa kuhusu hatari za kupenda pesa. Maonyo hayo, kwa mara nyingine, yanathibitisha kwamba *"faida kubwa" ya* utuwa (**6:6**) haiwezekani iwe pesa. Paulo tayari ameshatuambia kwamba kupenda pesa kunamshusha mtu hadhi ya kuwa kiongozi wa kanisa (**3:3, 8**). Sasa anasema kuwa yaweza kuiharibu imani ya mtu. "Neno lililotafsiriwa 'kudhuru' [**6:9**] ni sawa na lile la Luka 5:7 linaloelezea kuzama kwa mtumbwi." (Ngewa 2009: 154). Hili linaelezea kile Paulo alichokisema katika **1:19** kuhusu hao, kama akina Himenayo na Alekzanda, ambao hawakuwa waaminifu, bali *"waliangamia kwa habari ya imani yao."* Tabia zetu kwenye pesa

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

na mali huenda ikawa ndiyo dalili kuu zaidi ya hali ya mioyo yetu. Ndiyo maana, tena na tena, Yesu alionya kuhusu hatari za kupenda fedha, alisema kwamba huwezi kuwatumikia mabwana wawili, na akasema kwamba kule tunakoweka hazina zetu ndiko iliko mioyo yetu (ona **Mat 6:19-34; 19:16-30; Mk 10:17-31; Lk 12:13-34; 16:10-13, 19-31; 18:18-27**). Je sisi kweli ni wanafunzi wake, au kuna sanamu ya dhahabu iliyopo kati yetu na Yesu?

2. Ingawa utajiri kama ulivyo unaweza kuwa kitu kizuri, Paulo na sehemu nyingine zote za Biblia huweka bayana kwamba utajiri unaleta pia hatari ya nyongeza kiroho. "Paulo hamaanishi kwamba waamini wabakie kuwa masikini. Badala yake, anaonyesha kwamba wale wanaoridhika na kile walicho nacho, wana furaha zaidi kuliko wale wasioridhika kamwe. Lakini hao watakao kuwa na mali huanguka katika dhambi nyingi (**6:9-10**)." (Andria 2006: 1476) Yesu alionya kwamba utajiri ni "mdanganyifu" na waweza kulisonga neno la Mungu ndani ya mtu (**Mk 4:18-19**). Katika Wakolosai Paulo anasema kwamba ubinafsi ni sawa na ibada ya sanamu, na kuonya kwamba ghadhabu ya Mungu itakuja juu ya watu hao wenye uchoyo (**Kol 3:5-6**). Yohana amesema kwamba kuupenda Baba hakumo ndani ya mtu aipendaye dunia, au mambo ya ulimwengu (**1 Yoh 2:15-16**). Vivyo hivyo katika la Agano la Kale, waandishi wa Mitahli wanasema azitegemeaye mali zake atamwacha Mungu (**Mit 11:28**), na mtu mwenye mali hujikuta anamkana Bwana (**Mit 30:8-9**). Ayubu alijua kwamba kutegemea mali ni dhambi ambayo inakupeleka katika hukumu kwa sababu ni sawa na kumkana Mungu (**Ayu 31:24-28**). Mifano ya Gehazi (**2 Fal 5:15-27**), Anania na Safira (**Mdo 5:1-11**), kijana mtawala aliyekuwa tajiri (**Mk 10:17-25**), na mtu tajiri aliyempuuza Lazaro (**Lk 16:19-26**), yote huonyesha hatari za kiroho zinazotokana na kuwa na utajiri na mali. Kama Adeleye anavyomalizia, "Kma mwisho wake, pesa hushindania nafasi ya kujitoa kwetu ambako ni mali ya Mungu. Una tabia ya kufanyika sanamu ambayo inaharibu maisha yetu. Hii ndiyo maana Yesu anatuonya zidi ya kuzitazama pesa kama tumtazamavyo Mungu" (Adeleye 1999: 97).

***Bali wewe mtu wa Mungu uyakimbie mambo hayo . . . ukafuate haki, utauwa, imani, upendo, saburi na upole:*** 1. Muktadha wa mara moja wa *"mambo haya"* ambayo Timotheo anapaswa kuyakimbia ni kupenda pesa, kutamani kuwa tajiri, na mambo mengine yote yanayoendana nayo. Kwa ujumla zaidi, bila shaka, Timotheo (na kingozi yeyote wa kanisa) anapaswa kuyakimbia mambo haya yote, dhambi, majaribu, utauwa wa uongo, mafundisho ya uongo yaliyojadiliwa katika waraka huu. Yote haya huaribu ushirika wetu na Mungu na wale ambao tumeitwa kuwatumikia. Hata hivyo, madhara ya tamaa ni hatari zaidi kwa sababu mara zote hupuuzika na haionekani. Sote huwa tunajua tunapokuwa tumedanganya au kufanya uzinzi. Tamaa haiko namna hiyo. Sote tunawajua watu walio na vingi kuliko tulivyo navyo na pasipo shaka yoyote ni wenye ubinafsi. Huwa tunapenda kujifananisha nao (Badala ya wale walio na vichache zaidi ya sisi). Ndipo tunahitimisha, "mimi si kama mtu yule. Ana tamaa. Mimi siko hivyo." Ndiyo maana, kuwa muwazi kwa mwenzi wako wa ndoa kuhusu mambo ya pesa kuna umuhimu, kuwajibika na mwenzi wa kukudhibiti, au kikundi cha uwajibikaji, na daima kufikiria mambo haya na kujitathimnini sisi wenyewe ni muhimu sana. Kupenda pesa ni sawa tu na mke wa Potifa, anong'onaye sikioni mwetu *"hebu lala nami"* (**Mwa 39:1-12**). Tunapaswa kuikimbia, kama vile Yusufu alivyomkimbia mke wa Potifa (**Mwa 39:13**). Pesa ni jaribu ambalo linaletesha anasa kimwili, lakini ina mauti rohoni, kama ilivyo ngono haramu.

2. Tunapaswa kukimbia kitu kimoja, na kutafuta kitu kingine. Paulo siyo tu anatuambia yale tunayopaswa *kuyakimbia*, (kupenda pesa). Anatuambia pia tunapaswa kukimbilia *nini* (haki, utauwa, imani, upendo, saburi na upole). Hilo linatuonyesha kwamba *hatuwezi kuwa na yote mawili.* "Walimu wa mafanikio" wanasema kwamba tunaweza *kuzipenda fedha* na *pia* kuwa viongozi wa kanisa, haki, utuwa, imani, upendo, nk. Paulo anasema, "Hapana, unapaswa kuchagua. Ni mojawapo au jingine." Lazima tuamue nani tumwamini: "walimu wa mafanikio" au Mtume Paulo? Uone jinsi mambo haya yote yalivyo muhimu—haki, utauwa, imani, upendo, saburi na upole—yanaenda pamoja? Yanakuwa kama "Tunda la Roho" katika **Gal 5:22-23**. Nayo pia huenda pamoja (kiukweli, katika **Gal 5:22** "tunda" ni moja, sio uwingi). Haya ni maswala ya tabia zetu ambayo yataonyesha jinsi maisha yetu na namna tunavyoishi. Ndivyo ilivyo kupenda pesa. Ni swala la tabia zetu (**Ebr 13:5**) ambalo litaamua namna tunavyoishi maisha yetu.

***Vipige vita vile vizuri vya imani; shika uzima ule wa milele ulioitiwa:*** 1. Hii ni mara ya pili Paulo ametumia masemo wa *"vipige vita vile vizuri vya imani."* Mara ya kwanza alikuwa katika **1:18**. Pale alikuwa anamwambia Timotheo kudumu katika uaminifu. Hapa anasema kitu kile kile, lakini kwa mukthadha wa kupinga kupenda pesa na badala yake atafute uchaji wa Mungu. Hapa Paulo anaongezea mbele ya maneno *"Vita vizuri"* maneno yasemayo *"vya imani."* Kwa Kiyunanii, pana mkazo wa "ile" kwenye neno "imani," m.y., *"piga vita vizuri vya ile imani."* Hii inatia mkazo kwamba, imani yetu, kwa asili yake, inahitaji juhudi kwa upande wa mwamini. Kushindana ni kwenye kupinga tamaa na majaribu ya kidunia na mwili (**1 Yoh**

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

**2:15-17**). Mwishowe, hata hivyo, *"kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya, katika ulimwengu wa roho"* (**Efe 6:12**). Kwa sababu "vita hivi vya imani" ni vya muhimu sana, ni lazima *"tutwae silaha zote za Mungu, tupate kuweza kushindana siku za uovu, na tukiisha kuyatimiza yote, kusimama"* (**Efe 6:13**). Tena, kuna fumbo: Kristo hatatuacha wala kutusahau kamwe (**Ebr 13:5**); tume*"hifadhiwa kwa ajili ya Yesu Kristo"* (**Yuda 1**); Licha ya hayo, tunapaswa kudumu katika uaminifu (**1 Tim 1:18-19; 5:12; Ufu 3:10**)—siyo tunavyofanya bidii *"kwa ajili ya"* waokovu wetu" bali "tunavyo *ufanyia kazi* wakovu" (**Fil 2:12-13**).

2. <u>"Kushika sana" uzima wa milele kunamaanisha kunga'ng'ania kwa nguvu na kushikilia.</u> Bila shaka kuna mtazamo wa kizamani katika hili: tunashikilia uzima wa milele tunapotubu dhambi zetu na kukiri kwamba Kristo ni Bwana na mwokozi wetu (m.y., *"Ungamo zuri mbele ya mashahidi wengi"* [**6:12**] ambako tumekufanya). Hata hivyo, kuna swala la mwendelezo wa kila siku wa kudumu kuhusu "kushika sana uzima wa milele." Yesu alisema, *"Na huu ndio uzima wa milele, wakujue wewe Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma"* (**Yoh 17:3**). Wakati Biblia inapolitumia neno "kujua" kuhusiana na wokovu, ni zaidi ya "kujua tu" au "Kuelewa kweli fulani kuhusu" Mungu na Kristo. Badala yake, Biblia mara zote hutumia neno "kujua" kwa maana ya kina ikihusisha nafsi, ya undani zaidi, na ya kimahusiano. Kwa mfano, linatumika kwenye tendo la ndoa kati ya mume na mkewe (*"Adamu akamjua mkewe"*—**Mwa 4:1**). Mungu aliposema "anatujua" sisi, maana yake ni pamoja na kutuchagua na kuweka kibali chake juu yetu (ona **Mwa 18:17-19; Amo 3:1-2; Mat 7:23; Rum 8:29**). Vivyo hivyo, "kumjua" Mungu na Kristo ni kuwa na ushirika sahihi pamoja nao (ona **Hos 13:3-5; 1 Kor 8:3; Gal 4:8-9**). Kila ushirika wa karibu (mume na mke; mzazi-mtoto; marafiki wa karibu) unapaswa kulelewa na kutiwa nguvu kwa kuwasiliana kikaribu, ushirika, na kujitoa, ambako kunaonyesha uthamani wa ushirikiano. Tunapofanya hivyo na Kristo, tuna*"shika sana uzima wa milele"* kwa maana yeye ndiye *'uzima"* (**Yoh 14:6**).

3. <u>"Kushikilia uzima wa milele" pia hutuonyesha ile tabia ya "tayari lakini bado" ya ufalme wa Mungu na wokovu wetu.</u> Tumeokolewa sasa, lakini bado hatujatukuzwa. Ufalme upo sasa, lakini bado haupo katika ukamilifu wake wote wa utukufu. Tunadumu katika ahadi za Mungu, na ushirika wetu na Kristo, hata kama maisha yetu yanaweza kuwa magumu sana kwa sasa, kwa sababu "kushikilia kwa bidii yaliyo ya uzima wa milele humpatia mtu kionjo cha utimilifu wa ushirika tutakaoufurahia mbinguni, 'tutakapomwona [Kristo] kama alivyo' (1 Yohana 3:2)" (Ngewa 2009: 159).

***Ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi . . . na mbele za Yesu Kristo, aliyeyaungama maungamo mazuri mbele ya Pontio Pilato:*** Mistari 12-13 iko sambamba kwa njia fulani. Katika **6:12** Timotheo anaelezwa kuwa "amefanya" (neno la Kiyunani *homologeō* hasa ni "kuungama") *"maungamo mazuri."* Katika **6:13** Kristo "kuungama" (neno la tofauti, lakini linaelekeana na "kukiri") *"maungamo mazuri."* Waandishi wengine wanafikiri kwamba "maungamo" ya Timotheo yanahusiana na kiapo alichokifanya wakati wa kuwekewa mikono kwake. Hata hivyo, "mstari unaonyesha kwamba mwito wa uzima wa milele ulitokea wakati ule ule wa maungamo ya Timotheo. Uwekaji wakfu /kuwekea mikono hakuwi kiurahisi mdiyo mwito wa uzima wa milele, lakini kuongoka /tukio la ubatizo ni dhahiri: Mwito wa Mungu juu ya maisha ya Timotheo kukisindikizwa na maungamo katika ubatizo wake." (Mounce 2000: 356) Kulingana na "maungamo ya Yesu", wasomi wengine "wanatambua maungamo hayo kwamba ni lile tamko la Yesu kwamba alikuwa ni mfalme wa Wayahudi (Math 27:11; Marko 15:2; Luka 23:3; Yohn 18:37). Hata hivyo, maneno yaliyotafsiriwa 'mbele ya Pontio Pilato' yanaweza pia kutafsiriwa hivi 'wakati wa Pontio Pilato'. Kama tafsiri hii ni sahihi, "maungamo" ya Yesu' yalikuwa ni yale yote aliyosema na yale aliyoyafanya wakati wa huduma yake yote duniani." (Ngewa 2009: 162) "Inaelekea zaidi katika muktadha huu, Paulo anazungumzia kuhusu uvumilivu wa Yesu katika huduma yake, siyo tu katika maisha haya . . . lakini hasa wakati wa kifo chake. Kielelezo hicho cha uvumilivu kinapaswa kimvuvie Timotheo kuendelea na kazi yake na kuwa mkweli katika kujitoa kwake kwa Kristo." (Mounce 2000: 358) Muunganiko kati ya "maungamo" ya Yesu na ya Timotheo unawakilishwa na Pontio Pilato ambaye, "hakuona kosa lolote kwa Yesu na akatangaza hana hatia (Yohana 18:38; 19:4, 6). Timotheo anapaswa kuchukulia maisha haya *bila madoa wala lawama yoyote* kama kielelezo cha huduma yake mwenyewe. Haitakuwa rahisi, na patahitaji mapambano ya kudumu, ambao yataishia wakati wa *kuja tena kwa Bwana Yesu Kristo (6:14)."* (Andria 2006: 1476)

***Ulinde amri hii pasipo mawaa:*** 1. <u>"Amri" hiyo haijawekwa bayana.</u> Wengine wanadhania ni kile ambacho Paulo alimwagiza Timotheo katika **6:11-12**. Wengine (labda kwa mtazamo mzuri zaidi) huitazama "amri" kwa upana zaidi. Kwa mfano, Mounce amechunguza: "Muitadha wa amri ni makini mno, ambayo imemtaja Mungu, Kristo, na wale walioshuhudia ungamo la Timotheo, na hivyo basi amri hiyo inapaswa kuwa na uthamani katika kiwango hiki cha ukuu. [Matumizi ya neno la msisitizo "hiyo" kwa 'amri'] huashiria kitu kinachojitegemea

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

ambacho kinajulikana sana. Fikira hizi zinaashiria kwamba amri hiyo ni ya ujumla, ikimhamasisha Timotheo kujitoa kwa Kristo na huduma yake, kujitoa kuhubiri injili ya haki, utauwa, imani, upendo, uvumilivu, upole, tofauti na mafundisho ya wapinzani, na kujitoa kunakoandna na uvumilivu hadi Bwana atakapo rudi. Amri inahusisha zaidi ya sehemu yoyote ya miktadha na kusema ukweli huchanganya yote." (Mounce 2000: 359)

2. *"Bila mawaa wala kulaumika"* inaonyesha kwamba jinsi tunavyoishi maisha yetu ni kitambulisho cha injili tunayosema tunaiamini. Neno lililotafsiriwa katika Biblia ya NASB kuwa *"bila mawaa"* ni rasmi kama limetumikavyo katika Agano Jipya kwa ajili ya mwenendo wa watu. Kuwa *"bila kulaumika"* ni sifa ya kwanza kwa wazee (**3:2**) na ni ya lazima kwenye familia zenye wajane (**5:7**). Katika **6:14** Kiyunani kinayaweka maneno haya karibu na *"amri,"* yakionyesha kwamba yanaielezea amri kuwa ni *"bila mawaa au bila kulaumika."* Kwa vile muktadha agizo kwa Timotheo, njia nzuri zaidi ya kufanya, ni kuunganisha mawazo hayo mawili: Kama Timotheo atajiepusha na mwenendo wake *"bila mawaa au kulaumiwa,"* ndipo *"amri"* itakuwa imetunzwa, na itaonekana na wengine, na kwa yenyewe kuwa ni *"sheria kamilifu"* (**Yak 1:25**), *"bila mawaa au lawama."*

***Hata kufunuliwa kwa Bwana wetu Yesu Kristo . . . heshima na uweza una yeye hata milele! Amina:*** 1. Hapa Paulo anazungumzia moja kwa moja kuhusu Kurudi kwa Mara ya Pili kwa Krsito. Paulo alikuwa anamsihi Timotheo *"kuvipiga vita vizuri"* na kutunza uaminifu wake. Kuzungumzia Kurudi Kwa Mara ya Pili kunafanya sababu ya nne kwa nini Timotheo (na sisi) tunapaswa kuvumilia: (A) Kuvumilia kwa sababu Mungu amekuita (**6:12**); (B) uvumilie kwa sababu ya "maungamo" mazuri uliyoyafanya mbele ya mashahidi wengi (**6:12**); (C) Kuvumilia kwa sababu ya Krsito na injili, ambayo yote ni takatifu na hupaswa kudumishwa katika utakatifu (**6:13-14**); (D) Uvumilivu kwa sababu Kristo atarudi tena (**6:14**).

2. Haya ni maelezo ya tatu ya kina au kusifu kwa nafsi ya Kristo. Mengine yalikuwa **1:17** na **3:16**. Kwa hiyo, Yesu ni mwanzo, katikati, na ni mwisho wa kitabu hiki. Paulo anatuambia kwamba yote ni kuhusu Yesu. Kama ilivyokuwa kweli kwa **1:17**, hivyo basi kule kuzungumzia hapa *"Yeye [ambaye] atauleta [huo] kwa majira yake"* (**6:15-16**) humfaa Baba. Hata hivyo, humfaa pia Kristo. Muktadha unazungumzia kuhusu Krudi Kwa Mara ya Pili kwa Kristo (**6:14**). Maneno *"Mfalme wa wafalme Bwana wa mabwana"* yanamhusu Yesu katika **Ufu 17:14** na **19:16**. Kristo ni Mungu Mwana, ambaye amekabidhiwa *"mamlaka yote . . . mbinguni na duniani"* (**Mat 28:18**). Kama kweli tunalitambua hili kutoka ndani ya kiini cha utu wetu, itatusaidia na kututia nguvu *"kuvipiga vita vizuri vya imani"* na kuvumilia hadi mwisho.

**6:17-19:** ***[17]Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune wala wasitumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini Mungu, atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha. [18]Watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, [19] huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate ule uzima wa kweli kweli.***

1. Hao *"walio matajiri wa ulimwengu wa sasa"* (**6:17**)? Inapofika kwenye swala la fedha na mali, watu wengi hupenda kujilinganisha na watu wengine ambao wana mali nyingi kuzidi ya wao, kuliko na wale walio na mali kidogo. Matokeo yake, watu wengi wanawaangalia wale wenye mali nyingi na kuwaza, "Huyu ni tajiri; mimi siyo" Hata hivyo, hiki si kipimo cha Ki-Biblia cha kulinganishia. Katika **6:6-8** Paulo anashauri, *"Kama tuna chakula na nguo za kuvaa, katika haya tutaridhika."* Akaendelea kwa onyo kali kuhusu kupenda pesa na tamaa ya kupata utajiri (**6:9-10**). Kipimo chetu ni Yesu. Yesu hakuwa *"na mahali pa kulaza kichwa chake"* (**Mat 8:20**). Alitufundisha kuomba kwa ajili ya *mahitaji yetu ya msingi* (*"Utupe leo ridhiki yetu ya kila siku"*) (**Mat 6:11; Lk 11:3**). Yesu hakuweka hazina tele duniani, na alituagiza tusifanye hivyo, bali tuweke hazina zetu mbinguni (**Mat 6:20**). Kwa vile *"mtumwa hawi mkuu kuliko bwana wake"* (**Yoh 13:16; 15:20**), tunapoangalia kwa macho ya Kibiblia, macho ya Yesu—"matajiri" ni wale walio na *zaidi ya "chakula na mavazi"* (m.y., zaidi ya alivyokuwa navyo Yesu). Kwa maneno mengine, yeyote huwa ni "tajiri" anapokuwa na zaidi ya anavyohitaji kwa mahitaji ya msingi. Ni kweli kwamba kuna viwango vya tofauti vya "utajiri": wengine wanaweza kuwa matajiri kidogo tu (wana ziada kidogo ya mahitaji yao ya msingi), wakati wengine wanao utajiri mwingi (wana kiasi kikubwa kuzidi mahitaji yao ya msingi). Pamoja na hayo, katika tamaduni zilizo masikini kabisa, watu wengi ni "matajiri."

2. Hii ni mara ya tatu kwa Paulo kutaja "tumaini." Katika **1:1** Paulo ametuambia ni nani mhimili, na ambaye ndiye chanzo cha tumaini letu: Yesu Kristo. Katika **4:10** Paulo alisema *"tumeliweka tumaini letu kwa Mungu."* Sasa, Paulo anatuambia kuwaagiza matajiri kwamba *"wasitumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini Mungu atupaye vitu vyote"* (**6:17**). Huu ni mkondo muhimu na na somo kwa ajili ya wote walio katika huduma kwa watu: Kama unajua kwanza kwamba ni nani na ni yupi ambaye ni chanzo cha tumaini, na ukaweka tuamaini lako mwenyewe kwa Yesu Kristo, je unas sifa hizo za kuwaambia wengine kuweka tumaini

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

lao kwa Kristo. "Kuweka tumaini la mtu kwa" tafsiri ya neno la Kiyunani, *elpizō,* amabalo linamaanisha "ujasiri" katika mambo unayotarajia, au "kuweka uhakika wako kwa mtu au katika kitu fulani," au tarajio la "tumaini" katika kitu fulani (ona Danker 2000: 319). Utajiri, kwa asili yake, "havina uhakika": hakuna uhakika wa kupata mali za kidunia; au hata kama utaupata, huna uhakika wa kuutunza [au kutokana na sababu za binafsi, au sera za esrikali, au hali za uchumi]; au hata kama unao, hutaweza kuhakiki hali ya afya yako au maisha yako ili uweze kuutumia huo utajiri. Kristo pekee anatupatia msingi imara wa ujasiri na tumaini.

3. Kwa namna nyingi, **6:17-19** inaendana na **6:6-12**. Katika **6:6-8** Paulo alikuwa anatuambia turidhike kama tuna angalau chakula na mavazi; sasa anatuambia cha kufanya pale tunapokuwa na ziada ya vyakula na mavazi. Katika **6:9** alikuwa anawaonya matajiri; sasa anawaelekeza matajiri. Katika **6:10** alikuwa anaonya kuhusu kupenda pesa; sasa anatupatia kipimo cha kuangalia tunapokuwa na pesa au hapana. Katika **6:11** alikuwa anatuambia kukimbia kutoka katika tabia mbaya na maisha yasiyofaa na kuagiza tutafute tabia sahihi na maisha yafaayo; sasa anatuonyesha kwamba tabia sahihi na maisha yafaayo ni yapi. Katika **6:12** Alimhimiza, *"kuvipiga vita vizuri vya imani";* sasa (**6:18**) anaonyesha uaminifu unaonekanaje.Katika **6:12** alituambia *"tushike sana"* uzima wa milele; sasa (**6:19**) tena anatumia neno lilelile *"shika sana,"* na anatuonyesha jinsi ya kufanya hivyo.

4. Wale walio na ziada kuliko mahitaji yao ya muhimu (m.y., "matajiri") wanatakiwa kuwa wakarimu katika kutoa, si kusudi wapate *kibali* cha Mungu, lakini kwa sababu tayari wamekwisha *kupokea* kibali kwa Mungu. Kama Paulo alivyoonyesha mwanzoni mwa kitabu (ona **1:2, 13-16**) tunaokolewa tu kwa msingi wa rehema na neema ya Mungu kwetu. Chochote tunachokifanya katika maisha kinapaswa kiwe *matokeo* ya ile neema: m.y., mwenendo wa maisha yetu ni udhihirisho kwamba tunatambua tusingeweza kujibadili wenyewe, lakini Mungu ametubadilisha. Ametupatia mioyo mipya na "nia ya Kristo"; sisi sio tena wafu (" tuliokufa katika dhambi na makosa yetu") ambayo tulizoea kuishi zamani. Kipengele cha muhimu kuhusu jinsi tunavyoishi, ni nini tunafanya kuhusu pesa na mali zetu. Katika **6:17, 19** analinganisha wale wanaoweka tumaini lao katika vitu ambavyo *"si vya kutumainika"* vya *"ulimwengu wa sasa"* na wale walioweka *"masingi mwema"* kwa ajili *"baadaye."* Katika **6:17-19** anavyotumia neno *"utajiri"* inaonyesha utajiri wa kweli ni upi na jinsi watu matajiri wanavyofanya. Anasema *"utajiri,"* kwa kuangaliwa tu kama mali na mtazamo wa ulimwengu huu, hazina "uhakika" (**6:17**). Kwa upande mwingine, Mungu anatupatia *"kwa wingi"* (**6:17**). Utajiri wake ni pamoja na dunia yote, mili yetu na akili, mali zilizopo na tunazozitengeneza (ona **Kum 8:18; Efe 4:28**), uzima mpya, Roho Mtakatifu anayekaa ndani yetu, kanisa (familia yetu) ambayo tunapaswa kuiendea ili kupata msaada wa mahitaji yetu, nk. Mambo yote haya ni mazuri, na yanapaswa kufurahiwa. Hii ni kama Paulo alivyosema katika **4:3-5**. Kwa hiyo, kwa vile Mungu ametoa *"kwa wingi"* sana kwetu, tunapaswa tuwe "*matajiri"* wa kazi njema na wakarimu kwa wengine (**6:18**).

5. Hata kama hatupaswi kufanya ukarimu katika kutoa kwa sababu ya kupata kibali cha Mungu, *tutalipwa* kwa sababu ya utoaji wetu. Wale wenye uhitaji wanafaidika kutokana na utoaji wa walivyo navyo. Hata hivyo, hilo silo analolisisitiza Paulo. "Kusudi la msingi liko bayana. Kwa kuwa wakarimu, matajiri hawapotezi mali zao. Badala yake, wanawekeza mbinguni, na kwa kufanya hivyo wanajiwekea msingi imara wa milele, kwa ajili ya uzima ambao ni wa kweli." (Mounce 2000: 368). Yesu alituambia tusiweke hazina zetu duniani, bali kuziweka mbinguni ambako kuna usalama (**Mat 6:20**). Katika mistari hii Paulo anatuambia *namna* ya kuweka hazina zetu mbinguni. Zaidi ya hilo, anatupa *kichoche*o cha ajabu cha kuwa watoaji: kile tunachotoa sasa hatukipotezi, bali ni sehemu ya msingi tunaouujenga kwa ajili ya umilele wa baadaye. Kwa maneno mengine, kile tunachofanya kwa pesa na mali zetu hapa, kitatupatia thawabu na manufaa ya milele katika nchi mpya ambayo tutaishi. Hata kama ni zawadi ndogo zitolewazo kumsaidia mtu kwa sababu mtoaji anampenda Yesu zitalipwa (**Mat 10:42**). Thawabu hizo zitadumu milele (ona **Mat 25:19-30**). Tutakuwa wapumbavu kama *hatutakuwa* wakarimu katika utoaji. Paulo anatuambia hapa kwamba tutabarikiwa zaidi ya kipimo kama tutakuwa ukarimu kiutoaji.

6. Tuwe tunajua au hatujui mafundisho ya Paulo na kuyafuata katika **6:17-19** ni swala la muhimu mkubwa kwa wakristo, kote kuwili-wakati wa maisha haya na ya hukumu ya milele. (A) *Kuhusiana na hukumu:* Utajiri huambatana na uwajibibikaji wa nyongeza. Sababu ya Mungu kutubariki kwa pesa ni *"ili apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji"* (**Efe 4:28**). Kuongezeka kwa wajibu kunakotokana na kuwa na utajiri wa mali kunaambatana na kuongezeka kwa uwajibikaji. Kila mtu anakabiliwa na hukumu ya Mungu kwa yale anayoyafanya, au anayoacha kufanya, katika maisha haya (**Ebr 9:27;** ona **Ufu 20:11-15**). Kanuni ya msingi ya hukumu ya Mungu, ni *"Kwa yule aliyepewa vingi, kwake vitatakwa vingi; naye waliyemwekea amana vitu vingi kwake huyo watataka na zaidi"* (**Lk 12:48b;** ona **1 Kor 3:10-15**). Kwa sababu ya utajiri wao unaambatana na majukumu ya nyongeza, na, kwa hiyo, uwajibikaji mkubwa zaidi, wale walio matajiri katika maisha haya wanakabiliwa kimsingi na hukumu yenye kibano zaidi ya wale wasio matajiri. Ndiyo maana, **Mith 11:4** panaonya kwamba utajiri hautaokoa siku ya hukumu. Kujilimbikizia utajiri mkubwa wa mali na kutokuutumia

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

kwa ajili ya kusudi lile ambalo Mungu anataka, kunavunja sheria ya Kristo na ni dhambi. Yesu alisema nondo na kutu huharibu hazina zifichwazo duniani (**Mat 6:19**). Mtume Yakobo alitumia lugha ya Kristo kuwaonya matajiri ambao hawakuutumia utajiri wao kama walivyotakiwa (m.y., wameruhusu utajiri wao "kupata kutu"), *"Dhahabu yenu na fedha zimeingia kutu; na kutu yake itawashuhudia nayo itakula mili yenu"* (**Yak 5:3**). Anaongezea kwamba kwa sababu ya hukumu wanayokabiliwa wenye mali, wanapaswa *"kuliea mkapige yowe kwa sababu ya mashaka yenu yanayowajia"* (**Yak 5:1**). Anamalizia kwa kusema wale *"waliofanya anasa katika dunia na kujifurahisha kwa tama kama kodoo au ngombe au nguruwe "mmejilisha mioyo yenu kama siku ya machinjo"* (**Yak 5:5**). (B) *Kwa maisha haya:* Njia mojawapo ambayo tunayoweza kuitumia kutambua kama tunapenda pesa (**6:9-10**) ni kuangalia ni watoaji wa aina gani (**6:18**). Kanisa la kwanza lilielewa kwamba injili ilimaanisha jinsi tunavyozisimamia fedha na mali zetu. Walijua kwamba *"aliyesamehewa vingi, hupenda sana"* (ona **Lk 7:36-50**). Matokeo yake, kanisa la kwanza lilikuwa na sifa ya *ukarimu mkuu.* Zakayo aliamua mwenyewe kutoa nusu ya mali zake kwa ajili ya masikini (**Lk 19:1-10**). Kanisa la kwanza la Yerusalemu (**Mdo 2:44-47** na **Mdo 4:32-37**) *"Walianza kuuza mali zao na nyumba zao na viwanja vayo na walikuwa wakishirikiana wote, ili wote wapate."* Kanisa la Antiokia, *"kila mtu akagawiwa kwa kadiri ya alivyohitaji, Na wale wanafunzi, kila mtu kwa kadiri ya alivyofanikiwa, wakaazimu kupeleka msaada kwa ndugu zao waliokaa Uyahudi"* (**Mdo 11:29**). Kanisa la Makedonia walijitolea kwa ukarimu ingawa wao wenyewe walikuwa na tatizo la *"umasikini mkubwa"* na*"dhiki nyingi"* (**2 Kor 8:1-5**). Mungu aliwabariki watu husika wote na makanisa: Alimimina neema yake (**Mdo 4:33; 2 Kor 8:1**); aliwapatia furaha kubwa (**Mdo 2:46; 2 Kor 8:2**); aliwahudumia mahitaji yao (**Mdo 4:34**); aliwaunganisha pamoja (**Mdo 2:44, 46; 4:32**); walipata kibali mbele za watu (**Mdo 2:47**); alisababisha ushuhuda wao kuwa na nguvu (**Mdo 2:43; 4:33**); na akawasababisha kuongezeka (**Mdo 2:47**). Tunachofanya na fedha na mali zetu ni ishara ya kimatendo, na mwonekano wa ki-nje inayoonekana kwa macho ya hali yetu ya kiroho iliyo kwa ndani.

**6:20-21:** ***[20]Ee Timotheo, ilinde hiyo amana, ujiepushe na maneno yasiyo ya dini, yasiyo ya maana, na mashindano ya elimu iitwayo "elimu ya uongo"—[21]ambayo wengine wakiikiri hiyo wameikosa imani. Neema na iwe pamoja nanyi.***

***Ee Timotheo:*** Hata maneno madogo-madogo ni ya muhimu. Paulo hakumalizia kwa kusema "Ilinde hiyo amana." Wala hakusema, "Timotheo, ilinde hiyo amana." Badala yake, alisema "*'Ee'* Timotheo, ilinde hiyo amana." Hayo maneno machache "Ee" ni neno la shauku. Tunasema "Ee" tunaposema na watu ambao ni wa muhimu kwetu, na tunapozungumzia mambo yaliyo muhimu sana kwetu. Paulo anaufungua moyo wake hapa. Anajua kwamba anakaribia mwisho wa kuishi maisha ya hapa duniani. Anataka kuhakikisha kwamba alichoyasema, na maisha aliyoishi, hayakuwa ni bure, bali yataendelezwa kwa maisha ya uaminifu ya Timotheo na, kupitia yeye, na kwetu sisi.

***Ilinde hiyo amana:*** Huwa "tunalinda" vitu ambayo ni muhimu kwetu. Kwa jambo hilo, Kwa hapa, ni Injili. Hii ni mara ya tatu Paulo anasema kuhusu "amana." Katika **1:11** alisema kwamba amewekewa amana*"Injili ya utukufu"*. Katika **1:18-19** alimkabidhi *"amri hii . . . uvipige vita vizur, ukiitunza imani na dhamiri njema,"* Timotheo. Sasa Paulo anamwambia Timotheo "Kulinda" kile alichowekewa amana. Tunailinda injili kwa kuijua, kuielewa, kuishi kwa hiyo, kuitangaza, kuifundisha, na *"kuikabidhi [hiyo] kwa watu waaminifu watakaowafundisha na wengine"* (**2 Tim 2:2**).

***Jiepushe na mambo yasiyo ya dini na maneno yasiyo na maana . . . na wakaikosa imani:*** Paulo anamalizia waraka wake kwa njia ileile aliyoanza nayo, kwa kumsihi Timotheo kuwa mwamininifu, na kwa kumwonya kahusu kukengeuka. Tatizo la mafundisho ya uongo halikwepeki. Kwa upande mwingine, mafundisho ya uongo ni kama sifuri tu lakini *"maneno yasiyo na matunda"* (**1:6**), *"hadithi za kidunia ziwafaazo wazee"* (**4:7a**), na *"maneno ya ubatili na maneno yasiyo na maana"* (**6:20**) Kwa upande mwingine, mafundisho ya uongo *"roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani"* kama chanzo chake. (**4:1**), yamejaa ubishi na ushindani wa maneno (**6:4**), husababisha *"kuchomwa moto dhamiri zao"* (**4:2**) na *"kuharibika akili zao"* (**6:5**) kwa wale wanaoyapenda hayo, "ni kuangamia" (**1:19**) au kusababisha wengine *"kupotoshwa"*(**6:21**) kutoka imani, na kusababisha kila aina ya "maswali" (**1:4**), *"husuda, ugomvi, matukano, shuku mbaya, na mashindano ya watu"* (**6:4-5**) ndani ya kanisa. Swala linahusu uzima wa milele na mauti. Kwa hiyo, Paulo anaanza na hilo, analijadili kwa undani sana katika kitabu hiki, na kumalizia kwa hilo.

***Neema iwe pamoja nanyi:*** Paulo alianza waraka wake kwa kusema "*Neema, rehema, na amani"* (**1:2**). Anamalizia kwa neno hilo hilo. Kwa kusema,*"neema na iwe pamoja nanyi,"* Paulo anatukumbusha sisi kwamba, ingawaje kudumisha uaminifu ni kugumu (na hivyo, katika *"kuvipiga vita vilivyo vizuri"*), hatuko

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

peke yetu. Vita tunavyopigana kinyume na dunia, mwili, na ibilisi, ndivyo vita vikubwa kuliko vyote ulimwenguni. Lakini hatupigani sisi wenyewe. Bwana yuko pamoja nasi: *"Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake,"* (**Fil 2:13**). Yeye mwenyewe alisema,*"Sitakupungukia kabisa wala sitakuacha kabisa"* (**Ebr 13:5**). Hilo linapaswa kututia moyo na kutufariji, kwa sababu neno la Kiyunani "ninyi" katika **6:21 l**iko katika uwingi, sio umoja. Mungu hakuwa na Timotheo peke yake, yupo pamoja nasi. Kwa hiyo, *"na tuvipige vita vile vizuri vya imani, tushike sana uzima ule wa milele tulioitiwa"* (**6:12**).

## 1 TIMOTHEO: KIJARIDA CHA MAFUNZO YA KIUTENDAJI

### 1 Timotheo 1:1-7

***[1] Paulo, mtume wa Kristo Yesu, kwa amri ya Mungu Mwokozi wetu na Kristo Yesu, taraja letu; [2] kwa Timotheo, mwanangu hasa katika imani. Neema na iwe kwako, na rehema, na amani, zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Kristo Yesu Bwana wetu. [3]Kama vile nilivyokusihi ukae Efeso, nilipokuwa nikisafiri kwenda Makedonia, ili uwakataze wengine wasifundishe elimu nyingine; [4] wala wasiangalie hadithi na nasaba zisizo na ukomo, ziletazo maswali wala si madaraka ya Mungu yaliyo katika imani; basi ufanye hivyo. [5] Walakini mwisho wa agizo hilo ni upendo utokao katika moyo safi na dhamiri njema, na imani isiyo na unafiki. [6] Wengine wakiyakosa hayo wamegeukia maneno ya ubatili; [7] wapenda kuwa waalimu wa sheria, ingawa hawayafahamu wasemayo wala mambo yale wayanenayo kwa uthabiti.***

**1:1-2—Paulo Mtume, tumaini letu, Timotheo, "mwana halisi katika imani".**

Paulo anaanza waraka huu Kwa kuonyesha hoja mbili zilizo muhimu sana:

1) Paulo alikuwa anamuandikia Timotheo katika mamlaka yake maalum kama Mtume wa Yesu Kristo. Paulo alikuwa amechaguliwa rasmi na kubadilishwa kimuujiza na Mungu (**Mdo 9:31**); Paulo kibinafsi alikuwa amemwona Yesu Kristo (**1 Kor 9:1, 15:8-9**); Paulo alikuwa ametengwa na Mungu kwa ajili ya huduma yake ya Utume na alikuwa amefundishwa kibinafsi na Mungu (**Gal 1:11-24**); Paulo alipewa ufunuo maalum na Mungu naye alitenda ishara zote za utume wa kweli (**2 Kor 12:1-12**); utume wa Paulo ulikuwa ni kwa agizo la Mungu, na mafundisho yake ni sawa na mafundisho ya Yesu mwenyewe (**1 Tim 1:1, 6:3**).

2) Nyuma ya Paulo anasimama Mungu mwenyewe na "Kristo Yesu aliye tumaini letu". Watu wengi huweka matumaini yao, na ndoto, na nguvu zao zote katika dunia hii, na maisha haya; wanafikiri kwamba dunia hii na maisha haya ndiyo kila kitu kilichopo. Kwa hiyo, Paulo alisema katika **1 Kor 15:19**, "Kama katika maisha haya tu tumemtumaini Kristo, sisi tu masikini kuliko watu wote." Hata hivyo, Paulo alitambua kwamba dunia hii na maisha haya siyo kila kitu kilichopo. Badala yake, kuna umilele: Kutakuwa na mbingu mpya na dunia mpya, na kuna uzima wa milele, unaoanzia sasa, kwa watu waliompokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wao. Yesu Kristo kusema kweli anatawala sasa juu ya uumbaji wote, na atawafanya wale walio wake kuwa katika mfano wa kufanana naye (**Mdo 2:22-36; Rum 8:26- 39; 1 Kor 15**). Kwa hiyo mamlaka ya Paulo kama Mtume, na Yesu Kristo, mamlaka ya mwisho na Bwana wa ulimwengu, wanafanya kile kinachonenwa katika kitabu hiki cha umuhimu mkuu.

**1)** Wakati watu wanataka kujua jinsi wanavyotakiwa kuishi—ili kujua matumaini na kugundua maana na utoshelevu—ni wapi wanakotazama, ni mamlaka gani wanazozitafuta, kuwaonyesha hayo?

- **A)** Vipi kuhusu wewe?

**2)** "Mtume," ni nani? Na nini umuhimu wa Mitume?

- **A)** Ni sifa gani huelekea kutuvutia?
- **B)** Ni sifa gani za kipekee alizokuwa nazo Paulo kama mtume?
- **C)** Timotheo hakuwa "mtume" kama Paulo. Yeye hakuwa na mafunzo maalum aliyokuwa ameyapata Paulo. Hata hivyo alikuwa mwalimu mwaminifu wa Neno la Mungu. Je ni sifa gani alizokuwa nazo Timotheo, na hii inakutiaje wewe moyo?
- **D)** Je zipi zinatakiwa ziwe baadhi ya ishara au dalili za Utume wa kweli katika kizazi chetu?
  - **1)** Ni ishara au alama gani ambazo Wakristo wanaokulia wazifuate ili wafuate mafundisho ya kweli ya utume leo?
  - **2)** Inakuwaje sisi kama viongozi wa kanisa tunapungukiwa katika kuonyesha kwamba tu warithi wa kweli wa mitume?
  - **3)** Je tunatakiwa kufanya nini kuhusu hilo?

**3)** Je watu wanatumainia nini zaidi?

- **A)** Watu wa kanisa lako wanatumainia nini zaidi?

**B)** Wewe unatumainia nini zaidi?

**4)** Mtume Paulo anatuambia nini kiwe (au kinatakiwa kiwe) ndiyo tumaini letu la kweli?
**A)** Je anamaanisha nini kwa hili—Ni kwa njia zipi na kwa nini Kristo Yesu ni tumaini letu?

**5)** Je ni kiasi gani tumaini hili lililo katika Kristo Yesu lina thamani kwa watu kanisani kwako unaowajua?
**A)** Je unawezaje kujua?
**B)** Je Yeye ana thamani kwako kiasi gani? Na kwa nini?
**C)** Je *unaonyeshaje katika maisha yako* kwamba Kristo Yesu ni tumaini lako?

**6)** Je matatizo gani unayaona katika desturi za Kiafrika katika kuwakuza viongozi wanaoibukia?
**A)** Tunawezaje kurekebisha matatizo haya ili kuwapata viongozi waliopevuka katika kanisa?

**7)** Wakati mwingine viongozi waliopo madarakani wanawaona viongozi wanaochipukia na wenye sifa zinazotakiwa kama ushindani na tishiokwao.
**A)** Je umelionaje hili likitokea katika kanisa la Afrika?
**B)** Ni hatua gani tunaweza kuzichukua kuwainua viongozi wapya ndani ya kanisa bila kuwafanya tishio kwa viongozi waliopo?

**8)** Paulo alimwita Timotheo "Mwanangu hasa wa imani." (Katika **1 Kor 4:17** Paulo pia alimwita Timotheo "mwanangu mpendwa, mwaminifu katika Bwana".)
**A)** Je mila au desturi za kiafrika zitauonaje uhusiano kati ya Paulo na Timotheo?
**B)** Je wachungaji wa Afrika wana mtu wanayemtazama kama "Timotheo"—m .y., kama "mwana hasa katika imani" ambaye wanaweza kumlea na kumwinua kama kiongozi katika kanisa?
**C)** Je ni tofauti gani tungeleta ndani ya kanisa kama tungeamua kimatendo kuwainua "wana hasa katika imani" ili kuchukua nafasi za uongozi?
**D)** Tunatakiwa tuchukue hatua gani katika *kuwakuza* viongozi wapya katika kanisa ili kuhakikisha kuwa wanakuwa "mwanangu hasa katika imani"?

**9)** Katika safari ya pili ya Paulo, alikutana na Timotheo (ambaye tayari alikuwa mwanafunzi), na akamtahiri kwa sababu ya Wayahudi katika eneo lile ambao watakuwa wakifanya kazi pamoja (**Mdo 16:1-5**). Baadaye katika safari ile ile, Timotheo aliendelea kufanya huduma katika Beroa baada ya Paulo kuelekea Athens. Hata hivyo Timotheo alikuwa muhimu kwa Paulo kiasi kwamba alitoa agizo maalum kwa kanisa la Beroa kumleta Timotheo kwake mapema iwezekanavyo (**Mdo 17:10-15**). Hivyo Paulo alianza kuwainua viongozi wapya kabisa tangu mwanzo. Paulo analiona hili kama jukumu muhimu.
**A)** Kama kanisa la Afrika lingefanya hivi, kungeleta utofauti gani?
**B)** Kama tungefanya hivi, je kungeleta tofauti gani kwenye huduma zetu wenyewe?

**1:2 Neema, Rehema, na Amani**

Paulo kwa kawaida huanza nyaraka zake na salamu "Neema na amani." Ni katika 1 Timotheo na 2 Timotheo tu anaongezea na neno "rehema" katika salamu zake (mstari wa 2). "Rehema" kikawaida hubeba wazo la huruma kwa mtu asiye na bahati na mhitaji. Mnenaji moja alitofautisha kati ya "rehema" na "neema" kwa namna hii: "[Rehema] siku zote hushughulikia kile tunachokiona kina uelekeo wa maumivu, majonzi, na kukosa raha, matokeo haya ni ya dhambi; na [neema] siku zote hushughulikia dhambi na hatia yenyewe. Moja huleta unafuu, na jingine msamaha; moja linatibu, kuponya, kusaidia; wakati jingine linatakasa na kurudisha heshima" (George W. Knight, *The Pastoral Epistles: A Commentary on the Greek Text,* NIGTC, Grand Rapids, MI: Eerdmans, 1992, 66)

**1)** Katika salamu yake ya kimaombi kwa Timotheo katika mstari wa 2, Paulo ni *chombo* cha "neema", rehema, na amani". Hata hivyo anaelezea kwamba neema", rehema, na amani zinatoka kwa Mungu aliye Baba na Kristo Yesu Bwana wetu" – m.y. Mungu Baba na Kristo Yesu ndio *chanzo* cha neema, rehema, na amani.
**A)** Kwa nini Paulo aliomba kwamba Timotheo apokee mambo haya matatu kutoka kwa Mungu Baba na Kristo Yesu aliye Bwana?
**B)** Kwa nini watu leo wanahitaji "neema, rehema, na amani" zitokazo kwa Mungu na Kristo?
**C)** Ni kutoka vyanzo gani leo watu wanajaribu kupata neema, rehema, na amani. katika maisha yao?
**D)** Ni matokeo gani yanatokea katika maisha ya watu wanapotafuta neema, rehema, na amani kutoka vyanzo vingine tofauti na Mungu kupitia Kristo (na nini kisingizio walicho nacho watu kinachowazuia kutafuta neema, rehema, na amani kutoka kwa Mungu katika Kristo)?

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

**E)** Ni kwa kiwango gani leo Wakristo wanaelewa neema, rehema, na amani, kutoka kwa Yesu Kristo?

**2)** Kuhusiana na viongozi wa kanisa kuwa vyombo ambavyo Kristo anadhihirishia neema, rehema, na amani, hebu fikiria yafuatayo:

**A)** Wakati mwingine viongozi wana wakati mgumu kuonyesha rehema kwa wale walio chini ya madaraka yao. Je una uzoefu gani kuhusu hali hiyo?
**B)** Kwa nini watu unaowalea kuwa viongozi katika kanisa wanahitaji rehema?
**C)** Je wewe ulionyeshwa rehema na mtu kwa jinsi gani? Je ilikuletea matokeo gani? Je ilileta matokeo gani kwa tabia yako ya baadaye?
**D)** Kama wewe ungejulikana kuwa ni mtu wa kuonyesha rehema kwa wengine, unafikiri hilo lingeleta matokeo gani kwa kanisa?

**1:3-4—Mafundisho potofu, hadithi, na nasaba**

Neno lililotafsiriwa kama "mafundisho mageni" hapo juu, limetumika tena katika **1 Tim 6:3** (ambapo limetafsiriwa kama "elimu nyingine"). Maana iliyopo hapo ni "kufundisha mafundisho ambayo kimsingi ni tofauti na injili ya Paulo." Ingawaje elimu nyingine ambayo Paulo anaizungumzia haikutajwa rasmi, inaelekea kuhusiana na: kuvutiwa na desturi na vizazi vya watu [m.y., mila za vyanzo vya watu] (**1 Tim 1:4, 4:7; 2 Tim 4:4; Tito 1:14, 3:9**); kuhusiana na sheria ya Kiyahudi (**1 Tim 1:7; Tito 1:10, 14, 3:9**); uelekeo wa udadisi, mivutano na ubishani (**1 Tim 1:4, 6; 6:4; 2 Tim 2:14, 16, 23; Tito 1:10; 3:9**); udanganyifu (**1 Tim 4:1-3; 2 Tim 3:6-13; Tito 1:10-13**); kushuka maadili (**1 Tim 1:19-20; 2 Tim 2:16, 19** na **2 Tim 3; Tito 1:15-16**); na tamaa ya kupata mali kwa njia ya mafundisho yao (**1 Tim 6:5; 2 Tim 3:2, 4; Tito 1:11**). Mafundisho ya udanganyifu yanaweza pia kuhusisha mbinu kali za kukataza watu kuoana na kuwazuia kula nyama (**1 Tim 4:1-5**), na mafundisho kwamba ufufuo wa wafu ulikwisha kutokea (**2 Tim 2:18**). Na kama mnenaji moja alivyojumuisha, mafundisho ya udanganyifu "yaliyochanganya vipande vya Imani kali ya Kiyahudi, udadisi wa imani za kimazingaombwe, na ikiwezekana pia uchawi." (William D. Mounce, *Pastoral Epistles* [Word Biblical Commentary, vol.46] (Nashville, Tenn.: Thomas Nelson, 2000), lxxxv).

Umuhimu wa hili upo katika neno alilolitumia Paulo katika kumwambia Timotheo "kuwakataza" wengine kutofundisha elimu nyingine (mst. 30). Usemi huo ungeweza kutafsiriwa "kuamuru." Kama anavyoongeza Mounce, usemi huo "hutumika kijeshi na kisheria pia, kuelezea amri ya kijeshi au hati ya kuitwa mahakamani." (Ibid., 18)

**1)** Viongozi wanahitaji kuielewa Biblia, lakini pia waweze kugundua mafundisho ya potofu.

**A)** Ni mafundisho gani ya kigeni (potofu) yaliyopo katika jumuia yetu ambayo tunatakiwa kuyakabili?
**B)** Ni mafundisho gani ya kigeni tuliyo nayo katika kanisa letu ambayo viongozi wanaochipukia wanapaswa kuyakabili?
**C)** Ni athari gani zinatokana na mafundisho hayo ya kigeni katika kanisa?
**D)** Ni hatua gani zi kuchukuliwe kukabili mafundisho hayo mageni?

**2)** Vipi mafundisho ya uongo yanawadhuru wakristo walio wachanga na wanaokua katika kanisa leo?

**A)** Je wanawezaje Wakristo walio wachanga na wanaokulia, kugundua na kutambua mafundisho ya kweli kuyatofautisha na mafundisho ya udanganyifu?

**3)** Paulo anatuambia tusisikilize "hadithi na nasaba zisizokoma." Hadithi au visa ni tunzi zilizotungwa kiustadi ili kutuonyesha jinsi ya kuishi au kujipatia umaana na kujitosheleza nafsi; wakati Nasaba ni maswala yanayohusiana na mababu zetu, mikondo ya damu, na makabila tuliyotokea.

**A)** Je ni hadithi gani unazijua ambazo ni muhimu kwa watu unaowafahamu (na kwako mwenyewe)?
**B)** Je ni mila gani watu hufanywa na watu fulani unaowajua ambazo huwasaidia kukubalika na mababu zao waliokufa?

**4)** Soma **Fil 3:1-11** na uone kile Paulo alichosema kuhusiana na uzao wake mwenyewe katika **Fil 4:3-5**.

**A)** Kwa nini Paulo alizungumzia uzao wake mwenyewe wakati amwambia Timotheo kutosikiliza nasaba na hadithi zisizo na ukomo?
**B)** Maoni ya Paulo yalikuwa nini kuhusu habari za ukoo na uzao zikilinganishwa na kumjua Kristo?
**C)** Kama Paulo angekuwa anaongea na wewe leo, ni maswala gani ambayo angekuwa anakuambia?
**D)** Je tunawezaje kuwasaidia watu wetu kushughulikia maswala hayo?

**1:5—Lengo la maagizo yetu**

**1)** Je ni malengo gani muhimu sana waliyo nayo watu?

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

**A)** Ni nini malengo yako makuu zaidi?
**B)** Nini malengo yetu makuu kama *waalimu* tunaposimama ili kuhubiri na kufundisha?
**C)** *Kwa nini* tunapenda kuhubiri na kufundisha?
**D)** Ninawezaje kujua kama msukumo wa kufundisha na kuhubiri kwangu siyo udanganyifu tu wa moyo wangu kwa ajili ya madaraka, majigambo, kutambulika, fedha, au kwa sababu yoyote isiyofaa?

**2)** Lengo la maelekezo ya Paulo lilikuwa zaidi ya kupata "ufahamu wa kichwani" au "diploma (m.y., "cheti cha makaratasi").
**A)** Paulo anaelezeaje lengo lake la muhimu sana la kutoa agizo lake [mst. 5]?
**B)** Kwa nini hili liwe ni lengo muhimu zaidi?
**C)** Kwa nini huwa tunapenda kusisitiza "Vyeti vya Makaratasi"?
**D)** Ni hatua gani tunaweza kuzichukua ili kukuza sifa za "ndani" za viongozi wetu?

**3)** Katika mstari wa 5 Paulo anajenga uhusiano kati ya kile tunachokifanya kwa nje (kuonyesha upendo), na jinsi tulivyo kwa ndani (moyo safi, dhamiri njema na imani ya kweli).
**A)** Kwa nini upendo wa kweli utoke kwa mtu aliye na moyo safi, dhamiri njema, na imani ya kweli?
**B)** Nini husababisha mioyo ya watu katika kanisa kuwa mbali na usafi?
**C)** Je Paulo angelishughulikiaje hilo?
**D)** Nini husababisha dhamiri ya watu katika kanisa kutukuwa njema?
**E)** Je Paulo angelishughulikiaje hili?
**F)** Nini kinasababisha imani ya watu kanisani kutokuwa ya kweli?
**G)** Je Paulo angelishughulikiaje hili?
**H)** Ni hatua gani tunaweza kuchukua kushughulikia maswala haya kama ambavyo angefanya Paulo?
**I)** Wakristo wengi wamekiri imani pasipo kudhihirisha upendo wowote au matendo mengine kuonyesha imani yao. Nini yaweza kuwa ni matokeo au athari za hali hii kwa kanisa?

**4)** Soma **Mk 12:28-34** kuhusiana na kile Yesu alichosema kwamba ndicho amri kuu kuliko zote.
**A)** Ukizingatia kile anachosema Yesu, na kile anachosema Paulo, kwa nini unafikiri hilo silo lengo la watu?
**B)** Kama kuna tofauti kati ya kusudio la msingi la maisha yako na lile Paulo analolisema kuwa ni lengo la agizo lake, je unafikiri unatakiwa kubadilisha lengo lako la msingi?
**C)** Utalichukuliaje hili—Ni hatua gani za kiutendaji unazoweza [ambazo utazifanya] kuonyesha upendo?
**D)** Je unawezaje kuwasaidia watu katika kanisa watathmini upaya maisha yao ili waweke malengo yao ya msingi kuhusiana na kile anachosema Yesu na Paulo?

**<u>1:6-7—Kugeukia mbali na lengo:</u>**
**1)** Paulo anasema watu wengine wamegeukia mbali na mambo haya (m.y., kutoka kwenye maelekezo ya Paulo na lengo la agizo lake). Maneno yao "hayana matunda." Hawayajui hata yale wanayoyasema.
**A)** Ni njia zipi ambazo mtu anaweza kujifunza mafundisho ya kweli ya Kikristo na jinsi ya kuishi maisha ya Kiristo?
**B)** Ni nini ishara iliyo bora kabisa inayoonyesha kwamba mtu anaelewa kwa dhati, Ukristo unahusu nini hasa — kwamba kweli amejifunza agizo la Paulo?

**2)** Kwa nini baadhi ya Wakristo leo wanafikiri kwamba unapoishika Sheria ya Musa unakuwa na mahusiano mazuri na Bwana?
**A)** Je twawezaje kushughulikia jambo hilo kisahihi, ili kwamba lisiwapelekee watu kufikiri kwamba wako huru kuishi maisha ya dhambi?

## <u>1 Timotheo 1:8-20</u>

***8Lakini tunajua kwamba sheria ni njema, kama mtu akiitumia kwa njia iliyo halali; 9akilifahamu neno hili, ya kuwa sheria haimhusu mtu wa haki, bali waasi, na wasio wataratibu, na makafiri, na wenye dhambi, na wanajisi, na wasiomcha Mungu, na wapigao baba zao, na wapigao mama zao, na wauaji, 10na wazinifu, na wafiraji, na waibao watu, na waongo, nao waapao kwa uongo, na likiwapo neno lolote linginelo lisilopatana na mafundisho yenye uzima, 11 kama vile ilivyonenwa katika habari njema ya utukufu wa Mungu ahimidiwaye, niliyowekewa amana.***

***12Nami namshukuru Kristo Yesu Bwana wetu, aliyenitia nguvu kwa sababu aliniona kuwa mwaminifu, akaniweka katika utumishi wake, 13ingawa hapo kwanza nalikuwa mtukanaji, mwenye kuudhi watu, mwenye***

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

***jeuri, lakini nalipata rehema kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga, na kwa kutokuwa na imani;*** 
14
***na neema ya Bwana wetu ilizidi sana, pamoja na imani na pendo lililo katika Kristo Yesu.*** 
15
***Ni neno la kuaminiwa, tena lastahili kukubalika kabisa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi; ambao wa kwanza wao ni mimi.*** 
16
***Lakini kwa ajili hii nalipata rehema, ili katika mimi wa kwanza Yesu audhihirishe uvumilivu wake wote; niwe kielelezo kwa watakaomwamini baadaye, wapate uzima wa milele.*** 
17
***Sasa kwa Mfalme wa milele, asiyeweza kuuona uharibifu, asiyeonekana, Mungu peke yake, na iwe heshima na utukufu milele na milele. Amina.***

18
***Mwanagu Timotheo, nakukabidhi agizo hilo liwe akiba, kwa ajili ya maneno ya unabii yaliyotangulia juu yako,ili katika hayo uvipige vile vita vizuri.*** 
19
***uwe mwenye imani na dhamiri njema, ambayo wengine wameisukumia mbali, wakaangamia kwa habari ya imani.*** 
20
***Katika hao wamo Himinayo na Iskanda, ambao nimempa Shetani watu hao, ili wafundishwe wasimtukane Mungu.***

**1: 8-11—Matumizi sahihi ya Sheria**

**1)** Sheria ni nini?

**A)** Sheria ya Mungu ni nini?
**B)** Je Paulo anasema sheria iliwekwa kwa ajili ya watu gani?
**C)** Kwa nini ni lazima kuwa na sheria?

**2)** Je, tunapotuhumiwa kuvunja sheria hutokea nini?

**A)** Je tunaleta heshima au aibu kwa baba zetu na familia zetu tunapovunja sheria?
**B)** Vipi kuhusu sheria za Mungu—Je tunaleta heshima au aibu kwa Baba yetu wa mbinguni na kwa familia ya Mungu tunapovunja sheria yake?
**C)** Biblia inatuambia nini kuhusu matokeo ya kuvunja sheria ya Mungu?
**D)** Je unamfahamu yeyote yule aliyeishika sheria ya Mungu kikamilifu—muda wote, na kwa nia njema?
**E)** Je wewe umefanya hivi?
**F)** Kwa nini watu kamwe hawafuati sheria—kikamilifu na kitimilifu, muda wote, licha ya sababu njema zote?

**3)** Kwa vile watu hawafuati kikamilifu sheria ya Mungu, wanafanya kila namna za taratibu na desturi na mambo mengine kujaribu kujifanya weyewe "wasafi" au watakatifu—kujaribu kuondoa dhambi zao na kujihesabia haki kwa Mungu.

**A)** Je ni taratibu na desturi gani, na mambo mengine yapi wanayojaribu kuyafanya watu?
**B)** Kwa nini taratibu na mapokeo hayo hayafanikiwi kuwafanya wawe wasafi na wawe watakatifu?
**C)** Je hiyo ni njia ya kweli ya kufanyika mtakatifu au ni "hadithi" tu?
**D)** Kama tunajaribu kufuata njia tofauti na zile alizosema Mungu, kwa nini hazimpi Yeye heshima?
**E)** Tunawezaje kuwasaidia watu tunaowajua waachane na tabia za kufuata desturi na mapokeo ambazo haziwasaidii (na pia hazimpi Mungu heshima)?

**1:12-20 Mfano wa Paulo**

**1)** Katika **1:12-17** Paulo anatuambia kuwa alipata jibu la kupata haki kwa Mungu.

**A)** Je Paulo aliweza kuishika sheria? Kama sivyo, alikuwa ni mtu wa aina gani?
**B)** Paulo aliwezaje kupata kibali kwa Mungu hata kama hakuishika sheria ya Mungu?
**C)** Ni kwa jinsi gani tunapata kibali kwa Mungu?
**D)** Je hili linaonyesha jambo gani kuwa ndiyo kusudio halisi la sheria?

**2)** "Neema" ya Mungu ni nini?

**A)** Nini ina nguvu zaidi, dhambi yako au neema ya Kristo?
**B)** Unaipokeaje neema hii?
**C)** Je "Kuamini katika Yeye" (mst. 16) kunamaanisha nini na kunahusikaje na maisha yetu? "Je kunaonekanaje?" Je ni swala la mara moja tu au ni swala la maisha yote?

**3)** 1Timotheo haiishii kumwelekeza Timotheo peke yake. Pia ni kwa ajili yetu.

**A)** Tunajuaje hili?

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

**1 Tim 2:1-7**

***[1]Basi, kabla ya mambo yote, nataka dua, na sala, na maombezi, na shukrani, zifanyike kwa ajili ya watu wote;***
***[2]kwa ajili ya wafalme na wote wenye mamlaka, tuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu. [3]Hili ni zuri, nalo lakubalika mbele za Mungu mwokozi wetu; [4]ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli. [5]Kwa sababu Mungu ni moja, na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni moja, mwanadamu Kristo Yesu; [6]ambaye alijitoa mwenyewe kuwa ukombozi kwa ajili ya wote, utakaoshuhudiwa kwa majira yake, [7]nami kwa ajili ya huo naliwekwa niwe mhubiri na mtume (nasema kweli, sisemi uongo) mwalimu wa mataifa katika imani na kweli.***

**2: 1-7—Kuombea wote, hasa kwa ajili ya viongozi wetu**

**1)** Watu siku zote hulalamikia mambo ambayo ni mabaya kuhusu serikari, viongozi, na watu wengine.

**A)** Paulo anasema tunatakiwa kufanya nini?

**B)** Je Paulo aliliona ni zito kiasi gani swala la kuwaombea wengine? Unawezaje kujua?

**C)** Kwa nini unafikiri maombi yana kupaumbele kiasi hicho kwa Paulo?

**D)** Je tunawezaje kuyafanya maombi yapate kipaumbele zaidi katika kanisa letu?

**2)** Mstari 1 unaorodhesha aina mbali mbali za maombi, ikiwa ni pamoja na: kuomba na kufanya dua kwa ajili ya wengine; maombi ya dhati na maombezi kwa niaba ya wengine; na shukurani kwa niaba ya wengine.

**A)** Kwa nini ni muhumu kufanya maombi ya aina mbali mbali kwa ajili ya watu wengine?

**3)** Katika mstari wa 2 Paulo anasema kwamba maombi haya yote yanatakiwa yafanyike "kwa wafalme na wote walio katika mamlaka."

**A)** Ni sababu gani anayotoa Paulo katika mstari wa 2 ya kuwaombea wale walio katika mamlaka?

**B)** Kwa nini ni muhimu kuishi "maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu?" Je huu ndio mwisho wake, au kuna umuhimu kwa sababu nyinginezo?

**C)** Katika mstari wa 4 Paulo anataja sababu nyingine kwa nini tunatakiwa kuwaombea wale walio katika mamlaka. Ni nini hiyo?

**D)** Kwa nini kuwaombea wale walio katika mamlaka ni muhimu?

**E)** Je "kuishi maisha ya utulivu na amani, katika utauwa wote na ustahivu." kunahusianaje na kueneza Injili kwetu, ili kwamba wale tunaowashughulikia waweze "kuokolewa na kuja kuijua kweli?"

**F)** Tunawezaje kuwa na "shukurani" kwa ajili ya "wafalme na wote walio katika mamlaka" ikiwa hatukubaliani na siasa zao? Kwa nini tunatakiwa kushukuru kwa ajili ya viongozi wa namna hiyo?

**1 Timotheo 2:8-15**

***[8]Basi, nataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata pasipo hasira wala majadiliano. [9]Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani; [10]bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu. [11]Mwanamke na ajifunze katika utulivu, akitii kwa kila namna. [12]Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu. [13]Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye. [14]Wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa. [15]Walakini ataokolewa kwa uzazi wake, kama wakidumu katika imani na upendo na utakaso, pamoja na moyo wa kiasi.***

Walter Liefeld katika *NIV Application Commentary, 1 and 2 Timothy/Titus* (Grand Rapids, MI: Zondervan, 1999), 95-96, anasema hivi kuhusu mistari hii: "Kusudi kuu la agizo hili katika 1 Timotheo 2:8-10 si kuamuru *tendo* la kusali (maagizo maalum ya kufanya sala yamekwisha kutolewa katika mistari ya 1-2) lakini *mwenendo* wao - waume na wanawake *wakati wa* kusali na kuabudu …. Paulo anashughulikia utendaji wa kimaadli kuhusiana na maswala ya kidini kwa wanaume na wanawake. Anasisitiza kwamba muonekano wao wa nje usiwe unagongana na tabia yao ya utu wa ndani. Katika mstari wa 9-10 mfano ni uchaji wa utu wa ndani wa wanawake unatakiwa ujionyeshe kwa matendo mema. Katika nyakati za kale za Uyunani na hata siku za Paulo, mavazi yasiyositiri mwili, usukaji wa nywele, na mapambo ya vito vya thamani, vilikuwa vinatazamwa kuwa ni kinyume na maadili mema ya uchaji wa kweli. Hivyo, wanawake Wakikristo walitakiwa kuvaa mavazi ya 'kujisitiri.'

Maelezo ya aina ya vazi, usukaji wa nywele, na vito vya thamani, yanaelekea kudokeza sababu mbili za kwa nini yalikuwa hayatakiwi. 1) Kwanza ni gharama kubwa inayohusika. Kule kutajwa kwa dhahabu kwanena kwenyewe, na sifa inayotumiwa kuelezea vazi lenyewe kwanenwa kwamba ni 'nguo za thamani.' 2) Sababu nyingine ni ya kuhusishwa na maadili ya kidesturi."

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

**2:8—Sala za wanaume zinapaswa kutokana na maisha matakatifu**

**1)** Katika mstari wa 8 Paulo anakazia kwa *wanaume*. Anasema wanaume na wasalishe "pasipo hasira wala majadiliano."

**A)** Kwa nini kusali "pasipo hasira wala majadiliano" ni muhimu kwa maombi yetu?

**B)** Kwa vile Paulo anazungumzia hapa hasa kwa wanaume, je mstari huu unaonyesha dalili za dhambi zipi ambazo wanaume huelekea kuzifanya?

**C)** Kwa nini unafikiri wanaume wanaelekea kuwa na "ghadhabu" (hasira) na kuwa rahisi kwao kuwa "wanajadili" (kubishana)?

**D)** Je tunaweza kufanya nini kuwasaidia wanaume wa kanisa letu kushinda dhambi hizi na, badala yake, kuishi "maisha mema na ya utulivu wote katika ustahivu na uchaji?"

**2)** Kusudi kuu ambalo Paulo analielezea katika mistari hii ni kwamba watu waweze "kuokolewa na kuijua kweli." Ametaja mara mbili "kuishi" kwetu kukihusishwa na sala zetu (mst. 2 na 8).

**A)** Ni vipi na kwa nini kuishi kwetu kunahusishwa na watu wengine kuujia ufahamu wa kuokolewa na Kristo?

**B)** Kama Kanisa, tunaweza kufanya nini kuifanya mistari hii iwe sehemu yetu ya kanisa?

**2:9-15—Sala za wanawake zinapaswa kutokana na maisha matakatifu**

**1)** Maneno "vivyo hivyo" katika mstari wa 9 yanaendeleza wazo la Paulo—m.y., kuwaombea wengine (hasa viongozi wetu) kunapaswa kutokane na maisha matakatifu. Na sasa anahusisha wazo hilo hasa kwa wanawake.

**A)** Ikiwa wanaume wana udhaifu wa dhambi ya hasira na kubishana, ni dhambi gani katika mistari hii ambazo zinaonyesha kwamba wanawake wana udhaifu nazo?

**B)** Je tunaweza kufanya nini kuwasaidia wanawake wa kanisa letu kushinda dhambi hizi na, badala yake, kuishi "maisha mema na ya utulivu wote katika ustahivu na uchaji?"

**C)** Kule kutajwa kwa "kusuka nywele, na kwa dhahabu na lulu, na kwa nguo za thamani" katika mstari wa 9 kunaonyesha kwamba Paulo alikuwa anawakusudia wanawake matajiri na wenye mali. Hata hivyo, kwa vile msingi wa mjadala wetu hapa ni *kusali*, kama wanawake walikuwa wana uwezo wa kuvaa dhahabu, na lulu, na mavazi ya thamani, je kwa nini kujali wanavaa nini?

**D)** Je viko vitu vyovyote vya ki-nje (urembo) katika jamii zetu ambavyo vinaweza kuleta tafsiri mbaya kwa watu kuhusu Ukristo na uchaji wa kweli ulivyo?

**E)** Je "matendo mema" (mst. 10) na "jifunza kwa utiifu" (mst. 11) kunahusianaje na jinsi mwanamke anavyojiremba? Je kuna jambo au hoja ya ndani hapa ambayo Paulo anainena?

**1 Timotheo 3:1-13**

***3Ni neno la kuaminiwa; mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema. 2Basi imempasa askofu awe ni mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, ajuaye kufundisha; 3si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu; bali awe mpole, si mtu wa kujadiliana, wala asiwe mwenye kupenda fedha; 4mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu; 5yaani, mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje kanisa la Mungu?) 6wala asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi. 7Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje; ili asianguke katika lawama na mtego wa Ibilisi.***

***8Vivyo hivyo na mashemasi na wawe wastahivu; si wenye kauli mbili, si watu wa kutumia mvinyo sana, si watu wanaotamani fedha ya aibu; 9wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi. 10Hawa pia na wajaribiwe kwanza; baadaye waitende kazi ya ushemasi, wakiisha kuonekana kuwa hawana hatia. 11Vivyo hivyo wake zao na wawe wastahivu; si wasingiziaji; watu wa kiasi, waaminifu katika mambo yote. 12Mashemasi na wawe wanaume wa mke mmoja, wakiwasimamia watoto wao vizuri, na nyumba zao. 13Kwa maana watendao vema kazi ya shemasi hujipatia daraja nzuri, na ujasiri mwingi katika imani iliyo katika Kristo Yesu.***

Walter Liefeld katika *NIV Application Commentary, 1 and 2 Timothy/Titus* (Grand Rapids, MI: Zondervan, 1999), 95-96, anasema hivi kuhusu mistari hii: Ni muhimu kuelewa kwamba hapa katika 1 Timotheo 3:1 Paulo anamzungumzia Askofu katika utendaji ("kazi inayoonekana au kujulikana"), na siyo kama cheo au ofisi. Hapa hawatii moyo watu watafute vyeo, bali wajibu.

**3: 1-13—Sifa za viongozi katika kanisa**

**1)** Itazame orodha ya sifa za waangalizi (yaani, askofu, mashemasi) katika mst. 1-7:

**A)** Ni sifa zipi ambazo watu huwa na matatizo nazo zaidi? Kwa nini hali ni hiyo?

**B)** Je tunaweza kufanya nini kama kanisa kuwasaidia watu wetu wapate sifa katika kila kipengele

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

kilichotajwa na Paulo?

**2)** Itazame orodha ya sifa za waangalizi (yaani, maaskofu, mashemasi) katika mst. 1-8:

**A)** Ni sifa zipi ambazo watu huwa na matatizo nazo zaidi? Kwa nini kuna hali hiyo?

**B)** Je tunaweza kufanya nini kama kanisa kuwasaidia watu wetu wapate sifa katika kila kipengele kilichotajwa na Paulo?

**3)** Sifa za wazee (mst. 1-7) na za maaskofu na za mashemasi (mst. 8-12) huelekea, ni za *kuelezea tu* na siyo *zote kabisa*, za sifa zote anazotakiwa kuwa nazo kiongozi. Tunaliona hilo kwa vile katika **Tito 1:5-11** pana orodha inayofanana (ingawaje hailingani kabisa) ya sifa za askofu. Linganisha orodha ya sifa za 1 Timotheo na ya Tito, halafu tafakari yafuatayo:

**A)** Kulingana na orodha hizo mbili za sifa:

**1)** Ni *ujuzi na uwezo upi* anatakiwa kuwa nao kiongozi wa kanisa?

**2)** Kwa nini *ujuzi na uwezo huo* ni muhimu?

**3)** Je tunawezaje sisi kama kanisa kujua kama mtu fulani anayetaka kuwa kiongozi anao *ujuzi na uwezo* huo?

**B)** Kulingana na orodha hizo mbili za sifa:

**1)** Ni *tabia na sifa gani za binafsi* anatakiwa kuwa nazo kiongozi wa kanisa?

**2)** Kwa nini *tabia na sifa hizo* ni muhimu?

**3)** Je tunawezaje sisi kama kanisa kutambua kwamba mtu fulani anayetaka kuwa kiongozi anazo *tabia na sifa* hizo?

**C)** Kulingana na orodha hizo mbili za sifa:

**1)** Ni *heshima au sifa gani na mahusiano ya namna gani kwa wasio-Wakristo* anatakiwa kuwa nazo kiongozi wa kanisa?

**2)** Kwa nini *heshima au sifa hizo na mahusiano kwa wasio -Wakristo* ni muhimu?

**3)** Je tunawezaje sisi kama kanisa kutambua kwamba mtu fulani anayetaka kuwa kiongozi anazo *heshima hizo na mahusiano hayo na wasio wakristo*?

**4)** Jamii na desturi mbali mbali huelekea kuthamini na kupendelea sifa tofauti na tabia fulani. Jamii nyingine husisitiza mambo kama ubinafsi na mafanikio ya mtu, mara nyingi huku familia na mahusiano ya vikundi yakiharibiwa sana. Jamii nyingine huelekea kusisitiza makubaliano ya vikundi, wakati mwingine kwa gharama za juhudi za mtu binafsi na mafanikio yake mwenyewe. Tunatakiwa kuwa macho na mambo ambayo desturi na jamii zetu zinayathamini, kwa sababu desturi zetu zinaweza kutothamini au kutoyapa nafasi yale yote ambayo Paulo anayaona kama sifa muhimu za viongozi wa kanisa.

**A)** Ni sifa zipi ambazo Paulo anazijadili katika **1 Tim 3:1-13** ambazo jamii zetu zinajitahidi kuzitekeleza?

**B)** Ni sifa zipi ambazo Paulo anazijadili katika **1 Tim 3:1-13** ambazo jamii zetu *hazizi*tekelezi?

**C)** Kwa sifa zile za uongozi ambazo jamii zetu *hazifanyi vizuri* katika kuzitekeleza, tunatakiwa tufanye nini kama kanisa kuwasaidia viongozi wetu waendane na sifa zote ambazo Paulo anasema wanatakiwa kuwa nazo?

**5)** Kumbuka kwamba neno pekee ambalo linafanana katika sifa za maaskofu (wazee) (mst. 4), mashemasi (mst. 8), na wanawake (mst.11) ni "ustahivu"/"wastahifu" (katika lugha ya Kigriki, neno hilo limewekwa kimatendo katika mst. 4; na katika hali ya jina katika mst. 8, 11). Neno hilo hilo lipo mwishoni mwa mstari wa **1Tim 2:2**. Neno hilo linamaanisha "mwenendo au tabia inayoonyesha kuwa mtu yuko juu ya hali ya kawaida na kwa hiyo *anastahili kupewa heshima maalum."* Mambo kama "asiyelaumika," unyofu," "heshima," na "utakatifu" humfanya mtu wa "ustahifu/astahiliye heshima maalum." Sifa hii ni dhahiri ya umuhimu mkuu kwa Paulo.

**A)** Ni jinsi gani sifa hii au ustahifu huu ni muhimu katika huduma za kuelimisha au kufundisha na kuhubiri kwenye makanisa yetu?

**B)** Je tunaweza kufanya nini ili kuhakikisha watu wetu—hasa viongozi wetu na wale chipukizi wenye uelekeo wa uongozi—waelewe umuhimu wa kuishi maisha "yanayostahili kupewa heshima maalum?"

**6)** Katika mstari wa 2, ambapo panasema mzee wa kanisa /mwangalizi au shemasi anatakiwa kuwa "mume wa mke mmoja," katika Kigriki, hasa panasema "awe na mke mmoja." Usemi huo huo unatumiwa katika mstari wa 12 kuhusiana na mashemasi (na usemi, "mke wa mume moja" unatumiwa katika **1 Tim 5:9**). Biblia haiwakatazi watu wenye wake zaidi ya mmoja kujiunga na kanisa, ingawaje wazo la Kibiblia ni kuwa na mwenzi mmoja. Yawezekana kwamba hali ya kuwa na mke mmoja inahitajika kwa wale ambao ni viongozi wa kanisa, kama wameoa au kuolewa (hali ya kuwa ameoa au kuolewa siyo inayotakiwa ili kuwa kiongozi wa kanisa). Msisitizo halisi wa sifa hii ni uaminifu wa mtu anaouonyesha kwa mke wake.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

**A)** Kwa nini uaminifu katika ndoa ni swala muhimu sana kiasi kwamba Paulo anarudia mara mbili yaani kwa maaskofu (wazee) na kwa mashemasi?
**B)** Ingawaje ndoa ya wake wengi ilikuwa inafanyika katika Israeli ya kale, wakati Paulo anaandika haya ilikuwa adimu sana. Je ndoa za mke au mume zaidi ya mmoja ni swala ambalo lipo katika jamii zetu na linahitajika kuzungumziwa katika desturi zetu, hasa linapohusiana na uongozi wa kanisa?
**C)** Kama mistari ya 2 na 3 haimruhusu mtu ambaye ana wake zaidi ya mmoja kuwa askofu au shemasi; kwa nini iwe hivyo – na je tutamwelezaje hili mtu, ambaye angeweza kufaa sana kuwa askofu (mzee) au shemasi, lakini ana mke zaidi ya moja?

**7)** Zingatia kwamba sifa tatu za mwisho kwa maaskofu/wazee (kuisimamia nyumba yake vizuri, asiwe mtu aliyeongoka hivi karibuni; na kushuhudiwa mema na walio nje ya kanisa [mst. 4-7]) ni za muhimu kwa Paulo, kwa sababu ni sifa pekee zinazoambatana na *maelezo* ya sababu za umuhimu wake.
**A)** Nini zinaweza kuwa ndizo sababu zilizomfanya Paulo ahusishe sifa nyinginezo katika mistari 2-12?
**B)** Wakati kanisa letu linamfanya mtu fulani kuwa mzee au shemasi, ni vigezo gani huwa tunatumia, na ni *sababu* gani huwa tunasimamia vigezo hivyo?
**C)** Je tufanye nini, kama kanisa kuhakikisha kwamba vigezo vya kuwapata wazee na mashemasi vinaendana na sifa za Paulo?

**8)** Sifa moja inayotakiwa ili kuwa askofu / mzee wa kanisa, ambayo *si* sehemu ya sifa za kuwa shemasi ni uwezo wa kufundisha (mst. 2). Na hii ni kwa sababu majukumu ya shemasi ni ya mwelekeo wa kimatendo: ni huduma ya masaidiano, au huduma, ya kukutana na mahitaji ya watu (ona **Mdo 6:1-6**). Jukumu la shemasi ni la umuhimu sana kiroho. Walter Liefeld katika *NIV Application Commentary, 1 and 2 Timothy/Titus* (Grand Rapids, MI: Zondervan, 1999), 138-39, anasema hivi kuhusu mashemasi: "Ili kutosheleza malengo ya mashemasi wa zamani, mambo matatu ni ya lazima: (1) Kanisa ni lazima lichukue uamuzi wa kuanza kuwatafuta wanaume na wanawake ambao wana maadili na msimamo wa kiroho ulio mnyofu unaoelezwa katika 1Timotheo 3. (2) Watu hao wanahitaji kuwa na maono, moyo, na kutaka kutumika, wenye utayari, na wanaoyathibitisha hayo hata kabla ya uteuzi wao kwa matendo ya wema. Wanapaswa *wawe* mashemasi kabla ya *kuitwa* kuwa mashemasi. (3) Kanisa linatakiwa liifanye huduma hii kuwa ni huduma ya kukusudiwa kwa niaba ya mwili wote. Inatakiwa iwe inaonekana kwa jumuia yote kwa ujumla, ili kwamba jumuiya siyo tu *ipokee*, bali pia *ielewe* huduma ya upendo wa kanisa.
**A)** Je tunafanya vizuri kiasi gani kama kanisa kutimiza wito huu wa mashemasi wetu?
**B)** Je mashemasi wetu wanawezaje kuelewa na kuikubali huduma hii muhimu ya kiroho wanayoitumikia?
**C)** Je tunatakiwa kufanya nini kama kanisa kurejesha jukumu muhimu la Kibiblia linalotakiwa kufanywa na mashemasi wetu?

## 1 Timotheo 3:14-16

***[14]Nakuandikia hayo nikitaraji kuja kwako hivi karibu. [15]Lakini nikikawia, upate kujua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu, iliyo kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msingi wa kweli. [16]Hakuna mashaka yoyote juu ya ukuu wa siri ya dini yetu:***

***Alionekana katika umbo la kibinadamu,***
***alithibitishwa na Roho kuwa ni mwadilifu,***
***akaonekana na malaika.***
***Alihubiriwa kati ya mataifa,***
***aliaminiwa popote ulimwenguni,***
***akachukuliwa juu mbinguni kaitka utukufu.***

Katika mstari wa 15 Paulo anatoa maelezo kuhusu Timotheo anakotakiwa kutumikia. 1) Nyumba ya Mungu; 2) Kanisa la Mungu aliye hai; 3) Nguzo na msingi wa kweli. Neno la Kiyunani la nyumba ya Mungu linaweza kumaanisha yote, mahali pa kukaa (nyumba) na kila kitu kilichomo ndani yake ("mali ya nyumba"). Hii inaonyesha angalau mambo mawili: 1) Mahali pa makao ya kudumu ya Mungu ("nyumba" yake) ni kanisa, watu wake; na 2) watu wa Mungu siyo ushirika wa kawaida tu, lakini ni kama familia ("mali ya nyumba" ya Mungu)— na tusifanye makosa kabisa: Ni familia ya Mungu, siyo yetu sisi.

["Kusanyiko" la kanisa kwa Kuyunani] la Mungu aliye hai" linaonyesha kwamba, linapokusanyika pamoja, linadhihirisha uwepo wa Mungu aliye hai kwa namna maalum. Kumbuka kwamba Yesu alililiita "kanisa langu": Yeye ndiye mwanzilishi wa kanisa (**Mat 16:18**); ni kichwa cha kanisa (**Efe 1:18-23**); na alisema kwamba "walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, niko katikati yao" (**Mat 18:20**).

Hiyo "nguzo na msingi wa kweli" inaonyesha angalau mambo mawili: 1) Kuna "kweli." Yesu ndiye kweli

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

(**Yoh 14:6**); Neno la Mungu ni kweli (**Yoh 17:17; 2 Tim 2:15**). 2) Kanisa ni la muhimu sana katika kuishikilia kweli na kuifanya ijulikane.

**1)** Kwa kuhusiana na "nyumba ya Mungu":

**A)** Je watu walio nje ya kanisa letu wanatuona sisi kama familia?

**1)** Kama sivyo, ni kwa nini?

**2)** Kama ndivyo, je wanatuona sisi kama familia ambayo inmekaa vizuri, au kama familia isiyofanya kazi?

**B)** Je tunajiona wenyewe kama familia, na je tunatenda kama viungo vya familia inayopendana kwa kila moja wetu?

**C)** Tufanyeje kama kanisa kuhakikisha kuwa watu wote kanisani wanachukuliwa au kuonekana kama wapendwa katika familia?

**2)** Kwa kuhusiana na "kanisa la Mungu aliye hai":

**A)** Je neno "kanisa" linasikika vizuri au vibaya katika jamii? Kwa nini ni hivyo?

**B)** Kwa vile kanisa ni maalum sana kwa Kristo, je kuna mambo tunayoweza kuyafanya ili kulifanya kanisa liwe maalum zaidi kwetu?

**3)** Kwa kuhusiana na Kanisa kuwa "nguzo ya msingi wa kweli":

**A)** Je wale wasio Wakristo katika jamii zetu wanaamini kwamba "iko kweli?" Kama ndivyo, wanafikiri *kweli* ni nini?

**B)** Je tunawaandaa watu wetu "kuisimamisha kweli" ya Kristo na Neno lake wanaposhirikiana na wasio Wakristo? Kama sivyo, tunatakiwa tufanye nini ili kuwaandaa vizuri?

**C)** Kanisa linaweza na linatakiwa kufanya mambo mengi, pia kuhusika na majukumu mengi, katika maisha ya watu.

1) Je ni majukumu gani makuu na wajibu wa kanisa letu kuyafanya katika maisha ya watu?

2) Je tunawezaje kuhakikisha kwamba mojawapo ya majukumu ya msingi ya kanisa letu ni kuwa "nguzo na msingi wa kweli?"

**4)** Tunapoyaangalia maswala yote aliyoyaelezea Paulo kuhusu kanisa lilivyo:

**A)** Je tunafanya mambo ambayo hatukutakiwa kuyafanya, kulingana na maelezo ya Paulo ya kanisa?

**B)** Je tumeacha kufanya mambo ambayo tulitakiwa kuyafanya, kulingana na maelezo ya Paulo ya kanisa?

**5)** Kweli kuu kuhusiana na Yesu Kristo—kufanyika mwili, kusulubiwa, kufufuka, kupaa, na kutukuzwa – kumewekwa katika mstari wa 16. Kulingana na kweli hizo:

**A)** Je watu wetu wanaelewa vizuri kuhusiana na kweli zimhusuzo Yesu, na utofauti wake wa kuutwa mwili, kusulubiwa, kufufuka, kupaa, na kutukuzwa? Kama siyo, je tunatakiwa tufanye nini kuhakikisha kwamba watu wetu wanaelewa kweli hizi za msingi mkuu?

**B)** Je sisi "tunamtangazaje Kristo" kati ya wasioamini katika taifa letu wenyewe?

**C)** Je kuna mambo ambayo tunatakiwa tuwe tunayafanya kitofauti ili kwamba Kristo atangazwe katika kweli—kwa yote mawili; kimaneno na kwa matendo?

**6)** Zingatia kwamba katika mstari wa 2, 4, 5, 12, na 15 kuna mahusiano katika familia/nyumba ya Mungu, na kanisa:

**A)** Ni jinsi gani familia zetu za leo zinafanana na Kanisa la Kristo?

**B)** Je familia zetu za leo *zingetakiwa ziweje* kama Kanisa la Kristo?

**C)** Je tunatakiwa kufanya nini ili kuzisaidia familia zetu ili ziwe vielelezo vizuri zaidi vya Kanisa la Kristo?

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

## 1 Timotheo 4:1-7a

***[1]Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani; [2]kwa unafiki wa watu wasemao uongo,wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe; [3]wakiwazuia watu wasioe, na kuwaamuru wajiepushe na vyakula, ambavyo Mungu aliviumba vipokewe kwa shukrani na walio na imani wenye kuijua hiyo kweli. [4]Kwa maana kila kiumbe cha Mungu ni kizuri, wala hakuna cha kukataliwa, kama kikipokewa kwa shukrani; [5]kwa kuwa kimetakaswa kwa neno la Mungu na kwa kuomba. [6]Uwakumbushe ndugu mambo hayo, nawe utakuwa mtumishi mwema wa Kristo Yesu, na mzoevu wa maneno ya imani, na mafundisho mazuri yale uliyoyafuata. [7]Bali hadithi za kizee, zisizokuwa za dini, uzikatae;***

### 4:1-7a—Tatizo la uzushi wa kidini katika kanisa

Paulo ameonyesha hapo nyuma kwamba kulikuwa na tatizo katika kanisa la Efeso (ambapo Timotheo alikuwa ndiye mchungaji), lililohusu mafundisho ya udanganyifu ya watu fulani (**1Tim 1:3-4, 18-20**). Amejadili swala muhimu la kanisa: umuhimu wa maombi yatokayo katika maisha matakatifu, ili kwamba watu waje kwenye ufahamu wa neema iokoayo ya Yesu (**2: 1-15**); umuhimu wa watu wema na waliofunzwa vizuri kuliongoza kanisa (**3:1-13**); sura ya kanisa lenyewe (**3:15**); na: siri kuu ya Uungu wake" umhusuo Yesu Kristo, ambao kanisa linaamini na kuutangaza (**3:16**). Sasa Paulo anageukia hasa kwa mafundisho ya udanganyifu katika kanisa, na jinsi Timotheo anatakiwa kuyakabili.

Watu wakati mwingine hufikiri kwamba kukataza mambo au vitu ambavyo Mungu ameviumba na kuturuhusu (kwa mfano kuoa, vyakula fulani) kunawafanya wao wawe watakatifu zaidi ya wengine. Walter Liefeld katika *NIV Application Commentary, 1 and 2 Timothy/Titus* (Grand Rapids, MI: Zondervan, 1999), 151, anasema hivi kuhusu mistari hii: "Kinamna fulani hao wenye mawazo ya maasi walikuwa wakiwazia mazingira ya kiroho yaliyopinda au yaliyoinuka mno, ambapo kuoa wala kula vyakula fulani kulikuwa si kwa lazima, kulikuwa ni makosa. Paulo anaonyesha kwamba mawazo ya namna hiyo ni ya upotofu asemapo kuwa watu "waaminio na . . . kuijua hiyo kweli" wakipokee chakula ambacho Mungu alikiumba kwa moyo wa shukrani. Twaweza kuhisi kwa mwelekeo uliopo kwamba Paulo angesema kitu hicho hicho kuhusu kuoa, lakini kadiri kifungu hiki kinavyoendelea, kinashughulikia chakula peke yake . . . Kukataa chakula maana yake ni kuikataa kazi ya uumbaji ya Mungu. Kuvipokea na kuwa na shukurani ni kuikubali kazi hiyo na hali yetu ya kumtegemea Mungu Wale walimu wa uongo ni dhahiri walikuwa hawana shukurani, dhambi iliyokaa kwenye kiini cha uasi wa mwanadamu kinyume cha Mungu (Warm 1:21)."

**1)** Kuna mwingiliano kati ya *imani* potofu (mst. 1) na matendo mabaya (mst. 3); kile watu wanachoamini hudhihirishwa kwa jinsi wanavyoishi (na kile wanachokifanya pengine ndiyo kiashirio kikubwa sana kuhusu kile wanachokiamini hasa). Imani potofu na matendo yasiyofaa huunganishwa mara nyingi na unafiki na uongo (mst. 2). Hebu fikiria yafuatayo:

**A)** Je Paulo anasema nini kuhusu chanzo *halisi* cha imani isiyofaa na potofu? Je hili linaashiria nini kuhusu umuhimu wa kurekebisha imani za mafundisho potofu?

**B)** Je kuna imani aina fulani au matendo fulani kati ya watu katika kanisa letu au jamii yetu ambayo kiukweli yako tofauti na neno la Mungu?

**C)** Kwa nini watu wanayaamini na kuyafanya hayo?

**D)** Tunatakiwa tufanye nini kuwasaidia watu hao wasiendelee kuyaamini na wasiendelee kutenda hayo?

**2)** Wakati watu wanafanya au wanakatazwa kufanya mambo fulani ili kuwa "watakatifu" zaidi, hata kama mambo hayo hayahitajiki katika Biblia, mara nyingi huishia kuwa watumwa kwa vitu hivyo.

**A)** Je, "kukataza kuoa au kuolewa," "kukataza vyakula," au kufanya au kukatazwa mambo mengine (ambayo hayatajwi na Biblia), kunakuwaje kinyume na "neema, rehema, na amani" ambayo imo katika Kristo Yesu?

**B)** Ikiwa Neno la Mungu halikatazi kitu fulani, lakini watu wakasema kinatakiwa kuachwa, je hilo linasema nini kuhusu mtazamo wao juu ya: 1) Mamlaka ya Biblia; 2) Neema ya Mungu; 3) Imani na matendo?

**C)** Kujaribu kuvunja tabia ambazo si ya Kibiblia huweza kuwa kugumu sana. Je tunawezaje sisi kama kanisa kuwasaidia watu kuachana na tabia zao ambazo si za Kibiblia na kisha kupata neema, rehema, na amani zitokazo katika mahusiano sahihi na Yesu Kristo?

**3)** Katika mstari wa 6 Paulo anasema kwamba mafundisho ya udanganyifu na matendo yasiyofaa yanatakiwa "kukumbushwa" kwa watu kanisani.

**A)** Je tunafanya hivi kwa watu wetu?

**B)** Kama sivyo, ni mambo gani yanayotakiwa "kukumbushwa," na tunawezaje kulifanya hilo kwa vizuri

zaidi?

**1 Timotheo 4:7b-16**

***[7b]Nawe ujizoeze kupata utauwa; [8]kwa maana kujizoeza kupata nguvu za mwili kwafaa kidogo, lakini utauwa hufaa kwa mambo yote; yaani, unayo ahadi ya uzima wa sasa, na ya ule utakaokuwapo baadaye. [9]Ni neno la kuaminika, tena lastahili kukubalika kabisa; [10]kwa maana twajitaabisha na kujitahidi kwa kusudi hili, kwa sababu tunamtumaini Mungu aliye hai, aliye mwokozi wa watu wote, hasa wa waaminio. [11]Mambo hayo uyaagize na kuyafundisha. [12]Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo na katika upendo na imani na usafi. [13]Hata nitakapokuja, ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha. [14]Usiache kuitumia karama ile iliyomo ndani yako uliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya wazee. [15]Uyatafakari hayo; ukae katika hayo; ili kuendelea kwako kuwe dhahiri kwa watu wote. [16]Jitunze nafsi yako, na mafundisho yako. Dumu katika mambo hayo; maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia.***

**4:7b-10—Jinsi mtumishi wa Mungu anavyojiandaa**

**1)** Mistari 7b-10 inataja mambo kadhaa ambayo Timotheo (na, kwa kupanua zaidi, viongozi wa kanisa letu) wanapaswa kuyafanya ili kujiandaa katika kupambana na mafundisho ya uongo na matendo yasiyofaa katika kanisa):

**A)** Ni mambo gani hayo ambayo viongozi wa kanisa wanatakiwa kuyafanya?
**B)** Je tunayatekeleza vizuri kiasi gani?
**C)** Kama tunataka kufanya vizuri zaidi katika eneo lolote kati ya yale aliyoyataja Paulo, tunawezaje kujiboresha ili tutumikie makusanyiko vizuri zaidi?

**2)** "Kujizoeza" (mst. 7b-8) huhusisha "utaratibu" wa kufanya jambo (kama kujizoeza kufanya mazoezi ya kimwili kunaotakiwa kumkamilisha mwanariadha). Kwa vile kujipa nidhamu ya uchaji ni muhimu zaidi kuliko mazoezi ya kimwili, je tufanye nini katika *kuwajibika* kwa "nidhamu" ya "uchaji wa Ki-Mungu?"

**4: 11-16—Dalili za mtumishi mwenye mafanikio**

**1)** Yapo mambo ya kuzingatia (maagizo) 10 katika mistari hii sita.

**A)** Ni yapi hayo?
**B)** Je tunawezaje, kama viongozi wa kanisa, kuwajibika katika kuyatekeleza yote ambayo Paulo anasema mtumishi mzuri wa Neno la Mungu anapaswa kuyafanya?

**2)** Katika **3:2** moja ya sifa zinazotakiwa kuwa mzee au askofu ni kuwa na uwezo wa kufundisha. Uwezo wa kufundisha ni wa *lazima* kwa kanisa. Hili linathibitishwa kwa jinsi Paulo alivyolirudia mara kwa mara. Kwa hiyo, katika **4:11** kiongozi anatakiwa "kuyaagiza na kuyafundisha mambo haya" [m.y., Neno la Mungu]; katika **4:13** anatakiwa "kufanya bidii . . . kuonya na kufundisha"; katika **4:16** anatakiwa "kuwa mwangalifu . . . kwa mafundisho [yake]"; katika **5:17** wazee watawalao vema na wahesabiwe kustahili "heshima maradufu," hasa wao wajitaabishao kwa "kuhutubu na kufundisha"; katika **6:2** anatakiwa "kufundisha na kuonya/ kuhubiri" katika **6:17** anatakiwa "kuwaagiza walio matajiri [kuhusu jinsi ya kutumia mali zao vizuri]."

Kwa mtazamo huu, inatakiwa kukumbukwa kwamba "baraza lote la Mungu" (**Mdo 20:27**) ni lazima lifundishwe. Sababu yake, bila shaka, ni kwamba," Kila Andiko, lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema" (**2 Tim 3:16-17**).

**A)** Kwa nini mafundisho yafaayo ya Neno la Mungu ni muhimu sana kwa uhai wa kanisa?
**B)** Je kuna maeneo katika Maandiko ambayo ama *yanapuuzwa,* au *yanatiliwa mkazo mno*?
**C)** Je maisha ya washirika wa kanisa letu yanaonyesha kwamba yanahitaji mafundisho makubwa zaidi kuhusu somo fulani au kuhusu maeneo fulani?
**D)** Je nguvu ya desturi na jamii zetu inaonyesha kwamba kunahitajika mafundisho zaidi kuhusu somo fulani au kuhusu maeneo fulani?

**3)** Katika mistari hii Paulo anaonyesha wazi kabisa kwamba *maisha binafsi* ya kiongozi wa kanisa hayawezi kutenganishwa na mafundisho yake; ni lazima yaendane mkono kwa mkono.

**A)** Ni tabia gani za maisha binafsi za kiongozi wa kanisa ambazo Paulo anazisisitiza?
**B)** Kwa nini ni lazima tabia ya kiongozi wa kanisa iendane na mafundisho yake?
**C)** Ni hatua gani, kama zitakuwapo, zichukuliwe (au tunatakiwa kuzianzisha) ili kuwafanya viongozi wetu wawajibike nazo:

**1)** Kwa maisha yao binafsi?

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

**2)** Kwa mafindisho yao?

**4)** Katika mstari wa 12 Paulo anasema, "Mtu awaye yote asiudharau ujana wako." Mstari unaonyesha kwamba, ili mradi mtu "si mwamini mchanga" (**3:6**), basi viongozi wa kanisa wanaweza kupatikana hata kati ya "vijana," kama wanatosheleza sifa nyinginezo alizozitaja Paulo.

**A)** Je kuna maswala ya kidesturi mengi ambayo tunatakiwa kuyashughulikia ili kuhakikisha kwamba viongozi wa kanisa letu hawadharauliwi kwa sababu ni vijana?

**B)** Kwa upande mwingine, je *tunawatenga* washiriki "vijana" wasiwe viongozi ati kwa sababu ya ujana wao? Kama ndivyo, tunatakiwa kufanya nini kuhusu hili?

**5)** Mstari wa 13 unasema kwamba msisitizo unatakiwa kukazia "kusoma Maandiko mbele ya wote."

**A)** Kwa nini hili ni muhimu?

**B)** Je hili linafanyika vya kutosha kanisani kwetu sasa?

**C)** Je kuna matatizo yoyote ya watu kutokujua kusoma na kuandika katika jamii yetu, kiasi kwamba kusoma maandiko mbele ya wote ndiyo njia pekee ya watu kujifunza Maandiko?

**D)** Ikiwa kutojua kusoma na kuandika ni tatizo, je kuna kitu chochote kwetu kama kanisa tunachoweza (au tunatakiwa) kukifanya kuhusu hili, ili kwamba watu waweze kusoma Maandiko peke yao?

**6)** Mstari wa 15 unasema kwamba viongozi wanapaswa, "kuyatafakari hayo; wakae katika hayo; ili kuendelea kwao kuwe dhahiri kwa watu wote."

**A)** Je watu wanapotutazama sisi, wangeelekea kusema kwamba tuna"tafakari hayo", na "tunakaa katika hayo"; ilil kuendelea kwetu [kuwe] dhahiri kwa watu wote?"

**B)** Kama sivyo, tunatakiwa tufanye nini kuhusu hili?

## <u>1 Timotheo 5:1-2</u>

***1 Mzee usimkemee, bali umwonye kama baba; na vijana kama ndugu, 2 wanawake wazee kama mama, wanawake vijana kama ndugu wa kike, katika usafi wote.***

### <u>5:1-2—Kushughulikia waumini wa kanisa kama vile baba, ndugu, mama, na wanawake vijana</u>

Paulo sasa anaonyesha jinsi ipasavyo kuhudumia watu mbali-mbali katika kanisa.

**1)** Kifungu cha 1-2 chasemaje kuhusu tabia ya kanisa (au *linavyopaswa* kuonekana) ?

**A)** Je hili linahusikaje kuimarisha kile Paulo alichosema katika kifungu cha **3:15**?

**2)** Viongozi wa kanisa wanapaswa kuwarekebisha wazee kama wafanyavyo kwa baba zao:

**A)** Je kuwarekebisha wazee *kama baba* kunahusisha nini katika kuwaonya wazee?

**B)** Je kuna desturi zozote za kitamaduni ambazo tunapaswa kuzizingatia tunapowaonya wazee?

**C)** Je kuna mambo tunapaswa kuyabadili katika kuonya wazee kanisani?

**3)** Viongozi wa kanisa wanapaswa kuwaonya vijana kama wawaonyavyo akina kaka.

**A)** Je kuwaonya vijana *kama vile ndugu* kunahusisha nini katika kuwaonya hao vijana?

**B)** Je kuna desturi zozote za kitamaduni ambazo tunapaswa kuzizingatia tunapowaonya vijana?

**C)** Je kuna mambo tunapaswa kuyabadili katika kuonya vijana kanisani?

**4)** Viongozi wa kanisa wanapaswa kuwaonya wakina mama wazee kama vile mama .

**A)** Je, kumwonya mwanamke mzee kama *mama* kunahusisha nini katika kuwaonya wanawake wazee?

**B)** Je kuna desturi zozote za kitamaduni ambazo tunapaswa kuzizingatia tunapomwonya mwanamke mzee?

**C)** Je kuna mambo tunapaswa kuyabadili katika kuonya mwanamke mzee kanisani?

**5)** Viongozi wa kanisa wanapaswa kuwaonya wanawake vijane kama vile dada.

**A)** Kuwaonya wanawake vijana *kama vile dada* kunahusisha nini katika kuwaonya hao wasichana?

**B)** Je kuna desturi zozote za kitamaduni ambazo tunapaswa kuzizingatia tunapowaonya wanawake vijana?

**C)** Je kuna mambo tunapaswa kuyabadili katika kuonya wanawake vijana kanisani?

**6)** Labda chanzo kikuu cha majaribu kwa viongozi wa kanisa ni kuwaonya wanawake vijana. Hivyo Paulo anaongezea maneno "katika usafi wote" mwisho wa mstari wa 2.

**A)** Ni sera zipi zilizopo (au tunapaswa kuwa nazo) ili kuhakikisha kwamba jaribu hili linapunguzwa, na

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

usafi wa kiongozi wa kanisa na usafi wa huyo dada kuadumishwa?

**1Timotheo 5:3-16**

***3Uwaheshimu wajane walio wajane kweli kweli. 4Lakini mjane akiwa ana watoto au wajukuu, na wajifunze kwanza kuyatenda yaliyo wajibu wao kwa jamaa zao wenyewe, na kuwalipa wazazi wao. Kwa kuwa hili lakubalika mbele za Mungu. 5Basi yeye aliye mjane kweli kweli, ameachwa peke yake, huyo amemwekea Mungu tumaini lake, naye hudumu katika maombi na sala mchana na usiku. 6Bali, yeye asiyejizuia nafsiyake amekufa ingawa yu hai. 7Mambo hayo pia uyaagize, ili wasiwe na lawama. 8Lakini mtu ye yote asiyewatunza walio wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini. 9Mjane asiandikwe isipokuwa umri wake amepata miaka sitini; naye amekuwa mke wa mume mmoja; 10naye ameshuhudiwa kwa matendo mema; ikiwa amelea watoto, ikiwa amekaribisha wageni, ikiwa amewaosha watakatifu miguu, ikiwa amewasaidia wateswao, ikiwa amefuata kwa bidii kila tendo jema. 11Bali wajane walio vijana ukatae kuwaandika hao, maana, wakizidiwa na tamaa kinyume cha Kristo, wataka kuolewa; 12nao wana hukumu kwa kuwa wameiacha imani yao ya kwanza. 13Tena, pamoja na hayo, hujifunza kuwa wavivu, wakizunguka-zunguka nyumba kwa nyumba; wala si wavivu tu, lakini ni wachongezi na wadadisi, wakinena maneno yasiyowapasa. 14Basi napenda wajane, ambao si wazee, waolewe, wazae watoto, wawe na madaraka ya nyumbani; ili wasimpe adui nafasi ya kulaumu. 15Kwa maana wengine wamekwisha kugeuka na kumfuata Shetani. 16Mwanamke aaminiye, akiwa ana wajane, na awasaidie mwenyewe, Kanisa lisilemewe; ili liwasaidie wale walio wajane kweli kweli.***

**5:3–16—Kuhudumia wajane**

William D. Mounce, *Pastoral Epistles* [Word Biblical Commentary, vol 46] (Nashville, TN: Thomas Nelson, 2000), 299, anazungumzia hoja ya msingi ya kifungu hiki cha maneno ya waraka wa Paulo kwa Timotheo: "Lengo la msingi la Paulo katika kifungu hiki ni kumsaidia Timotheo kuwatofautisha wajane ambao kanisa linatakiwa liwasaidie, na wale ambao kanisa halitakiwi Paulo anafundisha kwamba mjane wa kweli, mjane anayetakiwa kusaidiwa, anatakiwa awe yuko peke yake kabisa, asiyepokea msaada wowote wa kifamilia, na asiyetaka kuolewa tena. Ni lazima awe mwanamke mchaji wa Mungu aliyeweka matumaini yake kwa Mungu, na tabia yake iwe ya kiuchaji kweli kweli, kama vile kuwa mtu wa maombi, aliyekuwa mwaminifu kwa mume wake, akiwalea watoto wake, akionyesha wema na ukaribishaji, akiwaosha miguu watakatifu, akiwasaidia wasiojiweza, na kuwa na matendo ya kiuchaji kweli kweli. Pia, kwa vile tatizo kule Efeso lilihusisha wajane walio vijana, Paulo anasema mjane anapaswa awe na umri angalau miaka sitini ikiwa anataka aorodheshwe. Hii haina maana kwamba kanisa liwapuuze wajane wasiokuwa na sifa hizi. Ilikuwa na maana kwamba Kanisa lisiingie katika mikataba rasmi ya kimaisha na wajane ambao hawakuwa wa aina hiyo."

**1)** Ni jinsi gani zile sifa za Paulo za kupatiwa misaada zinatumika kama vivutio vya kuleta tabia nzuri za mkristo?

**A)** Ni jinsi gani kutoa vivutio vya kujenga mwenendo mzuri wa ukristo kuendane na masaidiano ya Kikristo, na wajibu wetu kuwasaidia kwa huruma na kwa kujitolea, wale walio katika uhitaji?

**2)** Ni utaratibu gani tulio nao sisi kama kanisa kushughulika na walio na uhitaji, kama vile majane?

**A)** Je tunaweza *kukataa* (au kutoa) msaada wa kifedha kwa wajane (au kwa watu wengine wenye uhitaji) *kwa misingi ya kanuni* fulani, kama vile Paulo anavyoelekeza?

**B)** Ikiwa hatuna utaratibu wa namna hiyo, je tunatakiwa kuuanzisha wa namna hiyo, na kama ni hivyo, unatakiwa uweje?

**3)** Je ni desturi gani na ni taasisi gani katika utamaduni wetu hutoa misaada kwa wajane na watu wengine?

**A)** Je desturi au taasisi hizo zinapaswa (au zinatakiwa) kuathiri vipi wajibu wetu kama Kanisa?

**4)** Je kuna msaada gani wa Serikali kwa wajane wenye uhitaji na kwa wengineo?

**A)** Je ni vipi misaada ya Serikali inaathiri (au inatakiwa) hali ya utoaji wetu wa misaada kama kanisa?

**5)** Kadiri watu wetu wanavyoongezeka umri, je tunahitajika kuandaa mipango yoyote ili kwamba tuwe tayari kutoa misaada kwa "wale wenye uhitaji wa kweli" wakati utakapofika?

**6)** Paulo aliwatofautisha wajane wazee walio wachaji wa kimungu kweli kweli waliokuwa wakiishi peke yao, na wajane waliokuwa na familia wenye mbinu nyingine za kuwasaidia.

**A)** Je iweje (au tunatakiwa kufanya nini) kunapokuwepo swala la maombi yanayoletwa ya wajane wenye familia, wakati jamaa zao wanakataa (au hawana uwezo) wa kuwasaidia?

**7)** Kuhusiana na swala la kawaida zaidi la watu kuhitaji misaada ya kifedha kutoka Kanisani:

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

**A)** Je kuna mazingira fulani ya kipekee katika kanisa letu au jamii yetu, ambayo ni tofauti, lakini yanawiana na, hali ile iliyokuwako katika kanisa la Efeso ambalo Paulo anaizungumzia?
**B)** Je ni *kanuni* gani za msingi za ushauri wa Paulo kwa Timotheo ambazo tunaweza kuzitumia katika mazingira yetu tofauti?

## 1 Timotheo 5:17-25

***17Wazee watawalao vema na wahesabiwe kustahili heshima maradufu; hasa wao wajitaabishao kwa kuhutubu***
***na kufundisha. 18Kwa maana andiko lasema, "USIMFUNGE KINYWA NG'OMBE APURAPO NAFAKA."***
***Na tena, "Mtenda kazi astahili ujira wake." 19Usikubali mashitaka juu ya mzee, ila kwa vinywa vya mashahidi***
***wawili au watatu. 20Wale wadumuo kutenda dhambi uwakemee mbele ya wote, ili na wengine waogope.***
***21Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, na mbele za malaika wateule, uyatende hayo pasipo***
***kuhukumu kwa haraka; usifanye neno lolote kwa upendeleo. 22Usimwekee mtu mikono kwa haraka, wala***
***usizishiriki dhambi za watu wengine. Ujilinde nafsi yako uwe safi. 23Tokea sasa usinywe maji tu lakini tumia***
***mvinyo kidogo, kwa ajili ya tumbo lako, na magonjwa yakupatayo mara kwa mara. 24Dhambi za watu wengine***
***zi dhahiri, zatangulia kwenda hukumuni; wengine dhambi zao zawafuata. 25Vivyo hivyo matendo yaliyo mazuri***
***ya dhahiri; wala yale yasiyo dhahiri hayawezi kusitirika.***

William D. Mounce, *Pastoral Epistles* [Word Biblical Commentary, vol. 46] (Nashville, TN: Thomas Nelson, 2000), 322, anaeleza kwamba, "Swala la nidhamu ya kanisa limekuwa siku zote ni jambo gumu, siyo tu kulielewa, bali hasa kulitekeleza. Historia ya kanisa, la kale na la siku hizi, limekuwa likikumbwa na hali ya kukataa kufuata Maandiko." Anaendelea kujadili kanuni iliyowekwa katika 1 Timotheo 5:17-25: "Katika 1 Timotheo 5:17-25 kuna maswala mengi yahusuyo nidhamu ya kanisa, kanuni zinazoenda sambamba na nyinginezo zilizopo sehemu nyinginezo, kama vile Math 18. (1) Dhambi ni lazima ikabiliwe. (2) Mashitaka ni lazima yathibitishwe na mashahidi wengi. (3) Si dhambi iliyotokea mara moja, bali ni dhambi ya kudumu inayotakiwa kufanyiwa kazi. (4) Kukemewa hadharani kunatakiwa kuwe kumetanguliwa na kuonywa binafsi uso kwa uso. Lakini maonyo ya mtu binafsi yasiposaidia, basi kukemewa hadharani ni lazima kufanyike. (5) Kukemewa hadharani, lengo lake hasa siyo kutoa adhabu, bali hasa ni kuingiza hofu itakayoponya. (6) Mtu anayetoa hukumu, hata kama ni wa hadhi ya Timotheo, lazima ajitahidi kuwa katika haki na usafi katika hatua zote za jambo hilo iwezekanavyo. (7) Kuwasimika wazee ni tendo zito sana, na kuna kuwajibika kwa yeye anayesimika kwa wale anaowasimika. (8) Hakuna mbadala wa tahadhari na wakati. Tabia ya kweli ya mtu na matendo yake si mara zote hugundulika haraka." (Ibid.)

**1)** Je sisi kama kanisa tuna utaratibu tuliouandaa wa kushughulika na:
**A)** Kuwasaidia kifedha viongozi wa kanisa letu, "hasa wao wajitaabishao kwa kuhutubu na kufundisha [mst. 17-18]?"
**B)** Mashitaka juu ya wazee [mst. 19]?
**C)** Wazee watendao dhambi na wanaendelea katika dhambi hiyo [mst. 20]?
**1)** Kama ndivyo, je kanisa letu linatofautisha kati ya dhambi binafsi, na dhambi ya hadharani; na kukemewa binafsi na kukemewa hadharani?

**2)** Kama hatuna utaratibu wowote wa aina hiyo, je tuuanzishe; na kama ndivyo, uweje?

**3)** Kama hatuwezi kuwasaidia kifedha viongozi wetu wowote wa kikanisa, je tuna utaratibu wowote wa kuwaonyesha wale "watawalao vyema" heshima na kuwatambua kinamna fulani?
**A)** Kama sivyo, je tunatakiwa kuanzisha utaratibu kama huo na, kama ndivyo, unatakiwa uweje?

## 1 Timotheo 6:1-2a

***1Wowote walio chini ya kongwa, hali ya utumwa, na wawahesabie bwana zao kuwa wamestahili heshima yote,***
***jina la Mungu lisitukanwe wala mafundisho yetu. 2Na wale walio na bwana waaminio wasiwadharau kwa***
***kuwa ni ndugu; bali afadhali wawatumikie, kwa sababu hao waishirikio faida ya kazi yao wamekuwa wenye***
***imani na kupendwa.***

### 6:1-2a—Mausia kwa watumwa

Kila mfumo wa kisiasa, kiuchumi, kielimu, na wa jamii tofauti hufanya watu wawe tofauti kati kati yao.Wengine ni viongozi; wengine ni wafuasi. Wengine ni matajiri; wengine ni masikini.Wengine ni waajiri; wengine ni waajiriwa. Wengine wana elimu sana; wengine hawana elimu nzuri. Wakati mwingine wale walio wa ngazi ya chini, wa kutumwa, na wale walio katika hali mbaya zaidi; wanaweza kuishinda hali yao na kubadili mambo; wakati mwingine hawawezi. Utumwa ulifanyiza msingi wa uchumi wa Kirumi. Utumwa umeondolewa

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

katika sehemu kubwa ya dunia leo. Hata hivyo watu wengi wanaofanya kazi kwa ajili ya kipato, hufanya kazi kwa watu wengine. Kwa hiyo, Paulo anaagiza kwa watumwa—na maagizo yao kwa matajiri baadaye katika sura hii–yana mengi ya kutufundisha.

**1)** Je watu wengi wanawachukulia wale wanaofanya kazi kwao kama "wanastahili kupewa heshima" [mst. 1]?"

> **A)** Ni kwa nini iwe hivyo au isiwe hivyo?
>
> **B)** Je mtu anawezaje kuonyesha "heshima" kwa mwajiri wake?
>
> > **1)** Hata kama Mwajiri huyo si Mkristo?
> >
> > **2)** Hata kama mwajiri huyo anaudharau Ukristo?
> >
> > **3)** Hata kama mwajiri huyo si mwajiri "mwema?

**2)** Je msukumo au sababu ya Paulo kuwaambia watumwa kuwaona mabwana zao "kama wastahilio heshima" ni nini?

> **A)** Kwa nini msukumo au sababu hii bado inafanya kazi hata leo, hata kama utumwa haupo tena?

**3)** Mstari wa 2 unahusiana na hali ambapo wote wawili, yaani bwana na mtumwa ni Wakristo. Hutokea kwamba, kufanana kwetu katika Kristo kunaweza kukatofautiana kimajukumu katika jamii zetu. Ni kweli, inawezekana mtumwa au mwajiriwa akashika nafasi ya madaraka makubwa zaidi katika kanisa kuliko mkuu wake au mwajiri wake.

> **A)** Je kuna mazingira ambapo waajiriwa wanakuwa na mamlaka makubwa zaidi katika kanisa kuliko waajiri wao?
>
> > **1)** Ikiwa ndiyo, je hilo limeleta msuguano kati yao, ama ndani ya kanisa, au nje ya kanisa?
> >
> > **2)** Kama kumekuwako na msuguano wa namna hiyo, je tufanyeje sisi kama kanisa kuwasaidia watu washughulikie matatizo kama hayo?
>
> **B)** Je kuna mazingira ambapo; ama mwajiri au mwajiriwa anachukulia mwanya wa kujinufaisha kwa mwingine eti kwa sababu wote wawili ni Wakristo?
>
> > **1)** Kama ndiyo, je tufanyeje kama kanisa kuwasaidia ili washinde hali hii ya kujinufaisha?
>
> **A)** Katika mistari hii, ni mambo gani ambayo Paulo anayaona kuwa yanaingiliana kimsingi?
>
> > **1)** Tunawezaje kutumia yale ambayo Paulo anayaona kwamba ni mambo yanayoingiliana kimsingi kuwasaidia watu kuondoa mivutano inayoinuka kutokana na kazi zao?

**<u>1 Timotheo 6:2b-19</u>**

***2b Mambo hayo uyafundishe na kuyaonya. 3 Mtu yeyote akifundisha elimu ya aina nyingine, wala hayakubali maneno yenye uzima ya Bwana wetu Yesu Kristo, wala mafundisho yapatanayo na uzima na utauwa, 4 mejivuna; wala hafahamu neno lolote; bali ana wazimu wa kuwazia habari za maswali, na mashindano ya maneno, ambayo katika hayo hutoka husuda, na ugomvi, na matukano, na shuku mbaya; 5 na majadiliano ya watu walioharibika akili zao, na walioikosa kweli, huku wakidhani ya kuwa utauwa ni njia ya kupata faida.***

***6 Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa. 7 Kwa maana hatukuja na kitu duniani, tena hatuwezi kutoka na kitu; 8 ila tukiwa na chakula na nguo tutaridhika na vitu hivyo. 9 Lakini hao watakao kuwa na mali huanguka katika majaribu na tanzi, na tamaa nyingi zisizo na maana, zenye kudhuru, ziwatosazo wanadamu katika upotevu na uharibifu. 10 Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha; ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na Imani, na kujichoma kwa maumivu mengi. 11 Bali wewe, mtu wa Mungu, uyakimbie mambo hayo; ukafuate haki, utauwa, imani, upendo, saburi, upole. 12 Piga vile vita vizuri vya imani; shika uzima ule wa milele ulioitiwa, ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi. 13 Nakuagiza mbele za Mungu anayevihifadhi hai vitu vyote, na mbele za Kristo Yesu, aliyeyaungama maungamo mazuri yale mbele ya Pontio Pilato, 14 kwamba uilinde amri hii pasipo mawaa, pasipo lawama, hata kufunuliwa kwake Bwana wetu Yesu Kristo; 15 ambako yeye kwa majira yake atakudhihirisha, Yeye aliyehimidiwa, Mwenye uweza peke yake, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana; 16 ambaye yeye peke yake hapatikani na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una yeye hata milele na milele. Amina.***

***17 Walio matajiri wa ulimwengu wa sasa uwaagize wasijivune, wala wasiutumainie utajiri usio yakini, bali wamtumaini Mungu atupaye vitu vyote kwa wingi ili tuvitumie kwa furaha. 18 Watende mema, wawe matajiri kwa kutenda mema, wawe tayari kutoa mali zao, washirikiane na wengine kwa moyo; 19 huku wakijiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, ili wapate uzima ulio kweli kweli.***

**<u>6:2b–5—Madhara ya mafundisho ya udanganyifu.</u>**

**1)** Katika mstari wa 2b-5 anarudi kwenye swala la wale wanaoyaeneza mafundisho ya uongo katika Kanisa, na matokeo yake:

> **A)** Je kuna "husuda, ugomvi, matukano, na shuku mbaya" katika kanisa letu au kati ya Wakristo katika

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

jumuiya yetu?
**B)** Kama ndivyo, nini sababu za matatizo hayo?
**C)** Je tunaweza kufanya nini kama kanisa kuhusiana na matatizo hayo?
**D)** Je tunawezaje kutofautisha mijadala ya kitheolojia ya kihalali na kile anachokisema Paulo katika mistari hii?

**6:6-19—Kupenda utajiri, maagizo kwa kiongozi wa kanisa, na maagizo kwa matajiri**

William D. Mounce, *Pastoral Epistles* [Word Biblical Commentary, vol.46] (Nashville, TN: Thomas Nelson, 2000), 341, anaeleza kwamba: "Uchaji wa Mungu una thamani kubwa ikiwa unaambatana na kujitoa kwa dhati. Hii ni pamoja na kutambua kwamba watu watakufa kama vile walivyozaliwa: bila kitu chochote. Je si masumbufu basi kwao kutafuta utajiri? Uchaji wa Mungu ambao una thamani kubwa . . .. maana yake ni kutosheka na chakula na nguo. Lakini utajiri ambao wahusika waliutafuta haukuwa wa kujitosheleza. Badala yake, walitaka kuwa`matajiri, na kwa sababu ya tamaa zao, waliangukia katika mitego . . . ambayo iliwaangamiza, na wakaikataa Injili. Hii ni moja ya hukumu kali sana iliyoko katika Maandiko juu ya nguvu ya uharibifu ihusuyo mali Paulo amejifunza kutosheka siyo kwa sababu ana nguvu ya ndani, maalum, tofauti ya wanadamu wengine; au mazingira yamekuwa mazuri kwake. Kutosheka kwa Paulo kunatokana na kuotesha mizizi katika imani inayomfanya yeye asitegemee uwezo wake kufanya majukumu au kazi zake na kukidhi mahitaji yake, bali kwa kumtegemea Yeye aliye na uwezo peke yake, aliye Mungu. Kutosheka kwenye faida kubwa ni kule kunakotafuta usalama si katika utajiri wa dunia, bali katika Mungu."

**1)** Je swala la kutaka utajiri linaonekana ni muhimu kiasi gani katika kanisa letu au katika jumuiya yetu?
**A)** Je swala hili la kutaka kupata fedha linajionyeshaje?
**B)** Kulingana na Paulo, tatizo kuu ni la utu wa ndani, yaani *tamaa* ya kupata utajiri na *kupenda* fedha. Kwa nini tamaa hizi mbili za utu wa ndani ni muhimu sana?
**C)** Je tunawafahamu watu ambao wameanguka kwa sababu ya tamaa hizi? (au ambao, hata sasa, wako katika hatari ya kuanguka)?
**D)** Je tunawezaje sisi kama kanisa kuzungumzia maswala haya ya kutamani utajiri na kupenda fedha, ili kuwasaidia watu wetu?
**1)** Je tunazishughulikiaje tamaa hizi ndani yetu wenyewe?

**2)** Paulo anamuusia Timotheo "kuyakimbia mambo hayo" (m.y., mafundisho yote yaliyo potofu, tabia mbaya, na tamaa mbaya ambazo Paulo amezizungumzia katika mistari ya 3-10).
**A)** Ni jambo moja kukimbia kimwili kutoka jaribu la dhambi, kama Yusufu alivyokimbia kutoka kwa mke wa Potifa katika **Mwa 39:7-12**. Je tunawezaje "kukimbia" kutoka katika mambo ambayo Paulo anayataja—hasa kutokana na tamaa mbaya ya kutaka kuwa tajiri (ambayo ni mambo yaliyo ndani kwenye akili)?
**B)** Je tunawezaje kuwafundisha na kuwasaidia watu wetu "kuyakimbia mambo hayo?"

**3)** Katika mstari wa 11–14 Paulo anampatia Timotheo hoja muhimu tano—za mambo anayoagizwa kuyafanya.
**A)** Ni mambo gani hayo?
**B)** Je tunayatendea kazi vizuri kiasi gani?
**C)** Kama tunataka kufanya vizuri katika eneo lolote katika hayo ayasemayo Paulo, tunawezaje kubadilika ili tuyatumikie vizuri zaidi makusanyiko yetu?
**D)** Je tunawezaje, kama viongozi wa kanisa, kuwajibika kuyafanya yote yanayotajwa na Paulo kuwa mtumishi mzuri wa Neno la Mungu anatakiwa kufanya?
**4)** Fananisha sifa za Uungu katika mistari 15-16 na zile za **1:17** na **3:16**.
**A)** Je watu wengi wanaelekea kumwangaliaje au kumfikiriaje Yesu?
**B)** Je sisi na watu wetu kweli tunamwona Yesu kama anavyoelezwa katika mistari hii?
**C)** Kama kweli sisi na watu wetu tungemwona Kristo kama Paulo anavyomweleza, je hili lingeathirije (au lingetakiwa) kuathiri vipi maisha yetu?

**5)** Mstari wa 17-19 unashughulika na watu wenye utajiri.
**A)** Wakati mwingine viongozi wa kanisa wanaidharau dhambi ya matajiri, au huegemea kwa matajiri, au kuwaweka matajiri katika nafasi za mamlaka tu kwa sababu ya utajiri wao. Au hawakemei mienendo mibaya ya matajiri, kwa sababu viongozi wa kanisa wanataka matajiri hao wawe wanatoa fedha zao kwa kanisa.

**1)** Je tuna hatia katika kufanya mojawapo kati ya hayo?
**2)** Je ni nini msimamo wa Paulo kuhusu viongozi wa kanisa wanavyotakiwa kushughulika na matajiri?
**3)** Je tufanye nini, kama kipo, ili kuwasaidia vizuri wale walio na utajiri?

**B)** Kwa upande mwingine, wakati mwingine watu huwaonea wivu matajiri kwa ajili ya mali zao.
**1)** Je tumegundua wivu wowote kwa matajiri ndani yetu wenyewe au kwa watu walio katika kanisa letu?
**2)** Tunatakiwa kushughulikiaje dhambi ya wivu?

## 1 Timotheo 6:20-21

***20Ee Timotheo, ilinde hiyo amana; ujiepushe na maneno yasiyo ya dini, yasiyo na maana, na mashindano ya elimu iitwayo elimu kwa uongo; 21ambayo wengine wakiikiri hiyo wameikosa Imani. Neema na iwe pamoja nanyi.***

### 6:20-21—Kuhitimisha mausia kwa Timotheo

**1)** Je tunawezaje, kama viongozi wa kanisa, kivizuri kabisa "kulinda kile kilichowekwa amana kwetu?"
**A)** Je kuna watu wanaofahamu kwamba wapo "wale walioikosa imani?"
1) Kwa nini hilo liliwakuta hao?
2) Je tunaweza kujifunza nini kutoka kwao kama mfano?
**B)** Ni hatua gani tunatakiwa kuzichukua kuhakikisha kuwa hatu "potoki na kuikosa imani?"

**2)** Ni katika jinsi gani mafundisho ya Paulo yalifanana na mafundisho ya Yesu?
**A)** Ni katika njia gani viongozi wa kanisa wanatakiwa kufundisha ili kufanana na mafundisho ya Paulo katika kitabu hiki?

## BIBLIOGRAFIA

Adeleye, Femi. 1999. *Preachers of a Different Gospel.* Kampala, Uganda: International Fellowship of Evangelical Students.

Andria, Solomon. 2006. "1 Timothy." In *Africa Bible Commentary,* ed. Tokunboh Adeyemo, 1469-76. Nairobi, Kenya: WordAlive.

Beck, James, and Craig Blomberg, ed. 2001. *Two Views on Women in Ministry.* Grand Rapids, MI: Zondervan.

Belleville, Linda. 1986. "'Under Law': Structural Analysis and the Pauline Concept of Law in Galatians 3:21-4:11." *Journal for the Study of the New Testament* 26: 53-78.

Blomberg, Craig. 1999. *Neither Poverty Nor Riches: A Biblical Theology of Possessions* (NSBT 7). Nottingham, England: Apollos.

Carson, D. A. 1984. "Matthew." In *Expositor's Bible Commentary,* vol. 8, ed. Frank Gaebelein, 1-599. Grand Rapids, MI: Zondervan.

_______________. 2002. *Love in Hard Places.* Wheaton, IL: Crossway.

Danker, Frederick, ed. 2000. *A Greek-English Lexicon of the New Testament and Other Early Christian Literature.* Chicago: The University of Chicago Press.

DeLacey, D. R. 1982. "The Sabbath/Sunday Question and the Law in the Pauline Corpus." In *From Sabbath to Lord's Day: A Biblical, Historical and Theological Investigation,* ed. D. A. Carson, 159-95. Grand Rapids, MI: Zondervan.

Doriani, Daniel. 1996. *Getting the Message.* Philllipsburg, NJ: P&R.

Earle, Ralph. 1978. "1 Timothy." In *Expositor's Bible Commentary,* vol.11, ed. Frank Gaebelein, 341-90. Grand Rapids, MI: Zondervan.

Editorial. 2001. "The Prosperity Gospel: An *AJET* Editorial. *Africa Journal of Evangelical Theology* 20: 1-2.

Fee, Gordon. 1984. "The 'Gospel' of Prosperity—an Alien Gospel." *Reformation Today* 82: 39-43.

Grudem, Wayne. 1988. *The First Epistle of Peter* (TNTC). Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

Gundry, Robert. 1970. "The Form, Meaning and Background of the Hymn Quoted in I Timothy 3:16." In *Apostolic History and the Gospel,* ed. W. Ward Gasque and Ralph Martin, 203-22. Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Guthrie, Donald. 1990 (reprinted 2000). *The Pastoral Epistles,* rev. ed. (TNTC). Leicester, England: Inter-Varsity.

Ham, Clay. 2000. "The Christ Hymn in 1 Timothy 3:16." *Stone-Campbell Journal* 3: 209-28.

Hays, J. Daniel. 2001. "Applying the Old Testament Law Today." *Bibliotheca Sacra* 158: 21-25. Online: http://www.biblicalstudies.org.uk/article_law_hays.html#top.

Hodges, Melvin. 1953. *The Indigenous Church.* Springfield, MO: Gospel.

Kelly, J. N. D. 1960. *A Commentary on the Pastoral Epistles: Timothy I & II, and Titus.* Peabody, MA: Hendrickson.

Knight, George W. 1992. *The Pastoral Epistles: A Commentary on the Greek Text* (NIGTC). Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Koukl, Gregory. 2001. *Never Read a Bible Verse.* Online: http://www.str.org/site/News2?page=NewsArticle&id=5466.

Liefeld, Walter. 1999. *1 and 2 Timothy/Titus* (NIVAC). Grand Rapids, MI: Zondervan.

Lysaught, M. Therese. 2005. "Practicing the Order of Widows: A New Call for an Old Vocation." *Christian Bioethics* 11: 51-68.

Marshall, I. Howard. 1989. "Universal Grace and Atonement in the Pastoral Epistles." In *The Grace of God, The Will of Man,* ed. Clark H. Pinnock, 51-68. Grand Rapids, MI: Academie Books.

Metzger, Bruce, and Michael Coogan, eds. 1993. *The Oxford Companion to the Bible.* New York: Oxford University Press.

Moo, Douglas. 1984. "Jesus and the Authority of the Mosaic Law." *Journal for the Study of the New Testament* 20: 3-49. Online: http://www.djmoo.com/articles/jesusandauthority.pdf.

Mounce, William D. 1993. *The Analytical Lexicon to the Greek New Testament.* Grand Rapids, MI: Zondervan.

_______________. 2000. *Pastoral Epistles* (WBC, vol. 46). Nashville, TN: Thomas Nelson.

Ngewa, Samuel. 2009. *1 & 2 Timothy and Titus* (ABCS). Nairobi, Kenya: HippoBooks.

Ouedraogo, Adama. 2006. "Prophets and Apostles." In *Africa Bible Commentary,* ed. Tokunboh Adeyemo, 1434. Nairobi, Kenya: WordAlive.

Piper, John. 2000. "Are There Two Wills In God?" In *Still Sovereign*, ed. Thomas R. Schreiner and Bruce A. Ware, 107-31. Grand Rapids, MI: Baker Books. Online: http://www.desiringgod.org/resource-library/articles/are-there-two-wills-in-god.

_______________. 2003. *Let the Nations be Glad!* 2nd ed. Grand Rapids, MI: Baker Academic.

_______________. 2007. "Prosperity Preaching: Deceitful and Deadly." Online: http://www.desiringgod.org/ResourceLibrary/TasteAndSee/ByDate/2007/1993_Prosperity_Preaching_Deceitful_and_Deadly/

Webb, William. 2001. *Slaves, Women & Homosexuals: Exploring the Hermeneutics of Cultural Analysis.* Downers Grove, IL: IVP Academic.

Willard, Dallas. 1997. *The Divine Conspiracy.* New York: HarperSanFrancisco.

Winter, Bruce. 2001. *After Paul Left Corinth: The Influence of Secular Ethics and Social Change.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Wolvaardt, Bennie. 2005. *How to Interpret the Bible: A Do-It-Yourself Manual.* London: Veritas College.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

## MWANDISHI



Jonathan Menn anaishi Appleton, WI, USA. Alipokea shahada yake ya B.A. ya heshima ya sayansi ya siasa kutoka katika chuo cha Wisconsin-Madison, mwaka 1974, na baadaye alijumuika na Phi Beta Kappa kwa kuwa na heshima ya kijamii. Tena akapata J.D. kutoka kwa Shule ya Uanasheria cha Cornell, magna cum laude, mnamo mwaka wa 1977, na akawekwa kwenye mamlaka ya Kisheria ya Coif haki za heshima ya jamii. Akaitumia miaka iliyofuata 28 akifanya kazi za uanasheria, kama wakili, wa huko Chicago na baadaye akashirikiana na Shirika la mawakili liitwalo Menn Law Firm kule Appleton, WI. Alikuwa muumini na mfuasi wa Yesu Kristo tangu mwaka wa 1982. Kukua kwa pendo lake katika Thiolojia na Huduma vilimfanya aende akatafute Shahada ya Uzamili ya mambo ya Mungu katika chuo cha Trinity Evangelical Divinity School huko Deerfield, IL. Alipokea shahada yake ya M.Div. kutoka kwa TEDS, summa cum laude, mnamo Mei 2007. Kati ya 2007-2013 alikuwa Mkurugenzi wa Afrika ya Mashariki wa Equipping Pastors International. Sasa Jonathan ni Mkurugenzi wa huduma ya Equipping Church Leaders-East Africa (**www.eclea.net**). Vitabu vyake mbalimbali vya mafundisho ya biblia vinapatikana katika tovuti ya huduma **www.eclea.net**. Unaweza kuwasiliana na Jonathan kwa anuwani hii ya baruapepe: **jonathanmenn@yahoo.com**.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2007-2013. Haki zote zimehifadhiwa.